**31 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 31 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**SPIKA:** Hati za kuwasilisha mezani, Waziri wa Nishati kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Stephen Lujwahuka.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. JULIANA D. MASABURI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati kwa mwaka

wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe sasa aulize swali lake.

Na. 479

### Kuboresha maslahi na mazingira ya kazi kwa walimu

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali katika kuboresha maslahi na mazingira ya kazi kwa walimu ili kuwaongezea morali ya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi kwa kupeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya mafunzo kwa walimu ambapo shilingi bilioni 1.9 zimetumika. Aidha, vitendea kazi kama vile kompyuta, printa, *photocopy* na *projector* vimenunuliwa kwa ajili ya walimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imetoa vishikwambi kwa walimu wote wa shule za msingi na sekondari ili waendane na dunia ya sasa ya sayansi na teknolojia. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 2.03 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na taratibu za ununuzi zinaendelea. Vilevile, Serikali imetenga shilingi bilioni 5.04 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vituo 252 vya walimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuviimarisha vituo vya Walimu kwa ajili ya wao kukutana na kujengeana uwezo utakaowaimarisha katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji na itaendelea kuboresha maslahi ya Walimu kadri fedha zitakavyopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, pamoja na jitihada kubwa za Serikali kuboresha miundombinu na kutoa vifaa, nini mpango wa Serikali sasa kutoa posho ya kufundishia *(teaching allowance)* kwa Walimu wote nchini ili kuongeza morali ya kazi?

Swali la pili, nini mkakati wa Serikali sasa kutoa posho ya mazingira magumu kwa watumishi hasa Walimu wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu kijiografia kama ilivyo Ukerewe na Mafia? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kuhusu hii posho *(teaching allowance)* Serikali itaendelea kuangalia suala hili na kadri ya uwezo wake wa kibajeti tutaendelea kuliona ni namna gani tunaweza tukalitekeleza. Vilevile kuna Halmashauri ambazo

Wakurugenzi wao wenyewe kupitia mapato yao ya ndani wamekuwa wakitoa motisha kwa Walimu hasa wale ambao wanaenda kuripoti kwa kuwapa magodoro na vifaa vingine vya kwenda kuanzia maisha.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la posho ya mazingira magumu. Hili tunalipokea kama Serikali na tutaendelea kulifanyia *analysis* na kuona ni namna gani tunaweza tukapata fedha ya kuweza kulitekeleza hili lakini kwa sasa bado tutaendelea katika mazingira yote kuwa-*treat* watumishi wetu sawa na haki sawa katika maeneo yote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, uhamisho pia ni sehemu ya maslahi ya walimu, je upi utaratibu ambao Serikali inautumia kwa ajili ya kuhamisha walimu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ili waache kutufuata Wabunge tuwasaidie uhamisho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, suala hili la uhamisho kuwa ni sehemu ya maslahi ya walimu, utaratibu uko wazi na Mwalimu anapokuwa ameajiriwa kwanza atakaa mwaka mmoja wa *probation* katika eneo lake ambalo amepelekwa kufanya kazi. Baada ya hapo pia atatumikia nafasi hiyo kwa miaka mingine miwili kabla ya kuomba uhamisho.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili kumekuwa kuna *influx* kubwa sana ya watumishi kutaka kuhamia Mijini na kuhama maeneo ya pembezoni. Wakumbuke wakati wanaajiriwa waliajiriwa kwa sababu ya upungufu uliopo maeneo ya pembezoni ikiwemo maeneo mengine ya Halmashauri ya Wilaya ya Momba kule. Hivyo ni wajibu wao kubaki katika maeneo yale na kuhudumia Watanzania waliokuwepo kwenye maeneo yale.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, suala la mazingira magumu ni suala kubwa sana na kuna walimu wanaofundisha sehemu ambazo ni ngumu sana kama milimani, kuna wengine wanaishi mijini na tambarare. Serikali hamuoni kwamba ni muhimu kulichukua hili suala mara moja na kuliangalia kuliko kila wakati muwe mna *repostponed* na sehemu hizo ngumu zinakosa walimu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba kuna maeneo magumu ya mazingira magumu kama milimani kama Jimboni kule kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, tutaendelea kuliangalia kadri ya uwezo wa kibajeti wa Serikali tutaona ni namna gani tunaweza tukaanza kufanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya Mbunge wa Nyasa sasa aulize swali lake.

Na. 480

**Hitaji la wodi Kituo cha Afya Kihangara – Nyasa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga wodi katika Kituo cha Afya Kihangara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya Mbunge wa Jimbo la Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma za afya nchini, Serikali imeanza na uboreshaji wa miundombinu ya Vituo vya Afya, kipaumbele kikiwa ni utoaji wa huduma za dharura na upasuaji ambapo fedha iliyotolewa ilielekezwa kujenga jengo la wazazi, jengo la upasuaji, jengo la maabara, jengo la kufulia na nyumba ya mtumishi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) inakusudia kuanza ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa kwenye Vituo vya Afya ambavyo vilikwisha pokea fedha za ukarabati na ujenzi jumla ya vituo vya afya 807 vinahitaji kujengewa wodi za kulaza wagonjwa kikiwemo Kituo cha Afya Kihangara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza ninaishukuru sana Wizara pamoja na Madaktari wote wa Wilaya ya Nyasa kwa huduma ambayo inatolewa.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza kwa kuwa hali ya kituo hiki mbali ya kukosa wodi kabisa hasa ya akina mama pia hawana *ultrasound* kiasi kwamba hata inapofikia kupasua mama labda kwa ajili ya mtoto mimi naona ni suala la kubahatisha, hiyo inapelekea pia kuleta changamoto.

Je, ni lini Serikali itafikiria sasa kupeleka mashine hiyo ya *ultrasound* ili hawa wakina mama wafanyiwe huduma iliyo kamilifu?

Swali la pili, Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais wakati wa kampeni alipita katika Kata ya Lituhi na baada ya wananchi

kumuomba akaahidi wajengewe kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais ikizingatiwa kwamba ni Kiongozi Mkuu wa nchi na wananchi wanayo matumaini makubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Manyanya kuhusu hali ya kituo cha afya hiki ambacho ameulizia kwenye swali lake la msingi, tutaangalia katika bajeti ambayo tunaanza kuitekeleza mwaka wa fedha 2023/2024 kuona ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa ili waweze kununua *ultrasound* mara moja ambayo itaenda kuhudumia akina mama wajawazito katika eneo hili la Kihangara.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Kata ya Lituhi kuhusu kujengewa kituo cha afya. Naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kuweza kufika katika Kata ya Lituhi na kufanya tathmini, kuona uhitaji ambao upo, idadi ya watu waliopo katika eneo hili na kisha kuwasilisha taarifa hizi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ili katika mipango yetu tunayoweka ya ujenzi wa vituo vya afya, tuweze kuweka ujenzi wa Kituo cha Afya Lituhi ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kituo cha Afya cha Nzihi na Kituo cha Afya cha Mgama kwa kweli havina kabisa wodi za akina baba na wamekuwa wakilalamika muda mrefu na nimeshaomba mara kadhaa. Je, ni lini sasa Serikali itatujengea hizo wodi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa wodi katika Kituo cha Afya Nzihi na Kituo cha Afya Mgama kama nilivyokwishakusema kwenye majibu ya msingi, Serikali baada ya ujenzi wa vituo vya 807 sasa tunaenda kuona ni namna gani tunapata fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi kwenye vituo vya afya vilivyofanyiwa ukarabati na kupewa majengo yale ya awali yaliyoenda kujengwa katika vituo vya afya na tutaangalia pia kuhusu Kituo hichi cha Nzihi na Mgama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga Mbunge wa Itilima sasa aulize swali lake.

Na. 481

**Ujenzi wa Madaraja – Itilima**

**MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga madaraja katika Mto Garamoha, Isolo, Nyagokolwa, Mbogo na Mhuze Wilayani Itilima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Jimbo la Itilima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, *TARURA* iliajiri Mhandisi Mshauri ambao ni Chuo cha Ufundi Arusha kufanya uchunguzi wa kijiolojia katika Mto Garamoha ambapo kazi hiyo imekamilika kwa gharama ya shilingi milioni 35. Kwa sasa *TARURA* inaendelea na usanifu wa daraja hilo kwa lengo la kupata gharama halisi za utekelezaji wa ujenzi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mto Isolo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 41 kwa ajili ya kujenga daraja la mawe sehemu ya kwanza ya Mto Isolo. Ujenzi wa daraja la pili katika Mto Isolo usanifu wake utafanyika katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kutumia wataalam wa ndani wa *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mto Mbogo, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 40 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya usanifu wa ujenzi wa daraja kwa tekinolojia ya upinde wa mawe lenye ukubwa wa mita 15 ili kupata gharama halisi. Mto Mhuze umetengewa shilingi milioni 30 kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa kijiolojia ili kuwezesha kusanifu kwa daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa madaraja katika Mto Garamoha, Isolo, Mbogo na Mhuze utaendelea baada ya kukamilika kwa usanifu ili kupata gharama halisi za ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga swali la nyongeza.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na jinsi walivyojibu katika swali la msingi. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Daraja la Mto Garamoha ni daraja linalounganisha Kata tatu, Kata ya Mwaswale, Nkuyu na Ndolelezi na daraja lile hupelekea kipindi cha mvua wananchi kushindwa kupita katika eneo hilo kwenda kupata huduma katika Kata ya Sagata. Sasa kwa kuwa fedha ni kiasi kidogo cha bajeti ya *TARURA* kwa nini Serikali isiweke kwenye fedha za maendeleo ili kusudi wananchi waweze kujengewa daraja hilo?

Swali la pili, kwa kuwa katika Kata ya Mwaswale kuna barabara ambayo *TARURA* wamejenga kutoka Makutano hadi Mwakubija lakini bado kilomita 51 za kutoka Mwakubija kwenda Sopalodge. Serikali sasa haioni umuhimu wa kufungua barabara ya kutoka Mwakubija kwenda Sopalodge kwa ajili ya kwenda kufanya shughuli za kiutalii katika Wilaya hii ya Itilima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Silanga swali lake la kwanza kuhusu fedha iliyotengwa kwa ajili ya daraja hili la Mto Garamoha, tutaangalia katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 tuone fedha hii iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja hii inakwenda mara moja ili kuweza kujenga daraja hili kuweza kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Silanga.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la kujenga barabara hii ya kilometa 51 kutoka Maswale kuelekea Sopalodge. Barabara hii tayari ujenzi wake ulikuwa umeshaanza hapo awali na kwa sasa hii barabara inapita katika Pori Tengefu la Maswa katika maeneo ya Nyasosi kuelea Sopalodge ambapo barabara kufika Nyasosi pale wameishia pale na bado hizo kilometa 51. Kwa sababu barabara hii ni muhimu sana ambayo inafupisha wananchi wa maeneo haya badala ya kuzunguka kilometa 250 wanakuwa wanaenda chini ya kilometa 100 kufika katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuipa kipaumbele kadri ya upatikanaji wa fedha ili tuweze kujenga barabara kuanzia Gwalali kuelekea Makutano hadi kufika Mwakibija na kuelekea kule Sopalodge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madaraja ya kuunganisha Jimbo la Mbagala na Jimbo la Mkuranga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika,

Serikali ina mpango wa kujenga madaraja ya kuunganisha Wilaya hizi mbili au Mikoa hii miwili, Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa sasa, tumeweka daraja la Mto Kitonga kuhakikisha katika mradi wa *DMDP* II ambapo fedha hizi zitakapopatikana kuanzia mwaka wa fedha huu Novemba, 2023 tutaanza utekelezaji wa kujenga daraja hili. Barabara hii ni ya muhimu sana kwa sababu kuna huduma nyingi za mchanga unaotoka katika Wilaya ya Mkuranga kuelekea Mkoa wa Dar es Salaam inapita katika barabara hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura Kiswaga swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa, wananchi wa Kata ya Mwamanga Kijiji cha Mwamanga, Inolelo na Kisasa B, wanapata shida sana wakati wa mvua kwenda kwenye huduma hasa wanafunzi wa sekondari. Je, Serikali ina mpango gani wa kutupa fedha kwa ajili ya kujenga barabara na daraja hili kuunganisha hasa *bottleneck* ili wananchi wapate huduma hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nitakaa na Mheshimiwa Kiswaga tuone katika bajeti ya 2023/2024 ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi huu wa daraja katika Kata ya Mwamanga kule Wilayani Magu na kama haijatengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024 basi tutaangalia kutenga fedha kwenye mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige swali la nyongeza.

**MHE. CHATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Je, ni lini Serikali kupitia *TARURA* itajenga Daraja la Mto Juwe kuunganisha Kijiji cha Eyasi, Mdito, Oldonyosambu na Jema Wilayani Ngarongoro Mkoa wa Arusha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeanza usanifu wa Daraja la Mto Juhe katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kupitia Wakala wa Barabara Vijijini *(TARURA)* na ilikuwa imetengwa shilingi milioni 200 kama na nane hivi, kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa madaraja na makaravati katika barabara hii ambayo inapita katika eneo hili la Mto Juhe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja ya Mto Nyahende kule Nyansulula, Daraja la Mto Tabora kati ya Mbalibali na Lungabule pia Daraja la Mto Kikala kati ya …

**SPIKA:** Swali la nyongeza ni moja Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali lake la kwanza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la Mheshimiwa Amsabi Mrimi la Mto Nyahende kule Wilayani Serengeti tutaangalia katika mwaka wa fedha huu ambao tumeidhinishiwa na Bunge lako tukufu wa 2023/2024 kuona kama fedha ilitengwa ya kuanza ujenzi wa daraja hili. Kama fedha hiyo haikutengwa tutaangalia katika kuitenga kwenye mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu sasa aulize swali lake.

Na. 482

**Ujenzi wa Daraja la Juu Mto Mwamanongu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa daraja la juu katika Mto Mwamanongu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 43 kwa ajili kufanya usanifu wa Daraja la Mto Mwamanongu. Usanifu huo umekamilika na jumla ya shilingi bilioni 7.5 zinahitajika kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo. Serikali itajenga daraja hilo kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhudumia miundombinu ya Wilaya ya Meatu kwa kujenga, kukarabati na kufanya matengenezo ya barabara na madaraja kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru hadi hapo ilipofikia ni kazi kubwa imefanywa na Serikali, Mheshimiwa Rais Samia alipita njia hiyo akaiona hiyo adha kwenye hilo daraja. Je, Serikali iko tayari kutoa kipaumbele kwenye mwaka ujao wa fedha kwa sababu Wilaya tumetenga hizo fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mvua inaponyesha Kata ya Mwabuzo, Mwamanongu, Imaraseko, Mwamalole hukata mawasiliano na Wilaya. Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuja kuiona hiyo adha wanayopata Wananchi wa Jimbo la Meatu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kutoa kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili ambalo Mheshimiwa Mbunge aliliuliza kwenye swali lake la msingi na tutaangalia kadri ya upatikanaji wa fedha kwenye mwaka wa fedha 2023/2024, kuona ni namna gani tunaweza kuanza na kama fedha basi zitakuwa hazitoshi katika mwaka huo wa fedha tutaenda kuona tunatenga fedha kwa ajili ya kutekeleza pia ahadi hii ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la pili la kama nipo tayari kuongozana naye kwenda kuona namna miundombinu ilivyoharibika katika maeneo haya ya Jimbo lake kule Meatu. Nipo tayari kuongozana nae na baada tu tukihitimisha Bunge hili la bajeti tarehe 30 Juni mwaka huu, mimi nipo tayari kupanga na Mheshimiwa Komanya ili tuweze kuelekea wote kule Meatu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kata ya Mwamishali ina changamoto ya daraja la kutoka Mwambiti, Tongoleangamba hadi Buliashi ambayo ni Makao Makuu.

Je, ni lini Serikali itajenga daraja hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itajenga daraja hili la Mwamishali kuelekea Makao Makuu ya Kata kadri ya upatikanaji wa fedha. Tutaangalia katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 kuona kama fedha imetengwa kwa ajili

ya usanifu na ujenzi wa daraja hili na kama haijatengwa tutatenga katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 kadri ya upatikanaji wa fedha hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 483

**Vigezo vya ajira nchini**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali inaajiri kwa kigezo cha mwaka wa kumaliza chuo na kupitia mafunzo ya jeshi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutoa ajira kwa kada mbalimbali zinazohitajika katika Utumishi wa Umma, Serikali imekuwa ikizingatia Sera ya Menejimenti ya Ajira na Utumishi wa Umma Toleo la 2 la mwaka 2008 aya ya 4.2 ambayo inataka zoezi la ajira katika Utumishi wa Umma liendeshwe kwa wazi na ushindani ili kuwezesha Serikali kupata watumishi wenye utaalam na sifa stahiki kwa kuzingatia uwezo, weledi na umahiri wa waombaji fursa za ajira.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta ushindani katika soko la ajira, vigezo mbalimbali hutumika kuzingatia mazingira maalum au mazingira mahsusi ya waajiri. Katika vyombo vya Ulinzi na Usalama na Taasisi zilizoingia katika mfumo wa Jeshi USU kutokana masharti ya kazi hizo na mahitaji maalum au mahsusi ya vyombo husika,

ajira zinazotolewa kwa kigezo cha ukomo wa umri na kigezo cha kupitia Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa

Mheshimiwa Spika, kada nyingine katika Taasisi za Umma nje ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Taasisi zenye mfumo wa Jeshi USU kigezo cha Kupitia Mafunzo ya Jeshi hakitumiki. Hata hivyo, waombaji wa fursa za Ajira Serikalini kwa masharti ya kudumu Serikali wanatakiwa kuzingatia Kanuni ya D. 39 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 ambayo inawataka wasiwe na umri usiopungua miaka 18 na wasiozidi umri wa miaka 45 kwa lengo la kuwawezesha kuchangia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii walau kwa miaka 15 ili kustahili kulipwa pensheni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, ni zaidi ya miaka mitano imepita tulikuwa hatuna ajira katika Taifa letu, tunaonaje kama tusibadilishe angalau utaratibu kwa sababu wale wa miaka mitano ambao hawajaajiriwa na mkawataka wa hivi karibu hatuoni kama tunawaacha nje kwenye mfumo wale ambao walimaliza kwa miaka hiyo mitano ya nyuma? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa JKT zamani ilikuwa ni mujibu wa sheria kila mwanafunzi akimaliza anaenda mwaka mmoja JKT lakini sasa hivi bajeti kwa kuwa ndogo wananchaguliwa wachache. Hatuoni kwamba tunawanyima nafasi wale wachache ambao hawajachaguliwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na *gap* hilo la miaka mitano kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia kulihakikishia Bunge lako kwamba ziko jitihada za maksudi zinazofanywa na Serikali kuhakikisha kwamba *gap* hilo tunalitoa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI tumekwishaanza kufanya jitihada hizo na unayoyaona yanayotokea sasa ikiwemo kuongezeka kwa matangazo ya nafasi za ajira ni moja kati ya hatua hizo zinazofanyika.

Mheshimiwa Spika, juu ya jambo la pili, kuhusu vijana ambao wameachwa katika kipindi hiki cha miaka mitano iliyopita ambao hawajajiunga na JKT, ambao Mheshimiwa Mwakagenda anasema ni *group* la wasomi. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia kulihakikishia Bunge lako kwamba Serikali katika utaratibu huo huo imeendelea kufanya juhudi za maksudi kuhakikisha kwamba *gap* hilo nalo tunalifunga ili vijana wengi wa Kitanzania waweze kupata fursa hiyo. Kwa kweli katika jambo hili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa vibali vingi sana vya ajira katika kipindi cha mwaka 2022/2023 ambapo vibali 20,000 vilitoka pia 2023/2024 ambapo vibali zaidi ya 30,000 navyo vimetolewa kwa ajira mbalimbali ikiwemo ikiwemo ajira hiyo ya vijana ambao wamekosa sifa za kuingia JKT.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'azi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 484

**Vigezo vya kubaini kaya maskini – *TASAF***

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka wazi vigezo vya kubaini kaya maskini zinazostahili kupokea msaada wa *TASAF*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kumjibu Mheshimiwa Injinia Mwanaisha Ng'azi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vigezo vya utambuzi wa kaya za walengwa viko wazi na vinatambulika. Vigezo hivyo ni kama ifuatavyo ili kuweka *record* sawa katika Bunge lako:-

(i) Kaya ambazo hazina uwezo wa kupata kwa uhakika angalau milo miwili kwa siku;

(ii) Kaya isiyo na kipato cha uhakika na inayo wategemezi wengi wakiwemo watoto wanaokosa huduma za elimu na afya;

(iii) Kaya zinazoishi kwenye makazi duni yanayohatarisha usalama wa kaya;

(iv) Wazee wasio na msaada wowote;

(v) Watoto wanaoishi wenyewe bila wazazi au walezi.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivi ndivyo vimewezesha Serikali kuweza kuhudumia kaya za walengwa 1,378,000 ambao wanaendelea kunufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini *(TASAF)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nitaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, umaskini unatofautiana kutokana na mahali kwa mahali. Maskini wa jamii ya wafugaji, makazi siyo kitu cha msingi kwake, lakini maskini wa mahali pengine makazi inawezekana ikawa ni kitu cha msingi kwake. Kwa hiyo, ni lini Serikali itaona haja ku-*standardize* hivi vigezo vya kuzipata kaya maskini ili jamii ile iepukane na migogoro? *(Makofi)*

Swali langu la pili, nitazungumzia vile vipengele vinne vya Miradi ya *TASAF* na nitazungumzia suala zima la *Public Work Program* kwamba, kwa kuwa miradi hii inapokamilika inakabidhiwa katika mitaa au vijiji. Ni lini sasa Serikali itaweka utaratibu maalum kuhakikisha kwamba wanashirikishwa wanakijiji wote au jamii yote ili miradi ile iwe vipaumbele kwa jamii husika badala ya zile kaya zilizolengwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza juu ya ku - *standardize* vigezo. Utaratibu wa kupata wahusika au wafaidikaji ni utaratibu kwanza shirikishi. Wananchi wanashirikishwa katika ngazi ya kijiji, wanajadili juu ya taratibu zao, wanajadili juu ya vigezo na kutambua wapi ambao wanatakiwa kufaidika katika mradi huo. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie, tunapokwenda hata kwenye jamii ya wafugaji, wafugaji wenyewe wanashirikishwa ili kuweza kutambua na kutanabaisha vipaumbele vyao. Hivyo pia tunapokwenda kwenye jamii za wakulima na jamii mbalimbali. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba taratibu ziko wazi, vikao vinayokaa ni shirikishi na wanavyohitaji wananchi ndivyo ambavyo mradi wetu wa *TASAF* unakwenda kusimamia.

Swali la pili juu ya vipaumbele ambavyo vipo katika maeneo yetu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyokuwa nimejibu katika swali la msingi na maelezo ya ziada katika swali lake la kwanza la ziada, kwa uhakika kabisa nataka nimuhakikishie yeye na kulihakikishia Bunge lako kwamba tunapokwenda katika vijiji mambo yote yanayotakiwa na wanayohitaji wananchi ndiyo kipaumbele cha mradi huo wa *TASAF* na siyo vinginevyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo,

Mheshimiwa Justine Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

Na. 485

**Serikali kuongeza tija katika uzalishaji Pareto**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA K.n.y. MHE. JUSTINE L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la Pareto Wilayani Kilolo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbuge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tija ya sasa ni kati ya kilo 280 hadi 300 ya pareto kavu kwa ekari. Hata hivyo, tija inayoweza kufikiwa na wakulima wengi ni kati ya kilo 400 hadi 500 kwa ekari moja. Pamoja na mambo mengine tija ndogo inasababishwa na wakulima wengi kwa muda mrefu kuendelea kutumia mbegu ambazo zina tija ndogo na wakulima walio wengi kutopendelea kutumia mbolea katika uzalishaji wa zao la pareto.

Mheshimiwa Spika, aidha, kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo katika mwaka wa fedha 2022/2023 ilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 200 ambazo zilipelekwa *TARI* kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora na zenye tija. Upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora hizo unatarajiwa kuanza msimu 2023/2024. Mbegu hizo ambazo zitakuwa na tija kuanzia kilo 400 na zaidi kwa ekari zitasambazwa kwa wakulima wote wa pareto nchini ikiwa ni pamoja Wilaya ya Kilolo. Usambazaji huo utaenda sambamba na utoaji elimu ya mbinu bora za kilimo cha pareto kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuendesha tafiti za matumizi ya mbolea kwa zao la pareto. Utoaji wa elimu utafanywa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi hususan Wanunuzi na Wasindikaji wa zao katika Wilaya ya Kilolo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri yenye kutia matumaini, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali imekiri kwamba upatikanaji wa pembejeo ndiyo shida mojawapo inayofanya zao hili lisilete tija iliyokusudiwa. Je, Serikali haioni pamoja na kwamba mwakani itatusambazia hizo mbegu bure, je na pembejeo zingine kama mbolea tutazipata?

Swali la pili, kwa kuwa tunayo Bodi ya Pareto, je, Serikali haioni umuhimu wa kuiwezesha hiyo Bodi ya Pareto kwa kuwaongeza bajeti na kuwaongezea watumishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema pamoja na usambazaji wa miche bora ambayo itasaidia katika kuongeza tija pia wakulima wa pareto wanaingia katika mpango wa mbolea ya ruzuku. Kwa hiyo ni wanufaikaji na watanufaika pia kupitia mbolea hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusu bajeti kwenye Bodi ya Pareto tunaendelea kulifanyia kazi suala hili, tumeendelea kuijengea Bodi uwezo tofauti na miaka miwili iliyopita, lengo letu ni kulikuza zao la pareto ambalo limekuwa na manufaa makubwa. Kwa hiyo, Bodi tutawajengea uwezo kuhakikisha kwamba bajeti yao inaongezeka pia.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 486

**Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Kata ya Serya – Kondoa**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji katika Kata ya Serya utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Serya iliyopo katika Tarafa ya Kondoa Mjini ipo takriban kilometa 20 kutoka Kondoa Mjini. Mwaka 2007, Vijiji vya Mongoroma na Serya vilitenga eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta 3000. Pia Kijiji cha Mongoroma kilitenga eneo la ujenzi wa bwawa ambalo linapakana na eneo la pori la hifadhi ambalo lilikuwa tayari na aina mbalimbali za wanyama. Skimu inatarajiwa kutumia maji ya mvua pamoja na kuchepusha maji ya Mto Bubu na kuyahifadhi kupitia ujenzi wa Bwawa la Mongoroma. Eneo hili linastawisha mazao mbalimbali yakiwemo mahindi, mtama, mbaazi na mbogamboga zinazolimwa kwa kiwango kidogo pembezoni mwa Mto Bubu kwa njia ya Umwagiliaji wa kutumia pampu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali kupita Mfuko wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji ngazi ya Wilaya chini ya *ASDP 1* ilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina wa bwawa na skimu, pamoja na maandalizi ya awali ya jamii husika katika kushiriki katika ujenzi wa Skimu na Bwawa la Mangoroma/Serya.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi, ongezeko la watu na makazi kufuatia kasi ya kukua kwa Mji wa Kondoa eneo la bwawa kupakana na hifadhi Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kwa kushirikiana na Halmashauri ina mpango wa kuhuisha tafiti za awali zilizofanyika mwaka 2010/2011 pamoja na kufanya utafiti mpya wa athari za mazingira na jamii, matokeo ya uhuishaji wa tafiti hizo, yataiwezesha Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 kutega fedha za ujenzi wa Bwawa na Skimu ya Mongoroma/Serya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Makoa, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, ninakushuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yenye kuridhisha ya Serikali nataka kujua sasa, Je, hizo shilingi milioni 300 ambazo zilitengwa kwa kufanya kazi zilizotajwa na Mheshimiwa Waziri hapo, zilitolewa na zikafanya kazi iliyokusudiwa ama walifanya tafiti tu za awali?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali ina makusudio ya kufanya kuanza ujenzi mwaka ujao wa fedha, kwa kazi ya kuhuisha sasa hii skimu na hizi ripoti na tafiti, Wizara safari hii imetenga kiasi gani kwa ajili ya kazi hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya fedha shilingi milioni 300 kama zilitoka au la. Madhumuni makubwa ya fedha hizi zilikuwa ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ndiyo maana katika majibu yangu ya msingi nimesema katika kupata tathmini halisi, tumetenga fedha tena mwaka huu kuhakikisha ya kwamba tunalipitia eneo lote ili kupata taarifa sahihi na kuanza ujenzi wake kwa sababu tumepata changamoto miradi mingi ilipata changamoto kubwa, kwa sababu usanifu wa kina

haukufanyika na imekuwa siyo ya kudumu muda mrefu na hivyo kuleta athari kubwa kwa sababu mara kwa mara imekuwa ikibomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tunakwenda kurudia kufanya kazi hii kubwa katika umakini mkubwa zaidi na ku-*involve* wataalam wengi zaidi ili tupate kitu ambacho kitaleta tija kwa wananchi wa Kondoa Mjini.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusu fedha kama zimetengwa. Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ya kwamba tunajiandaa kufanya zoezi hili katika mwaka wa fedha 2023/2024 ili ujenzi uanze katika mwaka wa fedha unaokuja 2024/2025. Kwa hiyo, nimtoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaangalia namna ya kuweza kulifanikisha kwa uharaka kwa sababu tunajua wananchi wa Serya na eneo la Mongoroma ni wakulima wazuri hatutaki kuwachelewesha, tutafanya kwa uharaka ili wafanye kilimo cha umwagiliaji katika eneo lao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itajenga Skimu ya Umwagiliaji Muhuruzi - Nyakahura Wilaya ya Biharamulo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye kitabu chetu cha bajeti, kiambatisho Namba 11 Ukurasa wa 206 tumeitaja Skimu ya Muhuruzi katika Wilaya ya Biharamulo kama sehemu ambazo zitajengwa katika mwaka huu wa fedha unaoanza Julai. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kazi inafanyika katika mwaka wa fedha ujao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika Halmashauri ya Kasulu Vijijini ipo miradi ya umwagiliaji katika Kata ya Titye na Rungwe Mpya. Miradi hiyo haijakamilika kutokana na ukosefu wa fedha.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha miradi hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kwanza ambayo tuliifanya kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ni kuhakikisha tumepitia miradi yote ambayo haijakamilika na ili tujue changamoto ambazo zimefanya imekwama na tuweze kuikwamua. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba katika orodha ya miradi hiyo, miradi anayoitaja pia imo. Tutaikwamua ili wananchi wafanye kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 487

**Kuanzisha Benki ya Vijana**

**MHE. LUCY J. SABU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha Benki ya Vijana Wajasiriamali?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa uwezeshaji vijana kiuchumi, Serikali ipo katika hatua ya kuandaa mkakati wa upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati, ambao utawezesha vijana kupata mitaji kupitia benki, taasisi za huduma ndogo za fedha, masoko ya mitaji, mifuko na programu za Serikali za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya utekelezaji wa mkakati huu, Serikali inatarajia kuanzisha taasisi mahsusi ya fedha itakayosimamia upatikanaji na utoaji wa mikopo kwa makundi maalum wakiwemo vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo wamachinga. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy John Sabu swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii, naomba sasa niulize swali dogo la nyongeza.

Kwanza naipongeza Serikali kwa majibu mazuri, kwa kuwa katika mkutano wa vijana Mkoa wa Mwanza na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliahidi kwamba tutaanzisha Benki ya Vijana Wajasiriamali.

Je, ningependa kufahamu ni hatua zipi zimefikiwa katika mchakato wa uanzishwaji wa benki hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, awali ya yote naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Lucy pamoja na Wabunge wengine wote kwa kufuata nyanyo za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutaka kujua au kuona hali ya vijana wetu kiuchumi inaimarika.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sabu kwamba suala hili lipo katika hatua ya majadiliano katika kikao kazi cha Makatibu Wakuu,

litakapokamilika tu hatua iliyopo sasa, basi tutajulishwa ili wananchi wote wajue na hatua nyingine ziweze kuendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 488

**Hitaji la maeneo ya malisho ya mifugo – Ushetu**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga maeneo ya malisho ya mifugo katika Pori la *Usumbwa Forest Reserve?*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mahitaji ya Wananchi wa Ushetu na inaendelea kufanya tathmini ya eneo la Msitu wa Usumbwa *Forest Reserve* ili kujiridhisha kama unastahili kumegwa kwa ajili ya kutengwa eneo la kuchungia. Pindi tathmini itakapokamilika wananchi watajulishwa. Wakati Serikali inaendelea na tathmini hiyo wananchi wanashauriwa kuendelea kuheshimu maeneo hayo ili kuhifadhi msitu huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, wananchi wa Ushetu wanaheshimu sana mipaka ya Serikali kwenye mapori yetu na ni walinzi wazuri sana, lakini idadi ya ng’ombe wa wananchi wa Ushetu inazidi kuongezeka. Mpaka

sasa Wananchi wa Ushetu wana ng'ombe 176,000 na wanapakana na mapori haya hawana kabisa eneo la kuchungia.

Je, Serikali itamaliza lini hii tathmini ili wananchi hawa waweze kupata sehemu ya kulishia mifugo yao, badala ya kuendelea kugombana na watu wa maliasili?

Swali langu la pili, Halmashauri ya Ushetu ina mapori matatu. Inayo pori la *Usumbwa Forest Reserve*, *Ubagwe Forest Reserve* pamoja na Mpunze Saba Sabini, lakini *Ubagwe Forest Reserve* imekuwa na mgogoro mkubwa sana na Halmashauri ya Kaliua ambao umechukua sura mpya. Hata juzi wananchi wangu wamekamatwa wakawekwa ndani bila sababu za msingi, mbaya zaidi juzi kumekuwa na mgogoro kati ya maliasili wa *TFS* na Askari wa Maliasili wa Ushetu, Mheshimiwa Naibu Waziri huo mgogoro anaujua nilimtaarifu.

Nini kauli ya Serikali na Mheshimiwa Waziri ni lini tutaenda kutatua mgogoro huu kwa wananchi wangu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Katika eneo hili la kulishia mifugo, ninaendelea tu kumshauri Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Ushetu kwamba, kwa kuwa Wizara ya Maliasili imepewa dhamana ya kuyalinda na kuyasimamia maeneo haya, inapofika suala la mahitaji ya maeneo ya mifugo basi waendelee kuwasiliana na Wizara husika ili tukae Pamoja, tuone namna iliyo bora ya kutenga maeneo haya, tumepewa kazi ya kuyasimamia tu na kuyatunza maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine hili la kuhusu mipaka na migogoro kati ya *TFS* na Pori la Usumbwa *Forest Reserve* tunaendelea kuangalia namna ya kuainisha mipaka na kwa kuwa sote ni Serikali moja kwa maana ya Halmashauri na *TFS,* hakuna haja ya kugombania mipaka isipokuwa ni masuala ya

kiutawala tu kwamba hawa ni *TFS* na hawa ni Halmashauri ni kukaa pamoja tu ili sote tulinde haya mapori kwa pamoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji Mheshimiwa Esther Lukago Midimu Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 489

**Utekelezaji wa Mradi wa Maji Sumve, Malya na Malampaka**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya mradi wa maji Sumve, Malya na Malampaka baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa miradi ya maji Sumve, Malya na Malampaka kupitia chanzo cha maji cha Ziwa Victoria. Mji wa Sumve utapata maji kupitia mradi wa maji Ukirugulu – Usagala – Kolomije hadi Sumve. Mkandarasi yupo eneo la mradi anaendelea na kazi. Aidha, Miji ya Malya na Malampaka itapata maji kupitia mradi wa maji wa Hungumalwa na Mkandarasi ameajiriwa mwezi Mei, 2023.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo, na Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka hadi kukamilika kwa miradi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza kabisa ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Naomba uniruhusu nimshukuru Mheshimiwa Rais wangu ametupatia fedha shilingi bilioni 440 kwa ajili ya mradi wa Ziwa Victoria kuleta Simiyu na Wilaya zake Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu, mkataba tumesaini juzi tarehe 27 mwezi wa Tano. Ahsante sana Mama yangu.

Mheshimiwa Spika, swali dogo, kwa kuwa Mkoa wa Simiyu ni Mkoa wa wafugaji; je, napenda kujua mradi huu utahudumia na upande wa mifugo pia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa kutambua jitihada za Mheshimiwa Rais na tutaendelea kuunga jitihada zake kwa kuhakikisha tunasimamia vema fedha zote ambazo anazielekeza kwenye miradi hii mikubwa. Kuhusiana na mifugo wakati Mheshimiwa Waziri akisaini mradi huu mkubwa alioshukuru Mheshimiwa Mbunge Esther, tayari tumetenga malambo sita kwa ajili ya mifugo, hivyo mifugo pia itanufaika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba mradi wa kutoa maji kutoka Mto Mafumbo kwenda kwenye Mji wa Mlowo na Vwawa unatekelezwa kwa haraka, ili kuondoa adha ya wakazi wa Mlowo na Vwawa wanaokabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mto Mafumbo ni moja ya chanzo kilichogunduliwa na Ofisi yetu ya Bonde la Ziwa Tanganyika na tayari Ofisi ya Vwawa - Mlowo wanashughulika na chanzo hiki kuhakikisha kiweze kutumika. Wameshaandika *proposal* imekuja Wizarani, ninaahidi tutafanyia kazi kwa sababu ya umuhimu wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Natambua zaidi ya bilioni 10 zimetumika katika mradi wa maji Bunda kutoka Nyabeu kuleta Mjini. Bado kuna tatizo la usambazaji katika Kata zote 14, tunahitaji shilingi bilioni saba ili kata zote 14 zipate huduma ya maji safi na salama.

Ni lini sasa Serikali mtakamilisha usambazaji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo haya aliyoyataja Kata Saba tayari kama Wizara tunayafanyia kazi na usanifu unaendelea, tutahakikisha usambazaji hautachukua muda utakamilika ndani ya wakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 490

**Ukarabati wa Mnada wa Olokii**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa mnada wa ng'ombe na mbuzi wa Olokii?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara ya mifugo hapa nchini kwa kujenga na kukarabati minada ya mifugo ya awali, minada ya upili na minada ya mipakani. Kwa sasa kuna jumla ya minada 504 ya awali, 17 ya upili na 12 ya mpakani. Mnada wa Olokii (Themi) ni moja ya minada ya upili ambao upo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 na Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali imejenga na kukarabati minada 12 katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itafanya usanifu wa miundombinu ya mnada wa Olokii (Themi) ili uweze kuingizwa katika Mpango wa Bajeti wa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, mnada huo hakuna choo, hakuna maji na wananchi wanapeleka mifugo yao mara kwa mara pale na mnakusanya fedha nyingi pale. Je, Serikali haioni sasa kuna

umuhimu wa kuchukua hatua ya dharura kujenga choo na kupeleka maji pale ikisubiria mpango mkubwa?

Swali la pili, je, kwa kuwa mnada huo pia Wizara ndiyo inakusanya fedha, kwa nini fedha hizo ambazo mnazikusanya isitumike kwa ajili ya kukarabati mnada huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, jambo la kwanza tukiri changamoto ambazo Mheshimiwa Mbunge amezieleza na akiwa anahitaji hatua za dharura. Nimuondoe shaka kwamba hizo hatua za dharura kwa mahitaji hayo kama ya vyoo pamoja na maji basi tutawaelekeza wataalamu katika maeneo hayo waweze kuyafanyia kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusu makusanyo ya fedha ambazo zinakusanywa pale kwamba ndiyo zifanye ukarabati, nimwambie tu kwamba mnada ule unahitaji ukarabati mkubwa na ndiyo maana tunataka tufanye tathmini na tuujenge kwa viwango ambavyo vinastahili. Kwa hiyo tutalietekeleza hili kama ambavyo Serikali imepanga katika mipango yake, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nimekuwa nikiuliza mara kadhaa kuhusu ujenzi wa Soko la Samaki katika Jimbo langu la Mchinga, Kata ya Mchinga lakini mara zote nimekuwa nikipewa tu ahadi, ahadi, ahadi! Sasa naiomba Serikali inipe *commitment* kuhusu suala la ujenzi wa hilo soko la Samaki, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza ninakiri kwamba Serikali ni kweli imekuwa ikitoa ahadi kwa ajili ya ujenzi wa soko la samaki katika Jimbo la Mchinga na jambo hilo mpaka sasa hivi bado halijafanyika, sababu za kutofanyika ni kwamba mpaka sasa Serikali tunatafuta

fedha ili tufanye usanifu wa kina na baadae tulijenge soko hilo. Kwa hiyo, *commitment* ya Serikali iko pale pale kwamba soko hilo tutalijenga na wakati uliopo sasa ni kutafuta fedha, ninaamini kabla hatujamaliza hii miaka yetu miwili kuna hatua ambayo tutakuwa tumeifanya na kufikia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

Kwa kuwa, Waziri wa Mifugo alishatembelea mnada wa Duka Bovu katika Wilaya ya Monduli na akaahidi ukarabati utaanza mara moja; je, ukarabati huu utaanza lini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mnada katika eneo la Monduli ambalo Mheshimiwa Mbunge ameutaja upo katika mipango ya Serikali, tunachosubiri tu ni malipo ambayo tukiyapata kutoka Hazina basi sehemu ya fedha hizo zitakwenda kwa ajili ya ukarabati. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini mtaboresha miundombinu kwa minada ya Kibaya, Dosidosi na Sunya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu awali, kwa sasa tunatafuta fedha ili tuhakikishe kwamba hiyo minada ambayo

Mheshimiwa Mbunge ameitaja tunaikarabati na kuitengeneza kwa viwango ambavyo vinavyotakiwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge waondoe shaka wananchi kwamba Serikali ya Awamu ya Sita itatekeleza kama ilivyoahidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Mnada wa Kata ya Soya ni kati ya minada mikubwa ambayo inafanya shughuli za uuzaji wa mifugo kwa maana ya mbuzi, ng'ombe, kondoo pamoja na punda lakini mnada ule miundombinu yake ni chakav.

Je, Serikali mko tayari kuutembelea mnada ule nakujionea halia halisi ili muweze kutenga fedha itakayoweza kukarabati mradi huo ili wakulima wa mifugo waweze kuutumia mnada ule kwa tija na kwa maana ya afya kwa watumiaji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tuko tayari kufika katika eneo la Soya, bahati nzuri ni karibu hapa tunaweza tukapanga tu baada ya muda wa Bunge tukafika na kujionea hali halisi ili tuweze kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati huo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Idd Kassim Idd, swali la nyongeza.

**MHE. IDD K. IDD:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa Halmashauri ya Msalala imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 120 kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa mnada wa Kata ya Burige, sasa ni lini Serikali italeta fedha kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika mnada huo wa Burige?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwanza tuipongeze Halmashauri ya Msalala kwa kutenga fedha kwa ajili ya uzio wa mnada ambao Mheshimiwa Mbunge ameuainisha. Serikali tulishaweka *commitment* yetu kwa ajili ya kumalizia mnada huo, *commitment* yetu iko pale pale isipokuwa kwa sasa hivi tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha mnada huo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nilete tangazo la wageni ndiyo ninalo hapa mbele.

Tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika, kwanza ni wageni 127 wa Mheshimiwa January Makamba ambaye ni Waziri wa Nishati, sasa najiuliza anapigiwa Waziri au wageni wake kwa ujumla? Haya, ahsanteni sana. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni ni Ndugu Felchesmi Mramba - Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Athumani Mbuttuka - Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mhandisi Innocent Luoga - Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Wizara ya Nishati, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Ndugu Esther Kileo - Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi na Mjumbe wa Bodi *TANESCO* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Paul Makanza - Makamu Mwenyekiti wa Bodi *TPDC,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Janet Mbene - Mwenyekiti wa Bodi *REA*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya - Mwenyekiti wa Bodi *EWURA*, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Halfani Halfani, Mwenyekiti wa Bodi *PURA,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Profesa Shubi Kaijage -Mwenyekiti wa Bodi *TGDC*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Mhandisi David Ngula - Mwenyekiti wa Bodi *EWURA CCC,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Maharage Chande, Mkurugenzi Mkuu *TANESCO,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mussa Makame, Mkurugenzi Mkuu *TPDC,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mhandisi Hassan Said, Mkurugenzi Mkuu *REA,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. James Andilile Mkurugenzi Mkuu *EWURA,* karibu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Shemeji.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana, tusikilizane. Haya ngoja nirudie, ngoja nirudie Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Yupo Mhandisi Danstan Asanga, Kaimu Mkurugenzi Mkuu *PURA*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Ndugu Erasto Simon, Mtendaji Mkuu *PBPA,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mhandisi Mathew Mwangombe, Kaimu Meneja Mkuu *TGDC*. *(Makofi)*

Yupo Mhandisi Mohamed Abdallah Meneja Mkuu *ETDCO* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mhandisi Yusuph Kitivo, Kaimu Meneja Mkuu *TCPM* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Mhandisi Baltazari Mrosso Kaimu Meneja Mkuu *GASCO,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu James Sanawa Kaimu Meneja Mkuu *TANOIL* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Renata Ndege, Mkurugenzi wa Fedha *TANESCO*, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Balozi Mathias Chikawe, Mwenyekiti wa Bodi *TIPA,* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Mohamed Seif Mohamed, Mkurugenzi Mkuu *TIPPER,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Haruna Maseba ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati ya Bodi ya Wakurugenzi *EWURA,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Floriana Haule, Mjumbe wa Bodi *REA;* yupo Salvatory Ntomola - Mkurugenzi wa Bodi *TPDC;* yupo Ndugu Michael Mjinja - Kamishna wa Petroli na Gesi; yupo Ndugu Mpambika Chiume - Mkurugenzi *DPD;* yupo Ndugu Petro Liatuu - Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Nishati; na yupo Ndugu Ziana Mlawa - Mkurugenzi wa Rasilimali watu, Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Ndugu Derick Moshi, Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji *TPDC;* na yupo Ndugu Keneth Mutaonga, Mkurugenzi Utafutaji *TPDC*. *(Makofi)*

Pia wapo Chama cha Waagizaji na Wasambazaji Mafuta Tanzania *(TAOMAC),* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yapo pia makampuni wanaotekeleza mradi wa *LNG,* karibu sana. *(Makofi)*

Kipo Chama cha Waendelezaji wa Nishani JADIDIFU Tanzania *(TAREA),* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nishati kutoka Jimboni kwake, wageni kutoka Bumbuli, haya nadhani watapata nafasi badaye, amesimama mmoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya yupo mgeni wa Mheshimiwa January Makamba - Waziri wa Nishati ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Morogoro huyu ni Ndugu Mwinshehe Adam Yange, karibu sana na yupo pia Ndugu Hamoud Abuu Jumaa, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishani na hawa ni Mkurugenzi Mtendaji wa *Evosha Trading Company* Ndugu Jastin Ishengerema, karibu sana. Ameongozana na Ndugu Nathani Omary Kimaro, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wetu wengine ambao ni wa Wabunge sasa. Tunae mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria ambaye ni mchezaji wa *golf* na mshindi wa kwanza wa mashindano ya *Kenya Ladies Open 2023*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mgeni huyu kwa sasa hapa nchini ndiyo mcheza *golf* namba moja kwa upande wa wanawake. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa huyu ni mshindi namba moja, wale washindi wa humu ndani Bungeni tunaishia humu tu, yule ndiye mshindi kwa hapa nchini, sawa lakini nimejulishwa pia kwamba huu ni ushindi wake wa tano katika shindano hilo. Alishinda pia mwaka 2016, 2017, 2018 na 2019, kwa hiyo tunampongeza sana sana kwa kuiwakilisha nchi yetu vizuri na naamini wale Wabunge ambao wanaendelea na kujifunza *golf* hasa wanawake watakuwa wakimtumia yeye kama mfano, wanaweza nao kufanya vizuri sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko - Waziri wa Madini kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga kutoka Kalenga, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wagen 41 wa Mheshimiwa Hassan Mtenga ambao ni wanafunzi wa Vyuo kutoka Mtwara na Lindi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata kutoka Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Amandus Chinguile ambao ni Wakandarasi wa Miradi ya *REA* Jimbo la Nachingwea, Liwale pamoja na Mikoa mingine, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil ambao ni Wenyeviti wa Matawi na Wadi kutoka kwa Kwahani Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ravia Faina ambaye ni mtoto wake kutoka Makunduchi, Kusini Unguja, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo ambao ni walimu na wanafunzi wa Kingugi Sekondari ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 100 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Kilimanjaro ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 42 na walimu wanne wa *Southern Highlands School* ya Mafinga Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao, wageni wengine nimejulishwa wataingia baadaye, kwa sababu hawakupata nafasi ya kuingia sasa na wale ambao tumeshawatangaza tayari na wataingia baadae basi tangazo hili linawahusu na wao ili tuweze kuokoa muda, wale ambao hawajatangazwa kabisa tutawatangaza kadri wanavyopata nafasi ya kuingia hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Yusuph Makamba aje awasilishe hoja ya Wizara yake, Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii na naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/2023 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, tunaomba hotuba tuliyoiwasilisha mezani na kuwasilishwa kwenye Vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge iingie kama ilivyo kama Taarifa Rasmi za Bunge na hapa nitasoma muhtasari.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kuwajalia afya Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine mbalimbali. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdor Mpango, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa miongozo na maelekezo mbalimbali yaliyotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge, Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Wajumbe wote wa Kamati. Pia na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kipindi cha mwaka uliyopita unaoisha wa fedha mmetushauri, mmetutia moyo, mmetuhamasisha, mmetusaidia kuwa makini zaidi na matokeo na mafanikio tuliyoyapata katika Wizara yetu yanatokana na mchango wenu Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kwa heshima na tahadhima naomba nitoe shukurani zangu na pongezi mbalimbali kama zilivyofafanuliwa kwa kirefu katika sehemu ya utangulizi wa hotuba tuliyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nizungumzie mwelekeo wa dunia katika masuala ya nishati na maendeleo ya sekta nyingine hapa nchini pia niongelee utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha unaokwisha, pamoja na mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya mabadiliko ya tabiachi inayoendelea duniani na kutokana na vita baina ya Urusi na Ukraine mwelekeo wa dunia kwenye masuala ya nishati umebadilika kwa kiwango kikubwa sana. Malengo ambayo dunia imejiwekea katika kupunguza hewa ukaa yamepelekea msisitizo, mwelekeo na uwekezaji mpya na mkubwa kwenye nishati jadidifu kwa maana ya *renewable energies.* Mwelekeo huu

umesababisha masoko ya mitaji na misaada na mikopo ya miradi ya nishati kujielekeza katika kugharamia nishati inayozalishwa, nishati safi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwelekeo huu wa kidunia na Tanzania ikiwa ni sehemu ya familia ya Mataifa, hatuna budi sasa kutekeleza mikakati ya kuimarisha matumizi ya vyanzo vya nishati vyenye athari ndogo zaidi kwa mazingira. Hata hivyo, kama nchi hatutosita kutumia rasilimali zetu zote za uzalishaji wa nishati ili kukidhi mahitaji ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya Gesi asilia iliyokandamizwa *(CNG)* na umeme katika uendeshaji wa magari. Vilevile tutashirikiana na wadau mbalimbali ambao wameonesha nia ya kuwekeza katika teknolojia mpya za nishati ikiwemo *hydrogen*. Aidha, mwelekeo mpya wa Wizara ya Nishati sasa ni kuendelea kushamirisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili ifikapo mwaka 2023 asilimia walau 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, pia katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha mazingira ya biashara ya nishati ya mafuta ya duniani yamebadilika kwa kiwango kikubwa sana, hasa mafuta yanayotoka Urusi. Nchi ya Urusi ni nchi ya tatu kwa uzalishaji wa mafuta duniani hivyo kuondoka kwa kiwango kikubwa cha mafuta kutoka Urusi kwenye Soko la Dunia kumepelekea upungufu mkubwa wa mafuta duniani na hivyo kuongeza bei ya bidhaa hiyo duniani.

Aidha, nchi nyingi za Afrika ikiwemo nchi yetu Tanzania na kwingineko duniani zimekabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa Dola za kimarekani kwa ajili ya kulipia uagizaji wa mafuta hayo. Changamoto hiyo/hizi kama nilivyo eleza zimeikabili pia nchi yetu na kutoa viashiria vya tishio la upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na kupanda kwa bei.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali ilijidhatiti na kuchukua hatua za muda mfupi na wakati wa kukabiliana na changamoto hizi. Kwa sasa, Serikali inapanga mikakati ya muda mrefu ya

kujilinda na athari hizi na kuhakikisha kwamba nchi yetu wakati wote ina mafuta ya kutosha na kwa bei inayohimilika.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge ndiyo maana mwaka jana wakati tunasoma bajeti ya Wizara yetu bei ya *petrol* kwa lita ilikuwa shilingi 3,301 bila ruzuku na bei ya *diesel* ilikuwa shilingi 3,452 kwa lita bila ruzuku lakini leo bei ya mafuta hayo ni shilingi 2,871 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, menedeleo ya nchi yoyote yanahitaji uhakika wa upatikanaji wa nishati. Aidha upatikanaji wa nishati ya uhakika na kwa gharama nafuu ni kichocheo cha kuvutia uwekezaji na kuwezesha bidhaa na huduma zinazozalishwa kuwa shindani kwa masoko ya ndani na ya Kimataifa. Upatikanaji wa nishati ya uhakika na kwa gharama nafuu ni kichocheo cha kufanikisha mipango na malengo ya sekta nyingine za uzalishaji mali ikiwemo viwanda, kilimo, uvuvi, ufugaji, madini na maliasili. Mafanikio katika sekta hizi za uzalishaji mali na huduma, yanaongeza ajira na mapato kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo basi, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya uhakika wa nishati na uhakika wa ajira na mapato ya Serikali. Vilevile nishati ya uhakika ni muhimu katika utoaji wa huduma bora za kijamii ikiwa ni pamoja na afya, elimu, maji safi na mawasiliano, katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Aidha, upatikanaji wa nishati safi hasa vijijini unasaidia kuilinda nchi yetu dhidi ya athari za uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, nishati pia ni mhimili wa sekta ya usafirishaji. Reli tunayojenga sasa ya *SGR* inatumia umeme na kwa kweli itategemea upatikanaji wa umeme wa uhakika. Magari tunayotumia kusafirisha abiria na bidhaa yanatumia mafuta na yatategemea uhakika wa upatikanaji wa mafuta na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, tunayasema haya yote kuonesha ni kwa kiasi gani nishati imefungamanishwa na sekta zote za uchumi na huduma za jamii na hasa ndiyo muhimili wa maendeleo ya nchi na ustawi wa wananchi. Kwa msingi huo, uwekezaji katika sekta hii ya nishati ndiyo utakaotuhakikishia kufikia malengo yetu kama

nchi. Serikali imefanya kazi kubwa katika kuwekeza katika nishati. Kutokana na malengo yetu makubwa ya maendeleo, kutokana na kasi ya ukuaji uchumi, kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu na kutokana na kiu kubwa ya wananchi hasa wa vijijini kushiriki kwenye uchumi wa kisasa. Uwekezaji mkubwa Zaidi unahitajika kwenye sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalitambua hili na bajeti hii itaonesha dhamira ya Serikali kuongeza uwekezaji katika sekta ya nishati. Mahitaji ya umeme yameongezeka kwa kasi katika mwaka huu wa fedha unaokwisha, ambapo rekodi ya kiwango cha juu cha mahitaji ya umeme *(peak demand*) imevunjwa mara nane.

Mheshimiwa Spika, jambo hili siyo la kawaida katika historia ya mahitaji ya umeme nchini. Aidha, uzalishaji wa umeme hapa nchini kwa sasa hauendani na mahitaji ya shughuli za kiuchumi na kijamii ambayo yanaongezeka kwa kasi. Aidha, kuna upungufu mkubwa wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Vilevile baadhi ya miundombinu ni chakavu na mingine imezidiwa na matumizi ikilinganishwa na ilivyokusudiwa. Kwa upande mwingine pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupeleka umeme vijijini, takribani Vitongoji 36,101 kati ya Vitongoji 64,760 bado havijafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, pia mahitaji ya gesi asilia kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, matumizi katika taasisi, majumbani na viwandani na kwenye vyombo vya moto, yameendelea kuongezeka pasipo kwenda sambamba na kasi ya uzalishaji wa nishati hiyo. Katika bajeti hii Serikali imeweka mipango na mikakati kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba sekta ya nishati ndiyo mhimili wa maendeleo ya nchi, mwelekeo wa Wizara sasa ni kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka megawati 1,872.05 za sasa na kufikia megawati 5,810.22 itakavyofika mwaka 2025/2026 ili kukidhi mahitaji ya umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maono haya umezingatia umuhimu wa kutekeleza miradi ya uzalishaji wa umeme unaotokana na vyanzo mbalimbali *(energy mix)* ambapo ushiriki

wa sekta binafsi utazingatiwa. Kwa kuwa umeme ukishazalishwa lazima usafirishwe na kusambazwa kwa watumiaji, mwelekeo wa Wizara sasa pia ni kuongeza idadi na urefu wa njia za kusafirisha umeme, kutoka kilomita 6,110.28 za sasa, hadi kufikia kilomita 10,670.95 kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa njia za usambazaji umeme mwelekeo ni kufikia kuongeza njia hizi kutoka kilomita 154,567 za mwaka 2021/2022 hadi kufikia kilomita 226,302 kwa mwaka 2025/2026. Serikali itatilia mkazo matengenezo na utunzaji endelevu wa miundombinu ya umeme pamoja na kukabiliana na upotevu wa umeme. Dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na tija na ufanisi katika umeme unaozalishwa, unaosafirishwa, unaosambazwa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, azma ya Wizara ni kuhakikisha kwamba wananchi wote katika nchi yetu wanafikiwa na huduma ya umeme, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vitongoji vyote katika nchi yetu vinapata umeme ndani ya muda mfupi. Serikali itajidhatiti kuhakikisha kwamba wananchi wa vitongoji wenye kiu kubwa ya nishati ya umeme hawasubiri miaka 20 kupata nishati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2022/2023 uliongozwa na vipaumbele 12 kama vinavyofafanuliwa katika sehemu *D* ya hotuba yangu ambavyo utekelezaji wake umeelezwa katika nyaraka ambazo zitagawiwa. Mnakumbuka mwaka jana tuligawa kipeperushi vya vipaumbele vyetu 12, mwaka huu tumewaletea chati ya utekelezaji wa vile vipaumbele pamoja na vipaumbele vipya naamini vitagaiwa wakati wowote lakini pia ni sehemu ya hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha unaokwisha Wizara ya Nishati iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 2.91 hadi Aprili Mwaka huu Wizara ilipokea jumla ya shilingi trilioni 1.78 sawa na asilimia 61.17 ya bajeti iliyoidhinishwa. Katika mwaka huu wa fedha unaokwisha Serikali ilitekeleza miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya kuimarisha uzalishaji, usafirishaji, usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na umeme Mijini. Pia tulifanya kazi ya utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, uchakataji na usafirishaji na usambazaji wa

mafuta na gesi. Pia katika mwaka huu unaokwisha tulihamasisha kwa kiasi kikubwa matumizi ya nishati safi ya kupikia, vilevile tuliimarisha upatikanaji wa huduma zinazotolewa na Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusimamia masuala ya udhibiti katika sekta ya nishati sehemu *D* ya hotuba yangu inafafanua kwa kina utekelezaji wa miradi na kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha unaokwisha. Kutokana na hatua zilizochukuliwa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka huu unaokwisha kupitia utekelezaji wa miradi na kazi zilizopangwa yalipatikana mafanikio mbalimbali ambayo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwenye uzalishaji wa umeme, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja yafuatayo:-

Kwanza, tumeongeza uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika gridi ya Taifa kufikia Megawati 1,872.05 ikilinganishwa na Megawati 1,694.55 zilizokuwepo mwaka 2021/2022. Hili ni ongezeko la asilimia 10.5. Vilevile tumeongeza kasi na umakini katika kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere na kufikia asilimia 87 ikilinganishwa na asilimia 60.22 za mwezi Aprili mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, pia tumekamilisha mradi wa kuzalisha umeme wa *Kinyerezi One Extension* wa Megawati 185 ambapo mitambo yote sasa imewashwa na umeme ule wa Kinyerezi umeingia kwenye gridi ya Taifa. Pia mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo wa Megawati 80 umefikiaasilimia 99 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023.

Mheshimiwa Spika, pia tumenunua mtambo wa kuchoronga visima vya uhakiki *(drilling rig)* kwa miradi ya joto ardhi ambao utawezesha uchimbaji kwa maeneo yote yaliyoainishwa kuwa na viashiria vya joto ardhi. Pia tumekamilisha maandalizi ya miradi ya kuzalisha umeme ya Malagarasi Megawati 49.5, Kakono Megawati 87.8 na mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Megawati 150 ambayo sasa itaanza utekelezaji katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafirishaji na usambazaji wa umeme. Kulikuwepo na mafanikio yafuatayo:-

Kwanza, tumeongeza njia za kusafirisha umeme kufikia jumla ya urefu wa kilomita 6,363 sawa na ongezeko la asilimia 4.1, ikilinganishwa na kilomita 6,111.27 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Mei mwaka jana. Pia tumefanikiwa kuongeza miundombinu ya kusambaza umeme hadi kufikia kilomita 168,548.36 sawa na ongeezeko la asilimia 9.5 ikilinganishwa na kilomita 153,988.49 zilizokuwepo hadi kufikia Mei, 2022.

Mheshimiwa Spika, pia tumekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa *Kilovolt* 220 yenye urefu wa kilomita 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi na pia tumekamilisha kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi. Pia tumekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Msongo wa kilo *volt* 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 94, pia tumepata mafanikio katika ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka kwenye mradi wa Julius Nyerere hadi Chalinze wa kilo *volt* 400 wenye urefu wa kiloita 160 ambapo sasa tumefikia asilimia 93.5 ikilinganishwa na asilimia 44 zilizokuwepo mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, aidha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze ambayo ni sehemu ya mradi huu imefikia asilimia 64 ikilinganishwa na asilimia 3.59 zilizokuwepo mwaka 2021/2022. Pia tumeanza kutekeleza awamu ya kwanza ya mradi mkubwa kabisa wa kuimarisha gridi ya Taifa utakaogharimu takribani shilingi trilioni 1.9 ili kukabiliana na uchakavu wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Mtakumbuka mwaka jana mwezi Februari Ikulu tulisaini mikataba 29 kwa ajili ya mradi huu mkubwa wa gridi imara ambao unaenda kumaliza changamoto ya kukatika katika kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, aidha tumesaini mikataba 14 ya kuimarisha usambazaji wa umeme vijijini. Mafanikio mengine ni Serikali kukamilisha maandalizi ya mradi mkubwa kabisa wa thamani ya shilingi trilioni 1.38 wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilo *volt* 400 ya kilomita 650 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma unaoitwa TAZA ikiwemo ulipaji wa fidia. Mradi huu utaenda sasa kuunganisha

Mkoa wa Rukwa kwa mara ya kwanza katika gridi ya Taifa lakini utatuwezesha kufikisha umeme Zambia na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, pia tumefanikiwa kwenye ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa msongo wa *Kilovolt* 132 kutoka Tabora hadi Mpanda ambao utafikisha gridi ya Taifa kwa mara ya kwanza katika Mkoa wa Katavi, mradi huu umefikia asilimia 29.7 na unatarajiwa kukamilika mwezi wa kwanza 2024. Pia, tumefanikiwa kwenye ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa *Kilovolt* 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma kwa ajili ya uendeshaiji wa *SGR Lot Two.* Mradi huu umefikia asilimia 98 na unakadiriwa kumalizika mwezi Agosti mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine pia tumefanikiwa kuzima mitambo inayotumia mafuta katika Wilaya za Kibondo, Kasulu, Ngara na Biharamulo na Loliondo kwa kuunganisha Wilaya hizo na gridi ya Taifa na katika tukio la kihistoria kwa mara ya kwanza kabisa baada ya miaka mingi tumetimiza ahadi ya kufikisha gridi ya Taifa Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze kuhusu nishati vijijini. Kama nilivyofafanua awali maendeleo ya jumla na upatikanaji wa huduma bora kwa watanzania utahitaji upatikanaji wa nishati ya uhakika, safi na ya gharama nafuu kwa Watanzania wote. Safari ya kufikisha nishati hiyo vijijini ilianza muda mrefu na katika mwaka huu wa fedha unaokwisha Serikali iliendelea na safari hiyo kwa kuchukua hatua mbalimbali. Kutokana na hatua zilizochukuliwa tumepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Jumla ya vijiji vilivyounganishwa na umeme nchini imefikia vijiji 10,127 sawa na asilimia 82 ya vijiji vyote 12,318.

(ii) Serikali imeanza maandalizi ya zoezi la kusambaza umeme katika vitongoji vyote ambavyo havina umeme.

(iii) Tumekamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Ifakara na kuunganisha wateja katika maeneo hayo na katika Wilaya za Kilombero na Ulanga.

(iv) Pia tumekamilisha uandaaji wa mwongozo wa kanuni za utoaji mikopo kwa waendelezaji wa vituo vidogo vya mafuta vijijini.

(v) Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kusambaza umeme kwa kutumia nguvu ya umeme wa jua katika visiwa 28 vilivyopo Mikoa mbalimbali nchini mwetu. Miradi hii ina thamani ya shilingi bilioni 11.18.

(vi) Tumefanikiwa kwenye eneo la kupeleka umeme katika maeneo ya huduma, ambapo katika mwaka huu wa fedha unaokwisha tumepeleka umeme katika vituo vya afya 66, pampu za maji 333 zilizopo vijijini. Kazi hii imegharimu shilingi bilioni 34.5

(vii) Jumla ya taasisi 43,925 zinazotoa huduma mbalimbali za jamii ikiwemo elimu, biashara, pampu za maji, vituo vya afya, nyumba za ibada zimeunganishwa na umeme.

(viii) Serikali imeanza kutekeleza miradi ya kupeleka umeme katika maeneo 336 ya wachimbaji wadogo wa madini pamoja na maeneo ya kilimo na viwanda katika maeneo ya vijijini haswa. Miradi hii ina thamani ya shilingi bilioni 115.

(ix) Tumetoa bei elekezi kwa kampuni Sita za wazalishaji wadogo wa umeme, ambao bei hizo zinahamasisha sasa na kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi katika eneo hili.

(x) Tumeimarisha usimamizi wa miradi ya kupeleka umeme vijijini kwa kuchukua hatua mbalimbali. Baadhi ya hatua tulizochukua ni kuajiri Waratibu wa Miradi hiyo katika Wilaya zote na waratibu wao kama mnavyofahamu tumeeleza wawasiliane na Wabunge kuwapa taarifa na kuwajulisha kuhusu maendeleo ya miradi hii. Vilevile tumeajiri wahandisi 20 wa miradi ya umeme vijijini, tumenunua magari 21 kwa *REA* kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi,

(xi) Tumeboresha vigezo vya zabuni za kuwapata Wakandarasi wa miradi ya umeme vijijini ili kuhakikisha kwamba Wakandarasi wanaopatikana ni wale tu wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais kiliundwa kikosi kazi cha Taifa, kwa ajili ya uandaaji wa dira ya miaka kumi ya kuhamia katika nishati safi ya kupikia. Kikosi hiki kinajumuisha Wizara na taasisi za Serikali zinazohusika na masuala ya nishati safi ya kupikia, ambapo Wizara ya nishati ni sekretarieti ya kikundi hicho. Aidha imeundwa Kamati ya Mawaziri ya kusimamia uandaaji wa dira hiyo chini ya uenyekiti wa Waziri Mkuu. Tayari dira na mkakati wa nishati safi ya kupikia vimeshaandaliwa na wadau wameshirikishwa na uzinduzi wake utafanyika mwezi Julai, 2023 ili kuwezesha hatua za utekelezaji kuanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ndogo ya mafuta na gesi Serikali iliendelea kusimamia sekta hii ambapo yalipatikana mafanikio mbalimbali. Katika hatua ya kihistoria hatimaye Serikali imekamilisha mzungumzo kuhusu mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika *(LNG)*. Mazungumzo haya yalikwama kwa miaka saba, mikataba sasa iliyokubaliwa itawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri mwezi Juni, Mwezi ujao kwa ajili ya kuidhinishwa kabla ya kusainiwa.

Mheshimiwa Spika, mradi kuu utakaogharimu Dola za Kimarekani bilioni 42 utabadilisha sura na taswira ya uchumi wa nchi yetu. Timu ya majadiliano ya Serikali imefanya kazi nzuri ya kupata mikataba yenye tija na maslahi kwa Taifa vilevile kubwa zaidi, kampuni yetu ya Taifa ya mafuta *(TPDC)* sasa na yenyewe ni mbia na mwekezaji katika mradi huu. Sisi siyo watazamaji tu au kusubiri mapato. Sasa kampuni yetu ya *TPDC* na yenyewe ni mbia na mwekezaji katika mradi wa dola bilioni 42 ni jambo la kihistoria ambalo halijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeanzisha Ofisi Mahsusi ya Mradi *(Project Office)* ikiwa ni hatua ya kuhakikisha mradi huu unaratibiwa, kufuatiliwa na kuwezeshwa kwa tija na ufanisi ili manufaa yake yapatikane kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

Vilevile imekubalika kwamba, itungwe Sheria Maalum ya Mradi *(Project Law)*. Sheria hii italetwa Bungeni kwa utaratibu wa kawaida kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeongeza uzalishaji wa gesi asilia hapa nchini katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita kutoka futi za ujazo bilioni 59.09 hadi kufikia futi za ujazo bilioni 68.02 sawa na ongezeko la asilimia 13.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumekamilisha malipo ya fidia kwa wananchi mbalimbali waliopisha ujenzi wa mradi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Uganda. Wamebaki wananchi wachache, kazi ambayo itakamilika katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, vilevile jumla ya kampuni za ndani na za ubia 1,748 zimesajiliwa hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu, ambapo kampuni 190 zimepata fursa za kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali katika mradi huu wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Uganda.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumesaini mkataba wa nyongeza wa uzalishaji na ugawanaji wa mapato katika gesi iliyogunduliwa Antoria katika Kitalu cha Ruvuma. Mkataba huu ambao utekelezaji wake utawezesha kuendeleza gesi asilia katika kitalu hicho ambacho kina takribani futi za ujazo trilioni 1.6 ulisainiwa kati ya Wizara ya Nishati, *TPDC* na Kampuni ya ARA, Oman.

Mheshimiwa Spika, vilevile Watanzania wengi wamepata ajira ya moja kwa moja na ajira nyinginezo kupitia mradi wa *ECOP* ambapo Watanzania 160 waliajiriwa kwa ajili ya uchukuaji wa *data* za mitetemo za mfumo wa *3D* katika Kitalu cha Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumepata mafanikio makubwa kwa nchi kuendelea kuwa na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta katika kipindi chote cha kuanzia mwezi Julai, 2022

mpaka leo hii. Tumeendelea kuwa na akiba ya kutosha ya mafuta na uhakika wa upatikanaji wa mafuta na bei ambayo ni himilivu tofauti na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeanza kazi ya kudurusu mikataba kifani ya uzalishaji na ugawanaji wa mapato *(MPSA)* kwa lengo la kuhuisha ili kuendana na mazingira ya uwekezaji wa sasa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeendelea kufanikisha ushiriki wa sekta binafsi katika uendelezaji wa sekta ya nishati ambapo makubaliano, mikataba mbalimbali ilisainiwa. Mmojawapo ni mkataba baina ya Serikali na Kampuni ya Enock ya Serikali za Umoja wa Falme za Kiarabu kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikubwa cha biashara ya mafuta katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki, ambacho kitakuwa pale Kigamboni ambacho kitafanya nchi yetu iwe na uhakika wa mafuta ya kutosha ndani ya nchi na kuweza kuuza katika nchi jirani za ukanda huu.

Mheshimiwa Spika, makubaliano haya sasa yanaendelea kutekelezwa na ndani ya miaka miwili tutaona nchi yetu ina mabadiliko makubwa sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupanda kwa kasi kwa bei za mafuta katika soko la ndani Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilianza kuweka ruzuku kwenye bei ya mafuta ambayo ni petroli na dizeli ili kuleta unafuu kwa wananchi hadi pale mafuta yalipoanza kushuka na bei kuwa stahimilivu. Kiwango cha ruzuku kilichotolewa na Serikali kuanzia mwezi Juni hadi Disemba mwaka jana ni shilingi bilioni 479.37.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hatua alizochukua za kutoa ruzuku hii ambayo ilikuwa na manufaa makubwa katika kupunguza makali ya bei ya mafuta katika uchumi wetu na wa Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele vya Wizara katika mwaka huu unaokwisha ilikuwa ni kuimarisha utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilibadili madeni ya *TANESCO* yaliyofikia shilingi trilioni 2.4 kuwa mtaji wa Serikali katika shirika hilo. Aidha, Serikali ilibadili mkopo wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar-es-Salaam wa Dola bilioni 1.9 kuwa mtaji wa Serikali kwenye *TPDC*. Hatua hizi zitaimarisha mizania ya hesabu *(Balance Sheet)* za mashirika hayo na hivyo kuyawezesha kuvutia uwekezaji, kuvutia biashara na kuongeza utendaji na vilevile mapato.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* imeendelea kutoa huduma mbalimbali ikiwemo kuimarisha Kituo cha Miito ya Simu *(Unified Call Center)* ambayo sasa inafanya kazi saa 24. Vilevile tumebadilisha mfumo wa maombi ya kuunganishiwa umeme ambapo sasa wastani wa kuunganishiwa umeme umeshuka kutoka miezi mitatu huko nyuma mpaka ndani ya siku nne na vilevile hulazimiki kwenda *TANESCO* sasa hivi kuomba kuunganishiwa umeme. Tumeanzisha huduma inaitwa NIHUDUMIE ambayo imeongeza uwezo wa Serikali, uwezo wa *TANESCO* kuwasiliana na wateja kuhusu matatizo yanayowakabili na kushughilika nayo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *EWURA* vilevile tumeboresha mfumo wa *National Petroleum and Gas Information System* unaoiwezesha *EWURA* na Serikali kupitia mamlaka hiyo kupata taarifa za hali ya upatikanaji wa mafuta wakati wote hapa nchini. *EWURA* imeboresha mfumo wa kupokea maombi ya leseni ya umeme, mafuta na vibali vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utendaji katika mashirika haya, Serikali, Mheshimiwa Rais, tuliteuwa Bodi ya Wakurugenzi wa *EWURA* inayoongozwa na Waziri wetu na Mzee wetu anayeheshimika Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya,

ambapo pia, tuliteua Mtendaji Mkuu pia wa mamlaka hiyo mwenye uwezo mkubwa Dkt. James Andilile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali iliunda Bodi mpya ya *REA* inayoongozwa pia na Waziri Mstaafu mwenye uwezo, Mheshimiwa Mama Janeth Mbene, vilevile na kuajiri waratibu wa Kanda na Wilaya zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile kama mnavyofahamu Serikali pia, iliunda Bodi mpya ya *TPDC* ambayo inaongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Balozi Ombeni Sefue na kufanya mabadiliko makubwa kwenye *management* ya shirika hilo ambapo Serikali pia imeondoa *management* yote ya Kampuni Tanzu ya *TANOIL* na kutengeneza mkakati mpya wa biashara na uendeshaji wa kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, utabaini kwamba, kwenye taasisi za Wizara zetu tumeunda Bodi nzito zinazoongozwa na watu wazito tukiwa na imani kwamba, uzoefu wao katika siasa, katika utumishi wa umma, katika sekta binafsi, utatusaidia sisi kuimarisha *governance* katika taasisi zetu. Ndiyo maana unaona yuko Mheshimiwa Mzee Mwandosya, Balozi Sefue, Mheshimiwa Mama Mbene, Mzee Khalfan Khalfan, lakini pia na Wajumbe wa Bodi ni wazito. Hii yote ni katika kuimarisha utendaji wa mashirika haya kama tulivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya tuliyoyapata kulikuwa na changamoto mbalimbali ambazo zilitukabili katika utekelezaji wa majukumu yetu katika mwaka uliokwisha. Serikali imechukua hatua mbalimbali kushughulika na changamoto hizo kama tulivyoeleza katika hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka unaokwisha, napenda sasa kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa mwaka huu unaokuja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele vilevile tulivyojiwekea mwaka jana ambavyo vimeorodheshwa katika bajeti ambayo

tumewapatia, vilevile katika nyaraka ambazo mtagawawiwa. Ninachoweza kusema tu ni lengo letu, kama Wizara, dhamira yetu ya jumla ni kuifanya sekta ya nishati kushamirisha shughuli za biashara na uzalishaji mali na kuziwezesha sekta nyingine, hasa za huduma za jamii na uzalishaji mali kutimiza malengo yake.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie. Dhamira yetu sisi kwenye Wizara ya Nishati ni kuiwezesha sekta ya nishati kushamirisha shughuli za biashara na uzalishaji mali na kuziwezesha sekta nyingine zote za uchumi na huduma hapa nchini kutimiza malengo yake. Lengo letu ni kuifanya Wizara yetu iwe Wizara wezeshi kwa Wizara nyingine, vilevile tunataka kuifanya sekta ya nishati kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, kuboresha ustawi wa Watanzania na kufikiwa kwa malengo ya jumla ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka huu wa Fedha unaokuja pamoja na mambo mengine umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020, maagizo na maelekezo ya Viongozi wa Kitaifa kuhusu sekta ya nishati na Mwongozo wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha unaokwisha pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano wa 21/22 – 25/26. Miongozo mingine iliyozingatiwa ni sera, mikakati, programu mbalimbali za kisekta na kitaifa, pamoja na malengo ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030 kuhusu nishati.

Mheshimiwa Spika, miradi, mipango, mikakati na programu zilizotekelezwa kwa mwaka huu wa fedha unaokwisha na gharama za utekelezaji ni kama inavyofafanuliwa kisekta katika sehemu ya hotuba yetu ambayo tumeiwasilisha, lakini kwa ufupi naomba nieleze kwamba, katika mwaka huu unaokuja wa fedha Serikali kupitia Wizara ya Nishati itatekeleza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tutakamilisha Mradi wa Julius Nyerere. Naomba nirudie, katika mwaka huu wa fedha unaokuja tutakamilisha ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kubwa kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, katika kipindi cha wiki moja kuanzia leo bwawa letu litafikisha kiwango cha ujazo kinachowezesha kuanza uzalishaji wa umeme. Naomba nirudie tena; Kwa kuwa, siku za nyuma kumekuwa na shaka ya masuala ya mazingira na uwezekano wa bwawa letu kujaa maji, naomba niwatangazie rasmi kwamba, tumepata baraka kwamba, katika kipindi cha wiki moja kuanzia sasa tutafikia kiwango cha chini cha kuweza kuzalisha umeme kwa Bwawa … *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango cha chini ni mita 163 kutoka usawa wa Bahari na tumebakiza mita kama mbili kufikia kiwango hicho na tutafika huko, lakini vilevile katika mwaka ujao wa fedha Serikali itakamilisha ufungaji wa mitambo ya kuzalisha umeme. Vilevile tutamaliza kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka kwenye *Power House* kwenda kwenye *Switch Yard*. lakini tutakamilisha vilevile ujenzi wa barabara za kudumu, lakini vilevile katika mwaka ujao wa fedha tutafanya tukio jingine kubwa la kihistoria la kuingiza umeme wa Julius Nyerere kwenye Gridi ya Taifa kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini Wabunge baadhi hapa wamesafiri kwenda Julius Nyerere kutoka hapa Viwanja vya Bunge jana na wameona mradi huu. Vilevile katika mwaka ujao wa fedha Serikali kupitia *TANESCO* itaanza utekelezaji wa miradi ya *CSR*, miradi ya kijamii, inayotokana na makubaliano ya mkataba wa ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Serikali itajenga chuo kikubwa cha kisasa cha Kimataifa cha Ufundi wa Umeme na Mafuta na Gesi Mkoani Lindi, kuna vyuo vingine pia vitajengwa kama awamu zinavyokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea na miradi mingine ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia maji, Huruma Kali, Ruhuji, Kikonge, Malagarasi, Kakono na vilevile katika mwaka ujao wa fedha kwa mara ya kwanza, kama nilivyosema, hii ni historia nyingine mpya; katika mwaka ujao wa fedha kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu tutaingiza umeme wa jua

mega wati 50 katika Gridi ya Taifa ambapo juzi tulisaini mkataba kwa ajili hiyo. Mradi huu uko Kishapu, Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali itaanza taratibu za malipo kwa wananchi na maandalizi ya mradi wa kuzalisha mega wati 300 kule Mtwara, ambapo wananchi wa Mtwara wameusubiri kwa muda mrefu. Kulikuwa na changamoto ya watoaji fedha kuacha kufadhili miradi ya gesi, lakini safari hii Serikali ya Japani imetujulisha rasmi kwamba, iko tayari sasa kufadhili mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kutokana na changamoto mahususi za upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Mtwara na kwa kuzingatia kwamba, gesi inayotumika kuzalisha asilimia 70 ya umeme wetu inatoka Mkoani Mtwara, Serikali itachukua hatua za dharura zitakazozaa matunda ndani ya siku 90 za kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Mtwara. Tumekaa na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara, juzi na tumekubaliana hatua hizo za kuchukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme. Kama tulivyoeleza kutokana na changamoto za muda mrefu za uchakavu wa miundombinu na miundombinu isiyotosheleza, Serikali imeendelea na miradi mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo na katika mwaka unaokuja tutafanya mingine ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tutakamilisha mradi wa kutoa umeme kutoka Julius Nyerere mpaka Chalinze na kukamilisha kituo cha kupoza umeme pale Chalinze, kama mnavyojua, lakini vilevile tutakamilisha mradi wa njia ya kutoa umeme kutoka Singida – Arusha mpaka Namanga wa kilovoti 400. Vilevile tutakamilisha mradi wa kusafirisha umeme wa kilovoti 220 kutoka Geita, Nyakanazi na kujenga miundombinu ya usambazaji wa umeme katika vijiji 32 vinavyopitiwa na mradi huo.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tutaendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme, vituo vya kupoza umeme, pamoja na miundombinu ya usambazaji wa umeme katika mradi mkubwa tunaoendeleanao sasa wa kupeleka kiloviti 400 kutoka Nyakanazi

mpaka Kigoma. Naomba niwape taarifa ya faraja wana-Kigoma ule umeme ambao umekuja sasahivi wa gridi ni umeme mdogo wa kilovoti 33, tunaleta umeme wa msongo wa kilovoti 400 Mkoani Kigoma na mradi huu upo mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tutaendelea na kukamilisha utekelezaji wa mradi wa kusafirisha umeme wa kilovoti 132 kutoka Tabora mpaka Mpanda na hivyo kufikisha Gridi ya Taifa kwa mara ya kwanza katika Mkoa wa Katavi katika mwaka ujao wa fedha. Vilevile tutakamilisha ulipaji wa fidia na kuanza ujenzi wa mradi wa kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga, kupitia Mbeya na Tunduma pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme. Vilevile tutaendelea na maandalizi ya ujenzi wa mradi wa kilovoti 220 kutoka Benako, Kyaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa gridi imara katika awamu inayofuatia na tutaanza matayarisho sasa ya awamu ya pili, kama nilivyoeleza, awamu ya kwanza iligharimu trilioni 1.9 ilikuwa na mikataba 29 katika mwaka ujao tutaenda kwenye awamu inayofuatia.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine tutakayofanya ni mradi wa kupeleka umeme, kusafirisha umeme kutoka Sumbawanga – Mpanda hadi Kigoma. Kutoka Dodoma hadi Chalinze. Kutoka Segera – Same – Arusha na vilevile mradi unaosubiriwa sana wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme pale Manyoni na wenyewe tutaufanya katika mwaka huu unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao mradi mwingine mkubwa ambao tunakuja nao, mwaka ujao wa fedha tutafanya nao maandalizi. Mradi huu ni mradi wa kujenga *sub station* kwenye kila Wilaya hapa nchini. Mradi huu utagharimu shilingi trilioni 4.20, hapa nchini tuna Wilaya za ki-*TANESCO* 147, Wilaya zenye *sub stations* ni 46. Moja ya changamoto tunazopata za umeme mdogo, umeme unaochezacheza, umeme unaokatikakatika ni kutokuwepo kwa *sub stations.* Kwa hiyo, tumeanza safari ya kujenga *sub stations* kwenye kila Wilaya ili kuimarisha upatikanaji wa umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme vijijini. Kama nilivyosema katika mwaka wa fedha unaokuja tutakamilisha mradi huu mkubwa tunaoendelea nao wa *REA III, Round II,* ambapo vijiji vyote hapa nchini vitafikiwa na umeme. Naomba nirudie, mwaka wa fedha unaokuja ndio mwaka ambao tutamaliza kazi yote ya kupeleka umeme katika vijiji vyote hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inakamilisha uchambuzi kuhusu namna ya ugharamiaji wa mradi wa kupeleka umeme vitongojini. Kwa sababu nafahamu, hata ukifikisha asilimia 100 ya kupeleka umeme vijijini, bado kutakuwa na vitongoji vingi visivyo na umeme. Kwa hiyo, kazi yetu sasa ni kuanza kutafakari tunagharamiaje na tunapelekaje umeme katika vitongoji katika kipindi cha muda mfupi. Kwa sababu kwa utaratibu wa upatikanaji wa fedha wa sasa, itachukua miaka 18 mpaka 21; tunataka kazi hiyo tuifanye ndani ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusubiri kazi hiyo kuianza, lakini tumeona walau tuanze safari ya vitongojini. Kwa hiyo, katika mwaka ujao wa fedha, tumetenga shilingi bilioni 370 kuanza kupeleka umeme katika vitongoji 3,000 walau vitongoji 15 kila Jimbo, na naomba niwape taarifa njema Waheshimiwa Wabunge; tutawapa nafasi na fursa ya kuchagua hivyo vitongoji 15 ni vipi. Tutakapoanza kazi hiyo basi mwaka unaofuatia ndani ya Serikali tumejadiliana, ndipo safari kwa ukubwa ya kupeleka katika vitongoji vyote vya mpigo itaendelea *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kutekeleza miradi mingine ya *REA* ambayo imebakia, miradi ya ujazilizi, miradi ya kujenga vituo vya kusambaza mafuta na petroli, miradi ya kupeleka umeme wa mfumo wa jua katika maeneo ya visiwani na miradi mingine ya kuwawezesha waendelezaji wa miradi midogo ya umeme jadidifu katika Wilaya na Mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni hatua ya kuhakikisha nchi yetu inakuwa na vyanzo mbalimbali vya uzalishaji nishati, katika mwaka huu wa fedha unaokuja, nguvu pia zitaelekezwa katika kuendeleza vyanzo vya umeme vya joto ardhi kupitia miradi hii ambayo tumeielezea.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mwezi Julai Serikali inatarajia kuzindua Dira ya Taifa ya Nishati Safi ya Kupikia inayolenga kuhakikisha kwamba nchi yetu inahamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo 2033 na kuanza utaratibu wa utekelezaji wa dira na mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuwahamasisha wananchi kuhusu nishati safi, tutawategemea Wabunge na makundi mbalimbali yenye ushawishi katika kazi hiyo. Tutasimamia uanzishaji wa Mfuko wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia na uboreshaji wa miundombinu safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *REA* tutapanga sasa katika mwaka huu wa fedha unaokuja, kutekeleza Mradi wa Mifumo ya Kuzalisha na Kusambaza Gesi za *LPG, CNG* na *biogas* kwa ajili ya kupikia katika taasisi takribani 100 zinazohutubia.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie vizuri. Kwamba tumetenga fedha za kutoa ruzuku kwa taasisi takribani 100 kujenga mifumo ya kupikia kwenye taasisi hizo na tutachagua taasisi karibu katika Majimbo yetu yote. Waheshimiwa Wabunge mtatuambia taasisi gani ina watu wengi inayohitaji ruzuku na msaada wa kupelekewa mifumo ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, vilevile kupitia *REA* tutasambaza majiko banifu 70,000 katika maeneo mbalimbali, vilevile tumetenga fedha kwa ajili ya kununua mitungi mingine 200,000 kwa ajili ya kuisambaza katika maeneo mbalimbali nchini na kutoa hamasa ya kuhamasisha matumizi ya nishati ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu, *TPDC* kupitia *REA* inaendelea na usambazaji wa mifumo mbalimbali ya gesi katika maeneo yaliyoko pembezoni mwa mkuza wa bomba kuu la kusafirisha gesi inayotoka Mkoa wa Mtwara. Kwa hiyo, katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani, katika vijiji vile ambavyo vinapitiwa na bomba, tutawapelekea gesi asilia katika vijiji hivyo ili waone manufaa ya mradi huo wa bomba la mafuta.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka unaokuja wa fedha, Serikali kupitia *PURA* inataraji kunadi vitalu vya utafutaji wa

mafuta na gesi asilia katika duru ya tano ya zoezi hili. *PURA* itaendelea na usimamizi na ukaguzi wa shughuli zinazotekelezwa katika vitalu vyote hapa nchini, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba sheria na mikataba inafuatwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali kupitia *TPDC* itaendelea na kazi mbalimbali za utafutaji wa mafuta na gesi katika vitalu vya kimkakati vya Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi – Wembere, Songosongo Magharibi, Ziwa Tanganyika na vitalu vya 4/1B na 4/1C vilivyopo kwenye Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali itaendelea na shughuli mbalimbali za uendelezaji na uzalishaji katika vitalu vinavyozalisha sasa vya Ntorya, Songosongo na Mnazi Bay. Lengo ni kuhakikisha kwamba gesi ya kutosha inaendelea kupatikana nchini na mikataba katika vitalu hivyo inazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia, kama nilivyoeleza hapo awali, kukamilika kwa majadiliano ya mradi huu wa *LNG* kati ya Serikali na wawekezaji, pamoja na kuanzishwa kwa ofisi maalum ya mradi, katika mwaka ujao wa fedha Serikali itaanza kazi za awali za maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu. Vilevile tutawajengea uwezo watalaam wa Serikali katika uendeshaji na usimamizi wa mradi.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni, kama nilivyoeleza awali, tumeamua kuanzisha sheria maalum ya mradi, na sheria hiyo italetwa hapa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa na Wabunge, ambapo Waheshimiwa Wabunge wataona yaliyomo kwenye mkataba na kuyajadili na kuyapitisha kwa manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaanza kazi ya kuwaelimisha wajasiriamali wa nchi yetu kuhusu fursa zilizopo katika mradi huu na namna ya kuzifikia. Jitihada mahsusi zinatafanywa ili wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara waelewe nafasi na wajibu wao katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, ili kuwaandaa wataalam wa Kitanzania katika kufanya kazi katika

mradi huu, Serikali katika mwaka ujao wa fedha itajenga Chuo kikubwa cha Ufundi cha Kimataifa cha umeme, mafuta na gesi Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Spika, ili kupanua fursa na kushamirisha maendeleo ya ajira na viwanda, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaanzisha Eneo Maalum la Kiuchumi *(Special Economic Zone)* katika eneo la mradi wa *LNG* ili kuvutia viwanda na shughuli nyingine za kiuchumi ambazo zitanufaika na kuwepo kwa miundombinu itakayotokana na utekelezaji wa mradi huu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali itaendelea kushiriki katika mradi wa *EACOP* na kuhakikisha kwamba manufaa yake yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha pia, Serikali kupitia *TPDC* imepanga kujenga bomba lingine la gesi kutoka kwenye kitalu cha Ntorya hadi Madimba ili kuongeza uwezo wa uzalishaji wa gesi hapa nchini ambayo itatumika na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi mafuta ya kimkakati ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta na kutumia vizuri eneo letu la kijiografia la kuhudumia nchi jirani kwa ajili ya manufaa ya uchumi na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TPDC* itaendelea kushiriki kwenye shughuli na biashara ya mafuta kupitia kampuni yake tanzu ya *TANOIL.* Kampuni hii ya *TANOIL* tutawaalika wawekezaji au wabia kutoka sekta binafsi watakaoingia kwenye ushirika na *TANOIL* ili kampuni hii iweze kufanya biashara kwa kisasa, kwa ukubwa na kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru washirika wa maendeleo, Jumuiya ya Nchi Wahisani ambao wameendelea kuchangia katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Ni wengi na tumewataja katika hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kutoa shukrani kwa Serikali mbalimbali kwenye ukanda wetu huu na kwingineko ambazo tunashirikiana nazo katika eneo hili la nishati. Tumewataja katika hotuba tuliyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali kupitia Wizara ya Nishati, itaendelea kuimarisha utendaji na usimamizi wa sekta hii kwa lengo la kuhakikisha kwamba sekta hii inaendelea kuchangia ipasavyo ukuaji wa uchumi na ustawi wa Watanzania na maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nilisema hapo awali sekta hii ndiyo mhimili wa uchumi wa nchi yetu. Ukiongea mafuta, gesi na umeme, mambo yote hayo yakiharibika nchi inasimama. Sisi kama watu wa nishati tumedhamiria kutimiza wajibu wetu ipasavyo ili tuitendee haki nchi yetu kwa usimamizi bora na makini wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba umeme wa uhakika unapatikana na unachangia katika maendeleo ya viwanda na biashara. Vilevile Wizara itaendelea kuimarisha uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia ili mchango wa shughuli hizo katika maendeleo ya Taifa letu uendelee kuimarika.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine tutakazochukua ni kuimarisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia mijini na vijijini ili kulinda afya za wananchi na mazingira kutokana na nishati chafu na isiyo rafiki kwa mazingira. Vilevile, kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya nishati kwenye maendeleo ya nchi yetu, kama nilivyoeleza awali, tutahakikisha kwamba tunaweka mkazo katika upatikanaji wa nishati hii katika maeneo ya vijijini. Hili ni muhimu ili kuwaunganisha na kuwashirikisha wananchi wa vijijini katika uchumi wa kisasa na unaokua ili wasibaki nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize tena kwa shukrani kwako binafsi kwa jinsi unavyotuongoza, kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu, tumeshuhudia uimara wa Bunge letu, heshima ya

Bunge letu kutokana na uongozi wako, kwa hiyo tunakupongeza sana. Nirudie kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyofanya awali. Kama mnavyofahamu, Wizara yetu ina changamoto nyingi, ina maneno mengi, lakini kwa kweli mmetupa ushirikiano mkubwa sana, mmetupa hamasa kubwa sana, mmetushauri vizuri, mmetutia moyo na mmekuwa na subira na sisi hadi mambo yameanza kuwa mazuri. Kwa hiyo, tunawashukuru sana na tunawaomba muendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Wakili Stephen Byabato, kwa kweli ananisaidia sana katika kuiongoza Wizara na kuiongoza sekta. Wote mnajua na mnamuona hapa mbele umahiri wake na uwezo wake wa kutoa maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Katibu Mkuu, *Eng.* Mramba, pamoja na timu yake yote ya Watendaji katika Wizara. Tunapata ushauri mzuri wa kitaalam kuhusu mambo tunayoshughulika nayo na tuna hakika kabisa hatutaingia kwenye changamoto zozote za kiutendaji kutokana na ushauri mahiri tunaoupata kutoka kwa Katibu Mkuu na Wataalam.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Wenyeviti wa Bodi zetu zote na Wakuu wa Taasisi zetu za Wizara ya Nishati kuanzia Ndugu Maharage Chande wa *TANESCO,* Ndugu Mussa Makame wa *TPDC,* Ndugu Hassan Saidy wa *REA,* Ndugu Dkt. James Andilile *EWURA* na kampuni zetu tanzu, pamoja na Wenyeviti wa Bodi. Kwa kweli, utamaduni mpya wa kazi tulio nao kama Wizara umetusaidia kufanya kazi kwa ushirikiano na kupata mafanikio haya tunayoyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, watumishi wote wa Wizara na Taasisi za Wizara yetu katika nchi nzima ambao baadhi mmewaona kwenye mabanda pale nje, lile ndilo jeshi letu, sisi tuko mbele tu huku, lakini kwa kweli kazi kubwa sana inafanywa na wenzetu wa *REA, EWURA* na kadhalika. Moyo wao, weledi wao, uzalendo wao, uchapakazi wao baadhi mmeushuhudia katika Majimbo yetu, pia hata mlipotembelea mabanda mmeona mapokeo yao. Kwa hiyo, napenda niwashukuru sana na niwapongeze kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 3,048,632,519,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, shilingi 2,960,702,821,000 sawa na asilimia 97.1 ya bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,609,156,128,000 ni fedha za ndani na shilingi 351,546,693,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa vilevile, shilingi 87,929,698,000 sawa na asilimia 2.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 71,637,112,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 16,292,586,000 ni kwa ajili ya matumizi ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti, vishkwambi za Wabunge, lakini katika nyaraka tulizowagawia kuna ile *QR Code* ukipiga picha na simu unapata *link* unabonyeza, pia utaipata hotuba na utaupata huo muhtasari.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2023/2024 - KAMA ILIVYOWSILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa iliyowasil ishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2022/23 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2023/24.

**2.** MheshimiwaSpika, awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2023/24. Namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuende lea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine mbalimbali.

**3.** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini kusimamia Wizara hii. Aidha, maelekezo yake thabiti anayonipa, yananiwezesha kusimamia vyema Sekta ya Nishati ambayo ni muhimili muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Ni dhahiri kuwa Rais wetu amekuwa chachu na mwenye maono makubwa katika kutekeleza mipango mikubwa na yenye tija katika Sekta ya Nishati hapa nchini.

**4.** **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii pia kuwashukuru Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo mbalimbali wanayonipatia katika kusimamia Sekta ya Nishati. Nikiri kuwa maelekezo na miongozo ya viongozi wetu hawa ni msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Nishati. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kusimamia kwa umahiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**5.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa. Aidha, nitumie fursa hii kum pongeza Bi. Nenelwa Mwihambi, Katibu wa Bunge kwa usimamizi wa shughuli za Bunge. Ni dhahiri kuwa, chini ya uongozi wenu Bunge letu limeendelea kute keleza majukumu yake ya kikatiba ipasavyo katika kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza wajibu wa kuwaletea

wananchi maendeleo. Nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaonipa, unaoniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa.

**6. Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni Bunge lako Tukufu lilifanya uchaguzi wa wenyeviti wa Bunge. Nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb.), kwa kuendelea kuaminiwa na kuchaguliwa kwa kishindo kuongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Judith Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano na ushauri wao wanaotupatia katika kuboresha usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Nishati.

**7. Mheshimiwa Spika,** namshukuru Mheshimiwa Wakili Stephen Lujwahuka Byabato (Mb.), Naibu Waziri wa Nishati kwa kuendelea kunisaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Mha. Felchesmi Jossen Mramba kwa uchapakazi wake mahiri na ushirikiano anaonipa katika kutekeleza shughuli zangu za kila siku za Wizara. Nampongeza pia, Bw. Athuman Selemani Mbuttuka kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati. Nawashukuru pia Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumi shi wote kwa ujumla kwa ushirikiano na juhudi zao katika kufanikisha malengo ya Wizara.

**8. Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia pia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2022/23 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2023/24.

**9. Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, naomba sasa nizungumzie mwelekeo wa dunia katika masuala ya nishati, nishati na maendeleo ya Sekta nyingine, Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2022/23 pamoja na Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/24.

## B. MWELEKEO WA DUNIA KATIKA MASUALA YA NISHATI

**10. Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali ya mabadiliko ya tabia nchi inayoendelea duniani, mwelekeo wa sasa wa dunia ni kuhamia kwenye nishati safi (clean energy transition) kwa kutumia vyanzo vyenye kaboni kidogo au visivyokuwa na kaboni kabisa, na masoko ya mitaji yanajielekeza katika kugharamia miradi inayozalisha nishati safi. Mwelekeo huo utapelekea mabadiliko katika mfumo wa ugavi wa nishati pamoja na mitambo ya kutumia au kuzalisha nishati. Aidha, nchi mbalimbali kwa sasa zinaweka mkazo na uwekezaji mkubwa katika matumizi ya haidrojeni kwenye mitambo na nishati jadidifu katika kuzalisha umeme. Vilevile, nchi mbalimbali zilizo endelea zimejiwekea malengo ya kuondokana na magari yanayotumia mafuta ya dizeli na petroli ifikapo kati ya mwaka 2030 na 2050 pamoja na mipango mikakati mingine ya kuachana na matumizi ya vyanzo vya nishati visivyo rafiki wa mazingira.

**11. Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, kwa kuwa utekelezaji wa mpango huo utakuwa na athari hasi kwenye nchi zinazoendelea, ikiwemo kuzorotesha mipango ya kuwafikishia wananchi nishati bora na ya kutosha, na kwa kuzingatia kuwa Bara la Afrika limechangia chini ya asilimia tatu (3%) katika uchafuzi wa mazin gira duniani, Bara la Afrika na nchi nyingine zinazoendelea zimeona ni muhimu mwelekeo wa nishati safi kuwa wa haki (just transition) ambao utazingatia historia ya uchafuzi na ambao hautazuia maendeleo ya nchi zinazoendelea. Hivyo, nchi zinazoendelea zimeomba kupewa nafasi ili ziweze kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati vilivyopo, ikiwemo mafuta na gesi katika kuendeleza miradi yake ya nishati, hususan uzalishaji wa umeme.

**12. Mheshimiwa Spika,** kutokana na mwelekeo huo wa kidunia, na Tanzania ikiwa sehemu ya dunia, hatuna budi sasa kutekeleza mikakati ya kuimarisha matumizi ya vyanzo vya nishati vyenye athari ndogo kwa mazingira kama vile vyanzo vya maji, nishati jadidifu na gesi asilia ambayo imebainishwa kuwa chanzo cha nishati ya mpito (transitional energy) inayoweza kutumika hadi mwaka 2050. Pamoja na kutekeleza wajibu wetu kama nchi kwa kuongeza jitihada za matumizi ya nishati jadidifu, hatutasita kutumia rasilimali zote za uzalishaji wa nishati na kukidhi mahi taji

ya uchumi wa nchi yetu. Aidha, pamoja na kuendelea pia kutumia vyanzo vingine kuzalisha nishati ili kuendana na mahitaji, Serikali itaendelea kuhamasi sha matumizi ya CNG na umeme katika uendeshaji magari na pia kushirikiana na wadau mbalimbali wanaoonyesha nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa haidrojeni . Vilevile, mwelekeo wa Wizara ni kuendelea kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili ifikapo mwaka 2033, angalau asilimia 80 ya wanachi wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

**13. Mheshimiwa Spika,** pia, katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha, mazingira ya biashara ya nishati ya mafuta duniani yamebadilika kwa kiasi kikubwa kutokana na mafuta ya kutoka Urusi, nchi ya tatu duniani kwa uzalishaji mafuta duniani, kuondoka kwenye soko kutokana na vikwazo vilivyowekwa kwa bidhaa hiyo kutoka Urusi. Kuondoka kwa kiwango hicho kikubwa cha mafuta kwenye soko la dunia kumepelekea upungufu wa mafuta duniani na hivyo kuongeza bei ya bidhaa hiyo duniani.

**14. Mheshimiwa Spika,** vilevile, meli nyingi za kusafirisha mafuta kwenye soko la dunia kutoka Urusi zimezuiwa kufanya biashara hiyo na bei za bima ya kusafirisha mafuta zimepanda sana. Hali hii imepelekea kupanda kwa gharama za kusafirisha mafuta (premiums), jambo lililopelekea pia bei kuongezeka. Aidha, nchi nyingi za Afrika na kwingineko duniani zimekabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa Dola za Kimarekani kwa ajili ya kulipia uagizaji na ulipiaji wa mafuta hayo. Changamoto hizi pia zimeikabili nchi yetu na kutoa viashiria vya tishio la usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na kupanda kwa bei.

**15. Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Serikali ilijidhatiti na kuchukua hatua za muda mfupi na wa kati wa kukabiliana nazo. Kwa sasa Serikali inapanga mikakati ya muda mrefu ili kujilinda na athari hizi za kuhakikisha kwamba nchi yetu wakati wote ina mafuta ya kutosha na kwa bei inayohimilika. Ndiyo maana mwaka jana wakati tuna soma bajeti ya Wizara, bei ya petroli kwa lita ilikuwa Shilingi 3,301 bila ruzuku na bei ya dizeli ilikuwa Shilingi 3,452 kwa lita bila ruzuku lakini leo bei ya mafuta hayo ni Shilingi 2,871 kwa lita.

## C. NISHATI NA MAENDELEO YA SEKTA NYINGINE

**16. Mheshimiwa Spika,** maendeleo ya nchi yoyote yanahitaji uhakika wa upatikanaji wa nishati. Aidha, upatikanaji wa nishati ya uhakika na gharama nafuu ni kichocheo cha kuvutia uwekezaji na kufanya bidhaa na huduma zinazozalishwa kuwa shindani katika masoko ya ndani na kimataifa. Mwelekeo wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 ni nchi yetu kuwa Taifa la viwanda, lenye uchumi wa kati na lenye bidhaa na huduma zinazoweza kushindana katika masoko ya kikanda na kimataifa. Kwa kuwa viwanda vinahitaji nishati ya uhakika na gharama nafuu, kufikiwa kwa azma hii kunahitaji uwekezaji madhubuti katika mnyororo mzima wa uzalishaji, usa  firishaji na usambazaji wa nishati katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, viwanda vya bidhaa za ujenzi zikiwemo gypsum, marumaru, nondo, nyaya za mawasiliano (fiber optic cables), vioo, mbolea na dawa za binadamu (pharmaceuticals) vinatumia nishati ya gesi asilia katika uzalishaji wa bidhaa hizo, hivyo ustawi wake unahitaji upatikanaji wa nishati hiyo.

**17. Mheshimiwa Spika,**moja ya maeneo ambayo yamewekewa mkazo katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) ni uongezaji thamani katika bidhaa za kilimo, uvuvi, ufugaji, madini na maliasili. Upatikanaji wa nishati ya uhakika na gharama nafuu ni kichocheo kikubwa katika kufikiwa kwa azma hii kwani uhifadhi na uchakataji wa mazao ya kilimo, uvuvi, ufugaji na maliasili unahitaji kuwepo kwa nishati ya uhakika. Aidha, kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya umeme migodini kutachangia katika kupunguza gharama za utekelezaji wa shughuli hizo na hivyo kuimarisha tija na ufanisi na upatikanaji wa mapato ya Serikali. Vilevile, utekelezaji wa azma ya Serikali ya kutoa huduma bora za kijamii ikiwa ni pamoja na afya, elimu, maji safi na mawasiliano katika maeneo yote nchini, unahitaji uhakika wa nishati.

**18. Mheshimiwa Spika,** tukizungumzia suala la uzalishaji wa ajira nchini, hatuwezi kulitenganisha na upatikanaji wa nishati ya uhakika na gharama nafuu. Ukuaji wa shughuli za kiuchumi ikiwemo viwanda, kilimo, ufugaji, uvuvi, huduma na mawasiliano pamoja na shughuli za kujiajiri kupitia ufundi wa aina mbalimbali

na biashara ndogondogo ambao matokeo yake ni kukuwa kwa ajira, unahitaji kuwepo kwa nishati ya uhakika na gharama nafuu. Aidha, kuimarika kwa shughuli za kiu  chumi vijijini, ikiwa ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia pampu za maji za umeme, biashara, uzalishaji wa vyakula vya mifugo, kuhifadhi mazao wakati wa kutafuta masoko hususan yasiyoweza kukaa kwa muda mrefu (perishables), kukausha na kuchakata mazao ya kilimo, ufugaji wa samaki unaohitaji matumizi ya pampu za maji na uzalishaji wa bidhaa za ujenzi mathalan tofali na bidhaa za chuma, kunaimarisha ajira katika maeneo hayo na kupunguza kasi ya uhamiaji mijini hususan kwa vijana ili kutafuta ajira.

**19. Mheshimiwa Spika,** athari za uharibifu wa mazingira duniani na nchini zimeendelea kujitokeza, ikiwemo mabadiliko ya tabianchi. Uharibifu wa mazingira pamoja na mambo mengine, unatokana na matumizi ya vyanzo vya nishati visivyo rafiki wa mazingira, ikiwa ni pamoja na kuni na mkaa hivyo kusababisha uharibifu wa misitu na uoto wa asili. Kutokana na mwelekeo wa dunia kwa sasa wa kuelekea katika matumizi ya nishati isiyochafua mazingira, na kwa kuzingatia athari za mabadiliko ya tabianchi, ni muhimu kuwekeza katika kuwezesha upatikanaji wa nishati safi, ikiwemo vijijini ili kulilinda Taifa letu dhidi ya athari za uharibifu wa mazingira na pia kuendana na mwelekeo wa dunia kuhusu matumizi ya nishati safi.

**20. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa usafirishaji, nchi yetu inachukua hatua madhubuti za kuimarisha sekta hii, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa reli ya umeme ya SGR, kuimarisha huduma ya mabasi ya mwendokasi pamoja na kuhamasisha wananchi kutumia Gesi Asilia Iliyoshindiliwa (Compressed Natural Gas - CNG) kama chanzo cha nishati katika magari. Ni muhimu kutambua kuwa, ni kupitia upatikanaji wa nishati ya uhakika na gharama nafuu, azma ya kufikiwa kwa ari hii itafikiwa.

**21. Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa nishati ya uhakika na gharama nafuu ni chachu ya kuimarisha ustawi wa wanawake hususan vijijini, ikiwemo kuwawezesha kupata elimu kupitia vyombo vya habari kuhusu masuala mbalimbali yanayowahusu kama vile elimu ya masuala ya afya ya uzazi, lishe na malezi bora, haki za wanawake, shughuli za kiuchumi, athari za ndoa za

utotoni na unyanyasaji wa kijinsia. Aidha, upatikanaji wa nishati hiyo unawezesha uboreshaji wa huduma za afya vijijini, ikiwemo za uzazi na pia kuwapunguzia adha wakina mama ya kutembea umbali mrefu na kutumia muda mwingi kutafuta nishati ya kuni ambayo pia matumizi yake yana athari za kiafya hususan katika mfumo wa kupumua.

**22. Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya umeme yameongezeka kwa kasi katika mwaka huu unaoisha, ambapo rekodi ya kiwango cha juu cha mahitaji ya umeme (peak demand) imevunja mara nane, jambo ambalo siyo la kawaida katika historia ya mahitaji ya umeme nchini. Aidha, hali ya uzalishaji wa nishati ya umeme nchini kwa sasa haiendani na mahitaji ya shughuli za kiuchumi na kijamii yanayoongezeka kwa kasi na kuna upungufu mkubwa wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Vilevile, baadhi ya miundombinu ni chakavu na mingine imezidiwa na matumizi ikilinganishwa na ilivyokusudiwa. Pia, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupeleka umeme vijijini, bado kuna takribani vitongoji 36,101 kati ya vitongoji 64,760 ambavyo havijafikiwa na umeme. Pia, mahitaji ya gesi asilia nchini kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi katika Taasisi, majumbani na kwenye vyombo vya moto yameendelea kuongezeka pasipo kwenda sambamba na kasi ya uzalishaji wa nishati hiyo. Katika Bajeti hii, Serikali imeweka mipango na mikakati ya kukabiliana na suala hili.

**23. Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua kuwa Sekta ya Nishati ndiyo mhimili muhimu wa maendeleo ya nchi yetu, muelekeo wa Wizara ni kuongeza katika Gridi ya Taifa MW 218.67 na kufikia MW 1,913.22 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2022/23, MW 825 na kufikia MW 2,738.22 mwaka 2023/24, MW 2,475 ili kuwa na MW 5,213.22 mwaka 2024/25 na MW 597 ili kuwa na MW 5,810.22 mwaka 2025/26 ili kukidhi mahitaji ya umeme nchini na pia kufanya biashara ya nishati hiyo na nchi jirani. Aidha, utekelezaji wa maono hayo umezingatia umuhimu wa nchi kuwa na umeme wa uhakika na gharama nafuu, kupitia utekelezaji wa miradi ya uzalishaji umeme unaotokana na vyanzo mbalimbali (energy mix) ambayo utekelezaji wake utazin gatia pia ushiriki wa sekta binafsi.

**24. Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa umeme ukishazalishwa lazima usafirishwe na kusambazwa kwa watumiaji, muelekeo wa Wizara ni kuongeza idadi ya njia za kusafirisha umeme na kufikia Km 6,555.28 mwishoni mwa mwaka 2022/23, Km 7,966.28 mwaka 2023/24, Km 9,852.95 mwaka 2024/25 na Km 10,670.95 mwaka 2025/26 kutoka Km 6,110.28 za mwaka 2021/22. Kwa upande wa njia za usambazaji umeme, muelekeo ni kufikia Km 170,024.53 mwishoni mwa mwaka 2022/23, Km 187,026.98 mwaka 2023/24, Km 205,729.68 mwaka 2024/25 na Km 226,302.64 mwaka 2025/26 kutoka Km 154,567.75 za mwaka 2021/22. Maten genezo na utunzaji endelevu wa miundombinu ya umeme, pamoja na kukabiliana na upotevu wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini pia ni maeneo ya mkazo ili kuhakikisha kunakuwepo na tija na ufanisi katika umeme unaozalishwa, kusafir ishwa, kusambazwa na kutumika.

**25. Mheshimiwa Spika,** azma ya Wizara ni kuhakikisha wananchi wote nchini wana fikiwa na huduma ya umeme, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Vitongoji vyote vinapata umeme ndani ya muda mfupi, badala ya wananchi wa maeneo hayo, wenye kiu kubwa ya nishati hiyo kusubiri kwa takribani miaka 20 kwa utaratibu wa sasa wa upelekaji umeme katika Vitongojini na hivyo kuwacheleweshea maendeleo na kuendelea kuwanyima fursa na manufaa yatokanayo na nishati hiyo. Azma hiyo inakwenda sambamba na kuhakikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia yanaimarika nchini kwa lengo la kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira pamoja na kuiepusha jamii na athari za kiafya zitokanazo na matumizi ya nishati isiyo safi. Aidha, azma hii ni utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) ya mwaka 2030, hususan lengo Namba 7 linalozitaka nchi kuhakikisha uwepo wa nishati ya uhakika, safi, nafuu na endelevu kwa wananchi.

**D. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA KWA MWAKA 2022/23**

**26. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/23, Maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa ni kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme, ikiwemo kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa katika Mikoa ya Katavi, Kigoma na Kagera na mradi mkubwa wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization

Project); kutekeleza Miradi ya Nishati Vijijini pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika Vitongoji vyote nchini; kukamilisha mazungumzo ya mradi wa LNG na kuanza maandalizi ya utekelezaji wake; kutekeleza miradi ya nishati jadidifu ikiwemo jotoardhi, tun gamotaka, upepo na jua pamoja na matumizi bora ya Nishati (Energy Efficiency and Conservation); kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini; na kui marisha TPDC na Kampuni zake Tanzu za TANOIL na GASCO.

**27. Mheshimiwa Spika,** vipaumbele vingine vilikuwa ni kuboresha miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na Kituo cha Pamoja cha kupokelea Mafuta kutoka Melini (Single Receiving Terminal); kuimarisha utendaji na huduma zinazotolewa na taasisi za Wizara, hususan TANESCO, EWURA na PBPA; kuongeza ushiriki na uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Sekta ya Nishati na kuhakikisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia unaimarika pamoja na kufufua shughuli za utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Wizara pia iliweka kipaumbele katika kuim arisha matumizi ya nishati ya gesi ya kupikia (LPG) na gesi asilia kwenye magari na viwandani; na kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Nishati Safi ya Kupikia (Clean Cooking Energy).

**Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2022/23**

**28. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2022/23, Wizara ya Nishati iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi trilioni 2.91 ambapo Shilingi bilioni 82.95 sawa na asilimia 1.14 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi trilioni 2.82 sawa na asilimia 98.86 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, katika Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa Shilingi bilioni 14.73 ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake na Shilingi bilioni 68.23 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**29. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi trilioni 1.78 sawa na asilimia 61.17 ya bajeti iliyoidhin ishwa. Kati ya fedha

zilizopokelewa, Shilingi bilioni 15 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi trilioni 1.76 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU**
**D. 1: UZALISHAJI, USAFIRISHAJ NA USAMBAZAJI UMEE NCHINI**
**D.1.1: UZALISHAJI WA UMEME**


**30. Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali ya ukame (poor hydrology) uliopelekea mtiririko mdogo wa maji (low inflow) katika mabwawa ya vituo vya kufua umeme kwa kutumia maji, kulikuwepo na upungufu wa umeme kwa wastani wa MW 239 kwa siku katika kipindi cha mwezi Novemba, 2022. Hata hivyo, hali hiyo iliendelea kuimarika kutokana na mvua zilizoendelea kunyesha kwa vipindi tofauti kuanzia mwezi Desemba, 2022 na kufanya wastani wa upungufu wa umeme kuwa MW 157, MW 60, MW 46 na MW 92 kwa miezi ya Desemba, 2022, Januari, Februari na Machi, 2023 mtawalia. Hali hii iliweza kuimarika kuanzia mwezi Aprili, 2023 na hadi mwanzoni mwa mwezi Mei, 2023 kutokana na mvua zilizonyesha na kuongeza uzalishaji umeme katika vituo vya Kihansi na Kidatu.

**31. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Mei, 2023 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa umeongezeka kwa asili mia 10.5 na kufikia MW 1,872.05 ikilinganishwa na MW 1,694.55 zilizokuwepo mwaka 2021/22. Kati ya kiasi hicho, MW 574.60 sawa na asilimia 30.69 zina tokana na nguvu ya maji, MW 1,198.82 sawa na asilimia 64.04 gesi asilia, MW 88.13 sawa na asilimia 4.71 mafuta na MW 10.50 sawa na asilimia 0.56 tungamotaka (biomass).

**32. Mheshimiwa Spika,** ongezeko hili limetokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kukamilika kwa mradi wa Kinyerezi I Extension wenye uwezo wa kuzalisha MW 185.

**Kielelezo Na. 1: Mchanganuo wa Vyanzo na Uwezzo wa Mitambo ya Kufua Umeme katika Gridi ya Taifa**

| CHANZO | UWEZO | |
|---|---|---|
| | MW | ASILIMIA |
| Maji | 574.6 | 30.69 |
| Gesi Asilia | 1,198.82 | 64.04 |
| Mafuta | 88.13 | 4.71 |
| Tungamotaka | 10.5 | 0.56 |
| **JUMLA** | **1,872.05** | **100.00** |




*Chanzo: TANESCO*

**33.** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mitambo ya kufua umeme ambayo hai jaungwa katika Gridi ya Taifa, uwezo wa mitambo hiyo ni MW 39.302 ambazo zinajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO yenye uwezo wa kufua MW 34.302 na MW 5 zitokanazo na nguvu ya jua kutoka kwa mzalishaji binafsi hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini kufikia MW 1,911.35. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 10.3 ikilinganishwa na MW 1,733.38 zilizoku wepo mwaka 2021/22. Mchanganuo wa uwezo wa mitambo kufua umeme ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 1.

**34.** Mheshimiwa Spika, mahitaji ya umeme nchini yameendelea kukua ambapo katika kipindi cha mwaka 2022/23 wastani wa mahitaji ya umeme ni MW 1,363.94 sawa na ongezeko la asilimia 6.9 ukilinganisha na wastani wa MW 1,276.43 kwa mwaka 2021/22. Aidha, katika kipindi hicho, mahitaji ya juu ya umeme yame ongezeka na kufikia MW 1,431.59 (tarehe 15 Mei, 2023 saa 2:00 usiku) sawa na ongezeko la asilimia 6.8 ikilinganishwa na MW 1,340.68 zilizofikiwa mwaka 2021/22 (tarehe 26 Mei, 2022 saa 2:00 usiku). Kuongezeka kwa mahitaji haya kumetokana na kuongezeka kwa wateja wakubwa hasa viwanda na biashara ambao wameongezeka kwa asilimia 5.6 na kukua kwa shughuli za


kiuchumi na kijamii. Kielelezo Na. 2(a) kinaonesha wastani wa ukuaji wa mahitaji ya juu ya umeme kwa mwaka 2021/22 na mwaka 2022/23. Vilevile, Kielelezo Na. 2(b) kinaonesha ukuaji wa mahitaji ya umeme katika Gridi ya Taifa kuanzia mwaka 2010 hadi mwezi Mei, 2023 ambapo mahitaji hayo yamekuwa kwa asilimia 72.0 katika kipindi hicho.

**Kielelezo Na. 2(a): Wastani wa Ukuaji wa Mahitaji ya Umeme kwa Mwaka 2021/22 na Mwaka 2022/23**

| | MWEZI | JULAI | AGOSTI | SEPTEMB | OKTOBA | NOVEMB | DESEMB | JANUARI | FEBRUARI | MACHI | APRILI | MEI | WASTAN |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MWAKA | 2021/22 | 1,182.94 | 1,193.94 | 1,240.53 | 1,262.52 | 1,307.36 | 1,263.50 | 1,300.31 | 1,289.33 | 1,335.01 | 1,324.64 | 1,340.68 | 1,276.43 |
| | 2022/23 | 1,302.20 | 1,320.98 | 1,341.25 | 1,336.05 | 1,315.63 | 1,354.61 | 1,391.65 | 1,402.73 | 1,401.86 | 1,404.83 | 1,431.59 | 1,363.94 |
| **ONGEZEKO (%)** | | **10.1** | **10.6** | **8.1** | **5.8** | **0.6** | **7.2** | **7.0** | **8.8** | **5.0** | **6.1** | **6.8** | **6.9** |

*Chanzo: TANESCO*

**Kielelezo Na.2 (b): Mwenendo wa Ukuaji wa Mahitaji ya Umeme katika Gridi ya Taifa Kuanzia Mwaka 2010 hadi Mwezi Mei, 2023**




*Chanzo: TANESCO*

## D. 1.2: HALI YA USAFIRISHAJI UMEME

**35.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TANESCO imeendelea kutekeleza mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ambapo kwa sasa kazi inayoendelea ni kubadilisha nyaya (reconductoring) katika njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 Ubungo – Chalinze inayotarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2023 pamoja na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme. Uboreshaji wa miundombinu hiyo uta saidia kutatua changamoto za kuzidiwa kwa baadhi ya miundombinu ya kusafirisha umeme kutokana na ongezeko la wateja hususani katika njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 kutoka Ubungo hadi Chalinze na Chalinze – Hale – Tanga; kV 220 Kidatu – Iringa; na kV 220 Kihansi – Iringa. Vilevile, katika kuimarisha miun dombinu ya kusafirisha umeme kwa ujumla, Serikali kupitia TANESCO inatekeleza jumla ya miradi 48 ikijumuisha miradi 20 ya kuongeza uwezo wa miundombinu ya usafirishaji umeme, miradi 12 ya kuboresha mifumo ya uendeshaji wa Gridi ya Taifa na miradi 16 ya ukarabati miundombinu ya usafirishaji umeme.

**36.** MheshimiwaSpika, miundombinu hiyo ya kusafirisha umeme nchini imeendelea kuongezeka na kufikia jumla ya urefu wa kilomita 6,363.27 za miundombinu ya kusafirisha umeme sawa na ongezeko la asilimia 4.1 ilikinganishwa na kilomita 6,111.27 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Mei, 2022. Kati ya hizo, kilomita 670 ni za msongo wa kV 400; kilomita 3,384.7 ni msongo wa kV 220; kilomita 1,672.57 ni msongo wa kV 132; na kilomita 543 ni msongo wa kV 66. Kuongezeka kwa urefu wa njia za kusafirisha umeme, kumetokana na kukamilika kwa miradi ya njia ya kusafirisha umeme za msongo wa kV 220 zenye urefu wa kilomita 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi, kilomita 94 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi na kilomita 14 kutoka Kingolwira hadi Msamvu. Kielelezo Na.3 ni mchanganuo wa urefu wa njia za kusafirisha umeme hadi kufikia mwezi Mei, 2023.

**Kielelezo Na.3: Mchanganuo wa Urefu wa Njia za Kusafirisha Umeme hadi Kufikia Mwezi Mei, 2023**

| Na. | Njia za Usafirishaji wa Umeme | Urefu (Km) | |
|---|---|---|---|
| | | Mei, 2022 | Mei, 2023 |
| 1. | Njia za msongo wa kV 400 | 670 | 670 |
| 2. | Njia za msongo wa kV 220 | 3,225.70 | 3,477.70 |
| 3. | Njia za msongo wa kV 132 | 1,672.57 | 1,672.57 |
| 4. | Njia za msongo wa kV 66 | 543 | 543 |
| **Jumla** | | **6,111.27** | **6,363.27** |

*Chanzo: TANESCO*

**D.1.3: HALI YA USAMBAZAJI UMEME**

**37. Mheshimiwa Spika,** baadhi ya njia za kusambaza umeme zina urefu wa zaidi ya kilomita 400 na hivyo kusababisha umeme kukatika mara kwa mara au kuwa na nguvu ndogo (low voltage) kwa eneo kubwa inapotokea hitilafu katika njia husika. Hata hivyo, Serikali tayari imeandaa mpango wa kujenga vituo vya kupoza umeme katika kila Wilaya ambapo hadi sasa utambuzi wa maeneo kutakapojengwa vituo hivyo unaendelea. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme (Gridi Imara) unaondelea kutekelezwa unalenga kupunguza changamoto hizo kwa kiasi kikubwa.

**38.** Mheshimiwa Spika, miundombinu hiyo ya kusambaza umeme imefikia kilo mita 168,548.36 sawa na ongezeko la asilimia 9.5 ikilinganishwa na kilomita 153,988.49 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Mei, 2022. Kupitia miundombinu hiyo, Shirika limeweza kuongeza kasi ya kuunganisha wateja nchini na kuwezesha kufikia jumla ya wateja 4,319,258 hadi mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 12.4 ikilinganishwa na wateja 3,842,096 waliokuwepo mwezi Juni, 2022. Ongezeko hili limetokana na kuanzishwa kwa mfumo mpya wa maombi ya umeme wa Nikonekt pamoja na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme

vijijini inayote kelezwa na REA. Kielelezo Na. 4 ni mchanganuo wa urefu wa njia za kusambaza umeme hadi kufikia mwezi Mei, 2023.

**Kielelezo Na. 4: Mchanganuo wa Urefu wa Njia zaKusambazaha Umeme hadiKufikia Mwezi Mei, 2023**


| Na. | Njia za Usambazaji wa Umeme | Urefu (km) | | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| | | Mei, 2022 | Mei, 2023 | |
| 1. | Njia za msongo wa kV 33 | 48,965.73 | 55,045.55 | 12.4 |
| 2. | Njia za msongo wa kV 11 | 12,648.73 | 12,986.25 | 2.7 |
| 3. | Njia za msongo wa kV 0.4 | 92,374.03 | 100,516.56 | 8.8 |
| **Jumla** | | **153,988.49** | **168,548.49** | **9.5** |


*Chanzo: TANESCO*

**D.1.4: HUDUMA KWA WATEJA**

**39.** MheshimiwaSpika, Serikali kupitia TANESCO imeendelea kusimamia utoaji wa huduma kwa wateja nchini ikizingatiwa kuwa wateja ni kipaumbele muhimu katika Mpango Mkakati wa Mpito wa Shirika. Katika kuhakikisha huduma kwa wateja zin aboreshwa sambamba na uunganishaji wa umeme, Shirika limeboresha masuala mbalimbali, ikiwemo kituo cha miito ya simu (unified call centre) ambacho kinafa nya kazi saa 24; kuendelea kutumia mfumo wa maombi ya umeme wa Nikonekt ambao unawezesha wateja kuomba kuunganishiwa umeme hadi kufungiwa pasipo kufika ofisi za TANESCO; na kuanzishwa kwa mfumo wa Huduma ya Nihudumie ambao unatumika kuboresha huduma kwa wateja na kuwezesha utoaji wa taarifa kwa mteja kuhusu kushughulikiwa kwa suala alilowasilisha TANESCO hadpoka milika. Kielelezo Na.5 kinaonesha maboresho yaliyofanyika katika huduma kwa wateja.

## Kielelezo Na.5: Maboresho Yaliyofanyika katika Huduma kwa Wateja










*Chanzo: TANESCO*


## D.2: MIRADI YA KUZALISHA UMEME

### D.2.1: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI

**i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115**

**40. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 2,115 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji. Gharama ya mradi huu ni Shilingi trilioni 6.55 ambazo zinagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi huu katika maeneo yote kwa ujumla ulifikia asilimia 86.89 kutoka asilimia 60.22 zilizokuwa zimefikiwa mwezi Aprili, 2022 na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kielelezo Na.6 kinaonesha mwenendo wa utekelezaji wa mradi wa JNHPP kuanzia mwezi Aprili, 2022 hadi mwezi Aprili, 2023.

**Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa Utekelezaji wa Mradi wa JNHPP Kuanzia Mwezi Aprili, 2022 hadi mwezi Aprili, 2023**




*Chanzo: TANESCO*

**41.** Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Desemba, 2022 Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi zoezi la ujazaji maji katika Bwawa la Julius Nyerere kwa kufunga mageti ya njia ya kuchepusha maji. Tukio hilo la kihistoria lilihudhuriwa pia na Marais Wastaafu, Mheshimiwa Spika, Viongozi mbalimbali wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge, viongozi kutoka nchini Misri na wananchi. Hadi kufikia tarehe 23 Mei, 2023 kina cha maji ya Bwawa kili kuwa kimefikia mita 160.51 kutoka usawa wa bahari na ili kuweza kuzalisha umeme, kiwango cha chini cha maji kinatakiwa kufikia mita 163 kutoka usawa wa bahari. Ujazaji wa maji unaendelea kulingana na Mpango Kazi wa Ujazaji wa Bwawa ambapo hadi kufikia tarehe 23 Mei, 2023 kiwango cha maji kimefikia mita za ujazo bilioni 11.8 sawa na asilimia 39.3 ya kiwango cha juu ambacho ni mita za ujazo bilioni 30.



*Muonekano wa Mradi wa kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere kwa mwezi Mei 2023.*

**ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa kinyerezi I Extension – MW 185**

**42.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu upanuzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I – MW 150 kwa kuongeza mitambo itakayozalisha MW 185 na hivyo kuwezesha kituo hicho

kuzalisha jumla ya MW 335. Utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa asilimia 100 ambapo mitambo yote minne (4) imewashwa na inachangia MW 185 katika Gridi ya Taifa.

**43.** Mheshimiwa Spika, mradi huu umegharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muun gano wa Tanzania kwa asilimia 100 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 185 sawa na takriban Shilingi bilioni 430.33.



*Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension (MW 185)*

**iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo-MW80**

**44.** MheshimiwaSpika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 80 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera na unahusisha nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda ambapo kila nchi inapata mgawanyo sawa wa MW 26.67. Mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia ambapo gharama za mradi kwa upande wa Tanzania ni Dola za Marekani milioni 113 sawa na takriban Shilingi bilioni 262.85.

**45.** MheshimiwaSpika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi huu katika maeneo yote kwa ujumla ulifikia asilimia 99 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023.



*Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo (MW 80)*

**iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 49.5**

**46.** MheshimiwaSpika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 49.5 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi, mkoani Kigoma. Aidha, mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 yenye urefu wa kilomita 54 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe, mkoani Kigoma na kuunganisha vijiji saba (7) vitakavyopitiwa na njia ya kusafirisha umeme. Kazi zilizo fanyika ni pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi (Consultant); ununuzi wa vifaa vya umeme vya kuunganisha wateja (last miles connections material); kuendelea kulipa fidia kwa Wananchi wanaopisha mradi kutoka Mazumbwe hadi Kidahwe; na kuanza utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2024.

**47.** MheshimiwaSpika, gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 144.14 takriban Shilingi bilioni 335.28 na unatekelezwa kwa ufadhili wa AfDB (Dola za Marekani milioni 140) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itachan gia kiasi cha (Dola za Marekani milioni 4.14). Kazi inayoendelea kwa sasa ni taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Februari, 2024 na kukamilika mwezi Agosti, 2028.

**v) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87.8**

**48. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 87.8 kwa kutumia maji ya Mto Kagera. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 38.8 kutoka Kakono hadi Kyaka na kuongeza uwezo wa kituo cha kupoza umeme cha Kyaka kutoka msongo wa kV 132 hadi kV 220.Kazi zilizofanyika hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 ni pamoja na kukamilisha taratibu za kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi; kuanza taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi; na kuendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Mradi huu unafadhiliwa na AfDB (Dola za Marekani milioni 161.47, AFD (Euro milioni 110), EU (Euro milioni 35) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Dola za Marekani milioni 6.03). Jumla ya gharama za ujenzi wa mradi huu ni takriban Shilingi bilioni 724.28. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2024 na kukamilika mwezi Februari, 2029.

**vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua Shinyanga – MW 150**

**49.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia jua katika eneo la Kishapu mkoani Shinyanga wenye uwezo wa kuzal isha MW 150. Gharama ya mradi huu ni Euro milioni 115.30 sawa na Shilingi bilioni 294.02 kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Ufaransa (AFD). Mradi huu unatekelezwa katika awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza itahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 50 utakaogharimu kiasi cha Euro milioni 43 sawa na Shilingi bilioni 109.65 na awamu ya pili itahusisha ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa MW 100 utakaogharimu kiasi cha Euro milion 72.30 sawa na Shilingi bilioni 184.37.

**50.** Mheshimiwa Spika, hadi sasa, taratibu za kusaini mkataba na Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa Ujenzi zinaendelea baada ya kupata kibali kutoka kwa Mfadhili (Shirika la Maendeleo ya Ufaransa (AFD). Aidha, Serikali imetoa fedha kiasi cha Shilingi bilioni 1.83 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi 108 wanaopisha eneo la ujenzi wa mradi. Kwa sasa, Mpango wa Kuhamisha Watu (Resettlement Action Plan) unaendelea

kutekelezwa ikiwemo taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi hao. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa mradi inatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2023 na kukamilika mwezi Agosti, 2024 na awamu ya pili inatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2024 na kukamilika mwezi Juni, 2026.

**vii) Ukarabati wa Mitambo katika Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale- MW 21**

**51.** Mheshimiwa Spika, lengo la mradi huu ni kukarabati miundombinu ya kuzalisha umeme katika kituo cha Hale chenye uwezo wa kuzalisha MW 21 ili mitambo hiyo iweze kuendelea kuzalisha umeme kwa uwezo wake wa juu badala ya MW 10.5 zinazozalishwa kwa sasa. Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 21.2, sawa na takriban Shilingi bilioni 49.31 kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Sweden (Sida) ambapo Mkataba wa ufadhili ulisainiwa tarehe 16 Juni, 2022. Mradi unahusisha uchimbaji wa handaki (escape tunnel), kujenga barabara na kuweka mitambo ya uzalishaji pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 15. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Agosti, 2022 na una tarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2025.

**D.2.2: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTAYARISHAJI**

**i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara – MW 300**

**52.** Mheshimiwa Spika,mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia chenye jumla ya MW 300 katika Mkoa wa Mtwara ambacho kitagharimu Dola za Marekani milioni 1,062.75 sawa na Shilingi trilioni 2.47. Utekelezaji wa mradi huu utaenda sambamba na ujenzi wa njia ya kusa firisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 268 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu. Kwa sasa, mazungumzo kati ya Serikali na wafadhili yapo katika hatua za awali ambapo JICA imeonesha nia ya kufadhili kwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 719.05, AfDB kiasi cha Dola za Marekani milioni 103.23 na Serikali itachangia upatikanaji wa ardhi, gharama za usimamizi wa mradi na kodi. Aidha, taratibu za kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji

wa mradi zinaendelea na iwapo taratibu hizo zitakamilika kama inavyotarajiwa, ujenzi wa mradi utaanza mwezi Oktoba, 2025 na kukamilika mwezi Septemba, 2028.

**ii) Mradi wa Kulalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358**

**53.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 358 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji mkoani Njombe pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha uhuishaji wa Upembuzi Yakinifu wa mwaka 1998 na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi. Tathmini ya athari za mazingira na jamii zimekamalika na kuwasilishwa NEMC mwezi Machi, 2023 kwa ajili ya kupata cheti cha mazingira.

**54.** Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme baada ya kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 867.41 sawa na Shilingi trilioni 2.01 na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme zin akadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 20.49 sawa na Shilingi bilioni 47.66. Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zinatarajiwa kupatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia mkopo wa masharti nafuu (concessional loans). Hotuba ya Waziri wa Nishati 23 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2023/24 Aidha, TANESCO pia inafanya tathmini kuangalia uwezekano wa kupata fedha kupitia mauzo ya Dhamana za Kampuni (Corporate Bonds and Green Bonds) kupitia soko la Hisa na Mitaji, ikiwa ni njia mbadala ya kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2025 na kukamilika mwezi Juni, 2030 kama taratibu za kupata fedha zitakamilika kama zilivyopangwa.

**iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kikonge – MW 321**

**55. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 321 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhuhu mkoani Ruvuma na ujenzi wa njia ya kusafirisha

umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 96 kutoka Kikonge hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Gharama za mradi ni Euro milioni 708 sawa na Shilingi trilioni 1.8. Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu pia zinatarajiwa kupatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia mkopo wa masharti nafuu (concessional loans). Vilevile, tathmini inafan yika kupitia TANESCO ili kuona uwezekano wa kupata fedha za kutekeleza mradi huu kupitia mauzo ya Dhamana za Kampuni (Corporate Bonds and Green Bonds) katika Soko la Hisa na Mitaji.

**56.** MheshimiwaSpika, kazi zilizofanyika kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na: kukami lika kwa zoezi la kuweka mipaka katika eneo kitakapojengwa kituo cha kuzalisha umeme, bwawa la kuhifadhi maji na eneo la makazi ya wafanyakazi; kuendelea na kazi za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; na kuendelea na kazi ya utambuzi wa mipaka ya njia ya kusafirisha umeme kutoka eneo la mradi hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Taratibu za kupata fedha zikikamilika kama ina vyotarajiwa, ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2024 na kukamilika mwezi Oktoba, 2029.

**iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222**

**57. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 222 kwa kutumia maji ya Mto Rumakali mkoani Njombe na njia ya kusafiri sha umeme yenye msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 65 kutoka kwenye mitambo hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo mkoani Mbeya. Baada ya kuka milika kwa Upembuzi Yakinifu, gharama za ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme ni Dola za Marekani milioni 612.79 sawa na Shilingi trilioni 1.42 na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 21.72 sawa na Shilingi bilioni 50.3. Fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mradi huu zinatarajiwa kupatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia mkopo wa masharti nafuu (concessional loans). Aidha, TANESCO inafanya tathmini ili kuona uwezekano wa mradi huu kugharamiwa kupitia utaratibu wa mauzo ya Dhamana za Kampuni (Corporate Bonds and Green Bonds). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Serikali kupitia TANESCO imekamilisha uhuishaji wa

Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na iwapo taratibu za upatikanaji wa fedha zikikamilika kama inavyokusudiwa, ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2025 na kukamilika mwezi Julai, 2030.

**D.3: MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME**

**D.3.1: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI**

**58. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 160 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi kituo cha kupoza umeme cha Chalinze mkoani Pwani. Mradi huu wa njia ya usafirishaji umeme unagharimu Shilingi bilioni 158 ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wake umefikia asilimia 93.5. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze chenye uwezo wa MVA 1,500 na unagharimu Shilingi bilioni 134.19 ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wake umefikia asilimia 64. Mradi huu ulianza mwezi Agosti, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023.



*Kituo cha kupokea na kusafirisha umeme (switch yard) cha Julius Nyerere.*

**ii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi na Kituo cha kupoza Umeme Nyakanazi**

**59.** Mheshimiwa Spika, mradi huu ulihusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi; na kusambaza umeme katika vijiji 32 vinavyopitiwa na mradi. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni Euro milioni 45 sawa na takriban Shilingi bilioni 127 chini ya ufadhili wa KfW (Euro milioni 20), AFD (Euro milioni 14), EU (Euro milioni 7.6) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Euro milioni 3.4).

**60.** Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi umekamilika kwa asilimia 100 na kuzinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 16 Oktoba, 2022. Kwa upande wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi utekelezaji wake umefikia asilimia 42. Mradi wa usambazaji umeme vijijini unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2023.

**iii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha - Namanga**

**61.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Babati na Arusha. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme cha Lemugur katika eneo la Kisongo mkoani Arusha na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Singida pamoja na usambazaji wa umeme katika vijiji 19 vilivyo jirani na mkuza wa njia ya umeme katika mikoa ya Singida, Manyara na Arusha. Gharama ya mradi ni Dola za Marekani milioni 258.82 sawa na takriban Shilingi bilioni 602.04 kwa ufadhili wa AfDB (Dola za Marekani milioni 116.58), JICA (Dola za Marekani milioni 98.38) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Dola za Marekani milioni 43.86). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 ute  kelezaji wa mradi huu ulifikia asilimia 95 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2023.

**iv) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi**

**62.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 94 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi.

Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 35 sawa na takriban Shilingi bilioni 81.41 kwa ufadhiliwa AfDB (Dola za Marekani milioni 33.7) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Dola za Marekani milioni 1.3). Kwa ujumla mradi ulikamilika mwezi Februari, 2023.

**v) Mradi wa Njia yaKusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot II)**

**63. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma yenye urefu wa kilomita 414 kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 71.5 sawa na Shilingi bilioni 166.32 na unagharamiwa na Ser ikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 98 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2023.



*Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kV 220 katika mradi wa Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR)*

**vi) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

**64. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 620 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma. Mradi unahusisha pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kisada (Iringa), Iganjo (Mbeya), Tunduma (Songwe) na Sumbawanga (Rukwa). Mradi unalenga kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi za Kusini mwa Afrika *(Southern African Power Pool – SAPP)* kupitia Zambia na unafadhiliwa na Benki ya Dunia (Dola za Marekani milioni 455), AFD (Euro milioni 100), EU (Euro milioni 26) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Dola za Marekani milioni 10) sawa na jumla ya Shilingi trilioni 1.38. Aidha, mradi huu utawezesha kupeleka Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Rukwa na hivyo kuondokana na kutegemea umeme kutoka Zambia pamoja na uzalishaji umeme wa mafuta.

**65.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha taarifa za tathmini *(evaluation reports)* za zabuni za Wakandarasi Wajenzi wa mradi ambapo taratibu za kupata kibali (*No Objection)* kutoka kwa Wafadhili zimekamilika. Aidha, Serikali tayari imetoa Shilingi bilioni 16.43 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi 6,500 wanaopisha mradi na kazi ya ulipaji fidia imekamilika kwa awamu ya kwanza ambapo Wananchi 4,750 wamepokea Shilingi bilioni 13.67 na maandalizi ya awamu ya pili yanaendelea. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2023 na kukamilika mwezi Septemba, 2025.

**vii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma**

**66. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilomita 280. Mradi pia unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na usambazaji umeme katika vijiji 18 vilivyopo katika eneo la mradi. Gharama za

mradi huu ni Dola za Marekani milioni 186.93 sawa na Shilingi bilioni 434.98 chini ya ufadhili wa AfDB (Dola za Marekani milioni 123.39), EDCF (Dola za Marekani milioni 45) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Dola za Marekani milioni 18.54).

**67.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi wa njia ya usafirishaji umeme umefikia asilimia 53. Ujenzi wa mradi ulianza mwezi Januari, 2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2024. Kwa upande wa ujenzi wa vituo viwili (2) vya kupoza umeme vya Nyakanazi na Kidahwe (Kigoma) vyenye uwezo wa MVA 240 kila kimoja, taratibu za kumpata Mkandarasi zinatarajiwa kuka milika mwezi Novemba, 2023 na ujenzi wa mradi kukamilika Agosti, 2026.



*Ujenzi wa njia ya kusafirisha Umeme wa Msongo mkubwa wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma.*

**viii) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)***

**68.** Mheshimiwa Spika, mradi huu ambao unatekelezwa katika kipindi cha miaka minne (4), una jumla ya miradi midogo midogo 26 katika awamu ya kwanza ambayo inalenga kuimarisha miundombinu ya umeme katika mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufungaji wa mitambo na vifaa vya kisasa, ujenzi wa njia za usa  firishaji na usambazaji umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani bilioni 1.9 sawa na Shilingi trilioni 4.42 ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23 mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kuanza kazi za awali.

**69.** Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 ni pamoja na: kufanya usanifu wa mradi; kuwapata Wakandarasi watakaotekeleza mradi; kununua vifaa na kuanza utekelezaji wa mradi awamu ya kwanza. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha kuondokana na changamoto ya kukatika kwa umeme pamoja na umeme usiokidhi mahitaji (low voltage). Kielelezo Na.7 kinaonesha wigo wa Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa. Aidha, Kiambatisho Na.2 kinaonesha miradi 26 ya Kuimarisha Gridi ya Taifa inayotekelezwa katika awamu ya kwanza ambayo imeanza mwaka 2022/23 na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2024. Vile  vile, utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huu itaanza baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza.

**Kielelezo Na. 7: Wigo wa Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (Gridi Imara)**




*Chanzo: TANESCO*

**70.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizotekelezwa kupitia mradi huu ni pamoja na kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kupitia kituo cha Nyakanazi; kuunganisha Wilaya za Ngara na Biharamulo kwenye kituo cha Gridi ya Taifa Nyakanazi; na kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuimarisha miundombinu ya umeme katika mikoa mbalimbali nchini.

**ix) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi**

**71.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi yenye urefu wa kilomita 383 pamoja na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kupoza umeme vya Ipole, Inyonga na Mpanda. Gharama ya mradi huu ni Shilingi bilioni 168 na unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi kwa ujumla ulifikia asilimia 26.7 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2024.

**x) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Kigoma kupitia Urambo**

**72.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Kigoma kupitia urambo na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Urambo na Nguruka. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 114 na zinagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 15 na mradi una tarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024.

**xi) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa (TANESCO) Transmission Grid Rehabilitation & Upgrade Project – TTGRUP)**

**73. Mheshimiwa Spika,** Mradi unalenga kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kukarabati na kuboresha vituo tisa (9) vya kupoza umeme vya Mlandizi, Chalinze, Same, Kibeta (Bukoba), Mwakibete (Mbeya), Tabora, Mufindi, Nyakato (Mwanza) na Musoma. Gharama za mradi huu ni Euro milioni 69 sawa na takriban Shilingi bilioni 175.95 ambapo Euro millioni 67 zimetolewa na Shirika la Maendeleo ya Ufaransa (AFD) na Euro milioni 2 zimetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**74. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TANESCO imekamilisha taratibu za kuwapata Wakandarasi na kufanya malipo ya awali (advance payment) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ambapo kazi ya usanifu (design) na maandalizi ya eneo la mradi na vifaa vya ujenzi (site mobilization) zinaendelea. Utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Desemba, 2022 na umefikia asimia 20. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2025.

**D.3.2: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA YA UTAYARISHAJI**

**i) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Benaco hadi Kyaka**

**75.** Mheshimiwa Spika, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 167.17 kutoka Benaco hadi Kyaka mkoani Kagera, pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Benaco. Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 132.8 sawa na Shilingi bilioni 308.91 zinazofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (Arab Bank for Economic Development in Africa - BADEA), Mfuko wa Maendeleo wa Kimataifa wa Muungano wa Nchi

Zinazosafirisha Mafuta (OPEC Fund for Inter national Development), Mfuko wa Maendeleo wa Abu-Dhabi (Abu - Dhabi Fund for Development - ADFD), Mfuko wa Maendeleo wa Saudi (Saudi Fund for Devel opmnet - SFD) pamoja na Serikali ya Tanzania (GoT). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi; kufanya uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi; kukamilisha usanifu wa mradi; na kuanza hatua za awali za kumpata Mshauri Mwelekezi. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2023 na kukamilika mwezi Novemba, 2025.

**ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda, na Kituo cha Kupoza Umeme Mpanda**

**76.** Mheshimwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda yenye urefu wa kilometa 480. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 200.4 sawa na Shilingi bilioni 466.15 kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme na Dola za Marekani milioni 50 kwa upande wa kituo cha kupoza umeme. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Exim Benki ya Korea zimeonesha nia ya kufadhili mradi huu. Aidha, tayari Mhandisi Mshauri amepatikana na anaendelea na kazi ya kuhuisha taarifa ya Upembuzi Yakinifu (Upgrade of Feasibility Study) ambayo inatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2023. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2025 na kukamilika mwezi Januari, 2027.

**iii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kV 220 kutoka Makutupora hadi Tabora kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot III)**

**77.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 347 kutoka Makutupora hadi Tabora kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa ni Dola za Marekani milioni 90.65 sawa na Shilingi bilioni 212.58. Kazi zilizofanyika kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na kuanza kufanya Upembuzi Yakinifu ambapo kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi

Septemba 2023. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2024 na kukamilika mwezi Desemba, 2025.

**iv) mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Tabora hadi Isaka kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot IV)**

**78.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu unaokadiriwa kuwa kilomita 195 kutoka Tabora hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Gharama za mradi huu inakadiriwa kuwa ni Dola za Marekani milioni 56.1425 sawa na Shilingi bilioni 131.66. Katika mradi huu, kazi iliyofanyika kwa mwaka 2022/23 ni kuanza kufanya Upembuzi Yakinifu unaotarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2023. Ujenzi wa mradi huu unategemewa kuanza mwezi Januari, 2024 na kukamilika mwezi Desemba, 2025.

**v) Mradi wa Njia yaKusafirishi Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot V)**

**79.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 230 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 59.6 sawa na Shilingi bilioni 139.77. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Seri kali imekamilisha taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi na kuendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi. Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2023 na kukamilika mwezi Aprili, 2025.

**vi) Mradi wa Njia yaKusafirishi Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Segera – Same hadi Lemugur**

**80.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 368 kutoka Segera hadi Lemugur kupitia Same. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 165.6 sawa na Shilingi bilioni 388.35 kwa ufadhili wa AfDB. Katika mwaka 2022/23, kazi zilizofanyika ni kuanza taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu. Kazi ya Upembuzi Yakinifu wa mradi huu inate gemewa kuanza mwezi Julai, 2023 kwa

kipindi cha miezi 12. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2026 na utarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2028.

**vii) Mradi wa Njia yaKusafirishi Umeme (Submarine Cable) Msongo wa kV 220 kutoka Tanzania Bara (Ununio) hadi Zanzibar**

**81.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 kwenda Zanzibar kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa umeme Tanzania Visiwani (Zanzibar). Mradi utawezesha kutatua changamoto ya kuzid iwa kwa miundombinu ya kusafirisha umeme kwenda Zanzibar iliyopo kwa sasa. Kazi zilizofanyika katika mwaka 2022/23 baada ya kupata ufadhili wa fedha za kazi kutoka AfDB ni kuanza taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi ambapo gharama halisi za mradi huu zitajulikana. Kazi ya Upembuzi Yakinifu wa mradi huu inategemewa kuanza mwezi Julai, 2023 kwa kipindi cha miezi sita (6). Baada ya kupatikana kwa taarifa ya Upembuzi Yak inifu, Serikali itaanza maongezi na wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kupata fedha Hotuba ya Waziri wa Nishati 32 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2023/24 za ujenzi wa mradi. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24 baada ya kuanza.

**viii) Mradi wa Ujenzi waKituo chaKupoza Umeme Manyoni (Manyoni Substation – MVA 60)**

**82.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kupoza umeme chenye uwezo wa MVA 60 katika Kata ya Mkwese, Wilaya ya Manyoni, Mkoa wa Singida na unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 16.36 sawa na Shilingi bilioni 38.05. Kazi zilizofanyika kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na: kukamilisha Upembuzi Yakinifu (Feasibility Study); kuanza kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; na kuanza kufanya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi; na kuendelea na taratibu za kufafuta fedha kwa ajili ya ute kelezaji wa mradi. Ujenzi wa mradi huu unategemewa kuanza mwezi Agosti, 2024 na kukamilika mwezi Oktoba, 2025.

**D.3.3: UTEKELEZAJI WA MIRADI MINGINE NA MATENGENEZO YA MITAMBO**

**83. Mheshimiwa Spika,** TANESCO kwa kutumia mapato yake ya ndani imeende lea kufanya matengenezo ya miundombinu ya

kuzalisha umeme ikijumuisha matengenezo kinga (preventive maintenance) ambayo yanahusisha ukaguzi na matengenezo madogo (inspection and minor preventive maintenances), na matengenezo makubwa (major preventive maintenances/overhauls). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 matengenezo yaliyofanyika ni pamoja na: kufanya matengenezo kinga katika vituo vya Ubungo III, Kinyerezi I, Tegeta na Pangani; na kufanya maten genezo makubwa katika kituo cha Nyumba ya Mungu. Jumla ya Shilingi bilioni 25.69 zimetumika kwa ajili ya matengenezo hayo. Aidha, TANESCO inaende lea na ukarabati wa mitambo katika vituo vya Hale, Nyakato, Ubungo I na Mtwara ambao utagharimu Shilingi bilioni 54.06.

**84.** Mheshimiwa Spika, TANESCO imetekeleza jumla ya miradi 20 inayolenga kuongeza uwezo wa miundombinu ya usafirishaji umeme (transmission network upgrade projects), jumla ya miradi 12 ya kuboresha mifumo ya uendeshaji Gridi ya Taifa (improvement of Grid operation systems) na jumla ya miradi 16 ya kukarabati miundombinu ya usafirishaji umeme (transmission Grid rehabilitation and main tenance projects). Kukamilika kwa miradi hiyo kutasaidia kuongeza uwezo wa njia za kusafirisha umeme na vituo mbalimbali vya kupoza umeme ili kukidhi mahitaji katika maeneo husika na kusaidia kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mfumo wa Gridi kwa kuhakikisha inakuwa otomatiki (automation) ili kuongeza ubora katika utendaji wa mitambo pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji. Jumla ya Shilingi bilioni 248.23 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**85.** MheshimiwaSpika, vilevile, TANESCO imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kupanua miundombinu ya usambazaji umeme (distribution network exten sion projects), miradi ya kuboresha umeme (voltage improvement projects) na miradi ya kukarabati miundombinu ya usambazaji umeme (distribution repair and maintenance projects). Katika mwaka 2022/23, TANESCO inatekeleza jumla ya miradi 1,696 ya kupanua miundombinu ya usambazaji umeme ili kuyafikia maeneo ambayo miundombinu hiyo haijafika na vilevile jumla ya miradi 1,345 inayolenga Hotuba ya Waziri wa Nishati 33 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2023/24 kuboresha kiwango cha umeme kwenye maeneo ambayo wateja

wanapata umeme mdogo (low voltage). Utekelezaji wa miradi hii unaendelea na itakamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2023 ambapo jumla ya Shilingi bilioni 219.01 zitatumika.

**D.3.4: UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO (TCPM NA ETDCO)**

**86.** Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Kuzalisha Nguzo za Umeme za Zege Tanza nia (TCPM), ambayo ni kampuni Tanzu ya TANESCO imefanikiwa kusanifu na kuandaa Mwongozo wa Viwango vya Nguzo za Zege za Mita 17 kwa ajili ya kusa firisha umeme msongo wa kV 132. Aina hii ya nguzo za zenge za mita 17 haijawahi kuwepo nchini. Aidha, TCPM imeshiriki kutoa ushauri wa kitaalamu katika kuhaki kisha upatikanaji wa nguzo bora za mita 17 kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 kutoka Mkoa wa Tabora kwenda Mikoa ya Kigoma na Katavi.

**87.** Mheshimiwa Spika, vilevile, TCPM imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha inawekeza katika uzalishaji wa nguzo za zege kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi. Kampuni imeandaa Mwongozo utakaoelekeza namna bora ya kushirikiana na wawekezaji binafsi kwa kuzingatia ushindani na uwiano sawa wa faida katika ubia na wawekezaji binafsi. Pia, Kampuni inafanya taratibu za kupata fedha kwa ajili ya kununua na kufunga mashine za uzalishaji wa nguzo za zege Mkoani Tabora. Uzalishaji huu utafanyika katika jengo la Tabora Old Power Station lililokua likitu mika zamani kuzalisha umeme wa mafuta.

**88.** Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usa firishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO), ambayo pia ni kampuni tanzu ya TANESCO imeweza kuunganisha kwenye Gridi ya Taifa Mkoa wa Kigoma na Wilaya za Biharamulo na Ngara kupitia mradi wa ujenzi miundombinu ya msongo wa kV 33 yenye urefu wa kilometa 44 kutoka kituo kipya cha kupoza umeme cha Nyakanazi na hivyo kuwezesha kupunguza gharama za uzalishaji umeme kwa mafuta Mkoani Kigoma na Wilaya tajwa za Mkoa wa Kagera. Mradi huu uligharimu Shilingi bilioni 4.7.

**89.** Mheshimiwa Spika, ETDCO pia imeendelea na utekelezaji wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 wenye urefu wa kilometa 383 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Sikonge, Ipole na Inyonga. Mradi huu umekamilika kwa asili mia 48.89 na

utakapokamilika utawezesha Mkoa wa Katavi kuungwa katika Gridi ya Taifa na hivyo kuimarisha upatikanaji wa umeme katika mkoa huo na kuepuka gharama kubwa za kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta. Mradi huu ulianza kute kelezwa mwezi Julai, 2022 kwa gharama ya Shilingi bilioni 116.3 na unatarajiwa mwezi Januari, 2024.

**90. Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali kupitia ETDCO imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme wa msongo wa kV 33 na ufungaji wa mashineumba katika mgodi wa GGML Mkoani Geita ili kuhakikisha umeme wa uhakika unapati kana na hivyo kuepusha gharama kubwa za uzalishaji umeme kwa kutumia mafuta katika mgodi huo. Aidha, ETDCO imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kusam baza umeme vijijini katika Mikoa ya Katavi na Mbeya kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

**91. Mheshimiwa Spika,** kampuni ya ETDCO imeendelea kufanya vyema katika ute kelezaji wa miradi inayotekeleza, kwa kuzingatia ubora unaotakiwa, kwa wakati na kwa gharama nafuu. Kutokana na utendaji huo, ETDCO imeendelea kupata faida kwa miaka minne (4) mfululizo ambapo katika mwaka 2021/22 kampuni iliten geneza faida ya Shilingi bilioni 2.7 baada ya kuondoa kodi. Kampuni pia inatara jia kutokana na faida inayopata, kutoa gawio kwa TANESCO ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali katika kuhakikisha mashirika/makampuni yake yanaweza kujiendesha yenyewe na kwa kutengeneza faida.

## D.3.5: UWEKEZAJI WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA NDOGO YA UMEME

**92.** Mheshimiwa Spika, kupitia ushirikishwaji wa sekta binafsi, Serikali kupitia TANESCO imesaini Hati za Makubaliano (Memorundum of Understanding – MoUs) na Wawekezaji binafsi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu, gesi asilia na makaa ya mawe. Wawekezaji hao binafsi ni pamoja na: Total Eren (MW 200); Abu Dhabi Future Energy Company PJSC - Masdar (MW 2,000); Sumitomo (MW 300 – 600); Mbeya Power Ltd (MW 300); na Kilwa

Energy (MW 318). Kazi zinazoendelea katika utekelezaji wa miradi hii ni pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu (Bankable Feasibility Studies) na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) kwa ajili ya upatikanaji wa fedha za kute keleza miradi hiyo (Financial Closure).

**93.** Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa njia za kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Chalinze – Dodoma, Chalinze – Segera na Segera – Tanga pamoja na vituo vya kupoza umeme vyenye uwezo wa MVA 300 Segera, upanuzi wa kituo cha MVA 750 Dodoma (bay extension) na MVA 150 Tanga, Serikali imeanza taratibu za kuingia makubaliano na wawekezaji binafsi ambao ni Larsen & Toubro Ltd na Gridworks Development Partners LLP kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**94.** Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali kupitia TANESCO imeanza taratibu za kuingia makubaliano na kampuni ya AFRICA50 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kwa mfumo wa wasafirishaji binafsi wa umeme (Independent Power Transmission – IPT). Miradi hiyo ni Rufiji – Kibiti – Likong'o; Likong'o – Somanga Fungu; Mtwara – Tunduru – Songea; Segera – Same – Kisongo; na Kinyerezi – Somanga Fungu.

**95.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia EWURA iliendelea kuvutia Wazalishaji Wadogo Binafsi wa Umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 jumla ya mikataba 16 ya kuuziana umeme (Standardized Power Purchase Agreement- SPPA) ilisainiwa kati ya TANESCO na wazalishaji binafsi yenye jumla ya MW 46.27 (Kiambatisho Na. 3). Aidha, Kampuni hizo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya uzalishaji wa umeme.

**96.** Mheshimiwa Spika, vilevile, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, kulikuwa na jumla ya Wazalishaji Wadogo 17 waliozalisha jumla ya MW 70.17 ambapo 10 wanai uzia umeme TANESCO. Wazalishaji hao na viwango vya umeme wanaoiuzia TANESCO ni: TPC (MW 9 - Tungamotaka); Tulila (MW 5 – Maji); Next Gen Sola wazi (MW 5 – Jua); Mwenga (MW 4 – Maji); TANWAT (MW 1.5 – Tungamotaka); Andoya (MW 1 – Maji); Yovi (MW 0.95 – Maji); Luponde (MW 0.9 – Maji); Matem bwe (MW 0.59 – Maji); na Darakuta (MW 0.32 – Maji). Pia, wazalishaji watano (5) ambao ni Bagamoyo Sugar Ltd (MW 5 – Tungamotaka); Maweni Limestone Ltd (MW 7.5 – Mvuke); Tembo Nickel Corporation (MW 0.35 – Dizeli); SSI Energy (T) Ltd (MW 10 – Jua); na Suma Hydro Ltd (MW 4 – Maji) walipatiwa leseni

za uzalishaji katika kipindi cha utekelezaji kati ya Julai 2022 hadi April 2023. Kiambatisho Na. 4 kinaonesha orodha ya Wazalishaji Wadogo wa Umeme wenye Leseni/Vibali hadi kufikia mwezi Aprili, 2023.

**D.4: MIRADI YA NISHATI VIJIJINI**

**i) Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round II)**

**97.** Mheshimiwa Spika, mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzu nguko wa Pili una jumla ya Mafungu 39 na unahusisha kupeleka umeme kwenye vijiji 4,071 vilivyobaki kati ya vijiji vyote 12,318 pamoja na kujenga njia za umeme wa Msongo wa Kati zenye urefu wa kilomita 23,526, kujenga njia za umeme wa Msongo Mdogo zenye urefu wa kilomita 4,091, kufunga mashineumba 4,071 na kuunganisha wateja wa awali wapatao 89,232.

**98.** Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kupeleka umeme katika maeneo mengi ya vijiji, Serikali kupitia REA iliongeza wigo wa njia za Msongo Mdogo kutoka kilomita moja (1) hadi kilomita tatu (3) na kuongeza wateja kutoka 22 hadi 66 kwa kila kijiji ili kuhakikisha maeneo muhimu na kaya nyingi zaidi zinafikiwa na huduma hiyo. Ongezeko hili limepelekea njia za msongo mdogo kuongezeka kutoka kilo mita 4,091 hadi kilomita 12,159 na wateja kutoka 89,232 hadi 258,660. Kutokana na ongezeko la wigo wa mradi, gharama za mradi zimeongezeka kutoka Shilingi trilioni 1.24 hadi Shilingi trilioni 1.58 ambapo ongezeko hilo la Shilingi bilioni 335.35 limepatikana kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia.

**99.** MheshimiwaSpika, hadi kufikia mwezi Aprili 2023, Serikali kupitia REA iliendelea na ujenzi wa njia za usambazaji wa umeme, kuhamasisha wananchi kuungan ishiwa umeme na kuunganisha wateja ambapo utekelezaji wa kazi hizo umefikia asilimia 68.66. Aidha, jumla ya vijiji 1,880 kati ya 4,071 sawa na asilimia 46.18 vimeunganishiwa umeme. Muda wa kukamilika mradi huu unatofautiana kutokana na tarehe za kusainiwa kwa mikataba kwa kila fungu ambapo mafungu 32 yana tarajiwa kukamilika

ifikapo mwezi Desemba, 2023 na mafungu saba (7) ifikapo mwezi Juni, 2024.



*Kupatikana kwa huduma za umeme vijijini kumewezesha upatikanaji wa huduma za burudani na taarifa za matukio mbalimbali kupitia runinga na hivyo kupunguza uhitaji wa wananchi kufuata huduma hiyo mijini.*

**100.** Mheshimiwa Spika, Sababu za kuchelewa kwa utekelezaji wa Mradi wa Kusam baza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ni kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi wa mradi; kuchelewa kufika kwa vifaa hasa vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi kutokana na ugumu wa uzalishaji na usafirishaji wa vifaa hivyo uliosabishwa na athari za UVIKO 19, pamoja na nyongeza ya wigo wa mradi.

**ii) Mradi waKusambaza Umeme katika Vitongoji – (Hamlet Electrification Project – HEP)**

**101.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia REA ilifanya utambuzi wa wigo wa mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji vyote Tanzania Bara na kubaini kuwa viton goji ambavyo bado

havijafikiwa na miundombinu ya umeme nchini ni 36,755 kati ya vitongoji 64,760. Ili kufikisha miundombinu ya umeme katika vitongoji hivyo, Shilingi trilioni 6.7 zinahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa azma hiyo.

**102.** Mheshimiwa Spika, Serikali ilipata mkopo wa gharama nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kupitia dirisha la Extended Credit Facility ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 100 kimetengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huu katika vitongoji 654 katika Mikoa ya Songwe na Kigoma na hivyo kufanya viton goji ambavyo havina umeme kuwa 36,101. Hadi kufikia Mwezi Mei, 2023, REA ilikuwa katika hatua za mwisho za ununuzi kwa kutoa kusudio la kuingia mkataba (intention of award) kwa wakandarasi kwa muda wa siku saba (7) ili mikataba ya utekelezaji isainiwe na kazi kuanza.

**103.** MheshimiwaSpika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati inaandaa Mpango Maalumu wa kupeleka umeme katika vitongoji vyote nchini ndani ya miaka mitano (5), badala ya takribani miaka 20 kwa utaratibu wa sasa. Kwa sasa zoezi la uchambuzi wa namna ya ugharamiaji wa azma hiyo, ikiwemo kupitia ushiriki wa Sekta Binafsi linaendelea.

**iii) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili B**

**104. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye vitongoji 1,686 katika mikoa ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe na Songwe na kuunganisha jumla ya wateja wa awali 95,334. Gharama ya mradi huu ni Shilingi bilioni 234.4. Mradi huu unafadhi liwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD). Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 Wakandarasi walikuwa wanaendelea na kazi ya upimaji wan jia ya ujenzi wa mradi, kuandaa michoro pamja na ununuzi wa vifaa.

**iv)** Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili C

**105.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unalenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye vitongoji 1,880 katika mikoa ya Manyara, Iringa, Rukwa, Mtwara, Ruvuma, Simiyu na Mara kwa kujenga kilomita 6,562 za msongo mdogo na kufunga mashineumba 1,932 ili kuunganisha wateja wa awali 131,719. Gharama ya mradi huu ni Shilingi bilioni 293 kwa ufadhili wa Benki

ya Dunia na Serikali za Norway na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sasa Serikali imekamilisha taratibu za kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**v) Mradi wa Ujenzi waKituo chaKupoza Umeme Ifakara (220/33kV, 1x20MVA) na Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji Umeme**

**106.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa Kituo cha kupoza Umeme cha Ifakara na Ujenzi wa Njia ya Kusambaza Umeme Vijijini (Wilaya za Kilombero na Ulanga). Mradi unalenga kuwezesha na kuimarisha shughuli za kilimo katika eneo la SAGCOT (Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania) kwa kuwapatia wananchi huduma za umeme. Gharama za mradi ni Shilingi bilioni 23.62 ambazo zinalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya.

**107.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2023 ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme imekamilika kwa asilimia 100 ambapo wateja 1,588 wameun ganishiwa umeme katika vijiji nane (8) na vitongoji saba (7) katika Wilaya za Kilombero na Ulanga. Utekelezaji wa mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2023 ambapo maeneo 36 ya kutoa huduma za jamii, zikiwemo hospitali tatu (3), mashine za kusaga mbili (2), sehemu za ufugaji mbili (2), shule za msingi 10, shule za sekondari mbili (2) na nyumba za ibada 17 yameunganishiwa umeme. Aidha, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme chenye ukubwa wa MVA 20 umefikia asilimia 89.



*Ujenzi wa miundombinu ya umeme vijijini umewezesha kupatikana kwa umeme katika shule zilizopo vijijini na hivyo kuimarisha ufanisi katika utolewaji wa mafunzo kwa vitendo na kuongeza ufaulu wa wanafunzi.*

**vi) Mradi wa Peri Urban Awamu ya Pili**

**108.** MheshimiwaSpika, mradi huu unahusisha kupeleka umeme katika maeneo 153 yaliyopo katika majiji ya Arusha, Dodoma na Mwanza kwa kujenga miundombinu ya kusambaza umeme yenye urefu wa kilomita 751, kufunga mashineumba 143 na kuunganisha wateja wa awali 16,328. Gharama za mradi ni Shilingi bilioni 31.33 na fedha hizo zinatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 ujenzi wa mradi umekamilika kwa asilimia 91.0 ambapo maeneo 134 kati ya 153 yamefikiwa na umeme na wateja 11,425 kati ya wateja 16,328 wameunganishiwa umeme.

**vii) Mradi wa Peri Urban Awamu ya Tatu**

**109.** Mheshimiwa Spika,Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini imekamilisha ununuzi wa Wakandarasi ambapo tarehe 19

Desemba, 2022 Wakala ulisaini mikataba nane (8) na Wakandarasi watano (5) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Peri Urban Awamu ya Tatu katika mikoa nane (8) ya Geita, Kigoma, Kagera, Mbeya, Mtwara, Singida Tabora na Tanga. Jumla ya maeneo 416 yatafikishiwa miundombinu ya kusam baza umeme na wateja wa awali 22,105 watanufaika na huduma za umeme. Kwa sasa wakandarasi wote wamekamilisha upimaji na usanifu na wanaendelea na kazi ya ununuzi wa vifaa na kuanza ujenzi wa miundombinu. Gharama ya mradi huu ni Shilingi bilioni 76.9 ambazo zinatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miezi 18.

**viii) Mradi waKupeleka Umeme kwenye Vijiji katika Visiwa na MaeneoYaliyo Mbali na Gridi ya Taifa**

**110.** Mheshimiwa Spika,mradi huu unajumuisha ujenzi wa mifumo midogo ya kusam baza umeme (mini grids and stand-alone solar systems) katika maeneo yenye vyanzo vya nishati jadidifu kwa ajili ya kuzalisha umeme. Serikali kupitia REA ilika milisha mchakato wa kuwapata waendelezaji wa miradi ya kusambaza umeme kutokana na maporomoko ya maji ambapo mikataba miwili (2) ya miradi ya Ikon do-Matembwe Hydro Power ulisainiwa mwezi Februari 2023 na mkataba wa mradi wa Mwenga Hydro Power ulisainiwa mwezi Machi, 2023. Miradi hii itaunganisha jumla ya wateja wa awali 2,168 katika vijiji 42 kwa gharama ya Shilingi 3.06 bilioni.



*Miundombinu ya Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ijangala, uliopo katika kijiji cha Masisiwe, Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe. Mradi huu umefadhiliwa na Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini pamoja na wadau wengine na utazalisha umeme wa kilowati 360. Mradi huu unaratajiwa kuzinduliwa tarehe 24 Mei, 2023.*

**111. Mheshimiwa** Spika, Serikali kupitia REA imewapata waendelezaji watatu (3) wa miradi ya kusambaza umeme kwa kutumia nguvu ya jua, itakayotekelezwa katika visiwa 28 vilivyopo katika mikoa ya Kagera (8), Mwanza (13), Mara (3) na Lindi (4) na hivyo kuunganisha wateja 9,515 kwa gharama ya Shilingi bilioni 11.18. Waendelezaji hao wanaendelea na kazi ya kuandaa Upembuzi Yakinifu, Mpango wa Biashara, Vyeti vya Athari za Mazingira na Hati ya Kinga ya Malipo ya Awali (Advance Payment Gurantee). Serikali kupitia REA, itaendelea kuhamasisha waendelezaji binafsi wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu kuwekeza katika miradi ya kusambaza umeme katika maeneo yaliyo mbali na gridi ya Taifa yakiwemo ya visiwani.

**ix) Mradi waKuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vyaKusambaza Bidhaa za Petroli Vijijini kwa Njia ya Mkopo Nafuu (Credit Line Facility**

**112.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu kuwezesha ujenzi wa vituo vidogo vya kusambaza bidhaa za mafuta katika maeneo

mbalimbali ya vijijini nchini. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, Serikali ilikamilisha uandaaji wa Mwongozo na Kanuni za Utoaji Mikopo kwa waendelezaji wa ujenzi wa vituo vidogo vya mafuta Hotuba ya Waziri wa Nishati 40 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2023/24 vijijini. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali kupitia REA ilikamilisha majadiliano na Benki zitakazotumika kutoa mikopo ya riba nafuu kwa waendelezaji watakaoan zisha vituo vidogo vya mafuta vijijijini. Fursa hii imetangazwa kwa umma kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ajili ya kutangazwa katika Halmashauri mbalimbali nchini, Magazeti, Televesheni na katika tovuti ya REA (www.rea.go.tz).Tarehe ya mwisho kupokea maombi ni 30 Agosti, 2023.

**x) Mradi waKupeleka Umeme katika Vituo vya Afya na Pampu za Maji iliKuzuia Magonjwa yaKuambukiza na UVIKO-19**

**113.** Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu kusambaza umeme kwenye Vituo vya Afya 66 na Pampu za Maji 333 vilivyopo vijijini katika mikoa 25 Tanzania Bara. Wakala umewapata Wakandarasi wanne (4) kwa ajili ya kutekeleza mradi huu ambao umegawanyika katika Mafungu saba (7) kwa gharama ya Shilingi bilioni 34.5. Mikataba ya utekelezaji wa miradi hiyo ilisainiwa



tarehe 21 Novemba, 2022. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Wakandarasi walikuwa wamekamilisha usanifu wa mradi na kuendelea na ununuzi wa vifaa pamoja na kuanza ujenzi wa miundombinu ya mradi. Mradi huu utarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2023.

*Upatikanaji wa umeme vijijini umechangia kuboresha utolewaji wa huduma bora za afya ikiwemo shughuli za maabara na uhifadhi wa chanjo.*

**114.** Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya nishati vijijini hadi kufikia mwezi Aprili 2023 umewezesha kuunganisha jumla ya taasisi 43,925 ambazo zinatoa huduma kwa jamii zikiwemo za Elimu, Biashara, Pampu za Maji, Vituo vya Afya na Nyumba za Ibada kama inavyonekana katika Kiambatisho Na. 5.

**xi) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Maeneo ya Wachimbaji Wadogo wa Madini, Viwanda naKilimo**

**115. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu kupeleka umeme katika maeneo 336 ya wachimbaji wadogo wa madini, maeneo ya kilimo na viwanda katika maeneo mbalimbali Tanzania Bara. Serikali kupitia REA imekamilisha upatikanaji wa Wakandarasi watakaotekeleza mradi na mikataba ilisainiwa mwezi Februari, 2023 Ikulu, Dar es Salaam katika hafla iliyohudhuriwa na Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi unatarajiwa kuungani sha wateja wa awali 19,187. Gharama za mradi ni Shilingi bilioni 115 ambazo zin atolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Kwa sasa Wakandarasi wanaendelea na zoezi la upimaji wa kina wa njia za kusambaza umeme na ununuzi wa vifaa na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2024.

**xii) Mradi waKupeleka Umeme katika Shule na Mahakama za Mwanzo Vijijini**

**116. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu kupeleka umeme katika shule na mahakama za mwanzo vijijini ambazo hazina umeme. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Serikali imefanya utambuzi wa wigo wa Mradi ambapo jumla ya shule 729 na mahakama 292 zimebainishwa kuwa na uhitaji wa kuunganishiwa umeme. Aidha, REA na TANESCO wapo katika hatua za mwisho za kusaini makubaliano (MoU) ili TANESCO itekeleze kazi ya kuunganisha umeme katika shule na mahakama hizo. Mfumo huu utawezesha kutekelezwa kwa miradi hii kwa haraka na gharama nafuu zaidi kuliko kutafuta wakandarasi.

**xiii) Kuimarisha Usimamizi wa Miradi yaKupeleka Umeme Vijijini**

**117.** Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto ya kuchelewa kwa miradi ya nishati vijijini na haja ya wananchi kupata huduma ya umeme kwa haraka, Serikali kupitia REA na kuchukua hatua mbalimbali za kiusimamizi na ufuatiliaji ili kutatua changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa miradi hiyo. Hatua hizo ni pamoja na:

1) Kuajiri Waratibu wa miradi ya nishati vijijini kwa Wilaya zote za Tanzania Bara. Waratibu hao wana jukumu la kusimamia utekelezaji wa miradi na kutoa taarifa kwa Viongozi hususan Waheshimiwa Wabunge kuhusu maendeleo ya miradi katika Majimbo yao;
2) Kutolewa kwa kibali cha kuajiri Wahandisi 20 wa miradi ya REA, ili kuimarisha usimamizi wa miradi hiyo nchini ambapo kwa sasa taratibu za ajira zinaendelea;
3) Kununua magari 21 yatakayotumika katika usimamizi wa miradi ya REA katika mikoa mbalimbali nchini; Hotuba ya Waziri wa Nishati 42 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2023/24
4) Kuboresha vigezo vya ununuzi kwa kuweka vigezo vipya kwa wakandarasi kuomba zabuni, ikiwemo vigezo vinavyochuja wakandarasi wanaofanya vizuri katika miradi inayoendelea; na
5) Serikali kupitia REA inaandaa Muundo Mpya wa ununuzi wa wakandarasi ambao utabadilisha na kuboresha namna ya kuwapata wakandarasi kwa kutumia muundo unaoitwa "Framework Arrangement". Muundo huu utanunua wakandarasi wapya chini ya "Fixed Bugdet" (Bei Elekezi), ambapo wakandarasi watapewa wigo mdogo wa kazi na kuongezewa wigo mwingine kulingana na ubora wa utekelezaji ambapo mkandarasi anayefanya kazi vizuri na kumaliza kwa wakati ataongezewa mkataba mwingine, bila kuanza upya mchakato wa ununuzi kwa wigo mpya.

## D.5: UENDELEZAJI WA RASILIMALI YA JOTOARDHI

**118.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TGDC iliendelea na maandalizi ya Miradi ya Kimkakati ya Jotoardhi (Ngozi, Songwe, Kiejo-Mbaka, Natron na Luhoi) ambayo ni hatua mahsusi itakayowezesha kuwepo kwa uhakika na usalama wa nishati nchini kwa kuimarisha vyanzo vya kuzalisha umeme. Hatua ya

utekelezaji iliyofikiwa katika miradi iliyobainishwa hapo juu ni kama ifuatavyo:

**i) Mradi wa Jotoardhi Ngozi (Mbeya) – MW 70**

**119.** Mheshimiwa Spika, mradi huu ni kwa ajili ya uzalishaji umeme wa **MW 70** kwa kutumia Jotoardhi katika eneo la Ngozi mkoani Mbeya. Katika hatua ya awali mradi unalenga kuzalisha **MW 30** kwa gharama za **Dola za Marekani milioni 144** sawa na **Shilingi bilioni 339.** Kwa sasa, mradi umefikia katika hatua ya uhakiki ambayo inahusisha uchorongaji wa visima vitatu (3) vya uhakiki.

**120.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2023, kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha ununuzi na kuwasili nchini kwa mtambo wa kuchoronga visima (Drilling rig); kukamilisha uhuishaji wa taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; kupata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu wezeshi; kuendelea na taratibu za kuwapata Wakandarasi wa kuchoronga visima vya uhakiki; na kusaini Mkataba wa fedha za ruzuku kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Jotoardhi (Geo thermal Risk Mitigation Fund - GRMF) ulio chini ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC) wenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 2.7** sawa na **Shillingi bilioni 6.28** kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa mradi. **Kiambatisho Na. 6** kinaonesha mtambo wa kuchoronga visima vya uhakiki vya jotoardhi ambao tayari umewasili nchini.

**ii) Mradi wa Jotoardhi (Songwe) – MW 5**

**121.** Mheshimiwa Spika, mradi huu utahusisha uzalishaji umeme **MW 5** kwa kutumia jotoardhi na matumizi mengineyo (direct heat uses) kama kukausha mazao, ufugaji samaki, kilimo (green house) na kutotolesha vifaranga vya kuku. Gharama za kutekeleza mradi zinakadiliwa kuwa **Dola za Marekani milioni 32** sawa na **Shilingi bilioni 77.**

**122. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira; kuanza taaratibu za utwaaji wa ardhi kwa ajili ya utekelezaji mradi; kuendelea na ukamilishaji wa taratibu za kupata ruzuku kutoka GRMF kwa ajili ya uchorongaji wa visima virefu vinne (4); kuendelea na utekelezaji wa miradi ya majaribio ya matumizi ya moja kwa moja; kuendelea na taratibu za ununuzi wa Mkandarasi kwa ajili ya kuchoronga visima vifupi vya utafiti; na

kuanza maandalizi ya kuchoronga visima virefu kwa ajili ya kuanza uzalishaji umeme.



*Mradi wa Jotoardhi Kiejo-Mbaka (Mbeya) – MW 60*

**iii) Mradi wa Jotoardhi Kiejo-Mbaka (Mbeya) – MW60**

**123. Mheshimiwa Spika**, mradi unahusisha uzalishaji umeme wa **MW 60** na matumizi mengineyo. Katika hatua za awali, mradi unatarajiwa kuanza na uzalishaji wa **MW 10** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 75** sawa na **Shilingi bilioni 175.88.** Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; kuendelea na ukusanyaji wa taarifa za ziada za kisayansi za kijiofizikia katika eneo la mradi; kuanza tathmini ya ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za uchorongaji wa visima vya uhakiki; kuende lea na taratibu za kupata ruzuku kutoka GRMF; na kuanza taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi.

**iv) Mradi wa Jotoardhi Natron (Arusha) – MW 60**

**124. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusisha uzalishaji wa umeme kiasi cha **MW 60** kwa kutumia jotoardhi na matumizi mengineyo (direct heat uses). Utekelezaji wa mradi upo katika hatua za utafiti wa awali wa kisayansi (geoscientific surface exploration). Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 288** sawa na takriban **Shilingi bilioni 675.39.** Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina; na kuendelea na taratibu za kupata ruzuku kutoka GRMF kwa ajili ya utafiti wa kina wa kisayansi juu ya ardhi.

**v) Mradi wa Jotoardhi Luhoi (Pwani) – MW 5**

**125. Mheshimiwa Spika**, mradi huu upo katika hatua za uhakiki wa rasilimali ya jotoardhi ambayo inahusisha uchorongaji wa visima vya uhakiki katika eneo la mradi. Aidha, mradi huu utawezesha uzalishaji wa umeme wenye uwezo wa **MW 5** kwa kutumia jotoardhi na matumizi mengine. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 32** sawa na **Shilingi bilioni 77.** Hadi mwezi Aprili, 2023 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa Awali wa matumizi mengineyo; kukamilika kwa tathmini ya awali ya athari kwa mazingira; na kupatika kwa kiasi cha **Dola za Marekani million 3.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 7.5** kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Jotoardhi (GRMF). **Kiambatisho Na. 7** kinaonesha miradi ya kipaumbele ya jotoardhi na kiwango cha uzalishaji umeme kinachotarajiwa.

**D. 6: UTEKELEZAJI WA MIKAKATI NA MIPANGO MBALIMBALI YA UENDELEZAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU**

**126. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Nishati imeendelea kuandaa na kutekeleza Mipango na Mikakati mbalimbali ya kuendeleza Sekta ya Nishati. Mipango na Mikakati hiyo ni pamoja na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme (Power System Master Plan), 2020; Mkakati wa Nishati Jadi difu (Renewable Energy Strategy and Roadmap); Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati na Mpango wa Utekelezaji (EnergyEfficiency Strategy and Its Implemen tation Action Plan); na Mkakati wa Tungamotaka (Biomass Energy Strategy). Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya Mpango Kabambe wa Nishati Vijijini (Rural Energy Master Plan) unaohusisha

Mpango wa Usambazaji wa Umeme Vijijini pamoja na Mpango wa Nishati Safi ya Kupikia Vijijini. Kazi zilizo fanyika katika uandaaji wa Mipango na Mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:

**A. Uhuishaji wa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme (Power System Master Plan), 2020**

**127. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Sekta Ndogo ya umeme inaendana na maendeleo na mahitaji ya sasa ya sekta, ikiwemo matumizi ya nishati jadidifu na mahitaji halisi ya umeme, Wizara ya Nishati imepata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kazi ya kuhuisha Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme (Power System Master Plan 2020 Update).



**128. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23 Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake na wadau wengine, ilianza zoezi la uhuishaji wa Mpango huo, ikiwa ni pamoja na kuunda

Kikosi Kazi cha watalaamu wa ndani, kufanya makadirio ya mahitaji ya umeme kwa siku zijazo na kuanza ukusanyaji wa takwimu za mahitaji ya umeme kwa kila mkoa (Tanzania Bara na Visiwani). Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kuwajengea uwezo watalaamu wa Kikosi Kazi kupitia Mshauri Mwelekezi (ENGIE Impact) anayesaidia pia kazi ya kubainisha maeneo ya uwekezaji wa miradi ya nishati jadidifu na muda na kiwango cha Nishati Jadidifu (Jua na Upepo) kinacho takiwa kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Mwezi Oktoba, 2023.

**B. Mkakati wa Nishati Jadidifu na Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati (Renewable Energy Strategy and its Implementation Roadmap)**

**129.** heshimiwa Spika, ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015, Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 pamoja na mipango na mikakati mingine ya Serikali yenye lengo la kukuza mchango wa Nishati Jadidifu katika upa tikanaji wa nishati na kupunguza uharibifu wa mazingira, katika mwaka 2022/23 Wizara ilianza maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Jadidifu na Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati huo chini ya Mradi wa Tanzania Rural Energy Expansion Programme-TREEP). Mkakati huo unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya **Shilingi milioni 900** na unajumisha tafiti kuhusu upatikanaji wa maeneo ya uendelezaji wa Nishati Jadidifu na miundombinu ya kufikisha nishati hiyo kwenye gridi ya Taifa.

Hatua zilizofikiwa hadi sasa ni pamoja na kupata maoni ya wadau kuhusu masuala ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mkakati huo na Mpango wake wa utekelezaji, uandaaji wa rasimu ya kwanza ya Mkakati na kuanza tafiti za kubainisha maeneo ya uendelezaji wa miradi ya nishati jadidifu. Mkakati huu unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023.

**C. Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati na Uhuishaji wa Mpangokazi wa Matumizi Bora ya Nishati (Energy Efficiency Strategy and Update of the Energy Efficiency Action Plan)**

**130. Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 pamoja na mambo mengine, inahamasisha matumizi bora ya nishati (energy efficiency) ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, upotevu na gharama ya nishati; kutunza mazingira; kuongeza

ajira na kukuza mchango wa Sekta ya Nishati katika maendeleo ya nchi.

Mwaka 2018 Wizara ya Nishati iliandaa Mpangokazi wa Matumizi Bora ya Nishati (Energy Efficiency Action Plan) wenye maeneo makuu saba. Maeneo hayo ni uhuishaji wa Mpango na uandaaji wa Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati; uan daaji wa Viwango vya Chini vya Vifaa vya Nishati na Lebo (Minimum Energy Performance Standards (MEPS) and Labelling); uandaaji na utekelezaji wa Mfumo wa Uthibitishaji wa Viwango vya Nishati Vinavyohitajika katika Majengo Makubwa (Framework for Energy Performance Certification in Large Buildings) kwa lengo la kupunguza matumizi makubwa ya nishati; uandaaji wa mfumo sahihi wa upa tikanaji wa takwimu za matumizi ya nishati na uandaaji na utekelezaji wa Mfumo wa Utambuzi na Usimamizi wa Watumiaji Wakubwa wa Nishati (Framework for Management of Large Energy Consumers). Maeneo mengine ni kujenga uwezo wa wataalamu wa ndani kuhusu menejimenti ya Sekta ya Nishati na Ukaguzi wa Matumizi ya Nishati (Professional Qualifications and Skills in Energy Manage ment and Audit) na utoaji wa elimu ya kuhamasisha umma kuhusu matumizi bora ya nishati.

**131. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/2023 Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kupitia Mshauri Mwelekezi ilianza maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati na uhuishaji wa Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati ili kuendana na mahitaji halisi ya matumizi bora ya nishati kwa sasa. Kazi hii itagharimu takriban Shilingi milioni 170 na tayari Mshauri Mwelekezi amekamilisha rasimu ya kwanza ya Mkakati na Mpango na wadau wameanza kutoa maoni katika rasimu hiyo. Mkakati huo una tarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023.

**D. Mkakati wa Kitaifa wa Nishati ya Tungamotaka (Biomass Energy Strategy – BEST)**

**132. Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua mchango wa Nishati ya Tungamotaka katika maendeleo ya Sekta ya Nishati nchini, Serikali kupitia Wizara ya Nishati, inaandaa Mkakati wa Kitaifa wa Nishati ya Tungamotaka ili kuwa na mwongozo thabiti wa uendelezaji wa rasilimali ya tungamotoka ambayo ni endelevu na isiyokuwa na athari kubwa za kiafya na mazingira. Katika mwaka 2022/2023 Wizara ilikamilisha Hadidu za Rejea kwa ajili ya kumpata Mshauri

Mwelekezi atakayeandaa Mkakati huo pamoja na kukusanya maoni ya wadau kuhusu masuala muhimu ya kuzinga- Hotuba ya Waziri wa Nishati 47 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2023/24 tiwa katika Mkakati huo. Umoja wa Ulaya (EU) unafadhili uandaaji wa Mkakati huo unaotarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2024.

### E. Programu ya Maboresho ya Sekta ya Nishati (Energy Sector Reform Programme)

**133.** **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inalenga kuboresha utendaji wa Sekta ya Nishati ili kuimarisha mchango wa Sekta hiyo katika maendeleo ya nchi. Aidha, imelenga pia kufanikisha matokeo matatu ambayo ni (i) uboreshaji wa utendaji wa TANESCO (TANESCO Modernisation) kwa kuimarisha mfumo wa utendaji kazi, mipango ya Shirika na upatikanaji wa vitendeakazi (mitambo, mashine, mita) vyenye tija (ii) maboresho ya Sera, Mipango na Mikakati ya kuendeleza Sekta ya Nishati (iii) uim arishaji wa mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa takwimu za nishati.

**134.** Mheshimiwa Spika, Programu hii inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya kwa gharama za Euro Milioni 35 ambapo Wizara ya Nishati ni Mratibu. Taasisi nyingine zinazo husika katika utekelezaji wa Programu hiyo ni TANESCO, EWURA, NBS na REA. Awali, utekelezaji wa Programu hii ulikuwa ni wa Indirect Management ambapo mfadhili alikuwa na jukumu la kutoa fedha moja kwa moja kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za program. Hata hivyo, kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itakuwa inapokea fedha za ufadhili huo kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali (General Budget Support) na fedha zitakuwa zinatolewa kwa taasisi nufaika kwa utaratibu wa matokeo ya utekelezaji wa kazi zilizopangwa (Result Based Financing).

**135.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, programu hii itawezesha ununuzi wa vifaa muhimu vya kuboresha utendaji wa TANESCO; kujenga uwezo wa watendaji wa Wizara ya Nishati, TANESCO, EWURA, na REA pamoja na kuanza maandalizi ya utengenezaji wa mfumo sahihi wa ukusanyaji wa takwimu za nishati. Programu hii ni ya miezi 36 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025.

### F. Ukusanyaji wa Takwimu za Hali ya Upatikanaji na Matumizi ya Nishati Nchini (Energy Access and Use Situation in Tanzania Mainland)

**136.** **Mheshimiwa Spika**, ili kuwa na mipango thabiti ya upatikanaji wa nishati nchini, mwaka 2019 Serikali kupitia REA na NBS ilikusanya taarifa za hali ya upatikanaji na matumizi ya nishati Tanzania Bara iliyowezesha kuonesha ongezeko la upatikanaji wa huduma za nishati. Kwa kuwa ni muda mrefu wa takriban miaka mitatu sasa, maendeleo makubwa yamepatikana katika Sekta ya Nishati. Hivyo, ili kuweze sha kuwa na takwimu sahihi kuhusu upatikanaji wa nishati pamoja na kuwa na mipango thabiti ya kupima utendaji wa Sekta na kuongeza upatikanaji wa nishati katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma za nishati ya kisasa, Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na NBS pamoja na REA imepanga kukusanya taarifa za hali ya upatikanaji na matumizi ya nishati nchini.

## D.7: MIKAKATI MBALIMBALI YA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**137.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa watanzania wanatumia nishati safi na salama za kupikia, tarehe 1 - 2 Novemba, 2022 Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliandaa Mjadala wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia. Lengo la Mjadala huo

lilikuwa ni kutambua vikwazo, kubainisha changamoto na kupanua wigo wa upatikanaji wa teknolojia za nishati safi ya kupikia nchini.

**138.** **Mheshimiwa Spika**, Mjadala huo ulizinduliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika ufunguzi wa Mjadala huo, Mhe. Rais aliagiza kuundwa kwa Kikosi Kazi cha Kitaifa kitakachoandaa Dira ya Kitaifa ya Nishati Safi ya Kupikia itakayohakikisha kuwa asilimia 80 ya watanzania wanahamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia ndani ya kipindi cha miaka 10 pamoja na maandalizi ya Mkakati wa utekelezaji wake. Aidha, Mhe. Rais alielekeza Taasisi za Umma na Binafsi zinazolisha zaidi ya watu 300 kwa siku kuachana na matumizi ya kuni na mkaa ifikapo mwezi Januari, 2024.



*Mwananchi akitumia nishati ya kupikia ya kuni ambayo si salama kwa afya.*

**139.** Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo ya Mhe. Rais, kiliundwa Kikosi Kazi cha Kitaifa kwa ajili ya uandaaji wa Dira ya miaka kumi ya kuhamia katika nishati safi ya kupikia,

kinachojumuisha Wizara na Taasisi za Serikali zinazohusika na masuala ya Nishati Safi ya Kupikia, ambapo Wizara ya Nishati ni Sekretarieti ya Kikundi Kazi hicho. Aidha, imeundwa Kamati ya Mawaziri ya kusimamia uandaaji wa Dira hiyo chini ya uenyekiti wa Mhe. Waziri Mkuu, ambapo Waziri wa Nishati ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

**140.** Mheshimiwa Spika, Kikundi Kazi kinajumuisha Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Wizara ya Afya. Vilevile, Sekta Binafsi, Asasi Zisizokuwa za Kiserikali, Washirikia wa Maendeleo na wadau wengine wanashirikishwa katika utekelezaji wa kazi hii. Dira na Mkakati vinatarajia kuzinduliwa na kuanza kutumika mwezi Julai, 2023.

**141.** Mheshimiwa Spika, kwa sasa Timu ya Wataalamu inakamilisha Dira ya Taifa ya Nishati Safi ya Kupikia na Mpango Mkakati wa Utekelezaji (Implementation Strat egy). Aidha, rasimu ya Dira na Mkakati huo vimeshawasilishwa kwa wadau mbam bali, ikiwemo Sekta Binafsi, Asasi Zizokuwa za Kiserikali, Washirika wa Maendeleo na Watafiti, ambapo maoni yao yametumika kuboresha Dira na Mkatika husika ili kuhakikisha utekelezaji wake unaakisi hali halisi ya mahitaji. Sambamba na uan daaji wa Dira na Mkakati, Serikali imetoa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa Taasisi za umma na Binafsi zinazolisha zaidi ya watu 100 kuanzia mwezi Januari, 2024. Aidha, Taasisi hizi zitaongozwa na Dira na Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia katika kutekeleza katazo hili.

**142.** Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, inatekeleza mradi wa Integrated Approach to Sustainable Modern Cooking Solutions kwa muda wa miaka mitatu (2021 - 2024). Mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya mijini katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Pwani, Tanga na Tabora na unafadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU) kwa **Euro Milioni 30**. Mradi huu unajumuisha Mfuko wa Nishati ya Kupikia (CookFund) wenye jumla ya **Euro Milioni 17.** Fedha za Mfuko huo zinasimamiwa na United Nations Capital Development Fund (UNCDF) na lengo la mfuko huu ni kuwezesha Sekta Binafsi kuongeza usambazaji wa nishati safi ya kupikia kupitia ruzuku inayotolewa na Mfuko huu.

**143.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Desemba, 2022, Mfuko wa CookFund ulitoa jumla ya **Shilingi bilioni 3.21** kwa Kampuni 16 zinazotumia teknolojia ya nishati safi ya kupikia. Aidha, kupitia mradi huu kiasi cha **Euro milioni 4** kitatu mika katika uendelezaji wa teknolojia ya bioethanol kwa ajili ya kupikia. Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO) linasimamia utekelezaji wa mradi huu ambapo mbali na kuchangia upatikanaji wa nishati safi ya kupikia utawezesha pia kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, hususan kupitia viwanda vya sukari kwa kuchangia upatikanaji wa malighafi ya *bioethanol.*

**144.** MheshimiwaSpika, Serikali kupitia REA imeendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuwezesha Upatikanaji wa Nishati Bora na Safi ya Kupikia. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayebainisha aina ya nishati safi itakayotumika katika maeneo ya Taasisi za Umma zilikuwa zinaende lea. Wakala unakamilisha maandalizi ya mkataba na TPDC kwa ajili ya ujenzi wa

miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Pwani itakayoun ganisha wateja 980 wa awali. Vilevile, Serikali kupitia REA imetangaza fursa za usambazaji wa mitungi ya gesi kwa sekta binafsi kuwasilisha maombi yao ambapo mwisho ni tarehe 19 Mei, 2023. Wakala pia unaendelea na taratibu za kukamilisha Mwongozo wa Usambazaji wa Majiko Banifu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ambapo majiko 70,000 yatasambazwa katika maeneo ya vijiji na vijiji miji.


## SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

**145.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia na kuboresha mazingira ya uwekezaji katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia nchini katika nyanja za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, uchakati, usafirishaji na usambazaji wa bidhaa za mafuta na gesi. Kuimarika kwa uwekezaji katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia kutachochea kufikiwa kwa azma ya nchi kuingia katika uchumi wa mafuta na gesi ambao pamoja na mambo mengine, utaiingizia Serikali mapato mengi na kukuza ajira nchini.

## D.8: USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SHUGHULI ZA UTAFUTAJI NA UZALISHAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA

**146.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) iliendelea na usimamizi pamoja na udhibiti wa shughuli za uta futaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia katika Vitalu mbalimbali nchini. Aidha, PURA imeendelea kufanya kaguzi katika maeneo ya uzalishaji wa gesi asilia kwa lengo la kuhakiki ufanisi wa shughuli za uzalishaji na usalama wa mazingira. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 jumla ya kaguzi 12 zilifanyika katika Vitalu vya Songo Songo na Mnazi Bay ambapo uzalishaji wa gesi asilia unaende lea. Aidha, uzalishaji wa gesi asilia umeongezeka hadi kufikia Futi za Ujazo Bilioni 68.02 ikilinganishwa na Futi za Ujazo Bilioni 59.96 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 13. Ongezeko hilo limetokana na hatua zili zochukuliwa, za ukarabati wa visima vya uzalishaji wa gesi asilia. **Kielelezo Na. 8 kinaonesha** viwango vya uzalishaji wa gesi asilia katika Vitalu vya Mnazi Bay na Songo Songo.

### Kielelezo Na. 8: Uzalishaji wa Gesi Asilia katika Vitalu vya Mnazi Bay na Songo Songo kwa Mwaka 2021/22 na Mwaka 2022/23



*Chanzo: PURA*

**147.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia PURA inaendelea na shughuli za awali za utekelezaji wa Duru ya Tano ya Kunadi Vitalu vya utafutaji mafuta na gesi asilia kwa maeneo ya nchi kavu na baharini kwa lengo la kuongeza wawekezaji. Aidha, Ser ikali inaendelea kudurusu Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji wa Mapato (Model Production Sharing Agreement - MPSA) wa mwaka 2013 ili kuwa na MPSA mpya inayoendana na mazingira ya sasa. Vilevile, Serikali kupitia PURA inaende lea kuweka mipaka ya Vitalu vitakavyonadiwa na kuandaa Vifurushi vya Data (Data Packages) kwa kila Kitalu. Aidha, hadi sasa Vitalu 26 vinafanyiwa uchambuzi ili kupendekezwa kwa ajili ya kuingizwa katika mnada. Kati ya hivyo, Vitalu 15 vipo nchi kavu na 11 vinapatikana baharini. Serikali inatarajia kuzindua zoezi la kunadi Vitalu (Lauching of Licensing Round) kati ya mwezi Desemba, 2023 hadi Machi, 2024 baada ya kukamilika kwa shughuli za maandalizi zinazoendelea.

**148.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia PURA imekamilisha maandalizi ya rasimu ya Ramani ya Kidijitali (Interactive Digital Petroleum Reference Map) kwenye Mfumo wa Taarifa wa Kijiografia (Geographical Information System – GIS). Ramani hiyo iliyopo kwenye mfumo wa kielektroniki itatoa taarifa za Vitalu vya utafutaji na uzal ishaji wa mafuta na gesi asilia nchini na inatarajiwa kuanza kutumika rasmi mwezi Juni, 2023.

## D.9: MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

### i) Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini

**149. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC iliendelea na utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini kilichopo baharini, Kusini Mashariki mwa Tanzania. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha kazi za kupitia na kutafsiri taarifa za kijiolojia na kijiofizikia; kukamilika kwa muundo na mpango wa uchorongaji wa kisima cha utafutaji na kuendelea na taratibu za kumpata Mbia wa Kimkakati (Strategic Partner) kwa ajili ya uchorongaji wa kisima.

#### ii) Kitalu cha Eyasi– Wembere

**150.** Mheshimiwa Spika, Kitalu cha Eyasi - Wembere kipo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi anayetarajiwa kuanza kazi ya kukusanya na kuchakata data za mitetemo za mfumo wa 2D urefu wa kilomita 260 inayotarajiwa kuanza mwezi Juni 2023; kukamilika kwa kazi ya kuchakata sampuli za kijiokemia zilizo chukuliwa ili kuangalia viashiria vya uwepo wa mafuta ambapo tafsiri ya sampuli inaendelea na kutolewa kwa kibali cha kufanya utafiti wa awali (reconnaissance permit). Kwa sasa, zoezi la uelimishaji wananchi kwa ajili ya kuwaandaa na kazi ya ukusanyaji wa taarifa za mitetemo ya mfumo wa 2D inaendelea.

**iii)** Kitalu cha Songo Songo Magharibi

**151.** Mheshimiwa Spika, Kitalu hiki kipo katika kina kifupi cha bahari, Magharibi mwa Kitalu cha Uzalishaji cha Songo Songo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi iliyotekelezwa ni kupitia na kutafsiri taarifa za kijiolojia na kijiofizikia zilizopatikana miaka ya nyuma.

**iv)** Kitalu cha Ziwa Tanganyika

**152.** MheshimiwaSpika, Kitalu hiki kipo eneo la Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa moduli za data za usumaku na uvutano (Full Tensor Gravity - FTG) katika mfumo wa 3D; kukamilika kwa ukusanyaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D za ziada (infill 2D seismic acquisition plan) na kuendelea na taratibu za kumpata Mbia wa Kim kakati atakayeshirikiana na TPDC katika kuendeleza Kitalu.

**v) Vitalu Namba 4/1B na 4/1C**

**153.** MheshimiwaSpika, Vitalu namba 4/1B na 4/1C vipo kwenye kina kirefu cha Bahari Kuu. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Serikali kupitia TPDC imekamilisha nyaraka kwa ajili ya kumpata Mbia wa Kimkakati na kuandaa Moduli ya Kiuchumi. Aidha, Wizara ya Nishati imetoa Tangazo katika Gazeti la Serikali kwa hatua za kuvimiliki sha Vitalu hivyo kwa TPDC kwa mujibu wa Kifungu cha 50(3) cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015.

**154.** MheshimiwaSpika, Serikali kupitia TPDC na Mkandarasi imeendelea na utafutaji wa mafuta na gesi katika Kitalu cha Ruvu kilichopo katika Mkoa wa Pwani ambacho kina takriban Futi za Ujazo Trilioni 2.17. Jitihada za uhakiki zinaendelea ili kubaini kiasi ambacho kinaweza kuvunwa kwa faida ili kuweka mipango ya uendelezaji wa Kitalu hicho. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 data za mitetemo za aina ya 3D zilikuwa zimekusanywa na kubainisha maeneo ya kuchoronga visima vya utafutaji na uhakiki. Uendelezaji wa gesi asilia katika Kitalu hicho utawezesha upatikanaji wa gesi asilia kwa matumizi mbalimbali, ikiwemo viwanda vilivyopo na vinavyoendelea kujengwa katika Mkoa wa Pwani na maeneo mengine ya jirani.

**vi) Kitalu chaKilosa-Kilombero**

**155. Mheshimiwa Spika**, Kitalu cha Kilosa - Kilombero kinapatikana katika eneo la nchi kavu katika Mkoa wa Morogoro ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kibali cha kutumia maji ya

Mto Rufiji kilikuwa kimepatikana na taratibu za kumpata mkan darasi ili kuhuisha cheti cha mazingira zilikuwa zinaendelea. Aidha, kutokana na changamoto za kifedha zinazoikabili kampuni inayohusika katika Kitalu hiki, ambapo kwa sasa ipo chini ya mufilisi, Serikali kupitia TPDC inafanya taratibu za talu hicho katika umiliki wake ili kupanga namna nyingine ya uendelezaji wake.

**D.10: MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI KATIKA VITALU BINAFSI**

**156. Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuvutia uwekezaji wa Sekta Binafsi kwenye utafutaji wa mafuta na gesi asilia, mwezi Agosti, 2022 Serikali kupitia Wizara ya Nishati ilitoa nyongeza ya muda wa leseni ya utafutaji awamu ya pili kwa Kitalu cha Tanga. Aidha, Mwendeshaji wa Kitalu hicho anaendelea na shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia, ikiwemo kuchakata na kutafsiri upya data za mitetemo za mfumo wa 3D za zamani pamoja na kuandaa mpango wa uchorongaji wa kisima cha utafutaji.

**D.11: MIRADI YA UENDELEZAJI, UZALISHAJI NA USAFIRISHAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA**

**i) Kitalu cha Ruvuma (Ntorya)**

**157. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TPDC imeendelea na jitihada mbalimbali zenye lengo la kuongeza upatikanaji wa gesi asilia nchini ambapo Serikali, TPDC na mwekezaji wa Kitalu cha Ruvuma ambacho kina takriban Futi za Ujazo Trilioni 1.6 wamekamilisha majadiliano na kusaini Mkataba wa Nyongeza wa Gesi Asilia (Gas Addendum) tarehe 25 Novemba, 2022. Uendelezaji wa gesi asilia katika Kitalu hicho utawezesha kupatikana kwa futi za ujazo takriban milioni 40 hadi 60 kwa siku kwa kuanzia na takriban futi za ujazo milioni 140 kwa siku wakati uzalishaji wa juu (full field production) utakapofikiwa.

**158.** Mheshimiwa Spika, Majadiliano ya Mkataba wa Mauziano ya Gesi (Gas Sales Agreement - GSA) baina ya TPDC na mwekezaji yapo katika hatua za mwisho. Aidha, TPDC kwa kushirikiana na mwekezaji wanaendelea na maandalizi ya ujenzi wa bomba la urefu wa kilomita 35 kutoka Ntorya hadi kwenye kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Madimba. Kwa sasa, Serikali imekamilisha uthamini wa mali za wananchi watakaofidiwa kupisha mkuza wa bomba hilo ambapo wananchi

255 wamelipwa fidia. Vilevile, TPDC na mwekezaji wanaendelea kukamilisha Mpango wa Uendelezaji (Development Plan) wa gesi hiyo ambao utawezesha uzalishaji wa gesi kutoka katika Kitalu cha Ntorya ifikapo mwishoni mwa mwaka 2024.

**ii) Mradi waKuchakata naKusindika Gesi Asilia (Liquefied Natural Gas – LNG)**

**159. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unalenga kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu namba 1, 2 na 4 vilivyopo katika kina kirefu cha bahari ili kuwa kim  iminika kwa ajili ya kuuzwa katika masoko ya kimataifa. Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili; Mkondo wa Juu ambao utatekelezwa katika eneo la Mtwara na Mkondo wa Kati ambao utatekelezwa katika eneo la Likong'o Mkoani Lindi. Mradi unakadiriwa kuwa wa thamani ya Dola za Marekani bilioni 42.00 sawa na takriban Shilingi trilioni 98.7, ukijumuisha uwekezaji katika Mkondo wa Juu wa Dola za Marekani bilioni 26 sawa na takriban Shilingi trilioni 61.1 na uwekezaji katika Mkondo wa Kati wa Dola za Marekani bilioni 16 sawa na takriban Shilingi trilioni 37.6. Manufaa ya mradi huu ni pamoja na kuimarika kwa mapato ya Serikali yatakayotokana na mauzo ya gesi kwa mujibu wa Mkataba wa Uzalishaji na Uga wanywaji Mapato (PSA) baina ya Serikali na Wawekezaji kupitia mrabaha, mgao wa faida wa Serikali, tozo mbali mbali pamoja na kodi.

**160. Mheshimiwa Spika**, manufaa mengine ya moja kwa moja ya mradi huu ni kuongeza uzalishaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya ndani (Domestic Supply Obligation-DSO) na kuimarika kwa Kampuni ya Taifa ya Mafuta (TPDC) kupitia ushiriki wake kama sehemu ya wabia wa mradi huu. Aidha, mradi huu utazalisha ajira nyingi kwa wananchi kuanzia kipindi cha ujenzi mpaka uendeshaji; kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa kupitia sekta mbalimbali; kuongezeka kwa fedha za kigeni kupitia mauzo ya gesi nje ya nchi, kuongeza watalamu katika shughuli za gesi na mafuta kupitia ushiriki wa wazawa na kuchochea ukuaji na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, madaraja, viwanja vya ndege, vituo vya afya, bandari, mawasiliano ya simu, shule, maji na umeme. Mradi huu pia utaiongezea nchi kipimo

cha uaminifu kwa wawekezaji (investor confidence) na hivyo kuvutia uwekezaji zaidi kutoka nje ya nchi.

**161. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha majadiliano ya Mkataba wa Nchi Hodhi na Mkataba (Host Government Agreement-HGA) wa Uzalishaji na Ugawanywaji Mapato (PSA), baina ya Timu ya Majadiliano ya Serikali (GNT) na Wawekezaji katika Vitalu husika. Aidha, kwa sasa GNT ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mikataba ya ziada ya ulinzi na utumiaji wa miundombinu ya bandari inayotarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2023. Itakumbukwa kuwa, majadiliano haya yalianza rasmi mwezi Septemba, 2016 na yamekuwa yakifanyika na kuvunjika kwa vipindi tofauti katika kipindi cha takriban miaka saba. Aidha, Wawekezaji wa Mradi wa LNG na Serikali wanatarajia kusaini Mkataba wa Nchi Hodhi na Mkataba wa Ugawanaji Mapato (Amended Production Sharing Agreement – PSA) mwezi Juni, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, kwa kuzingatia ukubwa na upekee wa mradi huu, na ikiwa ni hatua ya kuhakikisha mradi unaratibiwa, kufuatiliwa na kuwezeshwa kwa tija na ufanisi ili manufaa yake yapatikane kwa wakati na kama ilivyokusudiwa, Serikali imeanzisha Ofisi Mahsusi ya Mradi huu, chini ya Wizara ya Nishati.

## D.12: Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji wa Gesi Asilia

### i) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani

**162. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC imeendelea na utekelezaji wa ujenzi wa vituo vitatu vya Kukandamiza Gesi Asilia (Compressed Natural Gas [CNG]) katika Mikoa ya Dar es Salaam (2) na Pwani (1) ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa usanifu wa mradi na Tathmini ya Athari kwa Mazingira pamoja na kupatikana kwa Mkandarasi wa ujenzi. Kazi ya ujenzi wa vituo hivyo inatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2023. Aidha, Kampuni ya Taqa Dalbit imeendelea na ujenzi wa vituo viwili (2) vya CNG, kimoja maeneo ya uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, mkabala na Terminal III

na kingine katika uwanja wa Posta uliopo barabara ya Sam Nujoma mkoani Dar es Salaam.

**163. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC iliendelea na ujenzi wa bomba la usambazaji wa gesi asilia lenye urefu wa kilomita 12.4 kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach kupitia barabara ya Bagamoyo ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 ujenzi ulifikia **asilimia 44.2** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023. Aidha, TPDC imeendelea na ujenzi wa bomba la kusambaza gesi katika maeneo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) na Mlimani City. Kupitia mradi huu, migahawa mitatu (3) na maabara moja (1) katika chuo cha DUCE pamoja na migahawa kumi na mbili (12) iliyopo Mlimani City Mall itaunganishwa.

## ii) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara

**164. Mheshimiwa Spika**,Serikali kupitia TPDC imeendelea na utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa sasa kazi zinazoen delea ni pamoja na ujenzi wa mtambo mkubwa wa kupunguza msukumo wa gesi (Mother Pressure Reduction System – MPRS) karibu na valvu namba tatu katika bomba kubwa la gesi kutoka Mtwara, ujenzi wa njia ya umeme yenye urefu wa kilo mita 3.8 kutoka makutano ya Mahumbika hadi kinapojengwa Kituo cha Kupunguza Msukumo wa Gesi (MPRS) na ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka valvu namba tatu (BVS 3) kuelekea Kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo mkoani Lindi. Utekelezaji wa kazi zote hizi umefikia asilimia 60 na kwa ujumla mradi wote unatarajiwa kuka milika mwezi Juni, 2023. Kukamilika kwa bomba hili kutawezesha nyumba 209 za awali zilizounganishwa na miundombinu ya gesi asilia kutumia gesi hiyo.



**iii) Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia Nchini kwa Ufadhili wa Mfuko wa Nishati Vijijini Unaosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini(REA)**

**165.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Usambazaji Gesi Asilia Vijijini kupitia TPDC kwa kushirikiana na REA. Kwa kuanzia, mradi huu utaunganisha nyumba 451 katika Mkoa wa Lindi pamoja na nyumba 529 katika Mkoa wa Pwani na Mkataba kati ya TPDC na REA kuhusu taratibu za utoaji fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, upo katika hatua za kusainiwa. Aidha, Serikali kupitia REA imetenga **Shilingi bilioni 6.8** kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa kazi hiyo.

**v) Ujenzi wa Mradi wa Vituo vya CNG katika Bohari za Dar es Salaam na Dodoma**

**166. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC imeendelea na taratibu zitakazoweze sha ujenzi wa vituo vya CNG katika bohari za Serikali zilizopo katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Nishati, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, TPDC, GPSA, TIC na TEMESA imeundwa na kupatiwa Hadidu za Rejea za kuhaki kisha mradi huu unatekelezwa haraka iwezekanavyo. Aidha, ujenzi wa vituo hivi utawezesha magari ya Serikali na binafsi kutumia gesi asilia katika magari. Katika kuongeza zaidi kasi ya ujenzi wa vituo vya kujazia gesi katika magari (CNG Vehicles Stations), Serikali imeshatoa vibali zaidi ya 20 kwa Kampuni binafsi kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo na miradi ya usambazaji wa gesi asilia nchini.

**v) Mradi wa Bomba laKusafirisha Gesi AsiliaKutoka Tanzania hadi Uganda**

**167. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda ziliendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Tanzania hadi Uganda. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Kamati ya Pamoja ya Wataalamu ilikamilisha uandaaji wa nyaraka muhimu za kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi. Nyaraka hizo zinajumuisha Bilateral Agreement, Joint Procurement Rules na Terms of Reference (ToR) ambapo kwa sasa nyaraka hizo zinafanyiwa maboresho kwa kuzingatia maoni ya wadau kabla ya kusainiwa.

**vi) Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Mombasa (Kenya)**

**168. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya ziliendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kusafir isha Gesi Asilia Kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Mombasa (Kenya). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Kamati ya Pamoja ya Wataalamu ilikamilisha uandaaji wa nyaraka muhimu za kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi.

Nyaraka hizo zinajumuisha Bilateral Agreement, Joint Procure ment Rules na Term of Reference (ToR) ambapo kwa sasa nyaraka hizo zinafanyiwa maboresho kwa kuzingatia maoni ya wadau kabla ya kusainiwa.

**D.13: MIRADI YA KUHIFADHI NA KUSAFIRISHA MAFUTA**
**i) Mradi wa Bomba laKusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline - EACOP)**

**169. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi (crude oil) kutoka Hoima-Kabaale nchini Uganda hadi Chongoleani-Tanga nchini Tanzania likiwa na urefu wa kilomita 1,443 ambapo kati yake kilomita 306 zitakuwa Uganda na kilomita 1,137 zitapita Tanzania. Kwa upande wa Tanzania Bomba litapita katika Mikoa 8 na Wilaya 24. Mikoa hiyo ni Kagera, Geita, Shin yanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi ni pamoja na kukamilika kwa malipo ya fidia kwa wananchi 387 kati ya 388 waliopisha maeneo 14 ya ujenzi wa kambi zitakazotumika wakati wa ujenzi wa bomba. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 wananchi 9,325 kati ya 9,508 wanaopisha eneo la mkuza wa bomba walisaini mikataba ya fidia na 9,024 walilipwa fidia zao na taratibu za malipo kwa waliobaki zinaendelea.

**170. Mheshimiwa Spika,** hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuendelea na ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa kupasha joto mabomba (thermal insulation plant) inayojengwa katika kijiji cha Sojo, Nzega Tabora ambao umefikia **asilimia 87.** Aidha, tarehe 21 Februari, 2023, Serikali kupitia EWURA ilikabidhi Kibali cha Ujenzi wa mradi ikiwa ni hatua muhimu katika maandalizi ya kuanza ujenzi wa Mradi mnamo mwezi Juni, 2023. Vilevile, elimu kuhusu manufaa na fursa zitokanazo na mradi imeendelea kutolewa katika mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. **Kiambatisho Na.8** kinaonesha ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa kupasha joto mabomba (thermal insulation plant) katika Kijiji cha Sojo wilayani Nzega.

**ii) Mradi wa Bomba la TAZAMA**

**171. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari, 2023 bomba la TAZAMA lilianza kusafirisha mafuta ya dizeli badala ya mafuta ghafi. Katika kusimamia usalama wa usafirishaji wa mafuta kupitia bomba la TAZAMA, mwezi Desemba, 2022 viongozi wa juu wa Serikali za Tanzania na Zambia walikutana na kufanya vikao vya kutafuta namna bora ya kuimarisha ulinzi na usalama wa bomba ambapo tayari ndege zisizo na rubani (drones) zimenunuliwa, doria za polisi zinaendelea na mikataba na wanavijiji imeingiwa ili kuimarisha usalama na ulinzi shirikishi katika mradi huo.

**iii) Mradi wa Uanzishwaji wa Hifadhi yaKimkakati ya Mafuta (SPR)**

**172. Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuhakikisha usalama na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta nchini pamoja na nchi jirani (Petroleum hub), tarehe 27 Januari, 2023 Serikali kupitia Wizara ya Nishati ilisaini MoU na Kampuni ya ENOC LLC ya Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikubwa cha kupokea na kuhifadhi mafuta jijini Dar es Salaam. Hatua hiyo itawezesha nchi kuwa na akiba ya mafuta muda wote na hivyo kutokuathiriwa kwa shughuli za kiuchumi. Eneo limeshapatikana kwa ajili ya ujenzi na Serikali ilishaunda Kikosi Kazi kinachosimamia utekelezaji wa mkataba wa majadiliano kati ya Serikali na Kampuni ya ENOC LLC.

**D.14: MRADI WA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA RASILIMALI ZA ASILI TANZANIA**

**173. Mheshimiwa Spika**, mradi huuunatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo Afrika AfDB)) ambapo Wizara na Taasisi nufaika za mradi ni pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Nishati, TPDC, TPA, PURA, ZURA, EWURA, NEEC, TRA, na ZRB. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kununua na kusimika midaki (scanners) miwili katika Bandari ya Dar es Salaam; kununua na kusimika vifaa vya kutunza takwimu za utafiti wa mafuta na gesi; kuandaa kanzidata ya watoa huduma katika Tasnia ya Uziduaji; mafunzo kwa watumishi 330; ununuzi na usimikaji wa miundombinu ya mfumo wa uondoshaji shehena mipakani; na kuwezesha tafiti mbalimbali kufanyika kwa taasisi husika.

**174. Mheshimiwa Spika,** manufaa yatokanayo na mradi huu ni pamoja na kuboreka na kuimarika kwa ukaguzi wa mizigo inayoingia na kutoka nchini kupitia Bandari ya Dar es Salaam; kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato kufuatia matumizi ya vifaa na mafunzo yaliyowezeshwa na mradi kwa Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA); na kuimarika kwa shughuli za usimamizi wa shughuli za uchimbaji wa mafuta na gesi asilia nchini ikiwemo uchakataji wa taarifa za mitetemo kupitia watalaam wazawa.

## D.15: SHUGHULI ZA KAMPUNI TANZU ZA TPDC

### Ushiriki wa TPDC Katika Biashara ya MafutaKupitia TANOIL

**175. Mheshimiwa Spika,** TPDC kupitia kampuni yake Tanzu ya TANOIL iliendelea kushiriki katika biashara ya bidhaa za mafuta ya petroli nchini. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kiasi cha bidhaa za mafuta kilichoagizwa kilikuwa lita 120,846,346 ambapo mafuta ya Dizeli yalikuwa lita 68,173,937 na Petroli lita 52,672,409. Aidha, TANOIL imeendelea na ujenzi wa vituo vya mafuta ambapo Mkandarasi amekabidhiwa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo viwili (2) vya mafuta katika mikoa ya Geita na Singida. Vilevile, TANOIL imeendelea kutafuta Wabia watakaoshirikiana nao katika biashara ya mafuta.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha TANOIL, Serikali ilielekeza kufanyika kwa ukaguzi maalum wa kampuni hiyo na kubaini changamoto mbalimbali za kiutendaji na kibiashara na tayari imechukua hatua kadhaa za kurekebisha changamoto hizo.

**176.** Mheshimiwa Spika, TPDC kupitia kampuni yake Tanzu ya GASCO imeendelea kuendesha na kukarabati miundombinu ya Taifa ya Gesi Asilia Nchini (National Natural Gas Infrastructures - NNGI) inayohusisha viwanda viwili vya kuchakata gesi asilia vilivyopo Madimba mkoani Mtwara na Songo Songo mkoani Lindi pamoja na bomba la kusafirisha gesi kutoka Songo Songo na Madimba hadi Dar es Salaam kwa kutumia wataalamu wa ndani wa Shirika bila kutokea kwa chan gamoto yoyote kubwa iliyosimamisha shughuli hizo. Aidha, Shirika limeendelea kushirikisha vijiji vinavyopitiwa na miundombinu pamoja na Jeshi la Polisi kuhakikisha usalama wa miundombinu hiyo.

**177. Mheshimiwa** Spika, kampuni ya GASCO pia imekuwa ikijihusisha na shughuli za ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi mbalim bali nchini. Katika mwaka 2022/23, Kampuni ilipewa kandarasi ya kuunganisha kiwanda cha Saphire kilichopo Mkuranga mkoani Pwani na matumizi ya gesi asilia ambapo hadi kufikia Aprili 2023, ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 35%** na unatarajia kukamilika mwezi Juni 2023.

**D.16: Hali ya Uagizaji na Upatikanaji wa Bidhaa za Mafuta ya Petroli Nchini**


**178. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutumia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Bulk Procurement System - BPS) katika uagizaji bidhaa za mafuta ya petroli nchini tangu ulipoanza kutumika rasmi mwezi Januari, 2012. Manufaa ya kutumia mfumo huu katika uagizaji wa mafuta yamekuwa yakionekana bayana kwa sababu imewezesha nchi kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli wakati wote na kwa bei stahimilivu hata katika nyakati za majanga ya kidunia na vipindi vya migogoro ya kidiplomasia. Aidha, mfumo huu pia umewezesha upa tikanaji wa takwimu sahihi za bidhaa za mafuta ya petroli yanayoingia nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi na yale yanayopita kwenda nchi jirani. Vilevile, mfumo umesaidia kurahisisha udhibiti wa ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli yanayoingia nchini.

**179.** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, jumla ya lita bilioni 6.57 za bidhaa za mafuta ya petroli ziliingizwa nchini kwa kutumia BPS kupitia Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 2.24 ikilinganishwa na lita bilioni 6.43 zilizoingizwa Julai, 2021 hadi Aprili, 2022. Katika mafuta hayo yaliyoingizwa mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 lita bilioni 3.21 sawa na asilimia 48.8 yalikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na lita bilioni 3.36 sawa na asilimia 51.2 yalikuwa kwa ajili ya nchi jirani. Kielelezo Na. 9 kinaonesha jumla ya kiasi cha mafuta kilichoingizwa kwa kila aina ya mafuta kwa kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023. Kielelezo Na.10 kinaonesha jumla ya kiasi cha mafuta kilichoingizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje katika kipindi hicho. Aidha, katika kipindi cha miaka nane (2015 hadi 2022) kiasi cha mafuta kilichoingizwa nchini kimeendelea kuongezeka kutoka wastani wa tani 350,000

kwa mwezi hadi tani 550,000 kwa mwezi katika mwaka 2015 na 2022 mtawalia; Kielelezo Na.11 kinaonesha mwenendo wa mafuta yaliyoingizwa nchini katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2022.


**Kielelezo Na.9: Jumla ya Kiasi cha Bidhaa za Mafuta Kilichoagizwa kwa Kipindi cha Julai,2022 hadi Aprili, 2023 katika Lita Bilioni**

| AINA YA MAFUTA | LITA BILIONI | ASILIMIA |
|---|---|---|
| DIZELI | 4.06 | 62% |
| PETROLI | 2.14 | 33% |
| MAFT. YA NDEGE/ TAA | 0.36 | 5% |
| JUMLA | 6.57 | 100% |





*Chanzo: PBPA*

**Kielelezo Na. 10: Jumla ya Kiasi cha Mafuta Kilichoingizwa kwa Ajili ya Matumizi ya Ndani na Nje ya Nchi**




*Chanzo: PBPA*

**Kielelezo Na. 11: Mwenendo wa Mafuta Yaliyoingizwa Nchini katika Kipindi cha Kuanzia Mwaka 2015 Hadi 2022**




*Chanzo: PBPA*

**180. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho jumla ya zabuni 92 zilitolewa kupitia zabuni shindanishi za kimataifa zinazofanyika kila mwezi, hii ni sawa na takriban zabuni 9 kwa kila mwezi. Aidha, jumla ya wazabuni saba (7) walishiriki na kush- inda zabuni hizo kwa nyakati tofauti. Wazabuni hushindanishwa katika gharama za uletaji mafuta nchini *(premium)*.

**181. Mheshimiwa Spika,** wastani wa gharama za kuleta mafuta nchini *(weighted average premium)* katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili 2023 zilikuwa ni **Dola za Marekani 132.89** kwa tani ambapo katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22, gharama hiyo ilikuwa ni **Dola za Marekani 32.21.** Gharama hizi za uletaji zimeongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na athari zinazotokana na vita ya Urusi na Ukraine ambavyo vimesababisha upungufu wa meli zinazobeba mafuta katika soko la dunia hali ambayo imesababisha kuongezeka kwa gharama za usafirishaji pamoja na gharama za *demurrage*. Vilevile, gharama za bima kwa meli za mafuta zimeongezeka kutokana na hofu za kiusalama.

**182. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mpito kuelekea uwekezaji wa miundombinu ya kupokea mafuta kwa pamoja, Serikali imeendelea

kutumia miundombinu ya Kampuni ya TIPER kama Kituo cha Kupokea Mafuta kwa Pamoja *(Single Receive- ing Terminal - SRT)* ambapo kila mwezi meli moja ya mafuta ya dizeli hupokelewa ambayo hata hivyo hayatoshelezi mahitaji kwa kuwa meli za mafuta ya dizeli zin- azoingia katika mwezi ni mbili (2) hadi nne (4). Kwa sasa, TIPER ina uwezo wa kuhifadhi jumla ya **lita milioni 253.65** na inaendelea na ujenzi wa matenki mawili yenye ukubwa wa **lita milioni 30** kila moja ili kuongeza uwezo wa kupokea na kuhifadhi mafuta na ujenzi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2023. Vilevile, TIPER inaendelea kusimika pampu za kuhamisha mafuta zenye uwezo wa kusukuma lita 800,000 kwa saa ili kuongeza kasi ya kuhamisha mafuta kwenda kwenye maghala ya Kampuni za Mafuta (OMCs).

**183. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TPA na PBPA imeendelea kuwekeza katika mifumo na vifaa vya udhibiti wakati wa upakuaji mafuta kutoka kwenye meli ili kupunguza upotevu ambao hubebwa na Wafanyabiashara ya Jumla ya Mafuta (OMCs). Serikali kupitia PBPA imekamilisha taratibu za kuwapata Wakandarasi wawili wa kusimika mfumo wa kielektroniki (SCADA) utakaosoma mita (flowmeter) zote zinazopima mafuta wakati wote. Wakandarasi hao wawili ambao ni TTCL na Giza Systems ya Misri walianza kazi mwezi Januari, 2022 na mwezi Septemba, 2022 mtawalia. Usimikaji wa mfumo huu unatarajiwa kukamilika Septemba, 2023. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari inaendelea na usimikaji wa mita za kupima dizeli inayopokelewa kutoka kwenye boya (Single Point Mooring - SPM) kupitia Kigamboni na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2023.

### D.17: MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA


**184. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, wastani wa bei ya mafuta ghafi katika Soko la Dunia ilikuwa Dola za Marekani 88.51 kwa pipa ikilinganishwa na wastani wa Dola za Marekani 85.68 kwa pipa kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Kuongezeka kwa bei kulitokana na mgogoro wa kivita kati ya nchi za Urusi na Ukraine ambao ulisa babisha upungufu wa mafuta katika Soko la Dunia. Kielelezo Na. 12 kinaonesha Mwenendo wa Bei ya Mafuta Ghafi mwaka 2021/22 na 2022/23.

| Mwezi | 2021/22 (DOLA/PIPA) | 2022/23 (DOLA/PIPA) |
|---|---:|---:|
| Julai | 74.25 | 105.15 |
| Agosti | 70.38 | 97.93 |
| Septemba | 74.88 | 90.85 |
| Oktoba | 83.71 | 93.30 |
| Novemba | 80.85 | 86.89 |
| Desemba | 74.80 | 81.68 |
| Januari | 85.57 | 82.50 |
| Februari | 94.10 | 82.59 |
| Machi | 112.46 | 78.43 |
| Aprili | 105.81 | 85.81 |
| **Wastani** | **85.68** | **88.51** |

*Chanzo: EWURA*

**185. Mheshimiwa Spika,** kuongezeka kwa bei ya mafuta ghafi katika Soko la Dunia kwa mwaka 2022/23 kulisababisha kuongezeka kwa bei ya mafuta yaliyosafishwa ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, wastani wa bei ya mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia ilikuwa Dola za Marekani 792, 881 na 891 kwa tani kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa/ndege mtawalia, ikilinganishwa na wastani wa Dola za Marekani 825, 751 na 748 kwa tani kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 15 na 16 kwa mafuta ya dizeli na mafuta ya taa/ndege mtawalia. Aidha, kwa upande wa mafuta ya petroli bei za mafuta hayo zilipungua kwa asilimia 4. **Kielelezo Na. 13** kinaonesha Mwenendo wa Bei za Mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia kwa Mwaka 2021/22 na 2022/23.

**Kielelezo Na. 13: Mwenendo wa Bei za Mafuta Yaliyosafishwa katika Soko la Dunia kwa Mwaka 2021/22 na 2022/23**




*Chanzo: EWURA*

**D.18: MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

**186. Mheshimiwa Spika,** kupanda kwa bei za mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia kuliathiri pia bei za mafuta katika soko la ndani hapa nchini. Mathalam, wastani wa bei za mafuta kwa Mkoa wa Dar es Salaam kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 kwa lita moja ilikuwa petroli Shilingi 2,958, dizeli Shilingi 3,135 na mafuta ya taa Shilingi 3,247 ikilinganishwa na wastani wa bei za mafuta hayo kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22 ambapo zilikuwa petroli Shilingi 2,510, dizeli Shilingi 2,352 na mafuta ya taa Shilingi 2,265 sawa na ongezeko la asilimia 15, 25 na 30 mtawalia.

**187. Mheshimiwa Spika**, kutokana na kupanda kwa kasi kwa bei za mafuta katika soko la ndani, Serikali chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ilianza kuweka ruzuku kwenye bei za bidhaa muhimu za mafuta ambazo ni petroli na dizeli ili kuleta unafuu wa bei kwa wananchi hadi pale mafuta yalipoanza kuwa na bei stahimilivu. Kiwango cha ruzuku kilichotolewa na Serikali kuanzia mwezi Juni hadi Desemba, 2022 ni Shilingi bilioni 479.37. Kwa upande wa mafuta yaliyoshushwa kupitia Bandari ya Dar es salaam kuanzia mwezi Julai hadi Desemba, 2022, kiwango cha ruzuku kilikuwa kati ya Shilingi 80 hadi 277 kwa lita kwa mafuta ya petroli na Shilingi 83 hadi 412 kwa kila lita ya mafuta ya dizeli.


**188. Mheshimiwa Spika**, wastani wa bei za mafuta zenye ruzuku katika kipindi hiki kwa mafuta ya petroli ilikuwa Shilingi 3,074 kwa lita na kwa upande wa dizeli ni Shilingi 3,162 kwa lita ikilinganishwa na wastani wa bei zisizokuwa na ruzuku ambazo kwa petroli ni Shilingi 3,238 kwa lita na kwa dizeli ni Shilingi 3,415 kwa lita sawa na wastani wa punguzo la Shilingi 164 kwa kila lita ya petroli na Shilingi 253 kwa kila lita ya dizeli. Kielelezo Na. 14 kinaonesha wastani wa Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soko la Ndani kwa Mwaka 2022/23na Kielelezo Na. 15 (A&B) kinaonesha mlinganisho wa bei za mafuta ya petroli na dizeli zenye ruzuku na zisizo na ruzuku.


**Kielelezo Na. 14: Wastani wa Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soko la Ndani kwa Mwaka 2022/23**

| Mwezi | Bei ya Petroli Bila Ruzuku (Sh./Lita) | Bei ya Petroli yenye Ruzuku (Sh./Lita) | Ruzuku ya Petroli (Sh./Lita) | Bei ya Dizeli Bila Ruzuku (Sh./Lita) | Bei ya Dizeli yenye Ruzuku (Sh./Lita) | Ruzuku ya Dizeli (Sh./ Lita) | Mafuta ya Taa (Sh./ Lita) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Julai-22 | 3,497 | 3,220 | 277 | 3,510 | 3,143 | 367 | 3,442 |
| Agosti-22 | 3,630 | 3,410 | 220 | 3,734 | 3,322 | 412 | 3,765 |
| Septemba-22 | 3,049 | 2,969 | 80 | 3,359 | 3,125 | 234 | 3,335 |
| Oktoba-22 | 3,019 | 2,886 | 133 | 3,358 | 3,083 | 275 | 3,275 |
| Novemba-22 | 2,996 | 2,886 | 110 | 3,197 | 3,052 | 145 | 3,111 |
| Desemba-22 | 2,827 | 2,827 | - | 3,330 | 3,247 | 83 | 3,252 |
| Januari-23 | 2,819 | 2,819 | - | 3,295 | 3,295 | - | 3,203 |
| Februari-23 | 2,819 | 2,819 | - | 3,105 | 3,105 | - | 3,061 |

*Chanzo: EWURA*

**Kielelezo Na. 15(A&B): Mlinganisho wa Bei za Mafuta Zisizo na Ruzuku na Zenye Ruzuku Kuanzia Julai hadi Desemba 2022**






*Chanzo: EWURA*

**D.19: UDHIBITI WA MASUALA YA NISHATI KUPITIA EWURA**
**D.19.1: USIMAMIZI WA UBORA WA VITUO VYA MAFUTA**

**189. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia ubora wa ujenzi wa vituo vya mafuta ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za mafuta katika maeneo yote nchini. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kulikuwa na jumla ya vituo vya mafuta 2,306 vyenye leseni na vinavyotimiza vigezo vya ubora na usalama ikilinganishwa na vituo 2,063 vilivyokuwepo katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 12. Aidha, Serikali imeendelea kuhamasi sha na kusimamia ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini vya gharama nafuu, ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa za mafuta zenye ubora na katika hali ya usalama katika maeneo hayo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 kulikuwa na vituo vya mafuta 352 katika maeneo ya vijijini ikilinganishwa na vituo 287 vilivyokuwepo katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 23.

**D.19.2: UDHIBITI WA BIASHARA YA VILAINISHI**

**190. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia ubora wa vilainishi vinavyoingizwa katika soko hapa nchini kwa kutoa leseni kwa wafanya biashara wanaofanya biashara ya jumla ya vilainishi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2023,

EWURA ilikuwa imetoa leseni 74 za Biashara ya Jumla ya Vilainishi na Leseni saba (7) za viwanda vya kutengeneza bidhaa hizo. Aidha, EWURA inashirikiana na Taasisi nyingine za Serikali, ikiwemo Tume ya Ushindani (FCC) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika kufanya ukaguzi wa pamoja ili kubaini bidhaa za vilainishi zilizopo sokoni ambazo hazikidhi viwango vya ubora stahiki na kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria. Ukaguzi uliofanyika kuanzia tarehe 11 hadi 28 Aprili 2023 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Dodoma na Tanga ulibaini uwepo wa bidhaa bandia na zisizokidhi viwango vya ubora katika mikoa hiyo. Kutokana na tatizo hilo, EWURA, TBS na FCC zinachukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria ikiwemo kuondoa bidhaa hizo sokoni. Pia kutokana na matokeo ya ukaguzi huo, EWURA imeanzisha kampeni ya ukaguzi kwa mikoa yote nchini ili kudhibiti tatizo hili.

**D.19.3: UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA UWEKAJI VINASABA**

**191. Mheshimiwa Spika,** Serikali iliendelea kutekeleza programu ya uwekaji vinasaba kwenye mafuta ili kuhakikisha mafuta yanayouzwa hapa nchini yamelipiwa kodi stahiki na pia kudhibiti ubora. Katika programu hii, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lina jukumu la kuweka vinasaba kwenye mafuta ya petroli na EWURA ina wajibu wa kufanya ukaguzi kwenye soko la ndani ili kuhakikisha mafuta yanayou zwa nchini yamezingatia kiwango stahiki cha vinasaba. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Aprili 2023, jumla ya lita bilioni 3.33 za bidhaa za mafuta ziliwekwa vinasaba. Kati ya hizo, lita bilioni 1.36 zilikuwa za petroli, lita bilioni 1.96 za dizeli na lita milioni 7.9 za mafuta ya taa. Hili ni ongezeko la asilimia 3.8 ikilinganishwa na jumla ya lita bilioni 3.21 za mafuta yaliyowekwa vinasaba katika kipindi kama hicho mwaka 2021/2022. Aidha, EWURA imechukua sampuli kutoka kwenye vituo 881 kwa ajili ya kupima vinasaba ambapo sampuli za vituo 852 sawa na asilimia 96.71 zilikidhi viwango vya vinasaba.

**D.19.4: SHUGHULI NYINGINE ZA KIUDHIBITI ZILIZOTEKELEZWA NA EWURA**

**192. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia EWURA katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za udhibiti wa Sekta ya Nishati kama ifuatavyo:

1. Kufanya ukaguzi wa miundombinu ya usambazaji umeme ili kutathmini ubora wa miundombinu hiyo kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa umeme kwa wananchi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 jumla ya miundombinu ya Mikoa 17 kati ya 29 ya ki - TANESCO ilikaguliwa;

2. Kutoa leseni 1,176 kwa Wakandarasi wa Umeme (electrical installations per sonnel) ikilinganishwa na leseni 902 zilizotolewa kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 23.3. Kati ya leseni hizo Daraja A wali kuwa (32); Daraja B (79); Daraja C (706); Daraja D (352); Daraja W (6); na Daraja S3 (1). Vilevile, EWURA iliendelea kufuatilia utekelezaji wa matumizi ya leseni hizo, ikiwemo kuhamasisha wananchi, taasisi za umma na binafsi kutumia mafundi umeme wenye leseni zitolewazo na EWURA;

3. Kuhuisha Kanuni mbili (2) za udhibiti, ambazo ni Kanuni ya Umeme ya Huduma za Ufungaji Mifumo ya Umeme – The Electricity (Installation Services) (Amend ment) Rules, 2023 na Kanuni za Usimamizi wa Miundombinu na Biashara ya Mafuta - The Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) (Amendment) Rules, 2023. Marekebisho hayo ya Kanuni yana lenga kuongeza ufanisi katika utoaji wa leseni na kuwezesha wananchi kumudu gharama za huduma. Ufafanuzi wa Kanuni zilizohuishwa na bei elekezi ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 9.

4. Kuendelea kuandaa na kuhuisha Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Udhibiti sambamba na utoaji wa bei elekezi kwa bidhaa za mafuta na umeme nchini. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, bei elekezi za Kampuni sita (6) za wazalishaji wadogo wa umeme ziliidhinishwa. Kampuni hizo ni, Husk Power Limited, Watu na Umeme Tanzania Limited, POWERGEN Renewable Energy Limited, Jumeme Rural Power Supply, na POWERCORNER Tanzania Limited. Bei hizi pamoja na mambo mengine, zinaendelea kuhamasisha na

kuchochea uwekezaji binafsi katika uzalishaji umeme. Vilevile, Serikali kupitia EWURA imeendelea kukokotoa na kutoa bei elekezi za mafuta kwa kila mwezi;

5. Kuboresha mfumo wa kupokea maombi ya leseni za umeme, mafuta na vibali vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta (Licensing and Order Information Sys tem – LOIS). Mfumo huu umerahisisha taratibu za maombi na upatikanaji wa leseni za Mafundi Umeme ambapo kwa sasa mara baada ya kuidhinishwa leseni humfikia muombaji moja kwa moja pasipo kufika ofisi za EWURA;

6. Kuendelea kuhakikisha kuwa wakati wote nchi ina mafuta ya kutosha ili kukidhi mahitaji kwa kusimamia mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (BPS) na kuhakikisha Kampuni za mafuta zina mafuta ya kutosha kwa kufuatilia akiba ya mafuta ya kila Kampuni kila mwisho wa Juma. Aidha, kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi Machi, 2023, kiasi cha LPG kilichoagizwa kilikuwa tani 203,291 na kiasi cha vilainishi kilichozalishwa ni lita 37,983,966. Vilevile, vilainishi vilivyoagizwa nje ya nchi ni lita 10,104,536. Kiwango cha LPG kim eongezeka kwa asilimia 8, wakati kiwango cha vilainishi kimeongezeka kwa asilimia 11 ikilinganishwa na bidhaa hizo zilizoingizwa kwenye soko katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22;

7. Kufanya ukaguzi wa miundombinu ya mafuta 561 ili kuhakiki kama inakidhi viwango, ambapo miundombinu 463 sawa na asilimia 82.53 ilikidhi viwango. Aidha, EWURA imechukua sampuli 494 za mafuta kutoka katika vituo ili kuhakiki ubora wa mafuta. Kati ya sampuli hizo, Sampuli 479 sawa na asilimia 96.96 zilikidhi viwango vya ubora;

8. Kutoa leseni 316 za vituo vya mafuta, leseni 29 za kampuni za mafuta, leseni mbili (2) za maghala ya kuhifadhi mafuta, leseni mbili (2) za kampuni za gesi ya LPG, leseni 19 za mawakala wa Gesi ya LPG, leseni nane (8) za vituo vya mafuta kwa ajili ya matumizi binafsi, leseni saba (7) za wauzaji wa jumla wa vilainishi, leseni mbili (2) kwa ajili ya

kuuza mafuta kwenye meli (bunker ing business licence) na kibali kimoja (1) cha Ujenzi wa Mradi wa Bomba la EACOP;

9. Kuboresha Mfumo wa Kukokotoa Bei Kikomo za Mafuta (Cap Price Compu tations Information System - CIPS) ili kurahisisha ukokotoaji wa bei kikomo za kila mwezi kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali yanayojitokeza katika Sekta Ndogo ya Mafuta;

10. Kuendelea kusimamia Kampuni zinazomiliki maghala ya mafuta ili kukamili sha kazi ya kufunga mita (inlet flowmeters) za kupima mafuta katika mabomba yote yanayoingia kwenye maghala yao ikiwa ni moja ya hatua zilizochukuliwa na Serikali ili kudhibiti kiwango cha upotevu wa mafuta na kuleta ufanisi katika mfumo wa upokeaji mafuta kwenye maghala. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 maghala 17 kati ya 20 yalikuwa yamekamilisha ufungaji wa mita;

11. Kuboresha National Petroleum and Gas Information System (NPGIS). Mfumo huu unawezesha Serikali kupitia EWURA kupata taarifa za hali ya upatikanaji wa mafuta nchini;

12. Kuendelea kudhibiti Sekta Ndogo ya Gesi Asilia kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika miundombinu ya uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Kupi tia ukaguzi huo, miundombinu ya gesi asilia hapa nchini ipo katika hali nzuri inayokidhi viwango vya ubora na usalama; na

13. Kutoa vibali vitatu (3) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kujaza gesi asilia (CNG) katika magari yanayotumia nishati hiyo kwa Kampuni ya Taqa Dalbit Jijini Dar es Salaam, TP Company Ltd Bagamoyo na Dangote Cement Limited Mkuranga mkoani Pwani. EWURA imetoa pia vibali vitatu (3) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia

kwa TPDC Jijini Dar es Salaam na Mnazi Mmoja Mkoani Lindi pamoja na Kampuni ya PanAfrican Energy Jijini Dar es Salaam.

**D.20: USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI**

**193. Mheshimiwa Spika**, Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ushiriki wa Watanzania katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi ambapo kwa upande wa Mradi wa EACOP jumla ya Watanzania 1,969 waliajiriwa kupitia ajira za moja kwa moja na Watanzania 160 waliajiriwa kwa ajili ya uchukuaji data za mitetemo za mfumo wa 3D katika Kitalu cha Ruvuma. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, jumla ya Dola za Marekani milioni 134.6 sawa na Shilingi bilioni 313.14 zilitumika katika ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka soko la ndani.

**194.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia EWURA iliendelea kuzitambua kwa kuzisa jili Kampuni za ndani na zile za ubia kwenye Kanzidata ya *Local Suppliers and Service Providers (LSSP)* kwa ajili ya kupatiwa kipaumbele cha fursa zilizopo kwenye miradi mbalimbali hususan Mradi wa EACOP. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 jumla ya Kampuni 1,748 zilikuwa zimesajiliwa ambapo Kampuni 190 zilipata fursa za kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali kwenye Mradi.

Aidha, uwezo wa kampuni za Watanzania umeendelea kuimarika ambapo kampuni ya kitanzania *(Solution Tag)* ilishinda zabuni ya kukagua na kusafisha bomba la gesi asilia (intelligent pigging) lenye urefu wa mita 800 linalotoa gesi asilia kutoka katika kisima hadi ulipo mtambo wa kuchakata gesi asilia wa Mnazi Bay. Kazi hii itahusisha vilevile kukagua na kusafisha bomba la kilomita 27 linalosafirisha gesi kutoka ulipo mtambo wa kuchakata gesi wa Mnazi Bay hadi kituo cha kupokea gesi asilia Mtwara mjini. Zabuni hii ina thamani ya takriban **Dola za Marekani 500,000** sawa na **Shilingi bilioni 1.6.**

**D.21:KUIMARISHA UTENDAJI KAZI NA UTOAJI HUDUMA**

**195. Mheshimiwa Spika,** ikiwa ni hatua ya kuimarisha mazingira ya utendaji kazi, Wizara ya Nishati iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Wizara katika Mji wa

Serikali Mtumba, Dodoma. Mradi huo unaotekelezwa na Mkandarasi, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) umefikia asilimia 62.82 na unatarajiwa kukamika mwezi Oktoba, 2023.

**196. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha taasisi zilizo chini ya Wizara zinaimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma, Wizara ilisimamia uidhinishwaji wa Miundo ya Taasisi, Miundo ya Maendeleo ya Utumishi na Miundo ya Mishahara kwa Taasisi za TANESCO, REA na PBPA. Aidha, Wizara iliendelea kuwajengea uwezo watumishi wake pamoja na Taasisi zilizo chini yake ambapo jumla ya watumishi 32 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 1,948 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika kada mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, watumishi wa Wizara wali kuwa 71, TANESCO 1,258, TPDC 305, REA 100, PURA 58, PBPA 30 na EWURA 158.

**197. Mheshimiwa Spika,** jumla ya watumishi 127 walipandishwa vyeo katika kada mbalimbali ambapo wa Wizara ni 23, EWURA 92, PURA mmoja (1) na TPDC 11. Vilevile, watumishi watatu (3) walibadilishwa Kada.

**198. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliendelea kuchukua hatua za kuimarisha Taasisi za TPDC na TANESCO ili kuvutia uwekezaji, utendaji na mapato ya Taasisi hizo. Mwezi Septemba, 2022 Serikali iliridhia kubadili madeni ya TANESCO yanayofikia Shilingi trilioni 2.4 kuwa mtaji wa Shirika hilo na pia kubadili mkopo wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba na Mitambo ya Kuchakata Gesi Asilia wa Dola za Marekani bilioni 1.19 kuwa mtaji wa Serikali kwa TPDC. Kwa sasa, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ipo katika hatua za mwisho za ubadilishaji wa madeni hayo kuwa mtaji wa Taasisi hizo ambapo taratibu hizo zina tarajiwa kukamilika ndani ya mwaka 2022/23. Kubadilishwa kwa madeni ya Serikali kwa TANESCO na TPDC kuwa mtaji wa mashirika hayo kutaimarisha Mizania ya Hesabu (Balance Sheet) za Taasisi hizo na hivyo kuziwezesha kukopesheka, kuvutia uwekezaji na kuimarisha mapato.

**199. Mheshimiwa Spika**, Serikali iliendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi za EWURA na TPDC, ambapo Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muun gano wa Tanzania alimteua

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA na Watendaji Wakuu wa Taasisi za EWURA na TPDC. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia utendaji wa Taasisi hizo ili zifanye kazi kwa tija inayotarajiwa.

**D.22: MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23**

**200. Mheshimiwa Spika,** mafanikio mbalimbali yamepatikana katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2022/23. Mafanikio hayo ni pamoja na yafuatayo:

1) Uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa umeongezeka kwa asilimia 10.5 na kufikia MW 1,872.05 ikilinganishwa na MW 1,694.55 zilizokuwepo mwaka 2021/22;

2) Ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP), MW 2,115 umefikia asilimia 86.89 ikilinganishwa na asilimia 60.22 za mwezi Aprili, 2022;

3) Hadi kufikia tarehe 23 Mei, 2023 kina cha maji ya Bwawa la JNHPP kilikuwa kimefikia mita 160.51 kutoka usawa wa bahari ambapo ili kuweza kuzalisha umeme, kiwango cha chini cha maji kinatakiwa kufikia mita 163 kutoka usawa wa bahari;

4) Mradi wa Kinyerezi 1 Extension wa MW 185 umekamilika ambapo mitambo yote minne (4) imewashwa na inachangia MW 185 katika Gridi ya Taifa. Utekelezaji wa mradi huo mwaka 2021/22 ulikuwa umefikia asilimia 88;

5) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo – MW 80 umefikia asilimia 99 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023, ambapo mwaka 2021/22 ulikuwa asilimia 91.6;

6) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi na Kituo cha Kupoza Umeme Nyakanazi umekamilika;

7) Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 94 umekamilika, ambapo mwaka 2021/22 utekelezaji ulikuwa umefikia asilimia 79;

8) Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze – kV 400 yenye urefu wa kilomita 160 umefikia asilimia 93.5 ikilinganishwa na asilimia 44 mwaka 2021/22. Aidha, ujenzi wa kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze ambacho ni sehemu ya mradi huo umefikia asilimia 64 ikilinganishwa na asilimia 3.59 mwaka 2021/22;

9) Miundombinu ya kusafirisha umeme imeongezeka na kufikia jumla ya urefu wa kilomita 6,363.27 sawa na ongezeko la asilimia 4.1 ikinganishwa na kilomita 6,111.27 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Mei, 2022;

10) Miundombinu ya kusambaza umeme imeongezeka na kufikia kilomita 168,548.36 sawa na ongezeko la asilimia 9.5 ikilinganishwa na kilomita 153,988.49 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Mei, 2022;

11) Serikali imesainiwa mikataba 26 na wakandarasi kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kuimarisha Gridi ya Taifa ili kukabiliana na uchakavu wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Aidha, imesainiwa pia Mikataba 14 ya kuimarisha usambazaji wa umeme vijijini;

12) Serikali imetoa Shilingi bilioni 16.43 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi 6,500 wanaopisha mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA) na Wananchi 4,750 tayari wamelipwa fidia zao;

13) Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi umefikia asilimia 26.7 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2024;

14) Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma kwa ajili ya uendeshaji wa Treni ya

Umeme (SGR Lot II) umefikia asilimia 98 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2023, ikilinganishwa na asilimia 88 za mwaka 2021/22;

15) Kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme ya Kakono (MW 87), Malagarasi (MW 49.5) pamoja na miradi ya kusafirisha umeme ya Tanzania – Zambia (TAZA);

16) Kuzima mitambo inayotumia mafuta ya Kibondo, Kasulu, Ngara, Biharamulo na Loliondo kwa kuunganisha Wilaya hizo katika Gridi ya Taifa na hivyo kuokoa takribani Shilingi bilioni 60 kwa mwaka zilizokuwa zinatumika kuendesha majenereta hayo;

17) Jumla ya wateja 4,319,258 wameunganishiwa umeme hadi mwezi Aprili, 2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.4 ikilinganishwa na wateja 3,842,096 waliokuwepo mwezi Juni, 2022;

18) Vijiji 1,880 kati ya 4,071 vilivyosalia katika kuunganishiwa umeme, sawa na asilimia 46.18 vimeunganishiwa umeme na vijiji vyote vitakuwa vimeunganishiwa umeme ifikapo Juni, 2024;

19) Serikali imeanza zoezi la kusambaza umeme katika vitongoji vyote 36,755 ambavyo kwa sasa havina umeme kati ya vitongoji 64,760 vya Tanzania Bara;

20) Kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Ifakara (220/33kV, 1x20MVA) na kuunganisha umeme kwa wateja 1,588 katika vijiji nane (8) na vitongoji saba (7) katika Wilaya za Kilombero na Ulanga;

21) Kukamilika kwa ununuzi wa mtambo wa kuchoronga visima vya uhakiki (drilling rig) kwa miradi ya jotoardhi. Kupatikana kwa Mtambo huu kutawezesha uchimbaji kwa maeneo yote yaliyoainishwa kuwa na viashiria vya jotoardhi na kupata matokeo stahiki kwa haraka;

22) Serikali imekamilisha uandaaji wa Mwongozo na Kanuni za Utoaji Mikopo kwa waendelezaji wa ujenzi wa vituo vidogo vya mafuta vijijini. Aidha, fursa za mikopo husika zimetangazwa na waombaji wanatakiwa kuwasilisha maombi hadi kufikia tarehe 30 Agosti, 2023;

23) Usimamizi wa miradi ya kupeleka umeme Vijijini umeimarishwa kwa kuchukua hatua mbalimbali, ikiwemo kuajiri Waratibu wa miradi hiyo katika Wilaya zote za Tanzania Bara, kutolewa kwa kibali cha kuajiri Wahandisi 20 wa miradi ya umeme vijijini, kununua magari 21 kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo na kuboresha vigezo vya zabuni za kuwapata wakandarasi ili kuhakikisha ni wakandarasi wenye sifa na uwezo tu ndiyo wanapewa kazi za miradi ya umeme vijijini;

24) Wamepatikana waendelezaji watatu (3) wa miradi ya kusambaza umeme kwa kutumia nguvu ya jua katika visiwa 28 vilivyopo katika mikoa ya Kagera (8), Mwanza (13), Mara (3) na Lindi (4) na kuunganisha umeme kwa wateja 9,515;

25) Bei elekezi za Kampuni sita (6) za wazalishaji wadogo wa umeme ziliidhinishwa na zinahamasisha na kuchochea uwekezaji binafsi katika uzalishaji umeme;

26) Wamepatikana Wakandarasi wanne (4) kwa ajili ya kusambaza umeme katika Vituo vya Afya 66 na Pampu za Maji 333 vilivyopo vijijini katika mikoa 25 Tanzania Bara;

27) Jumla ya taasisi 43,925 zinazotoa huduma kwa jamii ikiwemo za Elimu, Biashara, Pampu za Maji, Vituo vya Afya na Nyumba za Ibada zimeunganishiwa umeme ikilinganishwa na taasisi 40,408 mwaka 2021/22;

28) Wamepatikana wakandarasi kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo 336 ya wachimbaji wadogo wa madini, maeneo ya kilimo na viwanda katika maeneo mbalimbali Tanzania Bara;

29) Serikali imebadili madeni ya TPDC ya Dola za Marekani bilioni 1.19 na TANESCO ya Shilingi trilioni 2.4 kuwa mitaji ya mashirika hayo ili kuvutia uwekezaji pamoja na kuimarisha utendaji na mapato ya mashirika hayo;

30) Kimepatikana kibali cha utafutaji wa awali (reconnaissance permit) wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Eyasi Wembere kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC);

31) Kukamilika kwa majadiliano na Wawekezaji, ya Mkataba wa Nchi Hodhi (Host Government Agreement-HGA) na Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanywaji Mapato (PSA), kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG) wenye manufaa makubwa nchini na ambao utavutia uwekezaji wa Dola za Marekani bilioni 42.00 (takribani shilingi trilioni 98.7). Majadiliano ya mradi huu yamechukua takribani miaka saba (7) tangu yalipoanza rasmi mwezi Septemba, 2016;

32) Serikali imeanzisha Ofisi Mahsusi ya Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG), ikiwa ni hatua ya kuhakikisha mradi unaratibiwa, kufuatiliwa na kuwezeshwa kwa tija na ufanisi ili manufaa yake yapatikane kwa wakati na kama ilivyokusudiwa;

33) Kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi 387 kati ya 388 waliopisha maeneo 14 ya ujenzi wa kambi kwa ajili ya mradi wa EACOP pamoja na wananchi 9,024 kati ya 9,325 wanaopisha eneo la mkuza wa bomba ya mradi huo;

34) Jumla ya Kampuni za ndani na zile za ubia 1,748 zimesajiliwa katika Kanzidata ya Local Suppliers and Service Providers (LSSP) hadi mwezi Aprili, 2023, ambapo 190 zimepata fursa za kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali katika Mradi wa EACOP;

35) Jumla ya Watanzania 1,969 waliajiriwa kupitia ajira za moja kwa moja katika mradi wa EACOP na Watanzania 160

waliajiriwa kwa ajili ya uchukuaji data za mitetemo za mfumo wa 3D katika Kitalu cha Ruvuma;

36) Nchi imeendelea kuwa na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta ambapo katika kipindi chote cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 kumekuwepo na akiba ya mafuta ya kutosha;

37) Uzalishaji wa gesi asilia umeongezeka na kufikia Futi za Ujazo Bilioni 68.02 ikilinganishwa na Futi za Ujazo Bilioni 59.96 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 13;

38) Kuanza kwa kazi ya kudurusu Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji wa Mapato (MPSA) kwa lengo la kuuhuisha ili kuendana na mazingira ya uwekezaji wa sasa katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia;

39) Kukamilika kwa maandalizi ya rasimu ya Ramani ya Kidijitali (Interactive Digital Petroleum Reference Map) kwenye Mfumo wa Taarifa wa Kijiografia (Geographical Information System – GIS) inayotoa taarifa za Vitalu vya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini inayotarajiwa kuanza kutumika rasmi mwezi Juni, 2023;

40) Utiaji saini kwa mkataba wa nyongeza wa uzalishaji na ugawanaji mapato ya gesi iliyogundulika Ntorya katika kitalu cha Ruvuma. Mkataba huo ambao utekelezaji wake utawezesha kuendeleza gesi asilia ya Kitalu hicho ya takriban Futi za Ujazo Trilioni 1.6 ulisainiwa baina ya Wizara ya Nishati, TPDC na Kampuni ya ARA (Oman);

41) Serikali iliendelea kufanikisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika uendelezai wa Sekta ya Nishati ambapo Mikataba (MoUs) mbalimbali ilisainiwa. Mikataba hiyo ni baina ya Serikali na Kampuni ya ENOC LLC ya Falme za Kiarabu kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikubwa cha kupokea na kuhifadhi mafuta jijini Dar es Salaam; pamoja na Serikali na kampuni za *Total Eren (MW 200), Abu Dhabi Future Energy Company PJSC - Masdar (MW 2,000), Sumitomo (MW 300 – 600), Mbeya Power Ltd (MW 300)*

na *Kilwa Energy (MW 318)* kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu, gesi asilia na makaa ya mawe; na

42) Kufanyika kwa mjadala wa kitaifa wa Nishati safi ya kupikia tarehe 1 na 2 Novemba, 2022 ambapo matokeo ya mjadala huo ni pamoja na kuandaliwa kwa Dira na Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia utakaozinduliwa mwezi Julai, 2023 na kuanza kutumika.

43) Serikali imeunda Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, inayoongozwa na Waziri Mstaafu, Profesa Mark Mwandosya, pamoja na kuteua Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo;

44) Serikali iliunda Bodi mpya ya REA inayoongozwa na Waziri Mstaafu, Mama Janet Mbene; na

45) Serikali iliunda Bodi mpya ya TPDC, inayoongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Balozi Ombeni Sefue, na kufanya mabadiliko makubwa kwenye menejimenti ya Shirika hilo. Serikali pia imeondoa menejimenti yote ya kampuni tanzu ya TANOIL na kutengeneza mkakati mpya wa biashara na uendeshaji wa kampuni hiyo.

**E. CHANGAMOTO ZILIZOPO NA UTATUZI WAKE**

**201. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2022/23, mahitaji ya nishati ya umeme na gesi asilia nchini yameendelea kukua kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Hatua zinazochukuliwa na Wizara ili kupatia ufumbuzi ukuaji huo ni pamoja na kuhakikisha miradi ya uzalishaji, usafir ishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia inakamilishwa kwa wakati pamoja na kuendelea kuwekeza katika shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia. Aidha, kwa kuwa miradi ya nishati ni ya gharama kubwa, Wizara itaendelea kuvutia uwekezaji wa Sekta Binafsi ili kuimarisha upatikanaji wa fedha za kugharamia utekelezaji wake.

## MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

**202.** Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2022/23, sasa napenda kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24.

**203.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24 Wizara itaendelea kutekeleza vipaumbele tulivyoviweka mwaka jana, ikiwa ni pamoja kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; kuimarisha upatikanaji wa nishati vijijini na vitongojini pamoja na kuendeleza shughuli za mafuta na gesi nchini na kuwezesha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia. Aidha, mkazo utaelekezwa pia katika kuimarisha utoaji wa huduma kupitia Taasisi zilizo chini ya Wizara, kushirikisha Sekta Binafsi katika uendelezaji wa Sekta ya Nishati pamoja na ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia. Dhamira yetu ya jumla ni kuifanya Sekta ya Nishati kushamirisha shughuli za biashara na uzalishaji mali, kuziwezesha Sekta nyingine za huduma na uzalishaji mali kutimiza malengo yao na pia Sekta ya Nishati kuchan gia katika ukuaji wa uchumi na kufikiwa kwa malengo ya jumla ya nchi yetu.

**204.** Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/24 pamoja na mambo mengine, umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) 2021/22 – 2025/26, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020, Maagizo ya Viongozi wa Kitaifa katika Sekta ya Nishati, Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/23 pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26). Miongozo mingine iliyozingatiwa ni Sera, Mikakati na Programu mbalimbali za Kisekta na Kitaifa pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) ya mwaka 2030 kuhusu masuala ya nishati.

### SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

### F.1: MIRADI YA KUZALISHA UMEME

**205.** **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza awali, moja ya kazi kubwa zilizo mbele yetu ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inazalisha umeme wa kutosha. Ili kutimiza azma yetu na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya kuzalisha Megawati

5,000 ifikapo 2025, Serikali imeandaa miradi kadhaa ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na maandalizi.

**F.1.1: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI**

**i) Mradi waKuzalisha Umeme kwaKutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115**

**206. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Serikali itakamilisha Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115 ambapo jumla ya fedha za ndani Shilingi trilioni 1.5 zimetengwa. Ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha wiki moja kuanzia leo, bwawa letu litafikisha kiwango cha ujazo wa maji (yaani mita 163 kutoka usawa wa bahari) kinachowezesha kuanza uzalishaji wa umeme. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itakamilisha ufungaji wa mitambo ya kuzalisha umeme; kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka katika kituo cha kufua umeme (power house) hadi kituo cha kupokelea umeme (switchyard), kukamilisha barabara za kudumu katika eneo la mradi. Vilevile, katika mwaka ujao wa fedha, tutafanya tukio jingine la kihistoria la kuwasha mashine ya kwanza na kuingiza umeme kwenye Gridi ya Taifa.

**207.** Mheshimiwa Spika, vilevile, katika mwaka ujao wa fedha Serikali kupitia TANESCO inatarajia kuanza utekelezaji wa miradi ya kijamii (CSR) inayotokana na makubaliano ya Mkataba wa ujenzi wa mradi wa JNHPP. Kwa kuanzia, Serikali itajenga chuo kikubwa cha kisasa cha ufundi wa umeme na mafuta na gesi mkoani Lindi. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024.

**ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwaKutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension (MW 185)**

**208. Mheshimiwa Spika**, katika mradi huu ambao ujenzi wake umekamilika kwa asili mia 100 na kwa sasa unachangia MW 185 katika Gridi ya Taifa, Serikali itakamili sha kazi za ujenzi katika maeneo mengine ikiwemo ujenzi wa barabara na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 yenye urefu wa kilomita 19.2 kutoka Kinyerezi hadi Mbagala kupitia Gongo la Mboto.

Jumla ya Shilingi bilioni 40 fedha za ndani zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo.

**iii) Mradi waKuzalisha Umeme kwaKutumia Maji wa Ruhudji (MW 358)**

**209. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia mikopo ya masharti nafuu pamoja na kukamilisha tathmini ya kuangalia uwezekano wa kupata fedha kupitia soko la Hisa na Mitaji. Aidha, Serikali itaanza kufanya malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi pamoja na ujenzi wa miundombinu wezeshi ambapo Shilingi bilioni 6.27 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**iv) Mradi waKuzalisha Umeme kwaKutumia Maji wa Rumakali (MW 222)**

**210. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kutafuta fedha za ujenzi wa mradi huu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kupitia soko la Hisa na Mitaji, Serikali itaanza ujenzi wa miundombinu wezeshi ikijumuisha barabara za kufika eneo la mradi na kuanza kufanya malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi. Jumla ya Shilingi bilioni 5.25 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji waKikonge (MW 321)**

**211. Mheshimiwa Spika,** katika mradi huu, Serikali pia itatafuta fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa mradi na kupitia soko la Hisa na Mitaji ikiwa ni njia mbadala ya kupata fedha. Vilevile, Serikali itakamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) kwa ajili ya mradi wa kufua umeme pamoja na njia za kusafirisha umeme kutoka kwenye Bwawa hadi kituo cha kupoza umeme Madaba (Ruvuma). Jumla ya Shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo.

**vi) Mradi waKuzalisha Umeme kwaKutumia Maji wa Malagarasi (MW 49.5)**

**212. Mheshimiwa Spika,** Serikali itakamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa bwawa; kuanza ujenzi wa bwawa;

kuendelea na ujenzi wa njia ya kusa firisha umeme msongo wa **kV 132** kutoka kwenye bwawa la kuzalisha umeme hadi katika kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe; na kukamilisha ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha wateja. Jumla ya **Shilingi bilioni 15.52** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo ambapo kati ya hizo **Shilingi milioni 350** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 15.17** ni fedha za nje.

**vii) Mradi waKuzalisha Umeme kwaKutumia Maji waKakono (MW 87.8)**

**213. Mheshimiwa Spika,** Serikali imekamilisha upatikanaji wa fedha za kutekeleza mradi huu. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi wanaopi sha mradi; kukamilisha taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi; kuwapata Wakandarasi wa ujenzi; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 39.15** zimetengwa ambapo kati ya hizo, **Shilingi bilioni 2.62** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 36.53** ni fedha za nje.

**viii) Mradi waKuzalisha Umeme kwaKutumia Jua wa Shinyanga (MW 150)**

**214. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka ujao wa fedha, kwa mara ya kwanza katika his toria ya nchi yetu, tutaingiza umeme unaozalishwa kwa nguvu ya jua katika Gridi ya Taifa. Serikali itakamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 27.63** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo ambapo kati ya hizo, **Shilingi milioni 500** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 27.13** ni fedha za nje.

**ix) Mradi waKuzalisha Umeme kwaKutumia Gesi Asilia – Mawe Project (MW 150)**

**215. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu usimikaji wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya **MW 150** ambapo **MW 90** zitakuwa katika eneo la Tegeta (Dar es Salaam) na **MW 60** eneo la Mwanambaya – Mkuranga (Pwani). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Upembuzi Yakinifu wa mradi umekamilika na hatua za ununuzi zinaendelea. Gharama ya utekelezaji wa mradi huu ni **Shilingi bilioni 345.** Kazi zitakazotekelezwa ni kukam ilisha ununuzi na kusimika mitambo

ya kufua umeme katika maeneo tajwa. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 345** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2023 na kukamilika mwezi Julai, 2024.

**x) Ukarabati wa Kituo cha Kufua Umeme cha Hale Hydro Power Plant**

**216. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na kazi za ukarabati wa mradi ambapo **Shilingi bilioni 6.4** fedha za nje zimetengwa. Kazi zinazotarajiwa kufanyika ni kumalizia kazi za kuchimba handaki (escape tunnel), ujenzi wa barabara, uwekaji wa mitambo ya uzalishaji na kuanza matengenezo ya kituo cha kupoza umeme.

**F.1.2: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA MAANDALIZI**

**i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara (MW 300)**

**217. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaanza taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la ujenzi wa kituo cha kufua umeme na kazi ya uwekaji wa mipaka ya mkuza wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu na kuendelea na taratibu za kupata fedha kutoka Serikali ya Japan kupitia JICA. Jumla ya Shilingi bilioni 1.50 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

Kutokana na changamoto mahsusi ya upatikanaji wa umeme mkoani Mtwara, na kwa kuzingatia kwamba gesi inayotumika katika uzalishaji wa umeme nchini inatoka katika Mkoa huo, Serikali itachukua hatua za dharura, zitakazozaa matunda ndani ya miezi sita, za kuimarisha upatikanaji wa umeme katika mkoa wa Mtwara.

**ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia – Mwamba Project (MW 450) (Kinyerezi III)**

**218. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kuzalisha jumla ya **MW 450** ambapo **MW 300** zitazalishwa kwa kutumia gesi asilia na **MW 150** kwa kutumia mvuke (steam) katika eneo la Kinyerezi. Mradi umepangwa kutekelezwa katika awamu mbili ambapo awamu ya kwanza itahusisha ufungaji wa mitambo yenye uwezo wa **MW 300** na awamu ya pili itahusisha **MW 150** na hivyo kufikia

jumla ya **MW 450**. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Serikali imekamilisha kazi ya kuhuisha Upembuzi Yakinifu na kuanza kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA). Serikali inakusudia kuanza mazungumzo na Serikali ya Sweden kupitia Shirila lake la Export Credit Agency (EKN) kwa ajili ya kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi zinazokadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 500** sawa na **Shilingi trilioni 1.17,** kuanza taratibu za manunuzi, kumpata Mshauri Mwelekezi na Mkan  darasi na kuanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.5** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**F.2: MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME**

**219. Mheshimiwa Spika,** msingi wa kupata umeme wa uhakika ni kuwa na miundombinu thabiti na ya kutosheleza ya kusafirisha na kusambaza. Kutokana na changamoto ya muda mrefu ya miundombinu chakavu na isiyotosheleza kusafirisha na kusambaza umeme, Serikali imeandaa miradi kadhaa ya kukabiliana na changamoto hiyo ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na maandalizi.

**F.2.1: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI**

**i) Mradi wa Njia yaKusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga**

**220. Mheshimiwa Spika**, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 15.91** fedha za nje kwa ajili ya kukamilisha kazi za ujenzi wa mradi zikijumuisha kufanya majaribio ya miun dombinu iliyojengwa katika mradi huu.

**ii) Ujenzi wa Njia yaKusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

**221. Mheshimiwa Spika,** mradi huu utaiunganisha Gridi ya Taifa na mfumo wa Gridi wa nchi za Kusini mwa Afrika na kuwezesha biashara ya umeme kufanyika miongoni mwa nchi zetu. Vilevile, mradi huu utaimarishaji upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Songwe, na kufikisha Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Rukwa. Serikali kupitia TANESCO itakamilisha ulipaji fidia kwa Wananchi wanaopisha mradi na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme ambapo

**Shilingi bilioni 56.32** zimetengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa kazi hizo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 3.00** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 53.32** ni fedha za nje.

**iii) Mradi wa Njia yaKusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutokaKigoma – Nyakanazi**

**222. Mheshimiwa Spika**, kazi za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme, vituo vya kupoza umeme pamoja na miundombinu ya usambazaji umeme zinaendelea ambapo **Shilingi bilioni 34** zimetengwa. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 600** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 33.4** ni fedha za nje.

**iv) Ujenzi waKituo chaKupoza Umeme Shinyanga**

**223. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kupoza umeme chenye uwezo wa **MVA 315** cha Ibadakuli (Shinyanga). Utekelezaji wa mradi huu utawezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Shinyanga na hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi hususan uchimbaji wa madini. Aidha, kituo hiki kitakuwa chanzo cha umeme kwa ajili ya uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR) kwa maeneo ya Kanda ya Ziwa. Gharama ya mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 50** sawa na takribani **Shilingi bilioni 117.25.** Jumla ya **Shilingi bilioni 2.7** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**v) Mradi wa Njia yaKusafirisha Umeme kV 220 Geita – Nyakanazi**

**224. Mheshimiwa Spika,** Serikali itakamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme katika vijiji vyote 32 vilivyopitiwa na mradi ambapo **Shilingi bilioni 11.72** fedha za nje zimetengwa.

**vi) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Benaco hadiKyaka**

**225. Mheshimiwa Spika**, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 5.8** fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi; kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi; kuwapata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa ujenzi wa mradi; na kuanza ujenzi wa mradi.

**vii) Mradi wa Ujenzi wa Njia yaKusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi**

**226. Mheshimiwa Spika,** Serikali itakamilisha malipo ya fidia kwa wananchi waliosalia na kuendelea na malipo kwa kipindi cha uangalizi (retention money) kwa Mkandarasi wa ujenzi. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.84** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ambapo kati ya hizo **Shilingi milioni 225** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 3.62** ni fedha za nje.

**viii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Julius Nyerere hadi Chalinze na Kituo cha Kupoza Umeme, Chalinze**

**227. Mheshimiwa Spika,** Serikali itakamilisha utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze na kituo cha kupoza umeme cha Chalinze. Jumla ya **Shilingi bilioni 20.50** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi.

**ix) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization Project)**

**228. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi inayoendelea chini ya mradi wa kuimarisha Gridi ya Taifa katika maeneo mbalimbali nchini ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 473.40** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Serikali pia itaanza matayarisho ya awamu ya pili ya mradi huu ikiwa ni pamoja na: kuainisha maeneo itakapotekelezwa miradi hiyo; kufanya Upembuzi Yakinifu; kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA); kufanya uthamini wa mali za wananchi watakaopisha miradi; na kufanya usanifu wa miradi.

**x) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa (TANESCO Transmission Grid Rehabilitation & Upgrade Project – TTGRUP)**

**229. Mheshimiwa Spika**, Serikali itafanya ununuzi wa vifaa na kuanza kazi za ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 29.61** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**F.2.2: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTAYARISHAJI**

**i) Mradi wa Njia yaKusafirisha Umeme kV 400 Sumbawanga – Mpanda –Kigoma**

**230. Mheshimiwa Spika**, Serikali itakamilisha uhuishaji wa Upembuzi Yakinifu wa mwaka 2016; kukamilisha usanifu wa mradi; na kuendelea na taratibu za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa mradi baada ya taratibu za ufadhili kukamilika. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya Shilingi milioni 100 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**ii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma**

**231. Mheshimiwa Spika**, Serikali itakamilisha ulipaji wa fidia wa mali za wananchi watakaopisha mradi na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 500** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**iii) Mradi wa Njia yaKusafirisha Umeme kV 220 kutoka Makutupora hadi Tabora kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot III)**

**232. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TANESCO itakamilisha Upembuzi Yakinifu; kuendelea na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa ujenzi; kufanya tathmini ya mali za wananchi wanaopisha mradi; kufanya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa mradi.

**iv) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Tabora hadi Isaka kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot IV)**

**233. Mheshimiwa Spika**, Serikali itakamilisha Upembuzi Yakinifu; kuendelea na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa ujenzi, kufanya tathmini ya mali na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa mradi.

**v) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot V)**

**234. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TANESCO itakamilisha tathmini ya mali za wananchi wanaopisha mradi, kufanya malipo ya fidia kwa wananchi hao pamoja na kuanza ujenzi wa mradi.

**vi) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Segera – Same hadi Lemugur(Arusha)**

**235. Mheshimiwa Spika**, Serikali itakamilisha Upembuzi Yakinifu wa mradi na kuanza taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Gharama za kufanya Upembuzi Yakinifu ni **Dola za Marekani milioni 1** sawa na **Shilingi bilioni 2.35** na fedha hizi zinatolewa na AfDB.

**vii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme (Submarine Cable) Msongo wa kV 220 kutoka Tanzania Bara (Ununio) hadi Zanzibar**

**236. Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa mradi huu, Serikali itakamilisha Upembuzi Yakinifu wa mradi kwa ufadhili wa AfDB utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 1** sawa na **Shilingi bilioni 2.35**, kutafuta fedha na kuanza ute kelezaji wa mradi.

**viii) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Manyoni (Manyoni Substation – MVA 60)**

**237. Mheshimiwa Spika,** Serikali itakamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha taratibu za kufafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi; na kuanza taratibu za kumpata Mkandarasi Mjenzi wa mradi. Serikali kupitia TANESCO imetenga **Shilingi milioni 100** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizi za awali.

**ix) Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme katikaKila Wilaya Nchini**

**238. Mheshimiwa** SMpika, mradi huu unahusu ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Gridi ya Taifa katika Wilaya zote nchini. Mradi unalenga kupunguza upotevu wa umeme unaotokana na umbali mrefu wa njia za usambazaji umeme katika maeneo mbalimbali nchini. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Shilingi trilioni 4.20** na zitatolewa na Serikali. Mradi umepangwa kutekelezwa katika awamu tano (5) ambapo katika kila awamu vitajengwa vituo vya kupoza umeme kumi na tano (15).

**239. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24, Serikali kupitia TANESCO itaanza utekelezaji wa mradi huu kwa kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi; Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi; na

kuanza taratibu za kuwapata Wakandarasi na kutafuta fedha za ujenzi wa mradi. Serikali kupitia TANESCO imetenga **Shilingi bilioni 5.4** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. **Kielelezo Na. 16** kinaonyesha mpango wa utekelezaji wa mradi huu na gharama ya kila awamu. Aidha, **Kiambatisho Na. 10** ni mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa katika kila Wilaya kwa kila awamu.

**Kielelezo Na. 16: Mpango wa Utekelezaji wa Mradi na Gharama ya kila Awamu**

| Awamu | Muda wa Utekelezaji | Idadi ya Vituo | Makadirio ya Gharama (TZS) |
|---|---|---|---|
| Awamu ya Kwanza | (2024/25 – 2026/27) | 15 | 1,011,195,100,000.00 |
| Awamu ya Pili | (2027/28 – 2030/31) | 15 | 682,735,320,000.00 |
| Awamu ya Tatu | (2031/32 – 2033/34) | 15 | 776,347,805,000.00 |
| Awamu ya Nne | (2034/35 – 2036/37) | 15 | 872,309,300,000.00 |
| Awamu ya Tano | (2037/38 – 2039/40) | 15 | 853,886,150,000.00 |
| **Jumla** | | **75** | **4,196,473,675,000.00** |

**x) Mradi wa Kuboresha Utendaji Kazi wa TANESCO (Corporate Management System – CMS)**

**240. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kuboresha hali ya utendaji kazi wa TANESCO kwa kuanzisha mifumo itakayowezesha kuongeza ufanisi wa utendaji kazi. Mradi huu unatekelezwa sambamba na mradi wa kusafirisha umeme wa *Tanzania – Zambia Interconnector Transmission Project (TAZA)* kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 34.8** sawa na **Shilingi bilioni 81.61.** Serikali kupitia TANESCO itakamilisha taratibu za ufungaji wa vifaa vya mtandao na usalama wa mfumo na kuwajengea uwezo wataalamu kuhusu uendeshaji na usimamizi wa mifumo

itakayofungwa. Serikali imetenga **Shilingi bilioni 12.56** fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**xi) Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Masaka - Ibadakuli)**

**241. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 617 kutoka Tanzania hadi Uganda pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kyaka. Kwa sasa Serikali kupitia TANESCO inakamilisha Upembuzi Yakinifu pamoja na usanifu wa awali wa mradi. Kwa mwaka 2023/24 kazi zitakazofanyika ni pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii na kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi milioni 250** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**242. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mradi wa kusafirisha umeme kutoka Tanzania hadi Uganda, Serikali itaendelea kukamilisha taratibu za awali na kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kusafirisha umeme kwa ajili ya kuunga Gridi za Taifa za nchi jirani ikiwemo mradi wa kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Tanzania hadi Malawi (TAMA); kV 400 kutoka Tanzania hadi Msumbiji (MOTA); kV 400 kutoka Tanzania hadi DRC; na njia ya pili ya msongo wa kV 400 kutoka Tanzania hadi Kenya. Kukamilika kwa miradi hii pamoja na miradi inayoendelea ya Tanzania – Kenya na TAZA kutawezesha mauziano ya umeme kati ya Tanzania na nchi jirani.

**xii) Miradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 North East Grid (NEG 1, 2 na 3)**

**243. Mheshimiwa Spika**, mradi huu nahusu ujenzi wa njia za kusafirisha umeme msongo wa kV 400 na kV 220 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme. Mradi huu umegawanyika kwenye awamu tatu za utekelezaji ambazo ni NEG 1, NEG 2 na NEG 3.

**244. Mheshimiwa Spika,** awamu ya kwanza (NEG 1) inahusu ujenzi wa njia za kusafir isha umeme msongo wa kV 400 Chalinze – Kinyerezi – Mkuranga yenye urefu wa kilometa 135.5 na vituo vya kupoza umeme vya Kinyerezi, Mkuranga, Morogoro pamoja na upanuzi wa kituo cha Chalinze. Gharama ya mradi ni **Dola za**

**Marekani milioni 265.94** sawa na **Shilingi bilioni 623.66** kwa ufadhili wa Benki ya Exim China.

**245. Mheshimiwa Spika**, awamu ya pili (NEG 2) inahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 Chalinze – Dodoma yenye urefu wa kilometa 345, kV 400 Chalinze – Segera yenye urefu wa kilometa 181, kituo cha kupoza umeme cha Segera na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Dodoma. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 279.80** sawa na **Shilingi bilioni 656.16** na awamu hii inatarajiwa kutekelezwa kwa ushirikishwaji wa sekta binafsi.

**246. Mheshimiwa Spika**, awamu ya tatu (NEG 3) inahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 Chalinze – Bagamoyo yenye urefu wa kilometa 90, kV 220 Segera – Tanga yenye urefu wa kilometa 64, vituo vya kupoza umeme Bagamoyo, Tanga na Mwanza. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 139.00** sawa na **Shilingi bilioni 325.97** na pia awamu hii inatarajiwa kutekelezwa kwa kushirikisha wawekezaji binafsi.

### F.3: MIRADI MINGINE ITAKAYOTEKELEZWA, MATENGENEZO YA MITAMBO NA UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO (TCPM NA ETDCO)

**247. Mheshimiwa Spika,** TANESCO kupitia mapato ya ndani itafanya matengenezo kinga katika kituo cha Kinyerezi II na Tegeta na kufanya matengenezo makubwa ya mitambo miwili ya kufua umeme katika kituo cha Ubungo I. Aidha, Shirika litaendelea kutekeleza miradi inayolenga kuongeza uwezo wa miundombinu ya kusafirisha umeme, kuboresha mifumo ya uendeshaji Gridi, kukarabati miundombinu ya usafirishaji umeme, kuweka mifumo ya kisasa ya mawasiliano katika vituo vya kupoza umeme na kujenga vituo vidogo vya kuendesha Gridi *(unmanned substations)*. Vilevile, TANESCO itatekeleza miradi ya kuweka mifumo ya kisasa ya usambazaji umeme *(distribution network automation),* kufunga mita janja *(smart meters)* na miradi mingine ya matengenezo ya miundombinu ya usambazaji umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 407.13** zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kazi hizo.

**248. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia kampuni tanzu ya TANESCO ya TCPM imepanga kuanza uzalishaji wa nguzo za zege

Mkoani Tabora na kuanzisha mchakato wa kupata fedha kwa ajili ya kuanzisha uzalishaji Mkoani Mbeya kwa kutumia jengo la Iyunga Old Power Station lililokua likitumika zamani kuzalisha umeme wa mafuta. Pia Kampuni ina mpango wa kuingia makubalino ya ubia na Wawekezaji binafsi ili kuongeza mtaji wa Kampuni.

**249. Mheshimiwa Spika,** aidha, Serikali kupitia kampuni tanzu ya TANESCO ya ETDCO itakamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Urambo na kutoka Urambo hadi Kidahwe Mkoani Kigoma na hivyo kuimarisha zaidi upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mkoa wa Kigoma na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini katika Mikoa ya Geita na Kigoma kupitia REA.


**250. Mheshimiwa Spika,** TANESCO inafanya manunuzi mengi na ya gharama kubwa wakati wote na kwa mpigo. Kwa kuzingatia umuhimu wa manunuzi katika ufanisi wa utendaji wa Shirika, na kwa kuzingatia changamoto za miaka mingi ya nyuma katika eneo hili, Serikali na Menejimenti na Bodi ya Shirika imefanya mabadiliko makubwa ya kuboresha mfumo wa manunuzi ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Shirika. Pamoja na kuboresha mfumo wa manunuzi, watumishi na watendaji wa Shirika wasio waaminifu na wazembe wameondolewa na kubadilishwa katika nafasi zao. Kutokana na mabadiliko hayo, Shirika limeweza kufanya manunuzi ya miradi mikubwa ikiwemo wa Gridi imara kwa ufanisi mkubwa. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali na Shirika wataendelea na jitihada hizo kwa kasi zaidi kwa kuzingatia ushauri, mapendekezo na maelekezo ya Bunge kupitia Kamati ya Kisekta na Kamati ya PAC.

### F.4: USHIRIKISHWAJI WA SEKTA BINAFSI KATIKA MIRADI YA KUSAFIRISHA UMEME

**251. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya kuzalisha na kusafirisha umeme. Katika miradi ya kusafirisha umeme sekta binafsi zitahusishwa kukamilisha mizunguko ya kuelekea mikoa ya Kusini *(Ring D)* na Kaskazini *(Ring A)*. Kwa ujumla miradi ya kusafirisha

umeme kwa msongo wa **kV 400** inatekelezwa ili kukamilisha mizunguko mikuu minne nchini *(Ring A, B, C na D)* ili kuimarisha na kuboresha upatikanaji wa umeme nchini. **Kielelezo Na.17** kinaonesha mizunguko minne ya msongo wa **kV 400.**

**Kielelezo Na.17: Mizunguko Minne (Ring A, B, C na D) ya Msongo wa kV 400**




*Chanzo: TANESCO*

**252. Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali kupitia TANESCO itakamilisha taratibu na kuanza utekelezaji wa miradi ya kufua umeme inayotarajiwa kutekelezwa na wawekezaji binafsi ikiwemo: Total Eren; PJSC - Masdar; Kilwa Energy; na Mbeya Power Ltd. Utekelezaji wa miradi hiyo utawezesha Serikali kufikia azma ya kuwa na **MW 5,000** ifikapo mwaka 2025. **Kiambatisho Na. 11** kinaonesha miradi ya kuzalisha na kusafirisha umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme inayotarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka 2023/24 hadi 2025/26.

**F.5: MIRADI YA NISHATI VIJIJINI**

**253. Mheshimiwa Spika**, manufaa ya kichumi na kijamii yatokanayo na kuimarika kwa upatikanaji wa nishati vijijini ni mengi. Hivyo, katika mwaka 2023/24 Serikali kupitia REA itaendelea na utekelezaji wa miradi ya nishati vijijini kama ifuatavyo:

**i) Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round II)**

**254. Mheshimiwa Spika,** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa njia za umeme wa Msongo wa Kati na Mdogo; kufunga mashineumba; na kuunganisha wateja wa awali na hivyo kukamilisha kazi ya kufikisha umeme katika vijiji vyote 12,318 ifikapo mwezi Juni, 2024. **Shilingi bilioni 9.9** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha mradi huu.

**ii) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji – (Hamlet Electrification Project – HEP)**

**255. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua kwamba pamoja na mafanikio ya kufikisha umeme karibu katika kila kijiji, bado asilimia zaidi ya 50 ya vitongoji nchini havi jafikiwa na umeme. Serikali imedhamiria kufikisha umeme katika kila kitongoji nchini na mwaka ujao wa fedha safari hiyo inaanza. Kazi hii tutaifanya kwa awamu na kwa hatua, lakini pia kwa utaratibu mpya ambao utaharakisha utekelezaji wa mradi. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika vitongoji 2,034 nchini ambavyo bado havijafikiwa na miundombinu ya umeme. Serikali kupitia REA kwa kuanzia imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 377.05** fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**256. Mheshimiwa Spika,** Wizara inakamilisha kufanya uchambuzi na kuandaa mapendekezo ya namna ya kupata fedha zitakazowezesha kufikisha umeme katika vitongoji vyote vilivyosalia Tanzania Bara ndani ya miaka mitano, badala ya takriban miaka 20 kwa kutegemea vyanzo vya sasa vya Mfuko wa Nishati Vijijini.

**iii) Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili B**

**257. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia REA itakamilisha utekelezaji wa mradi huu na hivyo kuwezesha ujenzi wa jumla ya kilomita 4,246 za msongo mdogo, ufungaji wa mashineumba 1,277 na kuunganisha wateja wa awali 95,334 katika mikoa tisa (9) ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe na Songwe. Jumla ya **Shilingi bilioni 24.76** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**iv) Mradi waKuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vyaKusambaza bidhaa za Mafuta ya Petroli Vijijini**

**258. Mheshimiwa Spika,** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea kuwawezesha waendelezaji wa miradi ya ujenzi wa vituo vidogo vya bidhaa za mafuta katika maeneo ya vijijini ambayo hayana huduma hizo. Uwezeshaji utafanyika kwa njia ya mikopo ya gharama nafuu. Serikali imetenga Shilingi bilioni 10.00 fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Serikali pia itaboresha utaratibu wa utoaji wa mikopo kulingana na mahitaji ili wahitaji wengi zaidi wa maeneo ya vijiji waweze kuipata.

**v) Mradi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme Jua kwenye Makazi Yaliyo Visiwani**

**259. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu kufunga na kusambaza mifumo ita  kayozalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika makazi yaliyo kwenye visiwa 41 vya Mikoa ya Kagera (6), Lindi (3), Mara (10), Mwanza (11) na Rukwa (1). Mradi utahusisha ufungaji wa mifumo ya umeme jua 7,000 katika makazi. Gharama za Mradi ni **Shilingi bilioni 9.4** ambapo katika mwaka 2023/24, **Shilingi bilioni 3.52,** fedha nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**vi) Programu yaKuwezesha Waendelezaji wa Miradi Midogo ya Nishati Jadidifu Vijijini chini ya Utaratibu waKusaidia Uandaaji wa Miradi (PPSF)**

**260. Mheshimiwa Spika**, Programu hii inalenga kutoa msaada wa kiufundi na fedha kwa waendelezaji wa miradi midogo ya nishati jadidifu vijijini chini ya Utaratibu wa Kusaidia Uandaaji wa Miradi ili kupata ufadhili kwa ajili ya uendelezaji wa miradi yao. Programu hii itawezesha waendelezaji wa miradi nane (8) kuandaa maandiko ya miradi ikiwemo Mpango wa Biashara; Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; na Upembuzi Yakinifu. Serikali kupitia REA imetenga **Shilingi bilioni 4.70** fedha za nje kwa ajili ya kazi hiyo.

**vii) Mpango wa Uendelezaji Miradi ya Nishati Jadidifu Inayofua Umeme kwaKutumia Nguvu ya Maji**

**261. Mheshimiwa Spika**, Mpango huu unahusisha kuwawezesha Waendelezaji wadogo wa miradi ya kufua umeme kwa kutumia maji (mini grids) nchini. Lengo la Mpango huu ni kutoa motisha kwa Waendelezaji hao na kuvutia uwekezaji zaidi katika miradi hiyo. Katika Mpango huu, Serikali kupitia REA itatoa ruzuku kwa Waendelezaji wa wa miundombinu yenye uwezo wa kufua umeme hadi kufikia **MW 10.** Jumla ya **Shilingi bilioni 5.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**F.6: UENDELEZAJI WA RASILIMALI YA JOTOARDHI**

**262. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TGDC itaendelea na utekelezaji wa kazi za uhakiki na kufanya utafafiti wa Juu ya ardhi *(Surface exploration)* wa miradi ya Jotoardhi itakayowezesha uzalishaji wa **MW 200** kwa kuanzia. Aidha, kazi zilizo pangwa kutekelezwa mwaka 2023/24 kwa kila mradi ni kama ifuatavyo:

**i) Miradi wa Jotoardhi Ngozi (Mbeya)- MW 70**

**263. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TGDC itakamilisha utekelezaji wa programu ya uchorongaji wa visima vitatu (3) vya uhakiki ili kuhakiki hifadhi, kiwango na ubora wa rasilimali ya jotoardhi katika eneo la Ngozi (Mbeya). Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 7.0** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**ii) Mradi wa JotoardhiKiejo-Mbaka (Mbeya) – MW 60**

**264. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TGDC itakamilisha taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi *(Drilling Consultant)* na kuanza utekelezaji wa programu ya uchorongaji wa visima vinne (4) vya uhakiki, kutekeleza miradi ya matumizi mengineyo *(direct heat use projects)* na kuanza maandalizi ya awali ya upatikanaji wa mtambo mdogo wa kuzalisha umeme *(wellhead generator)*. Jumla ya **Shilingi bilioni 10.26** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Kati ya hizo, **Shilingi bilioni 7.00** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 3.26** ni fedha za nje.

**iii) Mradi wa Jotoardhi Songwe (Songwe)- MW 5**

**265. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TGDC itaendelea na utekelezaji wa miradi ya matumizi mengineyo na kufanya maandalizi ya kuchoronga visima virefu vinne (4) vya uhakiki. Serikali kupitia TANESCO imetenga **Shilingi milioni 316.70** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

iv) Mradi wa Jotoardhi Luhoi(Pwani) – MW 5

**266. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TGDC itaendelea na maandalizi ya kutekeleza programu ya uchorongaji wa visima virefu vitatu (3) vya uhakiki katika eneo la mradi pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa kina kwa ajili ya matumizi mengineyo. Jumla ya **Shilingi milioni 265.26** zimetengwa na Serikali kupitia TANESCO kwa ajili ya kazi hizo.

**v) Mradi wa Jotoardhi Natron (Arusha) – MW 60**

**267. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TGDC itakamilisha utafiti wa kina wa kisayansi juu ya ardhi *(detailed surface exploration)* katika eneo la mradi ambapo **Shilingi milioni 495.01** zimetengwa na Serikali kupitia TANESCO kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

**F.7: UTEKELEZAJI WA MIKAKATI NA MIPANGO MBALIMBALI YA UENDELEZAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU**

**268. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaendelea kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ili kuendeleza Sekta ya Nishati. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha uhuishaji wa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme *(Power System Master Plan),* 2020 na kutekeleza Mpango Kabambe wa Kupeleka Nishati Vijijini

*(Rural Energy Master Plan)*. Kazi nyingine ni kukamilisha maandalizi ya Mikakati ya Kitaifa ya Nishati Jadidifu, Matumizi Bora ya Nishati na Mkakati wa Tungamotaka pamoja na kuen delea na usimamizi na uratibu wa utekelezaji wa mradi wa Matumizi Bora ya Nishati na utekelezai wa Dira ya Taifa na Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia na Mwelekeo wa Maboresho Katika Sekta Ndogo ya Umeme *(Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap (ESI-RSR)*. Jumla ya **Shilingi milioni 468.56** fedha za ndani zimepangwa kwa ajili ya kazi hizo.

**F.8: UTEKELEZAJI WA MIKAKATI NA MIPANGO MBALIMBALI YA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA**

**269. Mheshimiwa Spika,** mwezi Julai, 2023 Serikali inatarajia kuzindua Dira ya Taifa ya Nishati Safi ya Kupikia inayolenga kuhakikisha Taifa linahamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka, 2033. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuandaa na kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia; kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia; kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo inayohusu nishati safi ya kupikia; kusimamia Mfuko wa Taifa wa Nishati safi ya kupikia; kusimamia uboreshaji wa miundombinu ya nishati safi ya kupikia; na kujenga uwezo wa wataalamu katika kusimamia masuala ya nishati safi ya kupikia. Serikali kupitia Wizara ya Nishati na REA imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 4.5** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**270. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia REA itatekeleza mradi wa kujenga mifumo ya kuzalisha nishati ya bayogesi kwa ajili ya kupikia katika taasisi takriban 100 zin  azohudumia watu zaidi ya 300 katika maeneo mbalimbali nchini. Serikali kupitia REA imetenga jumla ya Shilingi bilioni 9.00 fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**271. Mheshimiwa Spika**,Serikali kupitia REA itasambaza majiko banifu 70,000 katika maneo ya vijijini na vijiji-miji *(peri urban)* yaliyotengenezwa kwa teknolojia ambayo ina ubunifu wa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuwa na ufanisi mkubwa, hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira na uzalishaji wa

hewa ukaa. **Shilingi bilioni 4.70** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya usambazaji wa majiko hayo.



*Wafanyakazi wa REA, wakigawa Majiko ya aina mbalimbali yaliyotengenezwa kwa teknolojia inayopunguza matumizi ya kuni na mkaa ili kulinda uharibifu wa mazingira.*

**272. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia REA itatekeleza mradi wa utoaji wa ruzuku ya mitungi ya gesi ya LPG, majiko na vifaa vyake (gas cylinders, stoves and its accessories) katika maeneo ya vijijini, ambapo mitungi ipatayo 200,000 itatolewa kwa wananchi pamoja na mifumo ya kupikia kwa gesi asilia katika taasisi mbalimbali za umma. Serikali kupitia REA imetenga **Shilingi bilioni 10.00** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

**273. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC kwa kushirikiana na REA kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini, itaendelea na utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa mifumo ya kusambaza gesi asilia katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa mkuza wa bomba kuu la kusafirisha gesi asilia linalopita katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani ili wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo waweze kutumia gesi asilia kwa ajili ya kupikia. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; usanifu wa kina wa kihandisi; na ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha gesi asilia. Serikali kupitia REA imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 18.50** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo katika mwaka 2023/24.

## SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI

**274. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Serikali itaendelea kusimamia na kuendeleza Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi kwa kuchukua hatua mbalimbali, lengo likiwa ni kuhakikisha mchango wa Sekta hiyo katika maendeleo ya nchi unaimarika.

## F.9: UDHIBITI WA SHUGHULI ZA MKONDO WA JUU WA MAFUTA NA GESI ASILIA

**275. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia PURA inatarajia kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kupitia Duru ya Tano (5) ya zoezi hilo. Ili kuwezesha zoezi hilo, Serikali itakamilisha mapitio ya Mkataba Kifani wa Ugawanaji wa Mapato *(Model Production Sharing Agreement - MPSA),* 2013 kwa lengo la kuwa na MPSA mpya inayoendana na mazingira ya sasa. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2023. Aidha, kazi za kuweka mipaka ya Vitalu, kuandaa data na nyaraka za zabuni kwa ajili ya zoezi hilo zitakamilishwa. Zoezi la kunadi vitalu linakadiriwa kugharimu jumla ya **Shilingi bilioni 3.5.** Aidha, kwa mwaka 2023/24 Serikali kupitia PURA imetenga **Shilingi milioni 500** kwa ajili ya kazi za awali za maandalizi ya zoezi hilo.

**276. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia PURA itaendelea kusimamia shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Vitalu vya Kilosa-Kilombero, Tanga, Ruvu, Nyuni Area, Vitalu Namba 1, 2 na 4. Aidha, PURA itaendelea kusimamia shughuli za uendelezaji na uzalishaji katika Vitalu vya Ruvuma (Ntorya), Songo Songo na Mnazi Bay. Lengo ni kuhakikisha kuwa Kampuni hizo zinatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Mikataba. **Kiambatisho Na.12** kinaonesha Ramani ya Vitalu vya Utafutaji na Uendelezaji Maeneo ya Nchi Kavu na Baharini.

**277. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia PURA itasimamia shughuli ya kuchakata na kutafsiri taarifa za mitetemo zilizochukuliwa katika Kitalu cha Ruvuma eneo la kilomita za mraba 334 pamoja na usimamizi wa ukarabati *(work over)* wa kisima cha Ntorya -1 na uchorongaji wa kisima cha utafutaji (Chikumbi – 1). Aidha, PURA itaendelea na usimamizi na ukaguzi wa shughuli zinazotekelezwa katika vitalu vyote vya utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia nchini,

lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa Sheria na Mikataba husika inazingatiwa. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.774** fedha za ndani zimetengwa ili kuwezesha utekelezaji wa kazi hizo.

**F.10: MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI**

**278. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TPDC itaendelea na kazi mbalimbali katika Vitalu vya kimkakati vya TPDC ambavyo ni Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi– Wembere, Songo Songo Magharibi, Ziwa Tanganyika na Vitalu Na. 4/1B na 4/1C. Kazi zita kazotekelezwa ni pamoja na kutafuta Wabia wa Kimkakati watakaoshirikiana na TPDC katika uendelezaji wa Vitalu hivyo. Aidha, Serikali itaendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi atakayechoronga kisima katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini; kulipa fidia Wananchi watakaopisha mradi katika kitalu cha Eyasi - Wembere; ukusanyaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D urefu wa kilomita 260 za mstari katika kitalu cha Eyasi - Wembere; kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa mpango wa uchorongaji wa kisima cha utafiti katika Kitalu cha Songo Songo Magharibi; na kumpata Mkandarasi wa kukusanya taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D katika Kitalu cha Ziwa Tanganyika. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 24.86 kwa** ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2023/24 Serikali itakamilisha mchakato wa kutoa leseni kwa TPDC kwa Vitalu vya Kimkakati.

**279. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia PURA na TPDC itaendelea kusimamia Kampuni binafsi zinazofanya shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia hususan katika Vitalu vya Tanga na Ruvu. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia shughuli za uendelezaji na uzalishaji katika Vitalu vya Ruvuma (Ntorya), Songo Songo na Mnazi Bay. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa gesi asilia nchini na kuwa Kampuni hizo zinatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Mikataba na Sheria.

**F.11: MIRADI YA UENDELEZAJI, UCHAKATAJI NA USAFIRISHAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA**

**i) Miradi waKuchakata naKusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG)**

**280. Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya kihistoria, Serikali hatimaye imekamilisha mazungumzo na wawekezaji ambayo yalikwama na mikataba itawasilishwa katika Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuidhinishwa kama sheria inavyotaka kabla ya kusainiwa. Mradi huo utakaogharimu Dola za Marekani bilioni 42 utabadilisha taswira ya nchi yetu. Pia, Serikali imeanzisha Ofisi mahsusi ya Mradi wa LNG kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa mradi kwa ufanisi. Katika mwaka ujao wa fedha, kazi nyingine zinazotarajiwa kufanyika ni: kuanza kazi za awali za maan  dalizi ya mradi; kuanza tafiti mbalimbali za kitaalamu zikiwemo usanifu wa awali wa kihandisi *(Pre-FEED);* kuendelea kuwajengea uwezo Wataalamu wa Serikali katika uendeshaji na usimamizi wa mradi; kuendelea na stadi za kisayansi na stadi za mitambo itakayosimikwa katika eneo la mradi na kufanya tathmini kuhusu hali za wananchi waliolipwa fidia ili kupisha mradi *(post – compensation livelihood study)*. Jumla ya **Shilingi bilioni 6,** ambazo ni fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

Katika Kikao kijacho cha Bunge, Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria Mahsusi ya mradi huu, itakayosimamia uendeshaji na utekelezaji wa mikataba iliyoingiwa.

**281. Mheshimiwa Spika,** vilevile, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaanza kazi ya kuwaelimisha wajasiriamali wa nchi yetu kuhusu fursa zilizopo katika mradi huu na namna ya kuzifikia. Jitihada mahsusi zitafanywa ili wananchi wa mikoa ya Lindi na Mtwara waelewe nafasi na wajibu wao katika mradi na namna wanavyoweza kushiriki na kunufaika. Kama nilivyoeleza awali, ili kuwaandaa wataalamu wa kitanzania kufanya kazi katika mradi huu, Serikali katika mwaka ujao wa fedha itajenga Chuo kikubwa cha Kimataifa cha ufundi katika Gesi na Mafuta pamoja na Umeme mkoani Lindi. Vilevile, ili kupanua fursa na kushamirisha maendeleo ya viwanda na kuongeza ajira, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaanzisha Eneo Maalum la Kiuchumi *(Special Economic Zone)* katika eneo la mradi ili kuvutia viwanda

na shughuli nyingine za kiuchumi zitakazonufaika na miundombinu ya kiuchumi, ikiwemo bandari na umeme wa uhakika pamoja na gesi, itakayokuwepo kutokana na utekelezaji wa mradi huu wenye thamani ya **Dola za Marekani bilioni 42.**

**ii) Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Ntorya (Kitalu cha Ruvuma) hadi Madimba**

**282. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TPDC itaendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Ntorya hadi Madimba mkoani Mtwara. Lengo la mradi huu ni kuongeza uzalishaji wa gesi asilia ili kukidhi mahitaji yanay oendelea kuongezeka nchini. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 58.75** kwa ajili ya kazi hizo.

**F.12: MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA**

**iii) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani**

**283. Mheshimiwa Spika**, Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 12.6** kwa ajili ya usambazaji wa gesi asilia katika maeneo ya viwanda, majumbani, taasisi na matumizi ya gesi hiyo katika magari (CNG) kwa kuanzia katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, na Pwani kabla ya kuendelea katika mikoa mingine. Aidha, vituo viwili (2) vya CNG vitajengwa jijini Dar es Salaam na kimoja (1) mkoani Pwani.




*Mfano wa vituo viwili (2) vya CNG vitakavyojengwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.*

**iii) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara**

**284. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Lindi

na Mtwara kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani na taasisi mbalimbali. Serikali itakamilisha ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka valvu namba tatu (BVS 3) kuelekea Kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo mkoani Lindi. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 1.6** kwa ajili ya kazi hizo. **Kiambatisho Na.13** kinaoneshaujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka valvu namba tatu (BVS 3) kuelekea Kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo mkoani Lindi.

**v) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa Mingine**

**285. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia Nchini *(Natural Gas Utilization Master Plan 2016 - 2045) ulianza* kwa usamba  zaji wa gesi asilia katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam ambao unafanywa kwa njia ya mabomba ya mgandamizo mdogo kutokana na mikoa hiyo kufikiwa na miundombinu ya usafirishaji wa gesi hiyo. Kufikisha gesi asilia katika mikoa mingine kunahitaji teknolojia ya usafirishaji isiyohusisha mabomba kwa kuanzia *(virtual pipelines),* kutokana na teknolojia hizo kuonekana za gharama nafuu, ikilinganishwa na mabomba makubwa na miundombinu yake wezeshi.



*Kazi ya kuchimba mitaro na kuweka mabomba ya kusambaza Gesi Asilia kwa matumizi ya majumbani katika Mikoa waLindi.*

**286. Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kufikisha gesi asilia katika mikoa mingine, Serikali imeshirikiana na JICA kufanya tathmini na kuandaa Mpango wa Matumizi ya Gesi *(Domestic Natural Gas Promotion Plan - DNGPP).* Mpango huu unapendekeza kutumia teknolojia ya kufikisha gesi asilia katika maeneo yaliyo mbali na miundombinu ya mabomba kwa kusafirisha gesi kimiminika (LNG) au gesi iliyoshindiliwa (CNG) kwa njia ya barabara au treni. Aidha, tathmini ya awali iliyohusisha mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Dodoma, Tanga na Morogoro imeonesha uwepo wa mahitaji ya kutosha ya gesi asilia kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Aidha, mwezi Machi, 2023, Serikali kupitia Wizara ya Nishati ilisaini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na JICA kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Mpango wa DNGPP kwa kuanzia na mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Dodoma.

**287. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa mpango huu, TPDC ipo katika mazungumzo na wawekezaji binafsi ili kuboresha mazingira na kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika kuharakisha usambazaji wa gesi asilia katika mikoa mingine. Kwa kuanzia katika miradi ya CNG, Serikali imeweka utaratibu mfupi wa kampuni kuwekeza ambapo baada ya kupata idhini ya TPDC, mwekezaji huomba kibali cha ujenzi na leseni ya kufanya biashara ya CNG kutoka EWURA. Katika hatua nyingine, Serikali kupitia TPDC inaangalia namna bora ya utekelezaji wa miradi ya CNG, ikiwemo kuwa na kanda (zones) za ujenzi wa miundombinu ili pamoja na kuwezesha kufikisha gesi asilia katika maeneo mengi zaidi, wawekezaji waweze kurejesha gharama za uwekezaji wao.

**F.13: MIRADI YA KUSAFIRISHA GESI ASILIA KWENDA NCHI JIRANI**

**288. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya usafirishaji wa gesi asilia kwenda nchi jirani za Kenya na Uganda kwa kuzingatia Makubaliano ya Awali (MoU) yaliyofikiwa kati ya Serikali na nchi hizo. Aidha, Serikali itakamilisha uidhinishaji wa nyaraka muhimu za mradi pamoja na kuwapata Washauri Waelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa miradi hiyo. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi milioni 420.7** kwa ajili ya kazi hizo.

**289. Mheshimiwa Spika,** pamoja na majadiliano kati ya Kenya na Uganda yanayoendelea, Serikali imeanza majadiliano ya awali

na nchi za Malawi na Zambia ili kuona namna bora ya kupeleka gesi asilia katika nchi hizo kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Hii ni hatua mahsusi inayolenga kuboresha masuala ya kibiashara na kutekeleza makubaliano ya kikanda katika kuhakikisha rasimali za nchi moja zinaisaidia nchi nyingine.

**290. Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuongeza usalama na uhakika wa upatikanaji wa gesi asilia nchini *(security of supply)* pamoja na kuifanya nchi kuwa kitovu cha gesi asilia, Serikali imeanza mazungumzo ya awali na Serikali ya Msumbuji ili kuona uwezekano wa kujenga bomba la gesi asilia litakalounganisha nchi hizo. Ujenzi huu utawezesha kiasi kikubwa cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini Msumbuji kutumika Tanzania au kupita kuelekea nchi jirani na hivyo kufanya miundombinu yetu kuwa na faida zaidi.

**F.14: MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUHIFADHI MAFUTA**

**i) Mradi wa Bomba laKusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline - EACOP)**

**291. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kushiriki katika uwekezaji wa mtaji wa Kampuni ya EACOP kupitia malipo ya hisa za Kampuni hiyo; kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi; kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo kwa maeneo yanayopitiwa na mradi; na kuendelea kusimamia ujenzi wa mradi pamoja na wawekezaji wengine. Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 70.2,** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ambapo, **Shilingi bilioni 4.6** zitatolewa na TPDC kutokana na mapato yake ya ndani.

**F.15: UJENZI WA MIUNDOMBINU YA HIFADHI YA KIMKAKATI YA MAFUTA PAMOJA NA MIUNDOMBINU YA KUWEZESHA BIASHARA YA MAFUTA**

**ii) Ujenzi wa Miundombinu yaKuhifadhi Mafuta ya Kimkakati**

**292. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za mafuta na kuifanya nchi yetu kuwa kitovu cha upokeaji mafuta *(Petroleum Hub),* Serikali iliingia makubaliano na Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Umoja wa Falme za Kiarabu (ENOC) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi mafuta. Kwa sasa, Serikali kupitia TPDC inaendelea na taratibu za utwaaji wa eneo

lililopo Kigamboni jijini Dar es Salaam kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**iii) Ukarabati wa Tenki Namba 8 na Uanzishaji wa Hifadhi za Mafuta katika Maeneo yaKimkakati**

**293. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TPDC itakamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa Tenki Na. 8 lililopo eneo la TIPER Kigamboni kwa ajili ya kuhifadhia mafuta. Aidha, TPDC itakamilisha taratibu za upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa matenki matatu (3) ya kuhifadhia mafuta katika eneo la Kigamboni – Dar es Salaam. Serikali kupitia TPDC imetenga **Shilingi bilioni 17.1** kwa ajili ya kazi hizo.

**iv) Uboreshaji wa Miundombinu yaKupakiaKondenseti kwenye Meli**

**294. Mheshimiwa Spika,** katika kushamirisha biashara ya kondenseti inayozalishwa katika mitambo ya kuchakata gesi asilia iliyopo nchini, Serikali kupitia TPDC itaboresha miundombinu ya kupakia kondenseti kwenye meli kwa kuongeza urefu wa miundombinu hiyo kuelekea baharini kwa lengo la kuondokana na changamoto ya kusubiri maji kujaa ili upakuaji uweze kufanyika. Aidha, TPDC itamtafuta Mshauri Mwelekezi atakayeshauri namna bora ya ujenzi wa bomba hilo. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla **ya Shilingi milioni 717.5** kwa ajili ya kazi hiyo.

**F.16: USHIRIKI WA TPDC KATIKA BIASHARA YA UAGIZAJI MAFUTA**

**295. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC itaendelea kushiriki katika biashara ya uagizaji wa bidhaa za mafuta kama muingizaji *(supplier)* kupitia mfumo wa BPS ambapo jumla ya **Shilingi trilioni 1.57 zitatumika**. Aidha, ununuzi wa mafuta kupitia mfumo wa uagizaji kwa pamoja hauhusishi matumizi ya fedha taslimu bali kupitia dhamana ya benki ambapo kwa udhamini wa benki, TPDC hupokea mafuta kutoka kwa wauzaji na hulipia mafuta hayo baada ya kuyasambaza na kukusanya fedha kutoka kwa wanunuzi. Kiasi hicho kitatumika kuagiza shehena sita (6) za mafuta zinazokadiriwa kuwa na ujazo wa tani 100,000 kwa kila shehena.

**296. Mheshimiwa Spika,** Serikali ilianza shughuli za uagizaji wa mafuta kwa pamoja kupitia TPDC mwaka 2021/22 ambapo kwa sasa TPDC imekuwa ikiagiza na kutunza mafuta hayo katika maghala ya wawekezaji binafsi ambapo kumekuwa na gharama za ulipaji wa tozo za kuhifadhi mafuta. Ili kuhakikisha kuwa biashara hii inafanyika kwa ufanisi na kuleta manufaa yanayotarajiwa kwa nchi, ni muhimu kuiwezesha TPDC kuwa na maghala yake ya kupokelea na kuhifadhia bidhaa za mafuta. Katika kufanikisha azma hiyo, TPDC imekamilisha taratibu za utwaaji wa maeneo ya kujenga maghala ya kimkakati ikiwemo katika maeneo ya Tanga (Chongoleani), Dodoma (Zuzu) na Dar es Salaam (Kigamboni) kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa maghala hayo.

**F.17: MRADI WA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA RASILIMALI ZA ASILI TANZANIA**

**297. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi huu ambapo shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kudurusu Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato ya mafuta na gesi asilia (MPSA), 2013; ununuzi na usimikaji wa Kabati Maalumu za kutunzia takwimu za utafiti wa mafuta na gesi; kukamil  isha ununuzi na usimikaji wa miundombinu ya mfumo wa uondoshaji shehena mipakani; na kuwajengea uwezo watumishi takriban 100 katika tasnia ya uziduaji. Serikali imetenga **Shilingi bilioni 3.72** fedha za nje kwa ajili ya mradi huu.

**F.18: MAJUKUMU YATAKAYOTEKELEZWA NA KAMPUNI TANZU ZA TPDC (TANOIL & GASCO)**

**i) Ushiriki wa TPDC katika Biashara ya Mafuta Kupitia TANOIL**

**298. Mheshimiwa Spika,** TPDC kupitia kampuni yake Tanzu ya TANOIL itaendelea kushiriki katika biashara ya usambazaji wa bidhaa za mafuta nchini. Kwa mwaka 2023/2024 Kampuni ya TANOIL imepanga kutumia **Shilingi bilioni 555.5** katika biashara hiyo. Aidha, katika kuongeza mtandao wa biashara ya mafuta, Serikali kupitia TANOIL itakamilisha ukarabati wa vituo sita (6) katika maeneo ya Makuyuni (Arusha), Singida, Musoma na Tarime (Mara), Segera (Tanga) na Geita. Pia, TANOIL itatafuta Wakandarasi wa ujenzi wa vituo vipya vinne (4) katika mikoa ya

Kigoma (2), Dodoma (1) na Morogoro (1). Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 3.5** kwa ajili ya kazi hizo.

**299. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, TPDC kupitia TANOIL ina mpango wa kuwa na kituo angalau kimoja kwa kila Wilaya na tayari taratibu za upatikanaji wa viwanja vya ujenzi wa vituo hivyo zimeanza. Aidha, TANOIL itatafuta Mbia wa Kimkakati wa kimataifa mwenye uwezo, uzoefu na weledi katika biashara ya mafuta ili kushirikiana naye katika biashara hii muhimu.

**ii) Uendeshaji na matengenezo ya Miundombinu ya Taifa ya Gesi Asilia nchini kupitia GASCO**

**300. Mheshimiwa Spika,** TPDC kupitia kampuni yake Tanzu ya GASCO itaendelea kuendesha miundombinu ya Taifa ya Gesi Asilia nchini ambapo kwa mwaka 2023/24, TPDC kupitia GASCO imepanga kutumia **Shilingi bilioni 54.85** kwa ajili ya kulipia gharama za uendeshaji na usimamizi wa miundombinu ya kuchakata gesi asilia iliyoko Songo Songo na Madimba, bomba la gesi asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam na mtandao wa mabomba ya usambazaji gesi asilia iliyopo Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam.

**F.19: UDHIBITI WA MASUALA YA NISHATI KUPITIA EWURA**

**301. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia EWURA itaendelea kusimamia shughuli za udhibiti wa Sekta ya Nishati kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. EWURA itaendelea kutoa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta na gesi pamoja na kutoa leseni za kuendesha bishara hizo ikiwemo leseni ya kuendesha biashara ya CNG baada ya ujenzi wa vituo vinavyoendelea kujengwa kukamilika. Aidha, EWURA itaanza ujenzi wa majengo ya ofisi za kanda za Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini na kununua viwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Kanda ya Ziwa, Magharibi na Kati; na kuhuisha Kanuni mbalimbali ili kuboresha utoaji wa huduma.

**F.20: KUIMARISHA UTENDAJI KAZI NA UTOAJI HUDUMA**

**302. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kusimamia ukamilishaji wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Wizara katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Wizara imesimamia taasisi zinazotoa huduma kwa wananchi lakini pia zinazowezesha maendeleo ya

kiuchumi na kijamii. Kwa kutambua dhamana hiyo, Wizara itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha taasisi zilizo chini yake ili ziweze kujiendesha kwa tija na ufanisi na kutoa huduma bora kwa wananchi na wadau.

**303. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 174 na kuwahamishia Wizarani watumishi 76 ili kukabiliana na upungufu wa watumishi uliopo. Aidha, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 4,219.

**G. USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA**

**304. Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo, Jumuiya na nchi wahisani ambao wameendelea kutoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Napenda kutambua mchango wa: Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); *Arab Bank for Economic Development in Africa (BADEA);* Mfuko wa Uendelezaji wa *Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea);* Jotoardhi *(Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF)* pamoja na Taasisi na Mashirika ya: JICA (Japan), KfW (Germany), AFD (Ufaransa); Shirika la Fedha Duniani (IMF); SIDA (Sweden), NORAD (Norway); Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) na USAID (Marekani); *OPEC Fund for International Development; Abu - Dhabi Fund for Development* (ADFD); na *Saudi Fund for Development (SFD);*

**305. Mheshimiwa Spika,** nitumie nafasi hii pia kutoa shukrani kwa Serikali za Afrika Kusini, Algeria, Burundi, Canada, China, DRC Congo, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Iceland, India, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Malawi, Marekani, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, Norway, Rwanda, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uingereza, Uje rumani, Zambia, na nchi nyingine kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Sekta ya Nishati. Nazishukuru pia Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maende leo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu Sekta ya Nishati.

## H. HITIMISHO

**306. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Wizara ya Nishati itaendelea kuimarisha utendaji na usimamizi wa Sekta ya Nishati, kwa lengo la kuhakikisha kuwa sekta hii inaendelea kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi, uboreshaji wa huduma kwa wananchi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

**307. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau, ikiwemo Sekta Binafsi itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini unaoto kana na vyanzo mbalimbali ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na maendeleo ya viwanda, utoaji wa huduma na biashara. Wizara itaendelea pia kuimarisha uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia ili mchango wa shughuli hizo katika maendeleo ya Taifa letu uendelee kuimarika. Hatua nyingine zitakazochukuliwa ni kuimarisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia mijini na vijijini ili kulinda afya za wananchi na mazingira kutokana na matumizi ya nishati chafu na isiyo rafiki wa mazingira.

**308. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa nishati katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na burudani katika maeneo ya vijijini na vitongojini, Wizara itaendelea kuweka mkazo katika kuharakisha upatikanaji wa nishati katika maeneo hayo. Aidha, pamoja na hatua zilizochukuliwa hadi sasa za kuimarisha usimamizi wa miradi ya nishati vijijini, Wizara pia itaendelea kuimarisha na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati na kwa viwango vilivyokusudiwa.

**309. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 3,048,632,519,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi 2,960,702,821,000** sawa na **asilimia 97.1** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,609,156,128,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 351,546,693,000** ni fedha za nje; na

ii. **Shilingi 87,929,698,000** sawa na **asilimia 2.9** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 71,637,112,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 16,292,586,000** kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**310. Mheshimiwa Spika,** naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.nishati.go.tz. Vile vile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatishwa kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

**311. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, aje awasilishe maoni ya Bunge. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nianze kutumia fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameturuzuku uhai na afya njema.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Nishati Fungu Na. 58 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne kama inavyoelezwa kwenye taarifa ukurasa wa kwanza na wa pili. Naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na uzingatiaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati, kuhusiana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2023, Kamati ilikagua miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Tanga, Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyokaguliwa ni pamoja na mradi wa *REA* katika Mkoa wa Tanga Wilaya ya Korogwe, mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani, mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze (Namba ya Mradi 3272), mradi wa upanuzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I - *Kinyerezi I Extension MW 185* na mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika Mkoa wa Dar es Salaam, Lindi na Pwani na kituo cha kupokelea gesi asilia cha Kinyerezi *(GASCO)*.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya miradi hii yanapatikana kuanzia ukurasa wa tatu hadi wa 12 wa taarifa yetu nami nitayasema kwa uchache sana. Nijielekeze tu kwenye mradi wa upanuzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi. Mradi wa Kinyerezi *I Extension - MW 185* ulibuniwa ili kuongeza uwezo na upanuzi wa kituo cha Kinyerezi I chenye kuzalisha *MW* 335. Mradi unahusisha usimikaji wa mitambo minne (4) ya kuzalisha umeme kuongeza uwezo wa njia ya kusafirisha umeme inayotoka Kinyerezi hadi Gongolamboto yenye msongo wa Kv 132.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaukagua mradi ulikuwa umefikia asilimia 93.2. Kamati ilishuhudia mitambo mitatu kati ya minne ikiwa imewashwa na kuingiza *MW* 135 kwenye gridi ya Taifa. Aidha kazi ya kuunganisha mtambo wa mwisho ilikuwa inaendelea. Katika taarifa ya Wizara iliyosomwa hivi punde taarifa

inaonesha mradi wa nne ambao ulikuwa bado kukamilika sasa umekwisha washwa. Kamati inaipongeza Wizara kwa kutekeleza ahadi yake.

Mheshimiwa Spika, sasa eneo lingine ni maoni na ushauri kuhusiana na miradi hiyo ambayo ilienda kukaguliwa na maoni haya yanapatikana katika ukurasa wa 13 mpaka 15 la taarifa yetu. Eneo la kwanza ni kuhusiana na changamoto za Wakandarasi wa *REA*.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa kabla ya Wakandarasi wa *REA* kupewa mikataba ya kazi, uchunguzi wa kina *(Due diligence)* ufanyike ili kuufahamu undani wao ili kuepuka usumbufu katika utekelezaji wa miradi. Aidha, vipengele vya mkataba na Kampuni ya Tontan inayotekeleza mradi wa Lot 39 viangaliwe na hatua kali zichukuliwe ili iwe fundisho kwa Wakandarasi wengine ambao wamekuwa wakisuasua kukamilisha miradi licha ya kupokea fedha kutoka Serikalini.

Wakandarasi wazawa ambao wanatekeleza kazi zao vizuri ni vyema ukawekwa utaratibu utakao wezesha kupewa kipaumbele maalum ili Wakandarasi wengine wakubwa wanaposhindwa, Wakandarasi kutoka nje wanaposhindwa kukamilisha kazi zao basi kazi hizi wapewe wakandarasi wazawa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusu kuchelewa kwa miradi ya *TANESCO* na hapa tunapendekeza kwamba: -

Uchunguzi wa kina ufanyike kwa Wakandarasi wa nje ili kuepuka kukwama kwa miradi kunakotokana na maelezo kuwa Wakandarasi wamefilisika, vilevile tunapendekeza kwamba Serikali isiwaache peke yao wakandarasi wadogo wanaofanya kazi za *sub-contractors* kwa miradi mikubwa ya Wakandarasi kutoka nje na pale ambapo wakandarasi hawa wamefilisika basi fedha ambazo zinakuwa ni kwa ajili ya *Performance Guarantee Bond* ziweze kutumika kuwalipa wakanndarasi wazawa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwepo wa changamoto ya upatikanaji wa vifaa zikiwemo nguzo, Wizara ihakikishe vifaa vyote

zikiwemo nguzo za kutosha zinapatikana ili utekelezaji wa miradi usichelewe.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuchelewa kwa kukamilika miradi ya *TANESCO,* kutokana na kuchelewa huku mapendekezo yetu ni kwamba *TANESCO* ijengewe uwezo wa kiutendaji wa kusimamia miradi uweze kuimarishwa ili miradi iweze kukamilika kwa wakati. Pia *TPDC* iongeze kasi ya kuunganisha gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani na kwenye Taasisi. Aidha, Sekta Binafsi ishirikishwe ili kuleta ufanisi hususan katika kusambaza gesi ya kutumia kwenye magari na mwisho Wizara isimamie kikamilifu mradi wa bomba la mafuta la kutoka Hoima hadi Chalinze ili ujenzi wa mradi huu uende kwa kasi na kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa najielekeza katika uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli kufikia Februari mwaka 2023. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi bilioni 20.3 hadi kufikia Februari 2023, shilingi bilioni 4.4 sawa na asilimia 22 tu zilikuwa zimekusanywa kama inavyoonekana katika kielelezo Namba Mbili.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, chanzo hiki mara kwa mara kimekuwa hakifikii malengo inayojiwekea. Kamati inaona ipo haja ya kupunguza makadirio haya ili kuwa na uhalisia wa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha kufikia Februari, 2023. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Wizara ya Nishati ilitengewa shilingi trilioni 2.9 zinazojumuisha matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 82.9 na shilingi trilioni 2.28 kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2023 Wizara imepokea shilingi trilioni 1.5 sawa na asilimia 52.6 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba Tatu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini pia kuwa, fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni asilimia 39.8 tu. Kamati bado hairidhishwi na upatikanaji wa fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwa kiasi kikubwa Wizara imejitahidi kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kwa baadhi ya hoja ambazo zilikuwa bado hazijatekelezwa kikamilifu, Kamati itaendelea kusisitiza tena katika taarifa hii. Ni rai ya Kamati kuwa utekelezaji wa mapendekezo na ushauri huo uende kwa kasi ili kusaidia kuimarisha sekta ya nishati kama inavyoainishwa katika aya ya 63 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Uchambuzi wa malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama inavyoonekana kwenye taarifa ya kamati kwenye ukurasa wa 20.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya imekadiria kukusanya shilingi milioni 20.3 kama inavyoonekana kwenye kielelezo Namba Tano. Hata hivyo, Kamati inapata mashaka na makadirio ya makusanyo haya kutokana na kukosa uhalisia. Itakumbukwa kuwa, katika mwaka wa fedha 2021/2022 makusanyo kufikia Februari yalikuwa ni asilimia 28 tu. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 makusanyo kufikia Februari, 2023 nayo yalikuwa ni asilimia 21.7 tu ya lengo. Kamati inaona ni vema makadirio haya yawe na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara inakadiria kutumia shilingi trilioni 3.04. Fedha hizi zinajumuisha fedha za maendeleo shilingi tilioni 2.69 na matumizi ya kawaida shilingi bilioni 87.9. Kielelezo Namba Sita kinachanganua mchanganuo huu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, bajeti imeongezeka kutoka asilimia 4.9 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba Saba. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii. Hata hivyo,

ongezeko la fecha za maendeleo kutoka nje ni asilimia 109.9. Kamati inapata mashaka na uhakika wa upatikanji wake hasa ikizingatiwa kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia Februari, 2023 wakati Kamati ilipokuwa inapokea taarifa upatikanaji wa fedha hizi ulikuwa ni asilimia 39.86 tu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa masuala mahsusi. Kamati imefanya uchambuzi wa masuala mahsusi ambayo yana maslahi kwa Taifa kama ifuatavyo: -

(i) Hali ya upatikanaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati ina jukumu la kuhakikisha kuwa wakati wote uzalishaji wa umeme na uimarishaji wa miundombinu ya kusafirishia umeme nchini unakuwa wa uhakika. Hata hivyo, pamoja na malengo hayo, hali ya umeme bado siyo ya kuridhisha kutokana na umeme kuwa unakatika mara kwa mara. Kamati imebaini kufikia mwezi Februari, 2023 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulikuwa *MW* 1,822.05 kama inavyooneka kwenye Kielelezo Na.10 sawa na ongezeko la asilimia 7.52 ikilinganishwa na *MW* 1,694.55 zilizokuwepo kufikia mwezi Juni, 2022. Ni dhahiri kuwa, ongezeko la *MW* 127.5 ni dogo sana kuweza kuhimili kasi ya ongezeko la mahitaji ya umeme nchini kutokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Aidha, ongezeko hili dogo linaiweka nchi kwenye hatari ya kutoweza kuhimili changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza kwenye mitambo ya kuzalisha na kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Taifa letu kuwekeza zaidi rasilimali fedha kwenye sekta hii ili kuweza kuongeza na kuboresha miundombinu ya kuzalisha umeme. Naomba kurudia, Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Taifa letu, kuwekeza zaidi rasilimali fedha kwenye sekta hii ili kuweza kuongeza na kuboresha miundombinu ya kuzalisha na kusambaza umeme. Aidha ipo haja ya kuimarisha usimamizi wa miradi, na kuongeza kasi ya kukamilisha miradi ya kuzalisha umeme ambayo inaendelea nchini kwa sasa hususan mradi wa kimkakati wa Bwawa la Mwalimu Nyerere.

(ii) Hali ya mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini uwepo wa akiba ya mafuta inayokidhi mahitaji ya nchi. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2022 hadi Februari, 2023 akiba ya mafuta nchini imeendelea kuwa juu ya wastani wa siku za matumizi kwa zaidi ya siku 25 ikiwa ni zaidi ya asilimia 35 ikilinganishwa na siku 15 za akiba ya mafuta inayotakiwa kuwepo kulingana matakwa ya Leseni ya biashara ya jumla ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023, jumla ya tani milioni 4.2 za mafuta ziliingizwa kwa matumizi ya ndani ya nchi na nchi za jirani kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Namba 11. Tangu kuanza kutumika kwa mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja mfumo umeimarika na kuendelea kuaminika na nchi takriban saba na kuongeza kiwango cha mafuta yanayoagizwa katika nchi hizo kupitia mfumo huuwa uagizaji wa pamoja. Kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia vema uendeshwaji wa mfumo huu na tunasisitiza tusiruhusu jambo lolote liuvuruge mfumo huu kwani kuvurugika kwake kunaweza kusababisha mafuta haya kuondoka kwenye mfumo wetu nchini na hivyo kupoteza faida za kiuchumi tunazopata kutokana na mafuta haya kupitia nchini. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, uwepo wa mafuta haya kwenye hifadhi za nchi yetu kunatuhakikishia uhahika wa kuwepo kwa mafuta nchini, hivyo kama Taifa tuna kila sababu ya kuhakikisha hatuipotezi faida hii.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kwa vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine tangu mwezi Machi, 2022 kumeifanya dunia kushuhudia uwepo wa athari za kiuchumi zilizotokana na kuongezeka kwa bei za mafuta kwa kiwango kikubwa, na hivyo kusababisha kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa Dola ya Marekani. Nchini kwetu kampuni za mafuta zimejikuta zikichelewa kulipia shehena zao za mafuta na hivyo shehena hizo kulazimika kubaki katika maghala ya mafuta chini ya uangalizi wa mletaji mafuta hadi pale yanapolipiwa. Hali hii imesababisha uhaba wa nafasi ya kupokelea shehena nyingine ya mafuta jambo ambalo linasababisha kupungua kwa ufanisi wa mfumo wa *BPS*.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na changamoto ya upatikanaji wa Dola ya Marekani na hivyo shehena za mafuta kulazimika kubaki katika maghala chini ya uangalizi wa mletaji, ni rai ya Kamati kuwa Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ione umuhimu wa kuongeza kasi cha uuzaji wa Dola ya Marekani katika soko. Aidha, mapitio ya haraka ya mwongozo wa uendeshaji wa soko la fedha wa mwaka 2020 yanahitajika ili kuondoa vipengele vinavyokwamisha kufanyika kwa *Inter-Bank foreign exchange*. Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kuwa mafuta yanayoenda nchi jirani yanalipiwa na nchi husika na kwamba fedha zetu za kigeni zitumike kununulia bidhaa za nchi yetu tu ili kupunguza mzigo unaobebeshwa nchi yetu katika kulipia bidhaa za nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye maoni na ushauri wa mapendekezo ya kamati ya jumla. Baada ya uchambuzi huo wa kina, Kamati inapenda kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania *(TANESCO)* ni mapendekezo ya Kamati kuwa: -

a) Ili kuepuka changamoto ya kuchelewa kutekelezwa kwa miradi kwa wakati kama ambavyo imebainika kwenye ukaguzi wa miradi, *TANESCO* inapaswa kuwa na mkakati wa usimamizi wa miradi ili ile iweze kutekelezwa kikamilifu.

b) Kutokana na deni la mauzo ya gesi kutoka *TPDC* kwenda *TANESCO* kuendelea kukua hadi kufikia shilingi bilioni 720 wakati wa uchambuzi wa taarifa ya Wizara, Kamati inashauri kwamba mwaka huu wa fedha 2023/2024 deni hili lote lilipwe kwa mkupuo.

c) Taasisi za Serikali zinazodaiwa ankara za umeme shilingi bilioni 334.8, kwa mara nyingine Kamati inashauri hatua za maksudi zichukuliwe ili deni hili lilipwe kabla ya mwaka huu tunaoenda nao kukamilika.

d) Kutokana na ari kubwa ambayo nchi inayo katika kutekeleza miradi mikubwa kama Mradi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere, Serikali iangalie na kuanza mradi mwingine mkubwa wa kuzalisha umeme kama huu kwa kutumia fedha zetu za ndani ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini.

(iii) Wakala wa Umeme Vijijini – *REA*.

(a) Mkakati wa Serikali wa kutaka kuwasaidia Wakandarasi wa nje kwa kuwapatia dhamana *(Letter of Credit)* ujielekeze kwa Wakandarasi wazawa ambao ni wazalendo ili kuwainua.

(b) Vipengele vya mkataba na Kampuni ya Tontan inayotekeleza mradi wa Lot 39 viangaliwe na hatua kali zichukuliwe ili iwe fundisho kwa Wakandarasi wengine ambao wamekuwa wakisuasua kukamilisha miradi licha ya kupewa fedha na Serikali.

(c) Pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara na Serikali katika kuhamasisha nishati safi ya kupikia, Serikali katika mipango yake iwezeshe matumizi ya majiko ya umeme yenye presha *(pressure cookers)* zinazotumia umeme kidogo pamoja na Mkaa mbadala unaotokana na makaa ya mawe *(Rafiki Coal Briquette)* ambao umethibitishwa kutokuwa na hewa/kemikali zinazosababisha uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya ya watumiaji. Aidha, Serikali ione namna ya kupunguza kodi za uingizwaji wa majiko ya umeme yenye presha ili wananchi waweze kuyamudu.

(iv) Shirika la Maendeleo la Petroli *(TPDC)*

(a) Kamati imebaini kasi ya usambazaji wa gesi majumbani na kwenye Taasisi bado hairidhishi. Kamati inaitaka *TPDC* kuhakikisha lengo hili linafikiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha makampuni 20 ambayo yamepewa idhini ya ujenzi wa vituo vya kujazia gesi yanaanza ujenzi huo mara moja.

(b) Mahitaji ya gesi nchini yameongezeka ikilinganishwa na hali ya uzalishaji ilivyo. Kamati inatambua mpango wa Serikali wa kuendeleza vitalu kikiwemo Kitalu cha Ruvuma. Kamati inasisitiza uzalishaji katika Kitalu hiki uanze mapema na vitalu vingine ili kusaidia katika uzalishaji wa umeme nchini na matumizi mengine ya majumbani na viwandani.

(c) Tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi kuanzia mwaka 2016/2017 kiasi cha shilingi bilioni 342.34 zimekusanywa. Kamati inatambua nia ya Serikali ya kuhakikisha fedha hizi zinasaidia vizazi vijavyo, Hata hivyo, kutokana na nia ya kuendeleza miradi ya *TPDC*, Kamati inashauri Serikali kuharakisha kuleta Marekebisho ya Sheria ili katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 iweze kupitishwa na Bunge lako.

(d) Kwa kuwa, Kampuni Tanzu ya ya *TANOIL* ina umuhimu wa kimkakati katika biashara ya mafuta nchini. Kupitia ushiriki wake kwenye biashara hii kunaiwezesha Serikali kuwa na jicho la moja kwa moja katika kuisimamia sekta hii.

(e) Ili *TANOIL* iweze kutimiza majukumu yake kikamilifu, ipo haja kwa kampuni hii kupewa kila aina ya msaada unaohitajika ili iweze kujiimarisha kwa kuwa na wafanyakazi wenye taaluma ya juu waliojengewa uwezo katika masuala ya biashara ya mafuta. Aidha, *TANOIL* iwezeshwe kimtaji ili iweze kujenga mtandao mpana na imara wa kibiashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli – *PURA*. Kamati inarudia ushauri ilioutoa Mwaka 2022 kuhusu kuharakishwa kwa mchakato wa kunadi vitalu vilivyowazi maeneo ya nchi kavu na baharini katika Duru ya Tano, hasa ikizingatiwa kuwa mahitaji ya gesi nchini yameongezeka ikilinganishwa na hali ya uzalishaji ambayo ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA*). Jukumu la kuweka Vinasaba kwenye mafuta awali lilikuwa linatekelzwa na *EWURA*. Hata hivyo, baadae jukumu hili lilihamishiwa kwa *TBS*. Kamati imebaini kuwa,

kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa jukumu hili ikiwa ni pamoja na *TBS* kushindwa kutengeneza vinasaba vyake kama ilivyoshauriwa awali. Kamati inashauri:-

(a) *TBS* iwezeshwe ili iweze kutengeneza vinasaba hivi na hivyo kusaidia kupunguza gharama katika bei ya mafuta; na

(b) *TBS* iwezeshwe kwa kuwa na watumishi wa kutosha na vitendea kazi ili kuifanya kazi hii kwa weledi unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja. Kutokana na hatari inayoweza kutokea ya upungufu wa mafuta nchini kutokana na ukosefu wa Dola za Kimarekani nchini kwa ajili ya kulipia shehena za mafuta zinazoagizwa kutoka nje, Serikali ikiongozwa na Benki Kuu ichukue hatua za makusudi kuhakikisha nchi inakuwa salama.

(vi) Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania – *TGDC*.

(a) Sheria ya sasa inatambua rasilimali ya joto ardhi kuwa ni madini. Hata hivyo, matumizi makubwa ya joto ardhi ni katika umeme. Mkanganyiko huu unasababisha wawekezaji kushindwa kuja kuwekeza. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione umuhimu wa kuleta Sheria itakayowezesha rasilimali ya joto ardhi kujulikana kama nishati ili kusaidia kupata uwekezaji wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa mara nyingine napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Spika wetu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, kwa uongozi wako thabiti. Pamoja nawe namshukuru sana Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Mbunge na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi imara wa unaowezesha utekelezaji mzuri wa majukumu ya shughuli zetu za Kibunge na Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwanza kwa heshima waliyonipa mimi kuwa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na mwenzangu Mheshimiwa Judith Kapinga, Mbunbge kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Tunawaahidi ushirikiano wa

kutosha katika kuisimamia Serikali. Aidha, tunawashukuru sana Wajumbe kwa kujitoa wakati wa ziara na wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii. Taarifa hii ya Kamati ni juhudi za Wajumbe hawa ambao wana weledi mzuri katika Sekta hii ya Nishati kwa ujumla. Naomba kwa heshima majina ya wajumbe yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri wa Nishati Mheshimiwa Januari Yusuf Makamba - Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Stephen Byabato - Mbunge, Katibu Mkuu *Eng.* Mramba, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Athuman Mbuttuka, pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa ufafanuzi na ushirikiano wanaoipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba wakati wote.

Mheshimiwa Spika, namshukuru kipekee Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu. Michael Chikokoto *ndc*, Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Pamela Pallangyo, Ndugu Onesmo Laulau, Ndugu Jesca Sanga, Msaidizi wa Kamati Ndugu Rukia Shaban pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kutuhudumia wakati wote na kuchangia kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati, Fungu Na. 58 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[1], nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Nishati **(Fungu 58)** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**.**

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati kuhusu Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara inazozisimamia ikiwemo bajeti ya Wizara hii yameelezwa kwa kina katika fasili ya 7(1) (a) ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[2].

**Mheshimiwa Spika**, Uandishi wa Taarifa hii umezingatia matakwa ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 kama ifuatavyo:-

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa;

b) Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu uchambuzi wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na namna Wizara ilivyotekeleza Ushauri na Mapendekezo ya Kamati;

[1] 118 (9) Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja.

[2] 7.-(1) Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa yafuatayo:- (a) kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

c) Sehemu ya Tatu inachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne inatoa Ushauri na Mapendekezo yake kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

e) Sehemu ya Tano ambayo ni ya mwisho ni Hitimisho la Taarifa yenye kujumuisha shukrani na kutoa hoja.

### 1.1 Msingi na Muundo wa uchambuzi wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, inazitaka Kamati zote za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuchambua Taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa fedha unaofuata[3].

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa haya ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Nishati na Madini kuanzia tarehe 23 -27 Machi, 2023 ilitekeleza wajibu wake kwa kufanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati yenye fungu moja 58.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchambuzi wake kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023;

---

[3] Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata

b) Uchambuzi wa utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati;

c) Uchambuzi wa utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

d) Uchambuzi wa hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

e) Uchambuzi wa Upatikanaji wa fedha kufikia Februari 2023.

### 2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023[4], kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Nishati. Kamati ilifanya Ziara katika Mikoa mitatu (3) ambayo ni Tanga, Pwani na Dar es Salaam ili kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, ziara ililenga pia kubainisha mafanikio na changamoto ili kuweza kulishauri Bunge lako Tukufu na Serikali hatua za kuchukua.

### 2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara hiyo, yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi wa miradi iliyotembelewa na Kamati:-

#### 2.2.1 Miradi ya REA Wilaya ya Korogwe

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu wa Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (Lot 39) katika Wilaya ya Pangani, Korogwe na Mkinga unatekelezwa na Mkandarasi M/s Tontan Project Technology and Group Six International Ltd wenye lengo la kupeleka umeme katika **vijiji 79** kwa gharama ya **Shilingi 22,815,588,709.89/=**

[4] 117(1) Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa Wabunge, Kamati za Bunge za kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa siku zisizozidi saba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Wilaya ya Korogwe ambapo Kamati ilitembelea, Mradi unahusisha kusambaza umeme katika vijiji 54; ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 253; ujenzi wa njia za umeme wa msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 54; ufungwaji wa mashine umba 54 pamoja na uunganishaji wa wateja wa awali 1,188. Mradi ni wa miezi 18 na ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 14 Februari 2022 na unatarajiwa kukamilishwa mwezi Agosti 2023. Gharama za Mradi ni **Shilingi 12,496,697,661.284 (Pamoja na VAT)**. Mpaka sasa kiasi cha **Shilingi 2,499,339,532.26** zimekwisha lipwa sawa na **asilimia 20** ya gharama za mradi.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu umekuwa unasuasua kwani mkandarasi amesimamisha nguzo za njia ya msongo wa kati urefu wa kilomita **30 kati ya 253,** amesimamisha nguzo za njia ya msongo mdogo urefu wa kilomita **7 kati ya 54**, amejenga mtandao wa umeme wa njia ya msongo wa kati wenye urefu wa **kilomita 20** kati ya **253** alizopewa kwenye mkataba; amejenga **kilomita 4** kati ya **54** za njia za msongo mdogo, amefunga mashine umba **4** kati ya **54** na ameunganisha umeme kwa wateja wa awali **40** kati ya **1,800** sawa na **asilimia 11.**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na maelezo kuwa kuongezeka kwa bei ya vifaa kumesababisha mradi huu kuchelewa, hata hivyo, pamoja na kupitia upya gharama ya bei za vifaa, Mkandarasi kuandikiwa barua na kufanya nae kikao bado mkandarasi yupo nyuma ukilinganisha na mkataba. Kamati ilikutana na Mkandarasi na ilipomuhoji sababu za kuchelewa kutekeleza mradi alikiri ni kweli alipewa fedha kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.86** kwa ajili ya kutekeleza Mradi (Lot 39) katika Wilaya ya Pangani, Korogwe na Mkinga na fedha hizo alizitumia kwa shughuli nyingine. **Kamati imesikitishwa sana na kitendo cha Mkandarasi kutumia fedha za Umma kwa shughuli zake nyingine. Kitendo hiki kimeihuzunisha sana Kamati. Si hivyo tu, lakini pia Kamati haipendezwi na kasi ndogo ya utekelezaji wa Mradi huu ambao ni mfano kati ya mingi nchini. Maeneo mengi utekelezaji wa miradi hii umekuwa wa kusuasua kutokana na kutowajibika ipasavyo kwa baadhi ya Wakandarasi. Ni rai ya Kamati kwa Watendaji wa Serikali kuongeza umakini katika kutoa zabuni kwa Wakandarasi na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi hii.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kushuhudia uwashaji wa umeme katika vijiji viwili vya Mswaha Darajani ambapo umeme uliwashwa katika Shule ya Msingi, Msikiti na Kijiji cha Madumu umeme uliwashwa katika Shule ya Sekondari ya Chekelei.

### 2.2.2 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi – Chongoleani

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu ambao unahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi (*crude oil*) kutoka Hoima-Kabaale nchini Uganda hadi Chongoleani -Tanga nchini Tanzania likiwa na urefu wa kilomita 1,443. Kati ya hizo, kilomita 296 zitakua Uganda na kilomita 1,147 zitapita Tanzania. Kwa upande wa Tanzania bomba litapita katika Mikoa 8 na Wilaya 24. Gharama ya mradi ni **Dola za Kimarekani Bilioni 5.088** ambazo zinajumuisha fedha za wanahisa Total energies (62%), TPDC (15%), UNOC (15%) na CNOOC (8%). Hadi kufikia Februari 2023, kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 891.85** zilikuwa zimetolewa kama mchango wa kila mwanahisa kwa mujibu wa hisa zake na utekelezaji wa mradi huu ni wa kipindi cha miezi 36.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.5.** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu. Kufikia mwezi Februari 2023, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.8** kilikuwa kimetolewa sawa na **asilimia 53** ya fedha zote. Upatikanaji wa fedha hizo umewezesha kuanza utekelezaji wa hatua mbalimbali za mradi. Baadhi ya kazi ambazo Kamati imeelezwa na nyingine kushuhudia ni pamoja na utwaaji wa ardhi kwa **asilimia 98**, kusafishwa kwa eneo la mradi lenye kujumuisha maeneo mbalimbali kama eneo la kupokelea matenki ya mafuta ghafi na gati, kuanza kwa ujenzi wa Kempu ambao umefikia **asilimia 20** na inatarajiwa kukamilika mwezi huu wa Mei 2023, na kuchimbwa kwa mabwawa kwa ajili ya kupokea maji endapo mvua itatokea ili kutoathiri eneo la ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi una jumla ya Wafanyakazi 400 ambapo Wageni 50 na Watanzania 350. Kati ya Watanzania hao 150

wanatoka katika eneo la mradi (Chongoleani). Aidha, utekelezaji wa mradi huu unaenda sambamba na miradi mingine ya kimazingira na kijamii kama kujenga uwezo kwa wananchi, ujenzi wa barabara na kufundisha Watanzania 170 katika Vyuo vya VETA na Chuo cha Ufundi Arusha ambao watafanya kazi katika Mradi na tayari 40 wameshahitimu. Aidha, kwa miezi sita ijayo mpango ni kukamilisha ujenzi wa Kempu, barabara, na kuondoa udongo ambao kwa sasa upo **asilimia 40** na kuanza msingi wa matenki.

### 2.2.3 Mradi wa ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme cha Chalinze (Namba ya Mradi 3272)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) hadi Chalinze na kituo cha kupoza umeme cha Chalinze. Utekelezaji wa Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni: Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka JNHPP hadi Chalinze yenye urefu wa kilomita 160; na Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze, ambacho kinahusisha ufungaji wa mashine umba (transfoma) sita zenye uwezo wa MVA 250 kila moja.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100 ambazo ni **Dola za Kimarekani milioni 51.5 na Shilingi bilioni 39.12** kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na **Dola za Kimarekani milioni 44.06** na **Shilingi bilioni 30.85** kwa ajili ya kituo cha kupoza umeme cha Chalinze. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bunge liliidhinisha **Shilingi Bilioni 40** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu na kufikia Februari 2023 kiasi cha **Shilingi Bilioni 27.6** sawa na **asilimia 69** kilikuwa kimepokelewa. **Kamati inapongeza mwenendo wa upatikanaji wa fedha.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishuhudia na kuelezwa kuwa, utekelezaji wa njia ya kusafirisha umeme katika msongo wa kilovoti 400 kutoka JNHPP hadi Chalinze (kilomita 160) umefikia **asilimia 92** na kituo cha kupoza umeme cha Chalinze, ambacho kinahusisha ufungaji wa mashine umba (*transfoma*) sita zenye uwezo wa MVA 250 kila moja umefikia **asilimia 59. Kamati**

**inapongeza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, ujenzi wa Jengo la kuongoza mitambo umefikia wastani wa asilimia 25 na hivyo kuna umuhimu wa kuongeza kasi. Ni imani ya Kamati kuwa, mradi huu utakamilika mapema ili kuweza kupokea umeme kutoka katika Bwawa kama ambavyo Kamati ilihakikishiwa kufikia Juni 2023, Kituo kitakuwa na uwezo wa kupokea umeme kutoka Julius Nyerere kiasi cha MW 235 kutokana na kufungwa kwa mashine umba ya kwanza.**

**2.2.4 Mradi wa upanuzi wa Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I - *Kinyerezi I Extension MW 185* (Namba ya Mradi 3164)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Kinyerezi *I Extension* - **MW 185** ambao ulibuniwa ili kuongeza uwezo na upanuzi wa kituo cha Kinyerezi I chenye uwezo wa kufua umeme wa **MW 150**. Lengo ni kuimarisha na kuongeza uwezo wa gridi ya Taifa na kufanya jumla ya uwezo wa kituo cha Kinyerezi I kuwa **MW 335**. Mradi unahusisha usimikaji wa mitambo minne (4) ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi (*gas turbines*), vipoza hewa (chillers) sita (6) pamoja na viambata vyake na tayari vifaa vyote vimeshafika eneo la mradi. Aidha, mradi unahusisha kazi ya kuongeza uwezo wa njia ya kusafirisha umeme (*transmission line upgrade*) inayotoka Kinyerezi hadi Gongolamboto yenye msongo wa kilovoti 132.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi umefikia **asilimia 93.2** na Kamati ilishuhudia mitambo mitatu kati ya minne (Na. 5, 6 na 7) ikiwa imewashwa na kuingiza **MW 135** kwenye gridi ya Taifa. Wakati Kamati inatembelea mradi, mkandarasi alikuwa anaendelea na kazi ya kuunganisha mtambo wa nne na wa mwisho kwa mradi huu na Kamati ililezwa kuwa mtambo huu ungewashwa mwishoni mwa mwezi April. Kamati pia ilishuhudia ujenzi wa Tenki la maji ukiendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi unagharimiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 kwa kiasi cha **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi za Kitanzania Bilioni 435.48** na kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 154** kimeshalipwa sawa na **asilimia 82** ya

gharama za mradi. Katika Mwaka huu wa fedha 2022/2023 kiasi cha **Shilingi Bilioni 35** kiliidhinishwa na Bunge na kufikia Februari 2023 **Shilingi Bilioni 29.32** sawa na **asilimia 84** zilikuwa zimepokelewa. Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha inaridhisha. **Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mradi huu ni moja ya miradi ambayo utekelezaji wake umechelewa. Itakumbukwa kuwa, awali mitambo yote ilipaswa kuwa imewashwa mwezi Agosti 2022, hata hivyo baadae Kamati ilielezwa ingewashwa mwezi Disemba 2022. Mpaka Kamati inatembelea Mradi huu bado mtambo mmoja (Na. 8) ulikuwa bado haujawashwa. Kamati inaitaka Wizara isimamie vizuri mradi huu ili mtambo wa nne uwashwe kama ulivyopangwa ili kuongeza upatikanaji wa umeme nchini.**

### 2.2.5 Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Dar Es Salaam, Lindi na Pwani na Kituo cha kupokelea Gesi Asilia cha Kinyerezi (GASCO) (Namba ya Mradi 3162)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi huu wa miundombinu ya usambazaji wa gesi katika Kituo cha kupokelea gesi cha Kinyerezi Dar es Salaam. Mradi huu unahusisha mitambo ya kuchakata gesi asilia iliyopo Madimba mkoani Mtwara na Songo Songo Mkoani Lindi; Bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Madimba na Songo Songo hadi Tegeta, Dar es Salaam; na mtandao wa usambazaji gesi kwa watumiaji wa mwisho. Kazi zote za uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya Taifa ya gesi asilia zinafanywa na wataalamu wa GASCO kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla uchakataji wa gesi ghafi unafanyika katika mitambo miwili iliyopo Madimba mkoani Mtwara na Songo Songo mkoani Lindi, ambayo hupokea gesi ghafi kutoka kwa wazalishaji wa mkondo wa juu (*Upstream Operators*). Gesi asilia iliyochakatwa husafirishwa hadi Dar es Salaam kupitia bomba kuu la kusafirisha gesi asilia. Mitambo ya Madimba na Songo Songo kwa pamoja ina uwezo wa kuchakata futi za ujazo milioni 350 (Madimba 210 na Songo Songo 140) kwa siku. Kwa sasa matumizi ya gesi asilia yameongezeka na kiasi cha wastani wa futi za ujazo milioni 105 kinachakatwa kwa siku (105mmscfd).

**Mheshimiwa Spika**, Bomba la kusafirisha gesi asilia kwa ujumla lina urefu wa kilomita 551 kutoka Mtwara na Songo Songo hadi Tegeta, Dar es Salaam. Bomba lina uwezo wa kusafirisha gesi futi za ujazo milioni 784 kwa siku (784mmscfd) bila mgandamizo, na linaweza kusafirisha gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 1,002 kwa kuweka mitambo ya mgandamizo (*compression*). Kwa sasa usafirishaji kwa siku ni wastani wa futi za ujazo milioni 107 -155 sawa na wastani wa **asilimia 20** ya uwezo wa bomba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia, GASCO inatekeleza mradi wenye urefu wa Kilometa 15.3 na kuunganisha nyumba 125 na taasisi 4 (Sekondari ya Ufundi, Chuo cha Ualimu Ufundi, Chuo cha Ualimu kawaida na Gereza la Lilungu) kwa matumizi ya gesi asilia Mtwara, Mradi wa kuunganisha gesi katika kiwanda cha Rady-Mkuranga kwa urefu mita 802, mradi wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia yenye urefu wa Kilometa 4.3 na kuunganisha nyumba 85 (Mikocheni), miradi ya ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia yenye urefu wa Kilometa 16.4 na kuunganisha nyumba 155 na taasisi 2 (Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam).

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka huu wa fedha 2022/2023, **Shilingi Bilioni 1.048** zilitengwa na kufikia Februari 2023 **Shilingi Milioni 891** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 85** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kamati ilitembelea na kuona namna Kituo cha kupokelea gesi cha Kinyerezi kinavyoendeshwa ikiwa ni pamoja na kutembelea Kituo cha kupunguza mgandamizo wa gesi (*Pressure Reduction Station*) na Kituo cha kuangalia usalama wa bomba (*Control Center*). **Kwa ujumla kazi inaenda vizuri isipokuwa Kamati imebaini kuwa kasi ya uunganishwaji wa nyumba/viwanda/taasisi kwajili ya matumizi ya gesi upo chini na haiendani na nia ya Serikali ya kuhakikisha gesi inakuwa ni mkombozi kwa Watanzania. Aidha, uzalishaji wa gesi ni mdogo na hivyo kufanya hata bomba pamoja na ukubwa wake kusafirisha gesi kidogo kutokana na uzalishaji mdogo. Kuna umuhimu wa kuongeza uzalishaji wa gesi ili kukidhi mahitaji ya soko. Mwanasiasa Bill Richardson kutoka Marekani ambaye aliwahi kuwa Gavana wa New Mexico amewahi kusema "*Natural Gas is future, it is here*". Ni wakati sasa wa kutumia gesi hii ipasavyo.**


**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri inayofanywa na GASCO, Kamati ilielezwa uwepo wa changamoto zifuatazo:-

i) Ukosefu wa Bodi;
ii) Upungufu wa Wafanyakazi; na
iii) Deni kubwa inalolidai TANESCO kutokana na uuzaji wa gesi kiasi cha **Shilingi Bilioni 725.**

## 2.3 Tathmini ya Miradi

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla kasi ya utekelezaji wa miradi siyo wa kuridhisha kama ilivyoelezwa na zaidi kwa Mradi wa REA Wilaya ya Korogwe ambao umefikia **asilimia 11** tu. Wastani wa upatikanaji wa fedha kwa miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati ni **asilimia 85.1** kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1: Upatikanaji wa Fedha kwa Miradi iliyotembelewa**




*Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Nishati na usanifu wa Kamati*

## 2.4 Maoni, Ushauri na Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara hiyo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

**2.4.1** Kutokana na changamoto ya Wakandarasi kushindwa kutekeleza miradi kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa fedha:-

a) Kabla ya Wakandarasi wa REA kupewa Mikataba ya kazi, uchunguzi wa kina (*Due diligence)* ufanyike ili kuufahamu undani wao ili kuepuka usumbufu katika utekelezaji wa miradi;

b) Mkakati wa Serikali wa kutaka kuwasaidia Wakandarasi wa nje kwa kuwapatia dhamana (*Letter of Credit* - LC) ujielekeze kwa Wakandarasi wazawa ambao ni wazalendo ili kuwainua;

c) Vipengele vya Mkataba na Kampuni ya Tontan inayotekeleza Mradi wa Lot 39 viangaliwe na hatua kali zichukuliwe ili iwe fundisho kwa Wakandarasi wengine ambao wamekuwa wakisuasua kukamilisha miradi licha ya kupewa fedha; na

d) Kwa Wakandarasi wazawa ambao wanatekeleza kazi zao vizuri ni vyema wakazingatiwa na kupewa kazi ambazo Wakandarasi wa nje wameshindwa kuzitekeleza kwa wakati.

**2.4.2** Kutokana na baadhi ya Miradi ya TANESCO kuchelewa kwasababu ya kufilisika kwa wakandarasi:-

a) Uchunguzi wa kina *(Due diligence) u*fanyike kwa Wakandarasi wa nje ili kuepuka kukwama kwa miradi kunakotokana na maelezo kuwa Wakandarasi wamefilisika;

b) Wakandarasi wadogo (*Subcontractors)* ambao wengi ni wazawa wawe wanalipwa kwanza pale mkandarasi anaposema amefilisika kupitia *Performance Guarantee Bond* kwani wengi wamekuwa hawalipwi;

c) Wakandarasi wa ndani ambao ni waaminifu haswa kwa miradi ambayo inatekelezwa kwa fedha za ndani wapewe kipaumbele cha zabuni;

d) Mamlaka zinazohusika na ununuzi na utoaji wa zabuni zisimamiwe ili kufanya kazi kwa weledi na uadilifu; na

e) Kutokana na uwepo wa changamoto ya upatikanaji wa vifaa zikiwemo nguzo, Wizara ihakikishe vifaa vyote zikiwemo nguzo za kutosha zinapatikana ili utekelezaji wa miradi usikwame.

**2.4.3** Kutokana na kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi mingi ya TANESCO ukiwemo Mradi wa Kinyerezi I Extension, TANESCO inapaswa iwekeze katika usimamizi wa miradi yake *(Project Management*) ili iwe inakamilika kwa wakati na hivyo kuongeza uzalishaji wa umeme nchini. Aidha, TANESCO ihakikishe inasimamia kikamilifu utekelezaji wa Mradi wa *Kinyerezi I Extension* wa MW 185 ili Mtambo uliobaki ukamilike mapema na kuongeza upatikanaji wa umeme nchini.

**2.4.4** TPDC iongeze kasi ya kuunganisha gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani na kwenye Taasisi. Aidha, Sekta Binafsi ishirikishwe ili kuleta ufanisi hususan katika kusambaza gesi ya kutumia kwenye magari ( *Compressed Natural Gas*);

**2.4.5** Wizara isimamie kikamiilifu ili ujenzi wa mradi wa Bomba la mafuta uende kwa kasi; na

**2.4.6** Wizara iendelee kutoa elimu kwa jamii hususan kwa wananchi wa maeneo ya Mkuza wa Bomba kuhusu umuhimu wa kutunza mradi na kuwa walinzi.

## 2.5 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Vipaumbele vya Serikali kwa ujumla vinapaswa kuzingatia masuala mbalimbali kama vile Dira ya Maendeleo ya Taifa, Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa CCM na zaidi Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III), 2021/22 – 2025/26. Wizara ya Nishati ambayo ndiyo imepewa dhamana ya kusimamia Sekta ya Nishati nayo inapaswa kuzingatia haya ilikufikia malengo yaliyowekwa na Katiba yetu ibara ya 8 (1) (b) ya kuhakikisha ustawi wa wananchi[5].

[5] 8 (1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo ((b) lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;


**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara umebaini kuwa, Wizara imejitahidi kutekeleza vipaumbele vyake vya kuzingatia Mpango huo wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III), 2021/22 – 2025/26. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya vipaumbele hususan Kipaumbele Na.2 kinachohusu kutekeleza miradi ya umeme vijijini siyo cha kuridhisha kutokana na utekelezaji wake kusuasua kama ambayo imeonekana katika mradi uliotembelewa katika Wilaya ya Korogwe. **Ni Rai ya Kamati kuwa, changamoto zilizobainishwa na Kamati zifanyiwe kazi ili kuboresha ustawi wa wananchi**.

### 2.6 Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari 2023

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilikadiria kukusanya **Shilingi 20,393,000/=** kutoka vyanzo vyake vitatu ambayo ni Marejesho ya Fedha za Umma (*Recovery of Public Money*) kwa **asilimia 99.99** na **asilimia 0.01** kutokana na Stakabadhi nyinginezo na Stakabadhi za aina mbalimbali. Kufikia Februari 2023, Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 4,438,259/=** sawa na **asilimia 22** tu ya lengo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, chanzo hiki mara kwa mara kimekuwa hakifikii malengo inayojiwekea. Kamati ilhoji sababu za kutofikia malengo na ilielezwa ni kutokana na ukweli kuwa chanzo hiki kinategemea marejesho ya fedha za umma zitokanazo na masurufu (*imprest)* ambayo Watumishi hupewa na kufanya marejesho, hivyo basi kutokana na usimamizi thabiti wa marejesho na baadhi ya watumishi waliokuwa wanakatwa masurufu kumaliza makato yao, makusanyo ndiyo hayo. Kamati inaona ipo haja ya kupunguza Makadirio haya ili kuwa na uhalisia.

**Kielelezo Na. 2: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2023**





*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara 2023 na Usanifu wa Kamati*

## 2.7 Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha kufikia Februari 2023

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Wizara ya Nishati (**Fungu 58**)iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu **Shilingi 2,905,981,533,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Fedha hizo zinajumuisha Matumizi ya Kawaida **Shilingi 82,951,957,000/=** sawa na **asilimia 2.9** ya fedha yote ambapo **Shilingi 14,726,136,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (P.E) na **Shilingi 68,225,821,000/=** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ya Wizara. Aidha, Miradi ya Maendeleo iliidhinishiwa **Shilingi 2,823,029,576,000/=** sawa na **asilimia 97.1** ya fedha zote ambazo zinajumuisha fedha za ndani **Shilingi 2,655,556,128,000/=** na fedha za nje **Shilingi 167,473,448,000/=.**

**Mheshimiwa Spika**, kufikia Februari 2023, Wizara imepokea **Shilingi 1,546,042,818,494/=** sawa na **asilimia 52.6** ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa, kati ya fedha zilizopokelewa Mishahara ni **Shilingi 9,583,074,764/=** sawa **na asilimia 65.08** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 7,459,102,675/=** sawa na **asilimia 10.93** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.3**.

**Kielelezo Na. 3: Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida**





*Chanzo: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini pia kuwa, fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 1,550,392,616,642/=** sawa na **asilimia 66** ya bajeti iliyoidhinishwa ambazo ni fedha za ndani**.** Kwa upande wa fedha kutoka nje, Kamati ilielezwa kuwa kiasi cha **Shilingi 66,757,312,555.62** sawa na **asilimia 39.8** ya bajeti ya maendeleo kutoka nje kimepokelewa kwa utaratibu wa D-Fund ambao hesabu zake huingizwa kwenye Hesabu za Wizara baada ya Mwaka wa Fedha kukamilika. **Kamati bado hairidhishwi na upatikanaji wa fedha kutoka nje.**

**Mheshimiwa Spika**, **Kielelezo Na.4**. kinaonesha hali ya upatikanaji wa fedha kufikia Februari 2023

**Kielelezo Na. 4: Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kufikia Februari, 2023**




*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

## 2.8 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 iliyowasilishwa Bungeni mnamo tarehe 1 Juni, 2022 pamoja na mambo mengine, ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yapatayo 35 ili yafanyiwe kazi na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 23 Machi 2023, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo hayo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwa kiasi kikubwa Wizara imejitahidi kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo hayo ya Kamati. Aidha, kwa baadhi ya hoja ambazo zilikuwa bado hazijatekelezwa kikamilifu, Kamati iliomba ufafanuzi na majibu ya Wizara yalionesha nia ya Serikali katika kuyatekeleza. Kamati itaendelea kusisitiza tena hoja hizo ambazo bado katika Taarifa hii. **Ni Rai ya Kamati kuwa, utekelezaji wa Mapendekezo na Ushauri huo uende kwa kasi ili kusaidia kuimarisha Sekta ya Nishati kama ilivyoainishwa katika Aya ya 63 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 inayosema "*Katika miaka mitano ijayo,***

***Chama cha Mapinduzi kinakusudia kuimarisha zaidi sekta ya nishati kwa kuhakikisha kuwa nchi inazalisha umeme wa kutosha ili kukidhi mahitaji ya uchumi wa viwanda na soko la nje".***

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

b) Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

d) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024; na

e) Uchambuzi wa Masuala Mahsusi.

### 3.1 Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 umebaini kuwa, malengo na vipaumbele vya Wizara vimezingatia miongozo mbalimbali ukiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III), 2021/22 – 2025/26**.** Aidha, malengo haya yamezingatia dhima ya utekelezaji

wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) inayosema **"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu"** ambapo pamoja na mambo mengine bajeti ya Wizara itajumuisha utekelezaji wa miradi ya kipaumbele kama Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere na Miradi ya REA.

**Mheshimiwa Spika**, malengo ambayo Wizara imepanga kuyatekeleza katika Mwaka ujao wa fedha 2023/2024 na ambayo pia yameelezwa kwa kina na Waziri mwenye dhamana ni pamoja na :-

a) Kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;

b) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu na mbadala katika matumizi mbalimbali ya nishati;

c) Kuimarisha na kuendeleza matumizi bora ya nishati;

d) Kuimarisha uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za mafuta na gesi asilia;

e) Kuimarisha usambazaji na matumizi ya bidhaa za mafuta na gesi asilia;

f) Kuimarisha utoaji huduma kwa wadau wa Sekta ya Nishati;

g) Kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Kuzuia Rushwa; na

h) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waathirika.

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Nishati(Fungu 58)imekadaria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 20,393,000/=.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio

haya yanafanana na yale yaliyokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.5. Hata hivyo, Kamati inapata mashaka na makadirio ya makusanyo haya kutokana na kukosa uhalisia. Itakumbukwa kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 makusanyo kufikia Februari 2022 yalikuwa ni asilimia 28 tu. Aidha, katika Mwaka huu wa Fedha 2022/2023 makusanyo kufikia Februari 2023 nayo yalikuwa ni asilimia 21.7 tu ya lengo. Kamati inaona ni vyema makadirio haya yawe na uhalisia.**

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2022/2023 na 2023/2024**

| CHANZO | 2022/2023 | 2023/2024 | ONGEZEKO/UPUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Marejesho ya Fedha za Umma (Recovery of Public Money) | 20,391,000 | 20,391,000 | - | - |
| Stakabadhi nyinginezo | 1,000 | 1,000 | - | - |
| Stakabadhi za aina mbalimbali | 1,000 | 1,000 | - | - |
| **JUMLA** | **20,393,000** | **20,393,000** | **-** | **-** |

*Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati*


## 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia malengo na vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Nishati yenye Fungu 58, inakadiria kutumia **Shilingi 3,048,632,519,000/=** . Fedha hizi zinajumuisha Fedha za Maendeleo **Shilingi 2,960,702,821,000/=** sawa na **asilimia 97.1** ya bajeti yote na **Shilingi 87,929,698,000/=** sawa na **asilimia 2.9** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 2,609,156,128,000/=** sawa na **asilimia 88.1** ni fedha za ndani na **Shilingi 351,546,693,000/=** sawa na **asilimia 11.9** ni fedha za nje.

Aidha, kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Mishahara ya Watumishi (PE) ambayo ni **Shilingi 16,292,586,000/=** sawa na **asilimia 18.5** na Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 71,637,112,000/=** sawa na **asilimia 81.5**. **Kielelezo Na. 6** kinachanganua mgawanyo huo wa bajeti.

**Kielelezo Na. 6: Mgawanyo wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024**





*Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati pia imelinganisha bajeti ya Fungu 58 kwa Mwaka 2022/2023 na 2023/2024 na kubaini kuwa, Bajeti ya Wizara imeongezeka kutoka **Shilingi 2,905,981,533,000** Mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi 3,048,632,519,000** ambayo ni ongezeko la **Shilingi 142,650,986,000** sawa na **asilimia 4.9. Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii.**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa, ongezeko zaidi linaonekana katika Miradi ya Maendeleo na hususan fedha kutoka nje kwa **asilimia 109.9**. Aidha maeneo mengine ambayo bajeti imeongezeka ni pamoja na Mishahara (PE) **asilimia 10.6** na OC **asilimia 5**. Vilevile, Kamati imebaini fedha za Miradi ya Maendeleo ndani zimepungua kwa **asilimia 1.7** kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.7**.

**Kielelezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti 2022/2023 na 2023/2024**




| | MISHAHARA | OC | NDANI | NJE |
|---|---|---|---|---|
| | MATUMIZI YA KAWAIDA | | MAENDELEO | |
| 2022/2023 | 14,726,136,000 | 68,225,821,000 | 2,655,556,128,0 | 167,473,448,000 |
| 2023/2024 | 16,292,586,000 | 71,637,112,000 | 2,609,156,128,0 | 351,546,693,000 |
| ONGEZEKO/UPUNGUFU | 1,566,450,000 | 3,411,291,000 | -46,400,000,000 | 184,073,245,000 |

*Chanzo: Taarifa za Wizara na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji sababu za ongezeko la fedha za maendeleo kutoka nje na uhakika wa upatikanaji wake hasa ikizingatiwa kuwa katika Mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia Februari 2023 wakati Kamati inapokea Taarifa, upatikanaji wa fedha hizo ulikuwa ni **asilimia 39.86 tu.** Kamati ilihakikishiwa kuwa fedha hizo zitapatikana. Kwa ujumla, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele katika ongezeko la bajeti ya Wizara kwa Mwaka huu 2023/2024 ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 8.**

**Kielelezo Na. 8: Maeneo ambayo Bajeti imeongezeka**

| Na. | Eneo | Sababu |
|---|---|---|
| **1.** | Mishahara | Ajira Mpya, kupandishwa vyeo na Nyongeza ya Mishahara |
| **2.** | Matumizi Mengineyo | Ongezeko la Posho ya Kujikimu kutokana na Waraka wa Watumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2022 |
| **3.** | Maendeleo Nje | Kuongezeka kwa fedha za miradi kama ya REA, Rusumo, Kakonko, Malagarasi na North West Grid Extension |

*Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

## 3.4 Ulinganisho baina ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulienda mbali zaidi kwa kulinganisha Bajeti ya Wizara hii na Bajeti ya Taifa. Ulinganisho uliangalia bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024 dhidi ya bajeti ya Taifa kwa kipindi hicho. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa masuala mbalimbali yafuatayo:-

a) Bajeti ya Wizara kwa ujumla dhidi ya Bajeti ya Taifa imeshuka kutoka **asilimia 7.01** Mwaka 2022/2023 hadi **asilimia 6.87** Mwaka 2023/2024.


b) Bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara dhidi ya bajeti ya Taifa ya Matumizi mengineyo imeshuka kutoka **asilimia 0.90** Mwaka 2022/2023 kufikia **asilimia 0.66** Mwaka 2023/2024**.**

c) Bajeti ya Wizara ya Maendeleo dhidi ya bajeti ya Taifa ya Maendeleo ndani imeongezeka kutoka **asilimia 21.58** Mwaka 2022/2023 hadi kufikia **asilimia 21.97** Mwaka 2023/2024.

d) Bajeti ya Wizara ya Maendeleo nje dhidi ya bajeti ya Taifa ya Maendeleo nje imeongezeka kutoka **asilimia 6.20** Mwaka 2022/2023 hadi kufikia **asilimia 10.71** Mwaka 2023/2024.

**Kielelezo Na. 9(a): Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 58) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI NISHATI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 4,493,500,000,000.00 | 68,225,821,000.00 | 1.52 |
| **MISHAHARA** | 9,740,800,000,000.00 | 14,726,136,000.00 | 0.15 |
| **MAENDELEO NDANI** | 12,122,100,000,000 | 2,655,556,128,000 | 21.91 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,399,200,000,000 | 167,473,448,000 | 4.93 |
| **DENI LA SERIKALI** | 11,308,400,000,000.00 | | - |
| **JUMLA** | **41,064,000,000,000.00** | **2,905,981,533,000.00** | **7.08** |




**Kielelezo Na 9(b): Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 58) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI NISHATI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 5,578,433,000,000 | 71,637,112,000.00 | 1.28 |
| **MISHAHARA** | 10,882,126,000,000 | 16,292,586,000 | 0.15 |
| **MAENDELEO NDANI** | 11,873,900,000,000 | 2,609,156,128,000 | 21.97 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,282,100,000,000 | 351,546,693,000 | 10.71 |
| **DENI LA SERIKALI** | 12,771,500,000,000 | 0 | - |
| **JUMLA** | **44,388,059,000,000.00** | **3,048,632,519,000.00** | **6.87** |




*Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024 na Randama ya Wizara ya Nishati 2023/2024*

## 3.5 Uchambuzi wa Masuala Mahsusi

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchambuzi wa Bajeti, Kamati imefanya uchambuzi wa masuala mahsusi ambayo yana maslahi

kwa Taifa. Masuala hayo ni Hali ya uzalishaji wa umeme na Hali ya Mafuta nchini kama ifuatavyo:-

### 3.5.1 Hali ya Upatikanaji wa Umeme nchini

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Nishati ina jukumu la kuhakikisha kuwa wakati wote uzalishaji wa umeme, na uimarishaji wa miundombinu ya kusafirishia umeme nchini unakuwa wa uhakika. Hata hivyo, pamoja na malengo hayo, hali ya umeme bado siyo ya kuridhisha kutokana na umeme kuwa unakatika mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kufikia mwezi Februari, 2023 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulikuwa MW 1,822.05 unaozalishwa kutoka vyanzo vinne Maji MW 574.60, (31.54%), Gesi asilia MW 1,148.82 (63.05%), Mafuta MW 88.13 (4.84%) na Tungamotaka MW 10.50 (0.58%) kama inavyooneka kwenye **Kielelezo Na.10.**

**Kielelezo Na. 10: Hali ya Uzalishaji wa Umeme Nchini**




*Chanzo: Taarifa ya TANESCO na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba uzalishaji wa umeme ambao umeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa ni **MW 1,822.05** sawa na ongezeko la **asilimia 7.52** ikilinganishwa na **MW 1,694.55** zilizokuwepo kufikia mwezi Juni 2022 ni dhahiri kuwa ongezeko la **MW 127.5** ni dogo sana kuweza kuhimili kasi ya ongezeko la mahitaji ya umeme nchini hasa ikizingatiwa kua ukuaji wa shughuli za kiuchumi umekua mkubwa. Aidha,

ongezeko hili dogo linaiweka nchi kwenye hatari ya kutoweza kuhimili changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza kwenye mitambo ya kuzalisha na kusambazia umeme. Changamoto hizo ni pamoja na kuharibika kwa baadhi ya mitambo, kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa Gesi, na kushuka kwa kiwango cha maji kwenye mabwawa ya kuzalishia umeme na hivyo kulazimika kusitisha uzalishaji wa umeme. Ni kutokana na kuwepo kwa mazingira haya tunajikuta kwenye mazingira ya kuwa na umeme usio wa uhakika ambao unakatika mara kwa mara na hivyo kuleta athari kwenye uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Taifa letu kuwekeza zaidi rasilimali fedha kwenye sekta hii ili kuweza kuongeza na kuboresha miundombinu ya kuzalisha na kusambaza umeme. Kwani kwa kufanya hivyo tutaweza kujihakikishia kuwa na umeme wa kutosha na halikadhalika kuondokana na changamoto ya umeme kukatika mara kwa mara. Sambamba na hilo, ipo haja vilevile ya kuimarisha usimamizi wa miradi, na kuongeza kasi ya kukamilisha miradi ya kuzalisha umeme ambayo inaendelea nchini kwasasa hususan mradi wa kimkakati wa Bwawa la Julius Nyerere.**

### 3.5.2 Hali ya Mafuta Nchini

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Nishati ni kuimarisha usambazaji na matumizi ya bidhaa za mafuta na Gesi asilia nchini. Kwa upande wa mafuta, jukumu hili limeelekezwa kwa kwa Wakala wa Uagizaji wa mafuta kwa pamoja (PBPA). Majukumu mengine ya Wakala ni pamoja na kutathmini mahitaji ya mafuta nchini na kuratibu uagizaji wa mafuta hayo kwa Mfumo wa manunuzi ya pamoja (*Bulk Procurement System* – BPS). Vile vile Wakala umepewa jukumu la kuhakikisha mafuta yanayoletwa nchini yanakidhi mahitaji na ubora unaotakiwa na kuhakikisha mafuta yananunuliwa kwa njia yenye ufanisi (*efficient procurement*) kwa manufaa ya Taifa, na kuhakikisha kunakuwepo na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini (*Security of Supply*).


**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati kuhusiana na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini umebaini uwepo wa

akiba ya mafuta inayokidhi mahitaji ya nchi. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2022 hadi Februari 2023 akiba ya Mafuta nchini imeendelea kuwa juu ya wastani wa siku za matumizi kwa zaidi ya siku 25 ikiwa ni zaidi ya asilimia 35 ikilinganishwa na siku 15 za akiba ya mafuta inayotakiwa kuwepo kulingana matakwa ya Leseni ya biashara ya jumla ya mafuta.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Februari, 2023, jumla ya **Tani 4,263,245** za mafuta ya dizeli, petroli, ndege na taa ziliingizwa kwa matumizi ya ndani ya nchi (*local*) na nchi za jirani (*transit*) kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 11**. Katika kiasi hiki cha mafuta, jumla ya **tani 1,939,836** sawa na **asilimia 45.5** kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, na **tani 2,323,410** sawa na **asilimia 54.2** kwa ajili ya nchi za jirani.

**Kielelezo Na. 11: Kiasi cha Mafuta kilichoingizwa nchini**

| MWEZI | PETROLI | MAFUTA YA TAA/NDEGE | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Jul-22 | 232,365 | 26,884 | 684,828 |
| Aug-22 | 213,164 | 37,890 | 662,747 |
| Sep-22 | 222,123 | 26,830 | 687,926 |
| Oct-22 | 215,680 | 32,162 | 626,128 |
| Nov-22 | 12,720 | 26,660 | 317,275 |
| Dec-22 | 135,944 | 28,861 | 413,244 |
| Jan-23 | 141,340 | 15,500 | 410,126 |
| Feb-23 | 157,931 | 26,025 | 460,974 |
| JUMLA | **1,331,267** | **220,812** | **4,263,248** |




*Chanzo: Taarifa ya PBPA na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** tangu kuanza kutumika kwa mfumo wa Uagizaji Mafuta Kwapamoja (BPS), mfumo umekua ukiimarika siku hadi siku na kuendelea kuaminika na nchi takriban saba ambazo ni majirani zetu (Uganda, Rwanda, DRC Congo, Burundi, Zambia, na Malawi) na hivyo kuamua kuendelea kuutumia mfumo huu. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuendelea kuongezeka kwa kiwango cha mafuta yanayoagizwa na nchi hizo kupitia mfumo huu hapa nchini. Kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia vyema uendeshwaji wa mfumo huu na kutoruhusu kuvurugika. Kamati inaendelea kusisitiza **kuwa, kama nchi tusiruhusu jambo lolote liuvuruge mfumo huu kwani kuvurugika kwake kunaweza kusababisha mafuta haya kuondoka kwenye mfumo wetu nchini na hivyo kupoteza faida za kiuchumi tunazopata kutokana na mafuta haya kupitia nchini. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, uwepo wa mafuta haya kwenye hifadhi za nchi yetu kunatuhakikishia uhahika wa kuwepo kwa mafuta nchini, hivyo kama Taifa tuna kilasababu ya kuhakikisha hatuipotezi faida hii.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuimarika kwa mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja na hivyo kuihakikishia nchi uhakika wa usalama na upatikanaji wa mafuta nchini, kuendelea kwa vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine tangu mwezi Machi 202022 kumeifanya Dunia kushuhudia uwepo wa athari za kiuchumi zilizotokana na kuongezeka kwa bei za mafuta kwa kiwango kikubwa, na hivyo kusababisha kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa Dola za Marekani. Hali hii imeleta athari kubwa katika biashara ya mafuta kwa nchi mbalimbali ulimwenguni ikiwemo nchi yetu. Kwa hapa nchini Kampuni za mafuta zimejikuta zikichelewa kulipia shehena zao za mafuta na hivyo shehena hizo kulazimika kubaki katika maghala ya mafuta chini ya uangalizi wa mletaji mafuta (*Financial Hold*) hadi pale yanapolipiwa. Hali hii ya mafuta kuwa kwenye maghala chini ya uangalizi imesababisha uhaba wa nafasi ya kupokelea shehena nyingine jambo ambalo linasababisha kupungua kwa ufanisi wa mfumo wa BPS.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuondokana na changamoto ya upatikanaji wa Dola za Marekani na hivyo shehena za mafuta kulazimika kubaki katika maghala chini ya uangalizi wa mletaji, **Ni Rai ya Kamati kuwa Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ione umuhimu**

**wa kuongeza kiasi cha uuzaji wa Dola za Marekani katika soko. Aidha, katika kipindi hiki cha uhaba wa Dola za Marekani katika soko la ndani, mapitio ya haraka ya muongozo wa uendeshaji wa soko la fedha wa mwaka 2020 yanahitajika ili kuondoa vipengele vinavyokwamisha kufanyika kwa Inter-Bank foreign exchange (IFEM). Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kuwa mafuta yanayoenda nchi jirani yanalipiwa na nchi husika, na kwamba fedha zetu za kigeni zitumike kununulia bidhaa za nchi yetu tu ili kupunguza mzigo unaobebeshwa nchi yetu katika kulipia bidhaa za nchi jirani.**

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi huo wa kina, Kamati inapenda kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo

### 4.1 Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO)

a) Ili kuepuka changamoto ya kuchelewa kutekelezwa kwa miradi kwa wakati kama ambavyo imebainika kwenye ukaguzi wa miradi, TANESCO inapaswa kuwa na Mkakati wa usimamizi wa Miradi (*Project Management*) ili kuwezesha miradi kukamilika kwa wakati na hivyo kuongeza uzalishaji wa umeme nchini;

b) Kutokana na deni la mauzo ya gesi kutoka TPDC kwenda TANESCO kuendelea kukua hadi kufikia **Shilingi Bilioni 720** ikilinganishwa na **Shilingi Bilioni 526** za Mwaka wa Fedha 2022/2023. N kwa kuwa licha ya ushauri wa mara kwa mara wa Kamati wa deni hili kulipwa hali inayozoretesha utendaji kazi wa TPDC, **Kamati inashauri Mwaka huu wa Fedha 2023/2024 deni hili lote lilipwe;**

c) Kumekuwa na utaratibu usiofaa wa baadhi ya Taasisi za Serikali kutolipa ankara za umeme hali ambayo imepelekea deni kufikia **Shilingi Bilioni 334.8.** Kwa mara nyingine **Kamati inashauri hatua za makusudi**

**zichukuliwe ili deni hili lilipwe kabla ya Mwaka ujao wa Fedha 2023/2024 kuisha;**

d) Kutokana na baadhi ya maeneo nchini kutokuwa na umeme wa uhakika kutokana na ukosefu wa miundombiu isiyokidhi mahitaji kama vituo vya kupooza umeme (*Substation*) na Mashine umba (*Transfoma*), **TANESCO iboreshe miundombinu hiyo kwa kuharakisha ujenzi wa vituo vya kupooza umeme (*substations*) na kuweka mashine umba zinazoendana na mahitaji; na**

e) Kutokana na ari kubwa ambayo nchi inayo katika kutekeleza miradi mikubwa kama Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, **Serikali ianze mradi mkubwa wa kuzalisha umeme kama huu kwa kutumia fedha zetu za ndani ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini.**

**4.2 Wakala wa Umeme Vijijini –REA**

a) Kutokana na utekelezaji usioridhisha wa miradi mingi ya REA. Uchunguzi wa kina (*Due Diligence*) ufanyike kabla ya kuwapa wakandarasi kazi;

b) Mkakati wa Serikali wa kutaka kuwasaidia Wakandarasi wa nje kwa kuwapatia dhamana (*Letter of Credit* - LC) ujielekeze kwa Wakandarasi wazawa ambao ni wazalendo ili kuwainua;

c) Vipengele vya Mkataba na Kampuni ya Tontan inayotekeleza Mradi wa Lot 39 viangaliwe na hatua kali zichukuliwe ili iwe fundisho kwa Wakandarasi wengine ambao wamekuwa wakisuasua kukamilisha miradi licha ya kupewa fedha; na

d) Pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara na Serikali katika kuhamasisha Nishati safi ya kupikia, Serikali katika Mipango yake iwezeshe matumizi ya majiko ya umeme yenye presha (*pressure cookers*) zinazotumia umeme kidogo pamoja na Mkaa mbadala unaotokana na makaa

ya mawe (*Rafiki Coal Briquette*) ambao umethibitishwa kutokuwa na hewa/kemikali zinazosababisha uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya za watumiaji. **Aidha, Serikali ione namna ya kupunguza kodi za uingizwaji wa majiko ya umeme yenye presha. Mkurugenzi wa Kimataifa wa Energy and Extractive Industries Riccardo Pulit amewahi kusema " *Clean cooking must be a political, economic and environmental priority, supported by policies and backed by investments and multi-sector partneship. To make that kind of change, the level of commitment and the scale of investment matter* "**

## 4.3 Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC)

a) Kamati imebaini kasi ya usambazaji wa gesi majumbani na kwenye Taasisi bado hairidhishi. Katika Mwaka huu wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga **Shilingi Bilioni 20** kwa ajili ya kuunganisha wateja zaidi ya 1500. **Kamati inaitaka TPDC kuhakikisha lengo hili linafikiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Makampuni 20 ambayo yamepewa idhini ya ujenzi wa vituo vya kujazia gesi yanaanza ujenzi huo mara moja;**

b) Mahitaji ya gesi nchini yameongezeka ikilinganishwa na hali ya uzalishaji ilivyo. Kamati inatambua mpango wa Serikali wa kuendeleza vitalu kikiwemo Kitalu cha Ruvuma ambacho kina ugunduzi wa futi za ujazo **Trilioni 1.6** ambapo uzalishaji unatarajiwa kuanza na kiasi cha futi za ujazo **Milioni 40** kwa siku mwishoni mwa Mwaka 2023 na kufikia futi za ujazo **Milioni 140** mnamo mwaka 2027 pale uzalishaji utakapofikia kiwango cha juu. **Kamati inasisitiza uzalishaji katika Kitalu hiki uanze mapema na vitalu vingine ili kusaidia katika uzalishaji wa umeme nchini na matumizi mengine ya majumbani na viwandani;**

c) **Tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi kuanzia mwaka 2016/2017 kiasi cha Shilingi Bilioni 342.34 zimekusanywa. Kamati inatambua nia ya Serikali ya kuhakikisha fedha hizi zinasaidia vizazi vijavyo, Hata hivyo, kutokana na nia ya kuendeleza miradi ya TPDC, Kamati**

**inashauri Serikali kuharakisha kuleta Marekebisho ya Sheria hii ili katika Mwaka huu wa fedha 2023/204 iweze kupitishwa na Bunge; na**

d) Kwa kuwa Kampuni Tanzu ya ya TANOIL ina umuhimu wa kimkakati katika biashara ya mafuta nchini. Kupitia ushiriki wake kwenye biashara hii kunaiwezesha Serikali kuwa na jicho la moja kwa moja na hivyo kuiwezesha nchi kuwa na udhibiti katika biashara hii ikiwemo kuzuia mbinu za wafanyabiashara wasiowaaminifu kupanga njama za kukwepa kodi au kufanya makubaliano ya kupanga bei kwa lengo la kuua ushindani kwa manufaa yao. Ili TANOIL iweze kutimiza majukumu yake kikamilifu, **ipo haja kwa kampuni hii kupewa kila aina ya msaada unaohitajika Ili iweze kujiimarisha kwa kuwa na wafanyakazi wenye taaluma ya juu waliojengewa uwezo katika masuala ya biashara ya mafuta. Aidha, TANOIL iwezeshwe kimtaji ili iweze kujenga mtandao mpana na imara wa kibiashara hapa nchini; na hatimaye baada ya kujiimarisha iweze kuvuka mipaka na kufanya uwekezaji kwenye nchi jirani ambazo zinategemea bandari zetu kuingiza mafuta kwenye nchi zao.**

## 4.4 Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli - PURA

Kamati inarudia ushauri ilioutoa Mwaka 2022 kuhusu kuharakishwa kwa Mchakato wa kunadi Vitalu vilivyo wazi maeneo ya nchi kavu na baharini katika Duru ya Tano hasa ikizingatiwa kuwa mahitaji ya gesi nchini yameongezeka ikilinganishwa na hali ya uzalishaji ambayo ni ndogo.

## 4.5 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

Jukumu la kuweka Vinasaba kwenye mafuta awali lilikuwa linatekelzwa na EWURA. Hata hivyo, baadae jukumu hili lilihamishiwa kwa TBS. kamati imebaini kuwa, kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa jukumu hili ikiwa ni pamoja na TBS kushindwa kutengeneza vinasaba vyake kama ilivyoshauriwa awali. Kamati inashauri:-

a) TBS iwezeshwe ili iweze kutengeneza vinasaba hivi na hivyo kusaidia kupunguza gharama katika bei ya mafuta; na

b) TBS iwezeshwe kwa kuwa na watumishi wa kutosha na vitendea kazi ili kuifanya kazi hii kwa weledi unaostahili.

### 4.6 Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA)

Kutokana na hatari inayoweza kutokea ya upungufu wa mafuta nchini kutokana na ukosefu wa dola za kimarekani nchini kwa ajili ya kulipia shehena za mafuta zinazoagizwa kutoka nje (*Financial Holding)*, Serikali ikiongozwa na Benki Kuu ichukue hatua za makusudi kuhakikisha nchi inakuwa salama.

### 4.7 Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania - TGDC

a) Joto ardhi ni rasilimali muhimu katika uzalishaji wa Umeme. Umeme unaozalishwa kwakutumia rasilimali hii huwa na gharama ya chini sana pindi uwekezaji wa awali unapokuwa umekamilika baada ya utafiti wa kina. Kwakuwa nchi yetu inayo rasilimali hii kwa wingi, Serikali iiwezeshe TGDC ili iweze kutimiza majukumu yake na hatimaye kuwezesha rasilimali ya Joto ardhi kuweza kutumika kuzalisha umeme wa uhakika na wa bei nafuu;

b) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Sekta binafsi zione namna ya kuendeleza miradi mingine inayotokana na joto ardhi kama utalii, teknolojia ya utotoleshaji wa vifaranga kwa mashine(incubators); na

c) Sheria ya sasa inatambua rasilimali ya joto ardhi kuwa ni madini. Hata hivyo, matumizi makubwa ya joto ardhi ni katika umeme. mkanganyiko huu unasababisha wawekezaji kushindwa kuja kuwekeza. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione umuhimu wa kuleta Sheria itakayowezesha rasilimali ya Joto ardhi kujulikana kama nishatii ili kusaidia kupata uwekezaji wa kutosha.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kuchukua fursa hii kukushukuru Spika wetu Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb) kwa uongozi wako thabiti. Pamoja nawe namshukuru sana Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi imara wa unaowezesha utekelezaji mzuri wa majukumu yetu ya Kikatiba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwanza kwa heshima waliyonipa Mimi kuwa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na mwenzangu Mhe, Judith Salvio Kapinga (Mb) kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Tunawaahidi ushirikiano wa kutosha katika kuisimamia Serikali. Aidha, tunawashukuru sana Wajumbe kwa kujitoa wakati wa ziara na wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii. Taarifa hii ya Kamati ni juhudi za Wajumbe hawa ambao wana weledi mzuri katika Sekta hii ya Nishati kwa ujumla. Naomba kwa heshima wajumbe watambuliwe kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Judith Salvio Kapinga, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb
4. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb
5. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
6. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
7. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
8. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb
9. Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni, Mb
10. Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb
11. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb
12. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
13. Mhe. John Michael Sallu, Mb
14. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb
15. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb
16. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb
17. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb

18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb
19. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb
21. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb
22. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Waziri wa Nishati Mhe. Januari Y. Makamba (Mb), Naibu Waziri Mhe. Stephen L. Byabato (Mb), Katibu Mkuu Eng. Felchesm Mramba, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Athuman Mbuttuka, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa ufafanuzi na ushirikiano wanaoipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru kipekee Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (*ndc)* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto *(ndc*) , Makatibu wa Kamati yetu Ndg. Pamela Pallangyo, Ndg. Onesmo Laulau, Ndg. Jesca Sanga, Msaidizi wa Kamati Ndg. Rukia Shaban pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kutuhudumia wakati wote na kuchangia kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati (**Fungu 58)** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Dunstan Luka Kitandula, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
2023

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya kudumu ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge haya ndiyo maoni ya kamati yetu juu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hii, kabla sijaanza kuwaita hao wapo wageni 72 wa Mheshimiwa Pofesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia hawa ni Menejimenti ya WAMA *foundation* wakiambatana na Walimu 13 na wanafunzi 58 kutoka Shule ya Sekondari WAMA Nakayama kutoka Kibiti Mkoa wa Pwani. Karibuni sana Bungeni *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mambo mengine hawa ni watoto wa Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, tunakushukuru sana Mama kwa huduma unayoitoa kwa watoto hawa lakini kwa kuendeleza juhudi ambazo umeanza nazo muda mrefu. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza sasa uchangiaji na tutaanza na Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuwahisha zawadi yangu kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Nishati nikiwa mtu wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Julai nitakuwa nakamilisha miaka 39 tangu nianze utumishi kwenye sekta hii ya nishati, kwa hiyo kwa kuniteua niwe wa kwanza kuchangia umewahisha zawadi yangu ya miaka 39. Kuna lingine niliseme kwa wapiga kura wangu masuala ya umeme nimeyamaliza jana kwenye maonesho ya umeme ya karne. Maonesho yale yaliyofanyika jana hapa hoja zenu zote nimezipeleka kwa Meneja wa Wilaya na wa Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumza kuhusu mafuta na gesi tu umeme nimemaliza. Pia nimuombe Waziri ukatafute kitabu kinaitwa *Tanzania Oil and gas* cha Mzee Sylvester Barongo, kinaelezea historia ya mafuta na gesi kuanzia mwaka 1952, mwaka 1974 tukapata gesi ya kwanza Songo Songo akiwepo, 1982 Mnazi *bay* tukapata gesi Mzee Barongo akiwepo. Pia nafurahi Mzee Ntomola yuko pale, Mzee Khalifan yuko hapa, Mzee Mwandosya bosi wetu yuko hapa. Kitabu ni kizuri ana

kitawasaidia Wabunge waelewe sekta ya gesi Tanzania tunapojiandaa kwenda uchumi wa gesi.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza nizungumzie bomba la mafuta. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Rais Dkt. Jenerali Mseveni kwa kuwa na msimamo thabiti kuhakikisha bomba la kutoka Hoima mpaka Chongoleani linajengwa. Ujenzi wa bomba hili pamoja na kuleta faida za ajira litafungua njia za kuweza kuchochea wawekezaji katika sekta ya mafuta waweze kuweza zaidi. Sisi tunayo rasilimali ya mafuta lakini watu wengi wamekuwa hawaji hapa wakijiuliza mafuta ya Kigoma utayafikishaje Dar es Salaam, Eyasi Wembere utayafikishaje Dar es Salaam. Sasa kwa kujenga bomba la mafuta ni kwamba wawekezaji wengi watapata motisha. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo mimi ninaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwa kutumia bomba la mafuta ajira zitakazotengenezwa zaidi ya 10,000 ni kwamba vijana wa Kitanzania sasa wanakwenda kufundishwa stadi za Kimataifa, baada ya ujenzi wataweza kutumika katika viwango ya Kimataifa mahali popote duniani. Sambamba na hilo ninaipongeza Wizara na naipongeza Serikali kwa kumaliza rejea ya *product sharing agreement,* hili suala la *OPSA* limecheleweshа utafutaji mmefanya maamuzi mmeweza kushughulikia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la *bulk procurement* ununuaji wa mafuta kwa wingi. Bila kusema mengi naunga mkono mapendekezo ya Kamati iliyopewa dhamana ya kusimamia shughuli hii ya *bulk procurement.* Kama huwezi kujua adha angalia kwa mwenzako, mwaka mzima tumemaliza pamoja na mitikisiko ya kidunia hatukuweza kupata ukosefu wa mafuta nchini. Majirani wetu wamepata hiyo adha, hata Watasha huko Ulaya wamekosa mafuta lakini sisi tumekwenda vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wamehangaika kutafuta njia mbadala lakini ule ulinganisho wa kiasi cha kununua mafuta wengine wananunua bei ghali mara nne. *Premium* yetu iko kwenye 40 kuna wenzetu wananunua *premium* ya 160. Kitabu kile

cha Mzee Barongo ambae ni bosi wangu kinaelezea namna ya kutafuta *premium* mkitafute muweze kukisoma.

Mheshimiwa Spika, sasa zaidi niende kwenye mradi wa *LNG,* nilimwona Mama salma anapiga makofi, anashangilia tunakuja Lindi na mimi nakuja Lindi ujombani nami nifaidi. Mradi wa *LNG* ni mradi mkubwa wa dola bilioni 42 zaidi ya bajeti au sawa na bajeti yetu ni mradi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, mimi nimesoma suala la maamuzi. Nichukue fursa hii kipekee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanya maamuzi amefanya maamuzi, hivi visima havikuwepo leo lakini imekuwepo dana dana kwa miaka saba kama alivyosema Waziri, lakini Mheshimiwa Rais akatoa maamuzi. Mwezi Juni nilimsikia mwenyewe akasema nendeni mtekeleze haraka. Sasa niko hapa kuwaelekeza kwa nini Mheshimiwa Rais anataka tutekeleze mradi huo kwa haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa *LNG* utakapokuwa umefanyika uwezo wa Tanzania kuuza nje kwenye masoko ya Kimataifa utaongezeka, tutapata pesa nyingi za kigeni, ulali wa kuuza na kununua Tanzania tutakuwa na *advantage* tuta-*export* zaidi. Sasa hivi Tanzania tuna-*export* bidhaa zenye dola bilioni 12 kwa mwaka. Gesi peke yake itakuwa na uwezo wa kusukuma katika soko la Kimataifa zaidi ya uwezo huo.*(Makofi)*

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Profesa Mkumbo.

## TAARIFA

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mwijage, amesema dola bilioni 42 ni sawa na bajeti yetu, *actually* ni sawa na *GDP* yetu. Kwa hiyo, ni fedha nyingi ambazo ni pesa nyingi kwa kweli uamuzi anaouzungumza ni uamuzi mzuri na ni uamuzi mkubwa sana, kwa sababu ni fedha nyingi na zitabadilisha kabisa uchumi wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nizungumze taratibu aliyenipa taarifa ni Profesa na amesema anatoa taarifa kusisitiza Mheshimiwa Rais kufanya maamuzi, weka kwenye mabano nakubali taarifa hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini Mheshimiwa Rais amesema tuharakishe? Mafanikio ya kuanza kutumia gesi yataharakisha ujenzi wa uchumi wa viwanda. Siyo ujenzi wa viwanda ni kujenga uchumi wa viwanda ina maana chuma utakayoipata shughuli za kuendeleza sekta ya gesi *LNG* itatupatia pato, itafundisha watu. Kwa hiyo, tunapozungumzia sekta za uzalishaji iwe kilimo, mifugo, sekta zote tutaweza kuzalisha kwa tija. Pamoja na kuwa na mafuta tutaweza kuwa mabingwa katika dunia kwa kutumia haya mazao ambayo yamekuwa yakitusaidia siku moja, siku nyingine, tutauza kahawa nyingi, maziwa mengi, pamba nyingi ile *C to C* sasa tutaweza kuwa na viwanda vyetu hapa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwenye bomba la mafuta tunakwenda kutengeneza huo ndioy mfano kwenye chuo cha Lindi, tunakwenda kufundisha vijana wetu wawe wataalam katika sekta za mafuta ili Tanzania sasa miaka ijayo wawekezaji wanakuja kuchukua vijana wetu hapa na kwenda kufanya kazi sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kutenegenza huu mradi kwa kukubnaliana sasa wawekezaji mahili wa dunia wanajua kwamba Tanzania sasa ni mahali salama pa kuwekeza. Makampuni yanakuja sisi tuna *TCF* zaidi ya 68 hizi mlizonazo, mimi sio mtabiri lakini najua kwa uhakika hapa tuna mafuta, hapa tuna gesi lakini hauwezi kuyapata mafuta mpaka uyachimbe.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe sababu nyingine kwa nini tunafaidi kitu hiki. Faida nyingine katika utafutaji wa mafuta ni kwamba sisi Watanzania kwa fursa tuliyonayo tunakwenda kubeba nchi nyingine zilizotuzunguka. Tulikuwa na mradi wa mbolea ulikwama kwa kuangalia gesi tuitumie kwa namna gani, sasa bila kutetereka tutatengeneza kiwanda chetu cha mbolea na kitaweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe Wabunge wenzangu, na Mheshimiwa Jafo naona simuoni na wenzangu niliokuwa sisi ni mahiri wa gesi, sisi tunajua gesi. Gesi inayokuja ni neema tumekaa nayo tumejitafakari. Kwa hiyo, wale wanaofikiria kwamba gesi ni laana ni kwao. Sisi gesi tunaijua tumedhibiti mafuta tunajua namna ya kuitumia. Pia, lengo la nishati hii ni kwa ajili ya mapato na matumizi na ustawi wa Watanzania. Tunakwenda kujenga uchumi imara, uchumi wezeshi na uchumi ulio jumuishi. Kwa hiyo, naunga mkono maamuzi ya Mheshimiwa Rais kwamba tuharakishe ujenzi wa gesi ili iweze kuwafikia wananchi ili kusudi ichangamshe uchumi nan chi yetu iweze kuwa ni nchi yenye ushindani ambayo inakwenda kwenye uchumi mkubwa, uchumi wa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ajiandae.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi, afya njema niweze kusimama hapa kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya miaka miwili ya utawala wake, kwa kweli miradi yote ya kimkakati inatekelezwa na pia miradi mipya ameanzisha kwa kweli tumamshukuru sana na tunampongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii tena kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutuletea miradi mingi kwenye Jimbo la Kwimba katika kipindi hiki cha miaka miwili lakini niseme michache tu. Kwa kipindi cha mwaka mmoja huu tumepata hospitali mpya ya Wilaya, vituo vya afya viwili vipya. Kwenye masuala ya maji tumepata miradi mitatu

mikubwa ya maji Hungumalwa sasa hivi tuna maji ya bilioni nne, Shibumulo pia kuna mradi wa maji unajengwa pale. Mambo haya niyaseme kwa sababu kwenye Jimbo la Kwimba tuna Kata 15 sasa hivi Kata 14 tuna maji ya Ziwa Victoria yote ni kwa sababu ya mafanikio ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Tumebakiza Kata moja tu ambayo tunategemea mwaka ujao tutapata maji, maana yake Jimbo la Kwimba wananchi wote wanapata maji safi na salama ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda hautoshi nimesema miradi michache. Naomba nichukue nafsi hii kwenda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya matumaini uliyoisema hapa tunakupongeza sana. Mheshimiwa Waziri, tunakupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya wewe, Naibu wako, Watendaji wako wote wa Wizara ya Nishati, hongereni sana kwa kazi nzuri sana mnayoifanya. Vilevile, nichukue nafasi hii kupongeza taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara yako, wanafanya kazi nzuri inaonekana. Kwa kweli mwaka huu Mheshimiwa Waziri umekuja hapa hakuna kelele kwenye Wizara ya Nishati lakini nakumbuka mwaka jana ulipofika hapa kulikuwa na kelele nyingi kwenye Wizara ya Nishati, mwaka huu kidogo pametulia.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri nikupongeze kwa maonesho ya mwaka huu yaliyofanyika kwenye viwanja vya Bunge pale nje, kwenye maonesho ya nishati. Nimefika pale nimekutana na watu wa *REA* na maeneo mengine mbalimbali, kwa kweli maonesho ni mazuri sana. Pia, teknolojia mliyotumia kutoka viwanja vya Bunge mmenipeleka mpaka Julius Nyerere nimefika kwenye bwawa pale nashukuru sana nimepaona sina cha kusema. Niseme tu hongereni sana kwa kazi kubwa mnayoifanya kwenye bwawa, endeleeni Mungu awatangulie kuhakikisha kwamba mradi ule kama ulivyosema kwenye hotuba yako kwamba mwaka ujao mradi utakamilika nawatakia kila la kheri ule mradi ukamilike.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nitaongea hoja mbili tu. Hoja ya kwanza nitaongelea kuhusu *REA*. Mimi nawapongeza sana *REA* wanafanya kazi nzuri. Jimbo la Kwimba mimi nimebakiza

Kata mbili ambazo ni Kikubiji na Mhande ambapo sasa hivi ndiko wanakofanya kazi, wamesema mpaka Agosti mwaka huu watakuwa wamemaliza kuunganisha umeme kwenye vijiji vyote. Ninashukuru Jimbo la Kwimba mpaka Desemba tutakuwa tuna umeme kwenye vijiji vyote, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, changamoto tunazopata ni kwamba wanaunganisha vijiji vingi lakini tatizo liko kwenye vitongoji ambavyo vimebaki, kwa sababu watu wameshaona utamu wa kupata umeme jirani sasa wanataka na wao wapate umeme, hiyo changamoto ni kubwa Mheshimiwa Waziri kama ulivyosema kwenye hotuba yako kwamba utatuunganishia vitongoji 15 kwa mwaka ujao kwa kweli kwenye mahitaji ya Jimbo la Kwimba haitoshi nafikiri na wengine pia haitatosha, mimi ninashauri kwamba hivi vitongoji 15 havitatosha tunaomba uongeze angalau vifike hata kwenye vitongoji 50 kwa mwaka kesho kuunganisha kwa kila Jimbo angalau tutakuwa tumepunguza kero kwa wananchi. Hilo ni ombi langu kuja kwako kwamba tunaomba utusaidie kuongeza vitongoji angalau vifike 50 kwa mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Waziri ningependa kulizungumzia hapa ni kwamba Jimbo la Kwimba tuliahidiwa kuletewa taa za barabara za *REA*, nina Mji wa Ngudu pale nina lami kilomita nne inaelekea kilomita tano lakini hakuna taa hata moja ya barabarani.

Mheshimiwa Spika, tunaomba angalau tuliahidiwa taa 200 tutaletewa ili angalau na miji yetu ipendeze kidogo kwa sababu sasa umeme uko vijijini, umeme uko kwenye miji, kwenye nyumba za watu lakini barabara ni giza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningeomba wakati wa majumuisho basi unisaidie angalau kunipatia hata taa hizo 200 za barabara angalau miji yangu ya Hungumalwa, Shilima, Ngudu, Gojiro, Malege na Milama angalau vipate taa za barabara. Mheshimiwa Waziri naomba utusaidie kwenye taa za barabara.

Mheshimiwa Spika, lingine Mheshimiwa Waziri ningependa kulizungumzia sasa hivi hapa ni suala la *EWURA*. *EWURA* wanafanya kazi nzuri sana lakini Mheshimiwa Waziri Sheria na

Kanuni za *EWURA* zimepitwa na wakati. *EWURA* ilianzishwa na Sheria na Kanuni ambazo wakati ule tulikuwa hatuna *bulk procurement system*.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa sasa hivi Kanuni na Sheria wanazozitumia *EWURA* zimepitwa na wakati kwa sababu kwa mfano, ukienda mimi naomba ni-*declare* kwamba ni mdau wa Wizara, hii naji-*declare* kwamba *EWURA* wanapofanya vipimo vya vinasaba kwenye vituo, wamakuta wanaenda tofauti na sera za sasa hivi za Mheshimiwa Rais kwamba kazi iendelee wao wakifika wakikuta kuna tatizo kwenye kisima kimoja cha tenki wanafunga kituo kizima maana yake hawaendani na sera ya Mheshimiwa Rais ya kazi iendelee wao wanafanya kazi ifungwe.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri hivi vituo kufungwa ni kero na wakati unakuta Mheshimiwa Waziri ni kwamba kwenye kituo umekuta kuna mafuta aina tatu, unakuta tatizo lipo kwenye tenki moja lakini unafunga kituo kizima, sasa kile kituo ukikifunga maana yake mfanyabiashara yule amewekeza, ana madeni ya benki ana wafanyakazi wanafanya kazi halafu zile faini ni kubwa. Zile faini ni kubwa sana kwa hiyo, mimi ningeshauri hizi Sheria na Kanuni ziangaliwe upya kwamba zitatusaidiaje.

Mheshimiwa Spika, jingine Mheshimiwa Waziri niseme kwenye suala la *EWURA* kuna suala la ki-*technical* wanafanyafaga kukagua *Research Octane Number (RON)* inatengenezwa kwenye *refinery* haitengenezwi kwenye depo wa la kwenye kituo *RON* inatoka kwenye kiwanda *so* wanakuja wanapima *RON* wakipima *RON* ni neno la kitaalamu unakuta *RON* haiko sawa, isipokuwa sawa unapigwa penati ya milioni saba, milioni 20, unafungiwa kituo.

Mheshimiwa Spika, hili suala la *RON* linatengenezwa kwenye *refinery* haitengenezwi Tanzania, sasa mtu mwenye kituo ana makosa gani kama *RON* iko tofauti? Maana yake wakati meli au wakati shehena imetoka kwenye *refinery* imekuja Dar es Salaam watu wa *TBS* wanaopima mafuta hayo wana makosa hawakufanya ukaguzi vizuri pale, yale mafuta yameshuka mpaka

kwenye vituo, kwa hiyo mwenye depo hawezi kubadilisha *RON,* mwenye kituo hawezi kubadilisha *RON.*

Mheshimiwa Spika, *RON* inatengenezwa kwenye kiwanda, kwenye *refinery*. Kwa hiyo, mimi ningeshauri hizi kanuni na sheria za *EWURA* mziangalie upya zilianzishwa wakati hakuna *bulk procurement,* kazi wanafanya nzuri lakini sheria hizi ndiyo zimewabana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ndiyo huu tu ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nichangie hoja, ahsante sana. Naunga mkono hoja asilimia mia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena unapochangia zungumza na Kiti, kwa sababu nimemuona Mheshimiwa Waziri mpaka inabidi ageuke sasa ili amsikilize vizuri Mbunge anayezungumza na yuko nyuma yake. Zungumza na Kiti yeye anasikiliza, ukimwambia yeye maana yake unataka awe anakutazama maana unataka uwe unaongea naye yeye. Wewe ongea na Kiti ndiyo utaratibu wa kanuni zetu. Wewe unamtaja Spika Waziri anasikiliza, pongezi zake unampa lakini usimwambie yeye kana kwamba ndiyo lazima akusikilize kwa sababu anaweza akatoka nje kidogo, sasa akitoka nje utakuwa unamwambia nani hapa maana yeye mwenyewe atakuwa hayupo.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Joseph Mkundi, ajiandae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru *Allah Subhanahu Wa Ta'ala* lakini nikushukuru wewe kwa kuchangia siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama sikumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kumpa nafasi ya Uwaziri ndugu yangu January Yusuf Makamba kwa kweli Mheshimiwa Rais ametutendea haki sana Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ambayo watendaji wake wana-*combination* sawa sawa ni Wizara hii ya Nishati na Madini. Ukianza na Waziri mwenyewe Mheshimiwa Makamba, Naibu Waziri Stephen Byabato, Katibu Mkuu *Engineer* Mramba, Mkurugenzi wa *TANESCO* Maharage Chande Mkurugenzi wa *REA Engineer* Hassan Said, ukienda kwa Mkurugenzi wa *EWURA*, Daktari James Andilile mambo ni bambam kabisa kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika mambo watu wa kusini Mtwara, Lindi na Ruvuma tutayaandika kwenye historia yetu ya miaka na miaka ni mradi huu wa *LNG* ambao leo mazungumzo yamekwisha kamilika. Tangu miaka ya 2011 huko, tulikuwa na matumaini makubwa ya kupata mradi huu wa *LNG* tukatarajia sasa mambo ndiyo yanakimbia Mikoa ya Kusini, katikati mambo yalisimama. Ujio wa Daktari Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, mambo yamefunguka Kusini. Hakuna tunachoweza kumlipa Mheshimiwa Rais zaidi ya kumuombea dua kwa *Allah subhannah wasubuhanah* ampe maisha marefu neema ya Kusini tuione. Aendelee pia kumuamini Mheshimiwa January kwa sababu anayasimamia haya ambayo ndio dhamira ya ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara yenye watu wasikivu ni Wizara hii ya Nishati. Mtwara kwenye suala la *REA* tumekuwa miongoni mwa watu ambao kama Wizara ilivyosema kwenye taarifa yake, umeme wa Taifa ile asilimia 70 unatoka Mtwara lakini Mkoa wa Mtwara ndiyo Mkoa ambao vijiji vingi havina umeme, kwa usikivu wa Waziri na Mkurugenzi wa *REA* tumeshafanya na vikao Mkoani Mtwara, tukakaa na Wakandarasi lakini na juzi tumekaa tena na Wizara pamoja na Waziri, ametupa ahueni hapa ya siku 90 kwenda kukimbiza mambo Mkoa wa Mtwara ambao vijiji vingi havijapata umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupa vijana hawa ambao wanasikia. Tuliwaomba watupeleke kule mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kumbe wakati tunaomba wenzetu walishakimbia hatua mia mbele hatukujua, yale tuliyoyaona jana na juzi unapelekwa Bwawa la Mwalimu Nyerere ukiwa Dodoma

basi mpeleke na Mikoani watu waone taaluma ile. Kuona ni kuamini Watanzania wengi tunapozungumza mafanikio ya Bwawa la Mwalimu Nyerere wengi hawajaona kama haya ambayo Wabunge tumeyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwako Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla, pelekeni vile vifaa basi Mikoani, Wilayani tuwaoneshe Watanzania kazi mnayoifanya, kwamba Rais amewaamini na ninyi mnafanya, mnatekeleza na leo mmetupa ahueni nyingine kwamba mwakani mambo ni bambam, sasa tunataka nini tena Watanzania, eeh?

Mheshimiwa Spika, kama bwawa likijaa na mkaanza kutupa umeme ndiyo faraja yetu sisi, ndiyo faraja kubwa. Mheshimiwa Waziri nchi jirani ya Msumbiji sisi tunapakana na Mkoa wa Cabo Delgado sisi watu wa Mtwara lakini hatuko mbali na Mkoa wa Emba wenzetu nao wanayo gesi. Huu mchakato wa *LNG* ambao wewe umeuchangamkia, kama kuna namna ya ku-*fast track* hebu tuanze sisi kabla ya wenzetu kwa sababu na wenyewe wanautaka. Uone namna sahihi ambayo mnaweza ku-*fast track* hii *LNG* iweze kukimbia kwa haraka sana. Ni ni majirani sana sasa tukianza tutakuwa na fursa kubwa ya kuwauzia wenzetu wa nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, tuliopata bahati ya kwenda kwenye bwawa kwa kuona kabisa, zamani Daktari siyo Daktari kama wewe Dkt. Tulia wa Falsafa tunao Madaktari wasio wa Falsafa ndani humu. Daktari Musukuma alikuwa haelewi mambo ya Bwawa la Mwalimu Nyerere lakini ulitupa ujumbe wa Kamati na yeye, katika vitu ambavyo tunaweza kumpongeza Waziri January Makamba ni utashi wake wa utayari wa kuwa Mwalimu wa kufundisha na kueleza uhalisia.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa *site* kule Daktari Musukuma, Daktari wa Heshima, walikuwa hawakujui kwa nini amepewa Udaktari wa Heshima leo nikuambie kwa uwezo wa Musukuma mpaka kuanzisha biashara kubwa ametunukiwa Udaktari wa jambo hilo, kwa hiyo usipate shaka na Udaktari wake. Alikuwa haelewi kwamba January anafanya nini lakini tulipokwenda Bwawa la Mwalimu Nyerere tukakaa kwenye chumba akatupa

mpango wa Serikali, nini kilisimama, nini kinaendelea, leo kati ya Mabalozi wazuri wa Wizara hii, Musukuma atasema hapa atachangia, amekiri kwa sababu kuona ni kuamini, aliyoyaona leo nadhani katika bajeti ambayo tusingechangia wengi, maana mambo mengi tumeshayaona tayari, kila kitu kipo tayari, ilikuwa watu sita, saba ipite watu wakaendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kazi iliyofanywa na Wizara kuanzia semina tulizopata bora kabisa, kuelezwa mipango mizuri ya Serikali, jana tukapelekwa Bwawa la Mwalimu Nyerere, mimi nilitamani nikimaliza hapa tumalize mambo. Tumalize tu tupitishe hawa wakubwa wakafanye kazi tunataka matokeo. Tukipitisha hii bajeti tunataka matokeo 2024 kesho tunapokwenda hata marafiki zetu hawa basi wanaweza wakaja huku tukaungana nao kwa sababu wanaona matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama kuna jambo limetendewa haki kabisa ni hotuba na bajeti ya Wizara hii kwa namna ilivyoandaliwa kwa utashi mkubwa kwa umakini mkubwa, ubora mkubwa, umakini mkubwa, sina namna ya kuongeza zaidi ya kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa nikawa najiuliza sijui nimuite mtoa hoja aje ahitimishe? Ahsanteni sana, ni wazo zuri lakini maneno mazuri aliyoyasema Mheshimiwa Katani na Wabunge wengine nao wanataka waseme ili waeleze yale ya maeneo yao. Kwa hiyo, wacha na wao wapate nafasi. *(Kicheko/Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba nianze kwa kumshukuru Mungu hatimaye nikushukuru wewe, lakini kabla ya kusema jambo lolote niongezee pale ambapo ulizungumzia kuhusu wale watoto wangu.

Mheshimiwa Spika, wale ni watoto ambao wanatoka kwenye Shule ya Sekondari ya WAMA Nakayama iliyopo Mkoa

wa Pwani ndani ya Wilaya ya Kibiti, watoto hawa wamemaliza Kidato cha Sita hivi karibuni kwa hiyo wote ni watoto wa Kidato cha Sita. Jambo lingine la pekee hawa watoto wanatoka nchi nzima katika Taifa letu la Tanzania, ni watoto yatima na wanaotoka katika mazingira magumu, wapo pale kwenye shule ile wanagharamiwa na Taasisi ya Wanawake na Maendeleo kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nilitaka niongezee hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Daktari Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya katika Taifa letu la Tanzania. Hakuna mashaka hata kidogo kila Mbunge atakayesimama hapa hataacha kumpongeza Mama kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya. Kazi hiyo kwenye huduma za jamii kwenye afya, kwenye elimu kwenye miundombinu ya barabara na kila eneo Mama amefika.

Mheshimiwa Spika, kufika siyo kwamba yeye afanye ziara atembelee pale kwenye aidha Wilaya au Kijiji, uwepo wa miradi mikubwa ya maendeleo ni kwamba yeye ameshafika katika eneo husika, nampongeza sana Mama Mwenyezi Mungu amjalie na ampe maisha marefu ili azidi kuwatumikia watu Watanzania hawa na kutatua changamoto zao zinazowakabili, ahsante ama tunakwenda ahsante Mama tunakushukuru, ahsante mama tunakutakia maisha marefu yenye heri na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa nianze kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wetu wa Nishati January Makamba na Naibu Waziri wake bila kumsahau Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, hongereni sana. Nikupongeze sana Mheshimiwa January Makamba kwa maono yako makubwa ambayo umeyaonesha katika Wizara yako, lakini maono hayo ni yapi?

Mheshimiwa Spika, tendo la kutuwekea pale maonesho yale, yaani umeonesha ubunifu mkubwa na huu wala haujawahi

kutokea, hongera sana Mheshimiwa Waziri Makamba. Hii inadhihirisha kwamba wewe ni kijana mwenye maono, unategemea kufika mbali zaidi Mwenyezi Mungu akikuwezesha na tunaomba akuwezeshe, umeonesha kazi kwa vitendo na siyo maneno. Hongera sana kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niende kwenye eneo la kushamirisha Nishati safi ya kupikia. Kwa kweli, Mheshimiwa Waziri huyu ameweka historia ya aina yake na historia hiyo ni kwa mara ya kwanza nishati ya kupikia kutambuliwa, siku zote watu hawatambui nishati hiyo wakati hii ni muhimu sana. Hii nishati inatumika zaidi na wakina Mama wa kada zote, wakina Mama wenye kada ya juu, kada ya kati lakini kule kada ya chini wale maskini wale ndiyo wanaotumia nishati hii kwa kiasi kikubwa, kwa kuwatambua hawa kwa kweli umefanya jambo moja ambalo ni kubwa na jema.

Mheshimiwa Spika, kinachofurahisha zaidi asilimia 80 ifikapo mwaka 2023 tutakuwa tumeifikia nishati hii, lakini wapo wa nishati hii ina maana kwamba tutafanya mazingira yetu yawe salama zaidi watu waache kukata miti, kutumia kuni na kusababisha kutumia kwa nishati hii na mazingira yetu yanakuwa salama zaidi. Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nishati ametupa majiko 100 kila mtu amempa majiko 100, Wabunge wote sisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumepewa majiko 100, hata wewe umepewa, hata Mheshimiwa Waziri Mkuu amepewa hilo jiko, Mheshimiwa Katibu wa Bunge, yaani wote wamepewa ili wakayatumie. Sasa ninachokuambia, kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuko tayari kwenda kuyatangaza haya majiko Majimboni kwetu ili wananchi wetu watumie nishati iliyo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwepo wa nishati ya uhakika ni jambo la msingi kwa maendeleo endelevu na uchumi wa Taifa lolote lile hapa ulimwenguni. Nishati ni kila kitu, nishati ndiyo maendeleo, nishati ndiyo inayoinua uchumi wa watu. Nipongeze kwa nishati hii upande wa umeme, sasa hivi umeme tunao ndani ya vijiji vyetu,

umeme tunao ndani ya Kata zetu hali kadhalika umeme utapelekwa ndani ya vitongoji vyetu ili baada ya miaka michache ijayo ndani ya kata kutakuwa na umeme, ndani ya vijiji kutakuwa na umeme na ndani ya vitongoji vilevile kutakuwa na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, umeme huu ambao umepelekwa kule vijiji, kwa mfano mmesema vituo 66 vya afya vimepelekewa umeme nchi nzima. Ongezeni kupeleka umeme huu kwenye vituo vya afya, kwenye zahanati zetu ambako kule ndiyo kuna watu wengi, wakati mwingine watu wanatumia sijui nikisema vikoroboi mtanielewa, zile taa zile ndogo ndogo wanatumia vikoroboi wakati mwingine ya kufanyia hata mambo makubwa ya msingi. Pelekeni umeme huo kule vijijini na kwenye zahanati na vile vituo vya afya, hali kadhilika kwenye shule zetu, baadhi ya shule umeme hakuna, msisahau hili kwa sababu tunataka tuwe na elimu iliyokuwa bora, elimu haiwezi kuwa bora kama wanafunzi hawana umeme kule shuleni, hawatapata muda wa kujisomea. Huo ndiyo ushauri wangu tupeleke umeme wa kutosha kule kwenye taasisi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nije kwenye lile lenyewe kabisa. Jambo lenyewe kabisa ni suala la *LNG*. *LNG* inapatikana kule kwetu ndani ya Mikoa ile ya kwetu lakini hasa Manispaa ya Lindi, Manispaa ya Lindi iko ndani ya Mkoa wa Lindi, huu mradi unapatikana katika Manispaa lakini Jimbo la Lindi Mjini, Jimbo la Lindi Mjini Manispaa ile ina Majimbo mawili, Jimbo la Lindi Mjini na Jimbo la Mchinga. Sasa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa dhamira ya dhati ya kuleta ukombozi ndani ya Mikoa yetu ya Kusini, ndani ya Mkoa wa wetu wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema haya? watu wa kule wanaambiwa kila siku kipato chao kidogo, maskini. Huu mradi utakuwa ndiyo ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Lindi, wananchi wa Mtwara, wananchi wa Ruvuma na Tanzania kwa ujumla. Mapato yatakayopatikana hapa pia yatawanufaisha wanalindi, wanamtwara, wanaruvuma, yatanufaisha Taifa la Tanzania, yatanufaisha na watu wengi mbalimbali katika dunia

hii, kwa sababu kitakachopatikana kitauzwa nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona muda wangu umekaribia. Baada ya kuyasema hayo, mwisho kabisa mambo ni mazuri, ni makubwa, ninachoshauri, bajeti iliyopangwa ipelekwe kwa wakati. Kupelekwa kwa bajeti kwa wakati ndiyo mafanikio ya mipango yote katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa Shally Joseph Raymond ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu wa mawazo kwenye hotuba ya Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa nafasi aliyonipa, kuendelea kupumua lakini nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utendaji kazi wake mzuri lakini na ujasiri wake mkubwa katika kufanya maamuzi na kutenda kwa maslahi ya wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kukupongeza sana kwa umahiri wako mkubwa katika kutuongoza Bunge hili. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisipowapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati, kwa kweli wanaonesha umahiri mkubwa na wanatenda mambo mengi yenye maslahi kwa Taifa letu, tuna kila sababu ya kuwatia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa kwenye maeneo mawili, nikitambua umuhimu wa nishati kwa sababu tafiti mbalimbali zimeonesha mahusiano ya moja kwa moja kati ya nishati ya umeme na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwenye

Jumuiya mbalimbali, umeme hasa kwa ujumla ni jambo muhimu sana na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali yetu kusambaza nishati hii ya umeme tuna kila sababu ya kupongeza.

Mheshimiwa Spika, ninaushauri kwenye maeneo mawili, eneo la kwanza ni eneo la *REA*. Kazi kubwa imefanyika na kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, tuna vitongoji zaidi ya 36,000 ambavyo havijapata umeme, bado kuna kazi kubwa inatakiwa kufanyika. Ni kweli kwamba katika usambazi vijiji vingi vimepata nishati hii ya umeme lakini tuna kila sababu ya kufanya tathmini sasa tukiangalia vitongoji lakini tuende zaidi kwa kuangalia idadi ngapi ya kaya ambazo zimepata nishati ya umeme, itatupa changamoto na kuona namna gani tuna kazi nyingine kubwa ya kufanya ili tuweze kufikisha nishati hii ya umeme, kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *REA* imefanya kazi kubwa lakini bado tunahitaji tubuni vyanzo vingine kuweza kusaidia Mfuko wa *REA* ili angalau mfuko huu ukiweza kutuna basi nishati hii ya umeme iweze kusambaa zaidi kwenye vitongoji vyetu. Kwa hiyo, mimi kwa nafasi yangu ningeweza kupendekeza ikiwezekana hata kwenye nishati kwa mfano, kwenye mafuta ikiongezwa hata shilingi moja tuweze kuongeza vilevile kutunisha Mfuko wa Nishati hii ya umeme ili maeneo yetu yaweze kupata umeme. Kwa sababu pamoja na nishati hii kusambaa kwenye vitongoji, kwenye Jimbo kwa mfano la Ukerewe bado tuna vitongoji vingi havijapata umeme, mbaya zaidi kuna vitongoji ambavyo vimefikishiwa umeme umefika kwenye kitongoji lakini kaya nyingi bado hazipata nishati hii ya umeme. Kwenye vijiji kwa mfano kama Muruseni, Hamuyebe umeme umefika lakini bado kaya hazipata umeme *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilitamani nichangie ni kwenye maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa. Jimbo la Ukerewe tuna visiwa vingi ambavyo viko mbali na Gridi ya Taifa. Nikupongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu, mmepata ujasiri mkaweza kututembelea Ukerewe mkaangalia changamoto zilizoko kwenye Visiwa vyetu vya Ukerewe. Bado visiwa vyetu vingi havijaweza kupata nishati hii ya umeme. Kisiwa kama cha Ukara, Mheshimiwa Waziri unakifahamu kuna watu

pale Jumeme wanatoa umeme kama wanavyotoa kwenye Kisiwa cha Ilugwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitoe ushauri kwenye Kisiwa cha Ukara, hebu kaa na wataalamu wako ikiwezekana na inawezekana angalieni, uwezekano wa kutumia *sub-marine cable* ili kuweza kuiunganisha Ukara na Gridi ya Taifa na kwa sababu sasa hivi mnapeleka umeme mkubwa, nikupongeze Mheshimiwa Waziri na Wizara yako, kwa mradi ambao mmeuandaa mnapeleka umeme kwenye Visiwa vya Ukerewe ambao kutoka *KV* 66 mpaka *KV* 132, umeme huo utahitaji kupata mzigo na ili mzigo huu uweze kupatikana ni muhimu sana visiwa kama cha Ukara ambacho kina Kata zaidi ya tatu ili kiweze kuunganishwa na Gridi ya Taifa kuongeza mzigo kwenye umeme huu mnaopeleka kwenye Visiwa vya Ukerewe. Kwa hiyo, nikushauri kaa na wataalam wako ikiwezekana muweke *cable, sub-marine cable* muweze kuunganisha kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika ukurasa wa 39 wa hotuba yako umeonyesha namna ambavyo mnajiandaa kupeleka umeme kwenye maeneo yaliyoko mbali na Gridi ya Taifa. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri visiwa kama Gana, visiwa kama Burudi, Bwilo, Bweru, Sizu na kadhalika ambavyo kulikuwa na Wakandarasi walienda kwa ajili ya kupeleka umeme lakini wakaishia njiani, niombe sana kwa kushirikiana na halmashauri tunajitahidi kuondoa vikwazo vilivyopo ili sasa hawa wakandarasi walio tayari waende kupeleka umeme kwenye maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo nilitaka nichangie, yote haya tunawapongeza tuna wasifu kwa sababu kuna kazi inafanyika hasa kupitia Shirika letu la Umeme la *TANESCO,* lakini yote haya yanafanyika kwa sababu kuna watendaji, kuna watumishi, kuna wafanyakazi wanafanyakazi nzuri ndiyo maana shirika linafanya kazi nzuri. Mheshimiwa Waziri kuna minong'ono inaendelea chini kwa chini, wafanyakazi wako kwenye Shirika hili la *TANESCO* wanalalamika kuna mambo hayako vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mkataba wa kiutumishi waliokua nao kwa ajili ya kuboresha maslahi yao ya kiutendaji kazi, lakini

katika haya moja katika malalamiko yao Mheshimiwa Waziri kuna mabadiliko yamefanyika, huko nyuma ilikuwa watumishi wakienda likizo wanalipwa mshahara wa mwezi mmoja ili waende likizo wakirudi wanaendelea na majukumu yao, lakini katika mabadiliko yaliyofanyika sasa inasemekana kwamba sasa watumishi wakiondoka kwenda likizo hawapewi pesa yoyote, anatakiwa aende kwa nauli yake, akishalipa nauli yake atunze risiti, akirudi ndiyo aanze kudai alipwe fidia kwa zile risiti kutokana na namna ambavyo amesafiri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri jambo hili litawakatisha tamaa watumishi, liangalieni upya ikiwezekana mliondoe urudishwe utaratibu wa zamani ili watumishi hawa wafanye kazi wakiwa na *morale,* wakiwa na moyo kwa ajili ya kuleta sifa kwa shirika na tija kwa Taifa letu ili wananchi wetu waweze kupata huduma wanayoitarajia. Vilevile, Mheshimiwa Waziri wamekuwa hawana uhakika na mambo yao, wamekuwa na hofu kwamba inasemekana kwamba mnatarajia kupunguza watumishi kwenye shirika hili, mbaya zaidi taratibu hizi zinaendelea bila kuhusisha Chama cha Wafanyakazi, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, kama kweli haya yapo Mheshimiwa Waziri ninaomba uyafanyie kazi ili changamoto hizi ziondoke, watumishi wetu katika Shirika la Umeme la *TANESCO* wafanyekazi wakiwa na moyo, wakiwa na *morale* ili tija ile tunayoitarajia kutoka kwenye shirika letu hili iweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nikushukuru sana kwa nafasi hii, lakini ninakuomba tena Mheshimiwa Waziri Ukerewe tunakupenda tunakuhitaji na niwapongeze tena kwa ujasiri wenu kuja kututembela na kuona changamoto tulizonazo. Mtusaidie sana Visiwa vyetu vya Ukerewe ili waweza kufikia maendeleo tunayoyatarajia nishati ya umeme ni jambo muhimu sana, tusaidie sana, zaidi ya yote kwenye eneo la kisiwa cha Ukara kama nilivyoshauri, tafadhali kaa na wataalamu wako, wekeni *sub - marine cable* pale, muweze kuunganisha Kisiwa cha Ukara na Gridi ya Taifa. Vile Visiwa vingine vidogo ambavyo vina changamoto, changamoto zake mnazifahamu, tafuteni ufumbuzi wa haraka ili wananchi wetu waweze kwenda na kasi ya maendeleo na hasa kwa tija na kasi anayoionesha Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi, Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Kishoa atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu ajiandae.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba nitumie nafasi hii kukutakia kila kheri kwenye uchaguzi wa nafasi ya Urais Bunge la Dunia, wengine wanakusikia lakini sisi tumekuona na tunajua utendaji wako na *competence* yako kwenye nafasi hii ya Uspika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa namna ambavyo wameendelea kufanya kazi kwa umahiri mkubwa, lakini pia Viongozi mbalimbali wa Taasisi za Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita zaidi kwenye eneo moja na kutokana na umuhimu wake ndiyo maana nahitaji muda wa kutosha sana kuchangia eneo hili. Nitajikita zaidi kwenye eneo *due diligence* (Uchunguzi wa Kina).

Mheshimiwa Spika, tunajua ya kwamba hili ni eneo muhimu sana pale inapokuja wakati anatafutwa Mzabuni au Mkandarasi wa kutekeleza miradi ya maendeleo. Kuna Mwandishi mmoja wa vitabu anaitwa George Richard aliwahi kusema *"No man can find out the truth of something without doing investigation"* akimaanisha ya kwamba hakuna mtu yeyote anayeweza kugundua ukweli bila kufanya uchunguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunajua madhara ya kutofanya *due diligence* ya uhakika kwenye sekta au wakati unahitaji mkandarasi wa kutekeleza miradi ya Serikali. Moja ya madhara makubwa ni lazima utapa mkandarasi wa mchango kwa maana ya kwamba utapata Mkandarasi ambaye hana sifa, lakini cha pili endapo utafanya *due diligence* ambayo haina umahiri, utapata changamoto ya ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na la tatu hata kama miradi hiyo itatekelezeka basi itatekelezeka chini ya kiwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua *worldwide* yapo maeneo ambayo ni *key areas* kwa ajili ya kufanya *investigation* kwenye kuchagua Mkandarasi. Kwanza kabisa, huwezi kumchagua Mkandarasi au mzabuni bila kufanya *financial due diligence*. Nikisema *financial due diligence* nina maana kwamba unakagua *financial muscles,* misuli ya kifedha ya kampuni. Utaangalia masuala ya *cash flow,* utaangalia masuala ya *tax record,* utaangalia masuala ya *historical financial statements* za kampuni. Pia ni lazima utaangalia masuala ya *legal and regulatory compliances,* lazima ujithibitishie kwamba kampuni hiyo imekidhi matakwa ya kisheria. Utaangalia masuala ya leseni, utaangalia masuala ya vibali kama vimethibitishwa ili usije ukachukua kampuni ambayo iko kinyume na utaratibu na lazima pia uangalie masuala ya *legal disputes,* kama kampuni hiyo imeshapata pingamizi maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima uangalie masuala ya *operational due diligence,* ujithibitishie uwezo wa kampuni wa kutekeleza miradi. Utaangalia masuala ya *technology* lakini pia utaangalia masuala ya *products* zinazotakana na kampuni hizo na mambo mengine mengi sababu ya muda siwezi kusema yote, lakini kuna masuala ya *risk assessment* lazima wafanye, lazima ufanye *due diligence* kwenye *management profile,* lazima uangalie timu ya kwenye kampuni wale wahusika wa *management team* kama una *profile* nzuri unaweza ukachukua kampuni kumbe ni wala rushwa watupu, kwa hiyo lazima ujiridhishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, ni bahati nzuri sana nimeshiriki ziara zote za Kamati hii. Umetutuma tukaenda kukagua miradi ya Serikali, mambo ambayo tumeyakuta kule mengine yanatia kichefuchefu kwelikweli ni lazima tuseme. Tumekwenda Korogwe tukakagua miradi ya *REA*. Miradi ya *REA* kuna changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tumefika Korogwe tumekutana na Mkandarasi anaitwa Tontan, Mkandarasi huyu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amemkabidhi bilioni 3.9 kama malipo ya awali kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Vijiji vya *REA* vijiji 54, kwenye Wilaya ya Korogwe lakini Mkandarasi huyu tulipombana

akathibitisha mbele ya Kamati ya kwamba fedha zile amezipiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amethibitisha mwenyewe kwamba fedha zile ambazo amepewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bilioni 3.9 kwamba amezila kinyume na utaratibu. Tukauliza kuhusiana na masharti ya kimkataba, tulichoona mpaka leo ninavyozungumza hapa yule Mkandarasi hajachukuliwa hatua yoyote baada ya ubadhirifu mkubwa alioufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi Tarehe 14 Februari, mwaka huu Mkandarasi huyo huyo aliyefanya ubadhirifu mwaka jana, ndiyo huyo huyo kapewa tena *tender* kwenye gridi imara mwaka huu. Wote humu ndani tumekuwa tukizungumza kwamba Mama yetu anazunguka usiku na mchana kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Ni wajibu wetu kama Serikali na kama Bunge kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatumika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie wananchi wa Korogwe popote walipo kwamba Rais wao alitenga shilingi bilioni 3.9 kwa ajili ya watu hao kupelekewa umeme, kwenye vijiji vyao 54 lakini wameponzwa na Mkandarasi asiyekuwa na maadili, wameponzwa na baadhi ya watendaji kwenye Wizara ikiwepo watendaji wa *REA* kutopeleka fedha hizo mahali panapohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeisikiliza vizuri sana hotuba ya Kamati imeeleza vizuri suala hili na imeomba kwamba hatua kali zichukuliwe kwa kampuni hii na wahusika wote. Mambo haya yameendelea siyo tu Korogwe peke yake. Tumeona hata maeneo mengine kuna mradi wa *Kinyerezi One extension* wa *megawatt* 185. Alikuwepo Mkandarasi wa kwanza ambaye Serikali ikatenga fedha dola milioni 133, kati ya dola milioni 188 akatangazwa kufilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najiuliza hichi ni kitu gani? Tunakwenda wapi? Hii *due diligence* inafanyika kwa kiwango gani? Kama tuna kitengo ambacho kinaweza kuwapa nafasi wakandarasi

kutekeleza miradi halafu wakawa wanatabia ya kutangaza kufilisika, halafu wakawa wana tabia ya kutafuna fedha za wananchi wa Tanzania hatuwezi kukubaliana na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninao ushauri, kwanza ushauri wangu wa kwanza ninaliomba Bunge lako Tukufu ikikupendeza iiunde Tume ambayo itakwenda kukagua vitengo vyote vinavyo- *deal* na *due diligence* kwenye Taasisi ya Wizara ya Nishati. Yaani kwa maana ya kwamba *due diligence* na wenyewe ifanyiwe *due diligence*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninaomba baada ya kubainika taarifa ya kutoka kwenye ukaguzi huo iletwe Bungeni na Bunge liweze kuchukua hatua, wale wote wanaohusika kwenye masuala ya *ten percent* wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ningependa kuomba sana. Mheshimiwa Waziri pelekeni hawa watu wapate taaluma, vitengo hivi wapate taaluma. Wahusika waendelezwe. Ipo mifano mingi duniani ambayo imepitia changamoto kama hizi, ambapo Wakandarasi wakipewa *tender* wanatangaza kufilisika. Maeneo mengi Wakandarasi wanafuja fedha ya Serikali, kuna maeneo mengi ya kujifunza.

Mheshimiwa Spika, maeneo machache ambayo nimeweza kuyaangalia na ninaweza nika-*share* hapa Bungeni, kuna mradi wa *Solyndra Project* huko California, wali-*face the same coincidence* kama ya kwetu, nendeni kajifunzeni kule. Kuna Bwawa la Bakun ni *project* iko kule Malyasia wali-*face* changamoto kama ya kwetu, nendeni mkajifunze kule. Kuna Bujagali *Project* iko Uganda hapo, nendeni mkajifunze kule, kuna Fukushima *Power Plant* Japan wali-*face* masuala tunayoya-*face* sisi Wakandarasi kutangaza kufilisika, Wakandarasi kutafuna fedha za Serikali, nendeni mkajifunze kule walichukua hatua gani, mkiwa hamna ninazo hapa naweza nikawapatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hivi, tusiwe na haraka sana ya kuona matokeo ya mambo makubwa na wakati tuna mengine ya kawaida ambayo bado hatujayakamilisha.

Nimesikiliza taarifa nzuri sana ya Mheshimiwa Waziri lengo lake ni zuri sana, lakini napenda nishauri kwamba kama kuna vijiji 12,000 ambavyo bado havijapatiwa umeme, hakuna sababu ya kwenda kukimbilia vitongoji 36,000 kuvipatia umeme kabla ya kukamilisha vijiji hivi 12,000. Tuende tumalize hatua ya kwanza ya vijiji vyote, vikamilishiwe umeme, tuende hatua ya vitongoji. Lengo ni kuona kwamba watu wote kwa wakati sahihi wanapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond tutamalizia na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kipekee kabisa namshukuru Mungu kwa siku hii njema ambayo tunaizungumzia kwa maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya *TWPG* naomba nikupongeze sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuridhia wewe kugombea Urais wa *IPU*. Watu wakisikia wanadhani ni jambo dogo, huu ni Urais wa Mabunge yaliyopo Duniani. Dunia ina Mabara Saba, ina nchi 195, ina Mabunge 190 lakini ina *chambers* 268. Leo hii anasimama Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Tulia Ackson kwenda kugombea. Jambo hili ni la Kitaifa, jambo hili ni letu wanawake tunakuwekea dua na ninawaomba Tanzania nzima tukushike mkono kwa dua, kwa hali na mali. Baraka hizo pokea unakwenda kupita. Baada ya maneno hayo, ukituona tunatembea unadhani tuko kawaida, Hapana, tuko na wewe tumekubeba kwenye mioyo yetu tunakuombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba niunge mkono sana hii Wizara ya Nishati, hotuba aliyoisoma Waziri wetu January Makamba asubuhi ya leo, tumekuelewa. Tumekuelewa Mheshimiwa January tunakuombea upitishiwe hizo hela ulizoomba asubuhi hii ambazo ni shilingi trilioni tatu na ushee na nitashangaa sana nikiona mtu anaziletea kutokuelewa sijui

kamata mishahara ya Waziri, mimi sielewi hiyo mambo inataka nini kutupotezea muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme nina raha kwa ajili ya jambo lake Waziri alilosema katika mambo aliyoyapa kipaumbele lile la tisa, kuendelea kutekeleza mikakati ya programu mbalimbali za kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia *(clean cooking)* nchini na uanzishwaji wa vituo vidogodogo vya mafuta vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnamo Tarehe Mosi mwezi Novemba, uliniruhusu nikaenda Dar es Salaam, Mheshimiwa Rais akazindua jambo hili la nishati safi na salama ambalo linakwenda sambamba na lengo la Saba la *Millennium* ambalo ni *Clean and Affordable Energy*. Sasa tumeshakamata ile *affordable energy* na ametuhakikishia Waziri kwamba sasa tunakwenda kupika bila kulia machozi, tunakwenda kupika bila kunuka moshi, tunakwenda kupika kwa haraka na wepesi, tunakwenda kuwahisha watoto shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo tu, nikiwa mdogo nikiwa darasa la nne nilikuwa nasoma shule ya kijijini, nikaambiwa nikapike chai ya Mwalimu. Jambo hilo lilinifanya wazazi wangu wanihamishe shule ile nikapelekwa kusoma Kifungilo kwa sababu haikuonekana ni vema mwanafunzi kwenda, yaani wao hawakuona sawa nikaokote kuni na kuwapikia walimu. Leo hii inakuja *clean energy* ambayo sasa walimu wote wanaenda kupika chai kwa gesi. Nitangulize kumuomba Mheshimiwa Waziri naomba hayo majiko 200,000 uzipatie shule za *primary* wale watoto wetu waache kwenda kuokota kuni za kuwapikia walimu chai, waache kwenda kuwapikia walimu chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo gumu sana, mwnafunzi badala ya kusoma anaenda kupika chai, haiwezekani siyo miaka hii, tena lakini sambamba na hilo umetueleza kwenye hotuba yako kwamba, tutakuja tuchague. Mimi naomba nitamke hapa hapa naomba uzipelekee zile taasisi za *mission* kwa ma-*sister* wale, wakiwemo ma-*sister* wa Huruma uwatengenezee ile miundombinu waletewe gesi waweze kupikia. Wao haya majiko madogo hayatawatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kumuomba mdau mmoja, mdau huyo ni wa *Oryx, Benoit.* Endapo utazungumza na hao wadau wako wengine waende huko kwenye hizo taasisi kubwa kubwa wakatengeneze hiyo miundombinu. *Benoit* wa *Oryx* alikubali na mimi hapa niseme wazi unao wengi. Siwafahamu wote kwa sababu mimi situmii gesi nyingine zaidi ya *Oryx*. Kwa hiyo, naomba waungane wakatengenezee Magereza yetu, wakatengenezee shule za sekondari, wakatengenezee huko *mission* na kwingine kote sekondari ili sasa tuachane na kukata miti na kwenda kukoka moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaona kwamba wanaoteseka zaidi kwa kutumia hiyo nishati inayokatazwa sasa ya kuni ni wanawake. Hakuna jambo ambalo unaweza kulifanya bila kupika, hakuna anayekula chakula kibichi zaidi ya matunda labda hata matunda lazima yaive. Leo Mheshimiwa January Makamba ametuambia tunakwenda kuachana na hilo jambo ifikapo mwaka 2030. Kwa nini nisiseme kwamba leo ninasherehekea? *(Makofi)* Mheshimiwa Spika, ninaomba pia sambamba na elimu hiyo ya kutumia, kwa hii nishati ambayo tuliyonayo sasa kama huu umeme pia wanafunzi na hata sisi wengine tujifunze kutumia nishati hii kwa uangalifu. Ukitoka zima taa ili na mwingine afaidi, lakini siyo hilo tu, ukitoka zima *AC,* ukitoka tunza hata ile *socket.* Kwa kutumia nishati hii vibaya unakuta *lift* zinawakatikia watu, umeme umekatika, tunaishia kuilaumu *TANESCO.* Siamini kama kila umeme ukikatika ni *TANESCO.* Hili jambo nalikataa hata watumiaji sisi pia tunachangia. Tunachangia kwa sababu tunaacha vyombo vyetu hovyo vya moto, moto unawaka tunaanza kuita zima moto kumbe na sisi pia hatukufanya majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ninachokuomba Mheshimiwa Waziri na timu yako bila kuwataja kwa sababu hii *salutation* ilikuwa na *protocol* ndefu sana na mimi naunga mkono, kwa kuunga mkono ile hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Kitandula. Yale yote yaliyosemwa Wabunge wote tunakubaliana nayo na tunasema yaende hivyo hivyo lakini niseme neno moja tu kuhusu hii *bulk procurement* (hii kununua mafuta kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona kama inaenda kupata shida kwa sababu tumemsikia Mheshimiwa ambaye pia ni mmojawapo mwenye kufanya biashara hizo wanapata shida kwa kutokupata hela za kulipia sasa mzigo uliokwisha fika. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nilikuwa nakuomba tu hili jambo ulifanyie kama dharura, wapate hiyo hela ili lisije tena likatuingiza kwenye matata, amesema yeye aliye-*site* pia amesema Mwenyekiti wa Kamati. Ninaomba tu kwamba hili jambo lifanyiwe dharura ili wiki mbili zijazo tusije tukapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kusema hapa kwamba vyote tumeoneshwa kwenye maonyesho ni kweli lakini kuna Kamati ambazo hatujafika maana yake wanakwambia *seeing is believing*. Tumeoneshwa kama runinga, zile Kamati ambazo hazijafika kwenda kuona Bwawa la Mwalimu Nyerere, bwawa ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya kwa nguvu sana na umetuhakikishia linaenda kufunguliwa karibuni, basi ikikupendeza utoe ruhusa tukaende kuliona na sisi tuweze kuelezea kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye randama tumeona kwamba kuna maeneo ambayo hayataweza kufikiwa ni kwa sababu ya ukomo wa bajeti, lakini kama hapo kadri tunavyoelekea ikipatikana bajeti nyingine kidogo, tunaomba hii Wizara iongezewe kwa sababu hata pamoja na kuwa na simu zetu hizi, bila kuwa na umeme wa kuchaji simu huwezi kuitumia. Ukiwa na gari bila kuwa na mafuta ya kuendeshea gari huwezi kulitumia. Chochote kile kinahitaji hii sekta na ndiyo maana inaitwa sekta mtambuka, iweze kutumia nishati ili kutufikisha huko tunakotaka kufika. Kwa hiyo, ni sekta ambayo ni nzito sana lakini nishukuru Mungu Wizara hii imepatiwa kijana ambaye ni mchacharikaji. Wahenga walisema mzigo mzito mpe Mnyamwezi lakini nasikia yeye siyo Mnyamwezi lakini basi kama hiyo ndiyo lugha, basi pokea Unyamwezi wa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo mengi lakini kutokana na muda niseme kwamba narudia kuunga mkono hoja, niwapongeze sana wale aliewaona wabobezi wa kwenye siasa na pia wa huku ndani, tumemuona Profesa Mwandosya, tumemuona

Mheshimiwa Janeth Mbene, tumemuona Balozi Mathias Chikawe na Mheshimiwa Abuu Bin Juma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, niungane na Wabunge wenzangu kukushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri katika Bunge letu hili, pia nichukue nafasi hii kwa dhati ya moyo wangu kabisa kusema Taifa hili lina historia kubwa.

Mheshimiwa Spika, nchi hii imetoka mbali sana kwa ambao tunasoma historia tunajua Taifa hili limetoka wapi katika zana zote za maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. *Transformation* katika Taifa letu ni kubwa sana. Ninaomba niseme maneno yafuatayo na hili ninaomba niseme kwa dhati ya moyo wangu.

Mheshimiwa Spika, kuendesha na kuongoza Serikali ni jambo ambalo kwanza wanaoaminiwa huwa ni watu wachache sana lakini pia kuendesha na kuongoza Serikali ni jambo ambalo linaweza kuwa *captured* na kumudiwa na watu walio makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita nilikuwa nafuatilia mienendo ya siasa katika Taifa hasa katika mikutano ya hadhara. Nimesikia baadhi ya vyama vya siasa nje wakimkejeli Rais wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan na wamemkejeli katika maeneo wakisema kwamba Rais ameweka mabango mengi hata ndoto za kufikisha umeme kila kijiji hizi ni historia hakuna kitu kitakachowezekana.

Mheshimiwa Spika, naomba nikupe rekodi mimi kwenye Jimbo langu mimi Serikali ya Awamu ya Sita kwenye mambo ya umeme wametufanyia ndani ya miezi mitatu iliyopita. Ndani ya miezi mitatu iliyopita, Jimbo la Singida Magharibi na nina uhakika mifano hii iliyofanyika Singida Magharibi imefanyika nchi nzima. Hivyo nataka tutoe watu waelewe, Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyoko madarakani chini ya Rais Samia Suluhu Hassan siyo Serikali ya porojo, siyo Serikali ya maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wetu akiwemo Kaka yangu January pamoja na Naibu wako, *trust* mliyopewa na Rais nataka nikuambie January mchana kweupe Bungeni hapa leo, kazi hii wewe na Wizara yako mnaifanya kwa uadilifu na uaminifu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya miezi mitatu, Jimbo la Singida Magharibi ndani ya miezi mitatu nimewashiwa umeme Kijiji cha Germany, Igombwe, Chungu, Irisya, Munyu, Mwasutianga, Kintandaa, Maswea, Kipunda, Mtunduru, Mpugizi, Mpetu, Kinyampembee na Mhintiri, nimewashiwa umeme ndani ya miezi mitatu iliyopita. Hapa ninapozungumza, ninakwenda kuwashiwa umeme mwezi huu Vijiji vya Igilansoni, Msosa, Minyughe, Misake, Makilawa, Mteva, Mtavira, Mayaa, Mlandala, Kaugeri, Mduguyu, Uyumbu, Makyungu, Mgungira mpaka wamefika mpakani mwa Tabora kilometa 225 kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Nani kama Mama Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamani tunapozungumza utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ndiyo maana nataka niseme watu wasije wakatuona sisi Wabunge tunakuja hapa, Wabunge wa kusifia. Sisi ni Wabunge wasomi. Hiki Chama chetu ambacho kiko madarakani humu ndani kimeleta *cream* ya Wabunge wenye akili kichwani. Hapa siyo watu wa kuja kupigapiga makofi. Mkiona tunapiga makofi mjue yale tuliyoiagiza Serikali kwenye Ilani yetu ya chama yanafanyika kwa uzalendo na uaminifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nataka niseme kwa kazi inayofanyika wale wanaomkejeli Mama Samia nataka nikuhakikishie kwa sababu nimeona yamefanyika kwenye Jimbo langu, Rais Samia anakwenda kuandika rekodi ambayo mtangulizi wake Hayati Magufuli aliianzisha na Mama anakwenda kumaliza kazi, vijiji vyote vinakwenda kuwaka umeme. Nataka niwaombe Wabunge wote tuendelee kumuunga mkono January na Mama Samia na Wizara hii tuendelee kuwashika mkono, kazi wanayoifanya ni kubwa. Sisi kwenye Ilani tuliwatuma mtuwashie umeme, umeme unawaka unataka nisikusifie? Umeme unawaka tusiseme? Tutasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule wanakopita watu wa CHADEMA wanapiga *propaganda* kwamba Rais anaweka mabango, nataka nikwambie ukiona mtu anapiga kelele jua umembana vizuri, Mama amewashika kwelikweli kupitia Wizara yako January.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nataka nimpongeze sana Mama Samia na kwa kweli haya mambo tunayafanya kwa sababu hata tusiposema Mungu atatushangaa. Mradi huu unazungumzwa wa *LNG* toka *discovery* imefanyika mwaka 2012, tumejaribu mazungumzo 2016, 2017 kwenye kitalu Namba Moja, Mbili na Nne mazungumzo yakakwama. Tukafufua mazungumzo miaka ya 2017, 2019 mazungumzo yakakwama, kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa January Kaka yangu, kama kuna vitu ambavyo Taifa hili litakukumbuka ni kuyafufua mazungumzo ya mradi wa *LNG* na kuyafanikisha kwa kiwango kikubwa. Leo tunapozungumza hapa, tunapozungumza mradi ambao unakwenda kufanya *generation* ya fedha zaidi ya trilioni 80 huu ni uchumi mkubwa kwa Taifa, hakuna Mbunge ambaye ana akili ataacha kuunga mkono Serikali kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kukuamini, umekwenda kuyafufua mazungumzo haya na tunaona mafanikio yake. Ninataka nikuambie na wewe sasa kwa kazi uliyoifanya nzuri ya heshima, tunataka tuone matokeo mzee, *transition* ya dunia sasa hivi inakwenda kasi. *Transition* ya gesi sasa hivi dunia inakwenda kwenye umeme wa upepo, umeme wa jua na joto ardhi, mkichelewa kutekeleza mradi huu Mheshimiwa January mimi nakuambia hii gesi itabaki kuwa laana kwa Taifa. Harakisha haraka utekelezaji wa mradi huu, uweze kufanyika, Taifa liweze kupata *revenue* tuendelee kuwajengea watoto wetu mashule, tuendelee kuwekeza, tuendelee kutatua tatizo la ajira kwa Taifa, nchi yetu iweze kupiga hatua kwa maslahi ya watu wake, hongera sana Kaka yangu Mheshimiwa January. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumza, nikuombe Mheshimiwa January pamekuwa na maneno huko mtaani, watu wa *SONGAS* wanapiga kelele kuna uwezokano mkubwa *SONGAS* wanahisi kwamba Serikali haina mpango wa ku – *renew* mkataba. Wafanya kazi kule wana – *tension* kubwa

January, kama January umeweza kufufua mazungumzo ya *LNG* yaliyokuwa yamekwama toka 2016, ukaleta matumaini kwa nchi, ukaleta matumaini kwa *investor*. January kakipengele cha *SONGAS* katakushinda kufanya nao majadiliano Kaka yangu? Nenda kakae na watu wa *SONGAS* fanyeni nao majadiliano kama kuna vitu mnaviona kwenye mkataba wa kwanza vilikuwa havina maslahi ya Taifa piga chini tutakuunga mkono. Wakikubaliana na masharti ya Serikali na ile ndiyo *PPP* ya kwanza January ambayo imeleta mafanikio kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza *PPP best* ambazo zimeleta mafanikio ni pamoja na watu wa *SONGAS,* wanatuuzia umeme kwa *only* senti sita na ninasikia wako tayari kushuka zaidi. January fanya nao mazungumzo tuweke *tension* hii tuiondoe, kazi mnayoifanya mimi nilikuja Ikulu niliona *projection* mlizokuwa nazo za kuwekeza umeme mpaka tuuze umeme nje ya nchi. Niliona mipango ya kaka yangu Ndugu Maharage wa *TANESCO* na ninasema kabisa kwa dhati, Maharage asivunjwe moyo, kijana huyu ana – *vision* kubwa sana, maana tumekuwa kwenye Taifa letu tunapo – *hire brain* zenye uwezo wa kuleta mabadiliko tunaanza kuwapiga vita mara huyu anafanya hivi, Maharage Chande ni moja ya vijana wazalendo wa Taifa hili, aungwe mkono ni kijana mwenye *vision* kubwa ameonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikwenda Ikulu nikaona *projection* za namna nchi inataka kutengeneza umeme na kuuza nje ya nchi, nikaona *plan* zake ninawaomba Wabunge wenzangu tuwe wazalendo wa kuwaunga mkono vijana wote ambao ni zao la Taifa hili, ambao wanaweza wakalisaidia Taifa hili kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sika, jambo la mwisho naomba nimuombe Mheshimiwa January. Kwenye Jimbo langu la Singida Magharibi kuna vijiji vinne mliviruka, mliruka Kijiji cha Nkhoire Kata ya Isseke. Ninarudia Nkhoire ya Isseke January ninakuomba uikumbuke. Kijiji cha Mwaru ambayo ni Makao Makuu ya Kata mliiruka ninaomba muikumbuke, mimi kwa kazi hizi mlizozifanya 2025 niletee mtu yeyote mnayemtaka atapigwa saa mbili asubuhi, kwa kazi hizi za umeme. Ninachokuomba ni kwamba endeleeni kufanya kazi kwa uzalendo, Mungu awabariki sana, mnafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niseme nataka niwaambie Wabunge Spika huyu na mimi narudia, hata jana Spika wa Afrika Kusini na watu wao wamesema wao wanamu–*endorsed* huyu Brigedia Jenerali akagombee Bunge la Dunia. Sasa kama Mabunge makubwa yanamu – *endorsed*, Congo wako nae, Zambia wako nae, Botswana wako nae, Thailand wako nae, jamani ama namna gani? Tutashindwa jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kazi iendelee. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana leo. Ninayo mambo matatu kwa haraka, jambo la kwanza ni kuhusu mchango ambao ameutoa Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete kuhusu kugawa majiko.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu ya muda ule wa kuchangia huwa ni mfupi, mtu hawezi kuwa na nafasi ya kutoa ufafanuzi jambo alilolisema kwa ukamilifu. Ukurasa wa 89 wa kitabu cha hotuba ya Waziri wa Nishati inaongea kuhusu utekelezaji wa mikakati na mipango mbalimbali ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wakati akisema hotuba yake hapa, ameeleza mipango mbalimbali ya Serikali kuhakikisha tunatoka kwenye nishati chafu ya kupikia kwenda kwenye nishati safi. Sasa, Wabunge kama sehemu ya wananchi ambao wanaushawishi kwenye maeneo yao ya uwakilishi wanaweza kuwa ni watu wazuri ambao watapeleka ujumbe kwa wananchi kuhusu matumizi mazuri ya nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabungem kwa hiyo, isije ikaleta picha nyingine ni hoja hiyo katika kuhakikisha kama ambavyo Wabunge wameelekezwa namna ya kutumia hiyo nishati safi, pia wamehamasishwa kutumia nishati safi ndivyo na wananchi nao wanapaswa kuhamasishwa kutumia nishati safi. Ni dhahiri kwamba kwa sababu ni uhamasishaji hakuna Mbunge ana uwezo wa kwenda kugawa hayo majiko kwenye Jimbo lake lote,

lakini ili aweze kutoa ile elimu vizuri lazima awe na vile vifaa ili aweze kuelekeza namna ya kuweza kutumia hii nishati safi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo lazima iende kwa sura hiyo na wala Serikali inapofanya jambo hili haifanyi kwamba inao uwezo wa kuwagawia wananchi wote, lakini katika nia ya kuhamasisha ili mkakati huu ufanikiwe lazima uanzie mahali, ieleweke kabisa kwamba hiki kinachofanyika kipo kwenye bajeti na hata mwaka jana kilikuwepo. Kwa hiyo, huu ni utekelezaji wa bajeti hii inayoendelea na hata sasa huu ukarasa niliowasomea hapa Serikali imetenga nadhani imetajwa bilioni nne na kitu hapa.

Waheshimiwa Wabunge, ukurasa wa 89 naona kuna kiasi cha pesa kimetengwa hapo lakini nasikia mwingine anaeleza kwamba hapo kuna aina nyingine ya majiko, inaitwa majiko banifu nayo yametajwa hapo yametengewa kiasi cha fedha shilingi bilioni 4.7 naona hapo bilioni 4.5. Hivyo, Bunge hili lilipitisha jambo hilo siyo kwamba hayo majiko yametoka mahali halafu yakajikuta Hapana! Ni utaratibu tu wa kawaida na lazima ujumbe uende kwa sura hiyo. Wabunge kama ambavyo watu wengine wote ambao wanaushawishi kwa jamii Serikali inaweza kufanya hivyo ili kufikisha ujumbe kwa haraka zaidi kwa wananchi kwa namna inavyoeleweka.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la pili wale watakaochangia mchana. Tutakao anza nao tutakapokutana samahani alasiri ni Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo na wengine wataendelea kuitwa kadri muda unavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la tatu na la mwisho linahusu Mwongozo ambao uliombwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

Waheshimiwa Wabunge, katika Kikao cha 35 cha Mkutano wa 11 wa Bunge, Mkutanao wa Bajeti kilichofanyika tarehe 29 Mei, 2023, baada ya kipindi cha maswali na majibu alisimama

Mheshimiwa Mpina na kuomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 79 ya Kudumu za Bunge, Toleo la 2023. Mheshimiwa Mpina aliomba mjadala uliokuwa ukiendelea uahirishwe ili kujadili jambo ambalo alisema ni kubwa na la dharula.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mpina, alieleza kuwa jambo hilo linahusu Serikali kutowasilisha majibu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008. Alieleza kama ifuatavyo, nanukuu:

"Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 38(2)(b)(i) na kifungu cha 38 kifungu kidogo cha Tatu cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008 na Marekebisho yake ya 2020, kinaitaka Serikali wakati Taarifa ya *CAG* inawekwa mezani ije sambamba na majibu ya Serikali kuhusu Taarifa ya *CAG* inayowasilishwa Bungeni kwa Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Mwenyekiti lakini leo imezidi miezi miwili Serikali haijaweka mezani majibu ya hoja za mkaguzi. Haijaweka mezani taarifa ya mpango kazi ya shughuli za kujibu hoja za Mkaguzi na hivyo kulifanya Bunge lako kupata wakati mgumu sana katika kuisimamia Serikali" mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maombi hayo Kiti (Mheshimiwa Mwenyekiti) kilitoa maelezo ya awali kwa kufafanua kuwa Mheshimiwa Mpina alitumia Kanuni ambayo siyo sahihi wakati akiomba Mwongozo wa Spika. Kiti kilieleza kuwa Mheshimiwa Mpina alitumia Kanuni ya 79 wakati Kanuni sahihi ya kuomba Mwongozo wa Spika ni Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, ilifafanuliwa kuwa Mheshimiwa Mpina alileta Hoja ya kuairisha Shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharula. Kanuni mahususi kuhusu jambo hilo ni Kanuni ya 54 pamoja na maelezo hayo Kiti kilielekeza kuwa Mwongozo kuhusu jambo hilo utatolewa baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mpina aliomba Mwongozo wa Spika kwa Kanuni ya 79 badala ya Kanuni ya 76. Aidha, alitaka kutumia Kanuni hiyo kutoa hoja ili Shughuli za Bunge ziahirishwe ili kujadili jambo la dharula kwa jambo ambalo

halikuwa la dharula. Vilevile Mheshimiwa Mpina hakutumia Kanuni sahihi inayosimamia masuala ya dharula ambayo ni Kanuni ya 54.

Hata hivyo, napenda kutoa Mwongozo wangu ili kusisitiza Miongozo niliyowahi kutoa siku zilizopita katika Mkutano huu wa Bunge kuhusu Mjadala wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* nafanya hivyo, kwa sababu Mheshimiwa Mpina alipo omba Mwongozo alielezea utaratibu upo kwamba utaratibu huo uko nje ya kisheria, nje ya matakwa ya kisheria.

Waheshimiwa Wabunge, katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano huu kilichofanyika Tarehe 04 Aprili, 2023 nilitoa ufafanuzi mrefu kuhusu jambo hili. Sehemu ya maelezo yangu yalikuwa kama ifuatavyo: nanukuu "Kuna mambo mawili madogo ambayo la kwanza ni hii Taarifa ya CAG ambayo imepokelewa mwezi uliyopita na Mheshimiwa Rais, ambapo kwa utaratibu wa Sheria zetu na Katiba yetu ile taarifa italetwa hapa Bungeni kwa sheria ile ambayo tumetunga sisi na kwa mujibu wa Katiba yetu, ile taarifa itakapoletwa hapa Bungeni ndiyo inakuwa wazi kwa umma. Kwa hiyo, ile taarifa haikuwazi kwa umma mpaka sasa".

Waheshimiwa Wabunge, siku hiyo niliendelea kueleza kama ifuatavyo:

Ikishafika hapa Bungeni ipelekwe kwenye Kamati zetu za usimamizi, ikishaenda kule wale wanapata nafasi ya kupitia zile taarifa kwa kirefu na kwa undani na kuwasilikiza wale ambao zile taarifa zinahusu maeneo yao. Wakishamaliza ile kazi, wanaleta hapa ndani, wakileta hapa ndani ndiyo mjadala unaanza rasmi wa Bunge kuijadili Taarifa ya CAG. Baada ya mjadala tunaazimia sasa kama Bunge tunaiambia Serikali nini? Kwa hiyo, huo ndiyo mchakato wa namna Ripoti ya CAG inavyofanyiwa kazi, haijalishi ni mambo mazito kiasi gani yaliyotajwa mle ndani lakini utaratibu tuliyojiwekea lazima ufuatwe. Kwanini ni lazima? kwa sababu CAG ni jicho la Bunge. Yeye CAG siyo Bunge hafanyi maamuzi kwa niaba ya Bunge, Bunge linafanya maamuzi lenyewe ili Bunge liweze kufanya maamuzi lenyewe lazima tufuate ule utaratibu wa Kamati kushughulikia kwanza na hayo mambo kutuletea hapa

ndani ndiyo tunafanya maamuzi. Nadhani nimeeleweka mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati natoa maelezo hayo Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali likuwa haijawasilishwa Bungeni. Taarifa hiyo iliwasilishwa mezani na Waziri wa Fedha na Mipango mnamo tarehe 06 Aprili, 2023. Baada ya Taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni katika Kikao cha Sita cha Mkutano huu kwa mara nyingine nilitoa ufafanuzi zaidi kuhusu Taarifa hiyo na kueleza kama ifuatavyo:- nanukuu

“Waheshimiwa Wabunge, baada ya hatua hiyo na kwa mujibu wa maelezo niliyoyatoa siku ya 04, Aprili, 2023 taarifa hizo sasa zipo mikononi mwa Bunge na pia mikononi mwa Kamati zile zinazohusu usimamizi wa Fedha za Umma, nazo zinajipanga kuanza kushughulikia Taarifa hizo kikamilifu na kupokea majibu ya Serikali kwa hoja zote, kuwaita wadau wote muhimu kuwahoji na hatimaye kuandaa taarifa yake itakayowasilishwa Bungeni mwezi Novemba, 2023. Pamoja na mambo mengine umuhimu wa mchakato huu unatokana na ukweli kwamba nchi yetu inafuata misingi ya utawala wa kisheria ambapo haki ya kusikilizwa ni moja na vipengele vyake muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea Taarifa ya Kamati pamoja na maoni na mapendekezo Bunge hili katika kuteleza jukumu la kuisimamia Serikali litajadili kwa kina na hatimaye kutoka na maazimio ya Bunge kuhusu hoja mbalimbali zilizowasilishwa na *CAG,* maazimio hayo yatawasilishwa Serikali kwa utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua Madhubuti za kisheria na kinidhamu kwa Taasisi na Maafisa wote watakaobainika kujihusisha na matumizi mabaya ya fedha za umma” mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, maelezo hayo kuhusu utaratibu huo wa kushughulikia Taarifa za *CAG,* unatokana na misingi ya kisheria tuliyoiweka. Utaratibu aliyouleza Mheshimiwa Mpina kwamba Serikali inatakiwa kuwasilisha Bungeni majibu ya hoja za *CAG,* sambamba na Taarifa ya *CAG* siyo sahihi. Kwa sababu, utaratibu huo tuliubadilisha mwaka 2021 kupitia Sheria ya Fedha *(The Finance Act No. 3 of 2021)* Sheria hiyo ilifanya marekebisho

ya Kifungu cha 28 (3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, *(The Public Audit Act, Cap. 419)*.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya marekebisho hayo utaratibu unaotumika kwa sasa, ambao ulianza kutumika kwa mara ya kwanza 2022 unamtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha Bungeni majibu kuhusu hoja za *CAG (Consolidated Reports of the Responses and Action plan of the report of CAG)* kwenye Mkutano wa Bunge unaofuata baada ya kuwa *CAG* amewasilisha taarifa yake.

Waheshimiwa Wabunge, mabadiliko hayo ya utaratibu wa Bunge kufanyia kazi taarifa za *CAG* ulifanyika baada ya Bunge kujiridhisha kwamba upo ugumu kwa Serikali kuandaa na kuwasilisha majibu ya hoja za *CAG* ndani ya muda mfupi taarifa za *CAG* zinapokuwa tayari. Hivyo, Bunge liliona kwamba ni vyema utaratibu huo ubadilishwe na kutunga sheria inayoipa Serikali muda zaidi wa kutekeleza jukumu la kuandaa majibu ya hoja za *CAG*.

Waheshimiwa Wabunge, muda uliyowekwa kisheria kwa majibu ya Serikali kuletwa Bungeni bado haujaisha na Kamati za Bunge bado zinaendelea na taratibu za kushughulikia taarifa hizo. Baada ya Kamati kukamilisha kazi yake, Taarifa za Kamati zitawasilishwa Bungeni mnamo mwezi Novemba, 2023 ili zipate kujadiliwa kwa kina na Bunge na mwishowe Bunge litatoa maazimio kwa Serikali kwa utekelezaji.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kusisitiza kwa Mheshimiwa Mpina na Wabunge wengine pamoja na Watanzania wote kwa ujumla wawe na subira wakati mchakato wa kisheria wa kushughulikia taarifa za *CAG* na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali unaendelea kufanyika. Mchakato huo lazima uachwe ufanyike kwa kuzingatia misingi ya sheria zetu ili haki itendeke kwa pande zote zinazohusika katika jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo suala lilowasilishwa na Mheshimiwa Mpina haliwezi kupata nafasi ya kujadiliwa kama suala la dharura na vilevile lisingeweza kupata nafasi kwa njia ya Mwongozo wa Spika, kwa sababu limewasilishwa kinyume na

Kanuni zetu na Sheria yetu ambayo tumeitunga wenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wa Spika, kuhusu jambo hilo ni kwamba taarifa hii ambayo tunaisubiri kutoka upande wa Serikali kwa maana ya majibu, ni kwamba muda wake bado, wanapaswa kuwasilisha kwenye Bunge la mwezi wa Tisa. Kwa hivyo, bado wanao muda kwa mujibu wa sheria ambayo tumeitunga wenyewe, marekebisho yalifanyika 2021, 2022 yametumika na ndiyo yatakayotumika mwaka huu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa Kumi na Moja Kamili Jioni ya leo.

*(Saa 7.18 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel S. Baran) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mjadala uliopo mbele yetu wa bajeti ya Wizara yetu ya Nishati. Tutaanza na Mheshimiwa Costantine Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuitendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwa hiyo sifa zote ambazo Mheshimiwa Rais anapewa na Mheshimiwa Waziri anapewa, naweza kusema ninaziishi kwa sababu nipo kwenye Kamati hii. Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima wanazingatia vizuri ushauri wa Kamati na ushauri wa Wabunge. Kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa tu ni kwamba ninaipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ambayo inaendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika Nyerere *Hydro – Electric Power*, tumefika Chalinze tumeona kazi kubwa inayofanywa lakini tumepata taarifa ya kina kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa *TANESCO,* kuona namna ambavyo Tanzania ambayo inaandaliwa kuwa na umeme wa uhakika kazi ambavyo inafanyika. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa na timu nzuri. Jambo moja tu la msingi hapa Mheshimiwa Waziri tunacho chombo kwenye Wizara yako kiko *EWURA (Consumer, Consultative Council)* natamani sana ukiongezee nguvu.

Mheshimiwa Spika, kadri unavyoongeza kupanua huduma za umeme, matumizi ya gesi na kadhalika, wananchi wanahitaji chombo cha kuwatetea, wanahitaji chombo cha kutatua migogoro yao kabla haijawa mikubwa. Utakubaliana na mimi kwamba yamekuwepo malalamiko mengi ya utumiaji wa gesi, wengine mara gesi haitoshi, mara gesi iko hivi mara umeme uko hivi. Lazima chombo hiki kipewe nguvu, kipewe fedha kizunguke nchi nzima, kitoe elimu ili kuwafanya Watanzania wawe salama, naomba nikupongeze sana kwa juhudi kubwa ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo mawili mahsusi. Kwanza, Jimbo langu la Geita Mjini, limekuwa kwenye kuchelewa kupata umeme kwa takribani sasa tangu awamu ya kwanza ya *REA,* awamu ya pili sasa tunakwenda *lot* ya pili *phase three* kwa nini? Kwa sababu tuko Mjini tunayo ahadi ya *peri-urban*. Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwa juhudi kubwa ulizofanya, ulikuja Geita tukaenda Kata ya Burera ukazungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara wakakufurahia sana, ukawaahidi umeme utawaka itakapofika mwezi wa 12 mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sauti ya unyenyekevu nimefika kwenye banda pale nimeona mipango inaendelea, nimepata taarifa wameanza kuchimba nguzo lakini umeme haukuwaka Desemba. Mimi ni imani yangu kwamba baada ya bajeti hii kupita *speed* tuliyoiona kwenye mabanda yale itakwenda kufanya kazi yake wananchi wapate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza na wewe Mheshimiwa Waziri Jimbo la Geita Mjini mitaa 32 bado haijapata umeme na hiyo ndiyo iko kwenye *peri – urban,* vijiji 10 ambavyo kati ya 18, vinane vimepata umeme, kumi bado ndiyo kazi inayoendelea. Kuna maneno mengi kwamba bado Mkandarasi hajapitishiwa, sijui Mkandarsi bado kuna ushauriano, nikuombe Mheshimiwa Waziri kama tunaanza mchakato wa kupeleka umeme kwenye vitongoji, lakini tuna vijiji na tuna mitaa yenye tafsiri ya vijiji ambayo haijafikiwa na umeme tutakuwa tunawaacha watu wengine nyuma, tutakuwa na *double standard* kwenye nchi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba kwa kuwa hivi ni vijiji isipokuwa vile viko Geita Mjini, sijui Bukoba Mjini, huyo Mheshimiwa Naibu Waziri ana kesi kama ya kwangu. Ana vijiji na mitaa haijafikiwa umeme kwa sababu peri-*urban* haijaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri kama inawezekana tufike kwenye vijiji vyote na mitaa yote, halafu tuende kwenye vitongoji. Ni jambo jema Mheshimiwa Waziri umetushirikisha tutachagua vitongoji ambavyo vina uhitaji wa umeme na Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine la pili Mheshimiwa Waziri mimi ni Mjumbe kama nilivyosema wa Kamati ya Nishati na Madini. Tunakupongeza sana kwa kuchukua deni lililokuwa la *TPDF* na kuligeuza kuwa mtaji, jambo jema sana. Wanaomba hawa watu na siyo tu wanaomba, ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali inadaiwa fedha nyingi sana na fedha hizi ni Serikali yenyewe labda ufanye kama ulivyofanya kwenye deni lile Wizara, zile zikatwe juu kwa juu badala ya kuilipa *TANESCO*, ili *TANESCO* waweze kuwalipa *TPDF* kwa sababu visima ambavyo wanachukua vingine inavyoonekana vimeanza kupungua *capacity* na kwa nini? Ni kwa sababu pia hata uwezo wao wa ku

- *service* kwa muda, kwa sababu wanakuwa hawana *liquid* umekuwa mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kwamba *speed* yao ya kusambaza hata gesi ambayo ni *domestic* ni ndogo, kwa nini? Kwa sababu hawana pesa ya kutosha. Sasa kulichukua deni ni jambo moja kuwa na *cash* mkononi ya kuzunguka ni jambo jingine, Wizara yako iwasaidie kulipwa pesa hizo. Serikali iko humu, bilioni mia tatu na kitu kwa *TANESCO* ni pesa nyingi zingeweza kusaidia pia maeneo mengine tukapunguza madeni tukawahisha huduma kwa wananchi. Wananchi kwa kweli wanaipongeza Serikali kwa uwekezaji lakini wanasikitika wanapoona umeme upo unapita lakini *TANESCO* haina uwezo wa miezi miwili, mitatu kumuhudumia mlaji ambaye yuko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo umewekeza umeme una Megawati 1,800 unatumia 1,400 *plus,* una *surplus* ya 300 *though* haiko *very stable,* lakini una watu wanataka umeme wakupe pesa ili uweze kujiendesha halafu unachukua miezi minne, mitano haujawapelekea huduma, mimi nadhani hili jambo siyo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maoni tofauti kwa mfano, Mheshimiwa Waziri tunafahamu zamani vifaa vilikuwa vinanunuliwa madukani watu wanafungiwa umeme kwa bahati mbaya hapa katikati pakawa na vitu feki. Pengine mngelikuja na mkakati mwingine wa kuangalia mkawa na *quality assurance,* mkatafuta *vendors,* mkaondoa kabisa tatizo la mtu kusubiria mpaka vifaa viende. Unakuta kuna sehemu watu wamelipia umeme wanaanza kushindana na vishoka sasa kutoa rushwa ili waweze kupata huduma ya umeme. Mheshimiwa Waziri nadhani jambo hili siyo jambo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kule Geita kwangu kuna wachimbaji wa madini. Wachimbaji wa madini wanatumia gharama kubwa sana kusukuma mitambo na kutoa maji kwenye mashimo. Ikikupendeza ungemteua mtu aka-*deal* na hilo eneo tu, kwa sababu wapo watu kule Nyarugusu, kule Nyakabale, kule Ngusu wameomba umeme, wanataka umeme

kwa ajili ya kusukuma mitambo, wanachukua muda mrefu sana na gharama ya uendeshaji inakuwa kubwa, hawa ni watumiaji ambao Mheshimiwa Waziri watakuongezea kipato kikubwa sana hata kuliko watumiaji wa ndani wa umeme wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa sababu hili ni jambo la kiuchumi nakupongeza sana kwa ku-*diversify* pia uwekezaji wa umeme, leo tunapokwenda kuanzisha Bwawa la Umeme la Malagarasi tukawa na bwawa la umeme la Julius K. Nyerere, tunaifanya nchi iwe na mitandao ya umeme iliyogawanyika ambayo ni vizuri kuisalama. Wenzetu waliliona hao wa Ukraine kama wangelikuwa wana chanzo kimoja cha umeme na yule jamaa anayewapiga leo wangelikuwa giza, lakini ukipiga mtambo mmoja unawaka wa kaskazini, unawaka wa kusini, unawaka wa magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri kuwa na *sources* nyingi za vyanzo vya umeme, uwekezaji mwingi ili kusudi siku moja nchi isije ikaingia gizani kwa sababu tu Mwalimu Nyerere *Hydroelectric Power* imeshindwa kufanya kazi au gesi imeshindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi pia nichangie kwenye hotuba ya Wizara ya Nishati.

Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kama watangulizi wangu waliopita Wabunge wengine waliochangia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa ambayo inafanyika katika Wizara hii ya Nishati, hususani kwa niaba ya watu wa Biharamulo uzinduzi wa *substation* ya Nyakanazi ambayo sasa inatuondoa katika shida ya umeme tuliyokuwa tumeipata ya ku - *run* katika *low voltage*, licha ya hiyo inaingiza Mkoa wa Kagera kwenye gridi

bada ya kuunganisha na Rusumo nadhani hata ndugu zangu na majirani zangu wa Kigoma, wote ni mashahidi sasa hivi wananufaika kutokea Biharamulo, kwa hiyo nishukuru sana kwa ajili ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Msaidizi wake na Watendaji wote katika Wizara hii, kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya, ninazidi kuwashukuru tayari mgodi wetu wa Biharamulo *STAMIGOLD* tumepokea umeme. Hasara ile ya mafuta zaidi ya bilioni 1.2 yaliyokuwa yanatumika pale mgodini tuna umeme tayari, kwa hiyo ni hatua kubwa na mapinduzi katika Wilaya yetu ya Biharamulo, nina hakika mgodi ule kwa sababu ulikuwa unajiendesha kwa hasara sasa wataanza kufanya kazi kwa faida na hatimae hata *CSR* ambayo tumekuwa tunapambana nayo pale tunaweza kuipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pamoja na kubanana huko wamenisaidia juzi kwenye ujenzi wa shule ya sekondari ya Mavota, wamejenga vyumba viwili vya madarsa, ofisi, vyoo. Kwa hiyo, nina uhakika baada ya kuanza kupata umeme watafanya vingine vikubwa zaidi ili Biharamulo iweze kusonga mbele kwa kasi sawa na maeneo mengine yanayoendelea kukimbizwa chini ya utendaji wa Mheshimiwa wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu nilitaka kuongelea miradi ya *REA* kidogo, kabla ya kwenda kwenye mambo mengine ya Kitaifa. Ninayo ripoti hapa mimi kwangu nilikuwa na vijiji 25 *so far* ni vijiji Saba tu ambavyo vimeunganishwa na umeme. Sasa ukijaribu kuangalia kasi ya uunganishaji ni ndogo sana na sisi tunapokuwa tunazunguka kwenye ziara ukishawaambia wananchi Mkandarasi amepita hapa, wao hawajui kaunganisha kijiji gani? Kila mwananchi anataka apate umeme kwenye Kijiji chake, huwezi kwenda kwenye Kijiji ‘A’ ukamwambia Mkandarasi ameshaunganisha ‘B’ yeye akendelea kusubiria, kwa sababu umeme ni *demand* ya kila mwananchi hasa kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nina ushauri kama inawezekana *as long as* Mheshimiwa Waziri amekiri

mwenyewe kwamba wanatafuta mbinu mbadala ya kutafuta Wakandarasi wa *REA,* hebu liangalieni hili kumpa mkandarasi mmoja Mkoa mzima *it was a very big mistake,* ni mzigo mzito mno, ninapopiga mimi wa Biharamulo anaondoa timu anapeleka Ngara, akipiga wa Ngara anaondoa timu anapeleka Kyerwa ndivyo hivyo inavyofanyika, kwa hiyo tulikuwa tunaomba kama inawezekana tafuteni Mkandarasi kwa kila Wilaya, bora wakimaliza wataenda hivyo hivyo, hata kama wana miradi miwili, lakini wakimbize haraka hii kazi umalizike maana wananchi wamechoka kusubiri wanataka waone umeme sawa na kule walikowasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye miradi hii kumekuwa na maelekezo yale ya taasisi zipate umeme kwanza, sasa unakuta taasisi wanataka umeme na wananchi wanataka umeme. Sisi sote ni mashahidi, ujenzi wa Taasisi za Umma una vigezo vyake. Kigezo cha kwanza ni pamoja na taasisi kuwa na eneo kubwa ambalo wanaweza wakafanya miradi mingi, sasa unapoongelea ekari 20 za kujenga kituo cha afya, ukiongelea ekari 20 za kujenga shule *automatically* haziwezi kuwa kwenye *center* ya kile Kijiji. Kwa hiyo wengi wamejenga shule pembeni, kwa hiyo tunachoomba sasa, nilikuwa naomba nikuombe Mheshimiwa Waziri ulione hili pia andaa programu maalumu ya kupeleka umeme kwenye taasisi, achana na mambo yaani *REA* peleka umeme kwenye vijiji, lakini taasisi ambazo ziko pembeni pia utusaidie pia umeme ufike tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu nina shule ya sekondari kwa mfano shule ya sekondari Ruziba, shule ya sekondari Lusahunga, shule ya sekondari Nyakanazi ni shule kubwa lakini hazina umeme kabisa. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba siyo kwangu tu, huenda na maeneo mengine yapo vitu kama vituo vya afya, vitu kama shule ya sekondari, hebu iandalie *package* yake peke yake. Wapelekewe umeme wao *separate* tofauti na kwenye vijiji, maana ukienda kwenye ziara wanakijiji wanasema umeme hauko kwenye taasisi hawa wanasema umeme ubaki kijijini, kwa hiyo kidogo inaleta *confusion* hata kwa Mbunge uwaambie nini wale watu unaowawakilisha au wakutume nini? hilo nilikuwa naomba ulione ili uweze kutuisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa napitia na andiko hapa pia. Mimi ni mdau wa mambo ya gesi kwa sababu kidogo ni idara ambazo tumezipitia pitia huko hata kwenye masomo yetu. Kwanza ni pongezi, nitakuwa mnafiki na nitakuwa mtu ambaye kweli sitawatendea haki kwa uamuzi huu mkubwa ambao mmeufanya wa kulitoa Taifa letu hapa na kulipeleka mbele. Niyaaseme haya, walio wengi tumekuwa tuna - *deal* na nchi kama China na vitu vingine kama hivyo, nchi kubwa China na India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaposimama hapa China kwa mara ya kwanza hata sisi tunaeza tukasema ndani ya Bunge hili tutaanza kum - *supply* gesi, kwa sababu China hana *LNG* anaagiza, India hawana *LNG* wanaangiza, yale mataifa makubwa ambayo yanatumia hii gesi kwa wingi lakini hawana wanachokifanya wanaagiza. Sehemu kama China leo wana nchi zaidi ya 20 ambazo wana - *import* ile gesi pale ya *LNG*. Zaidi ya hiyo hata bei China nilikuwa naangalia mwezi uliopita tani moja ya *LNG* inaenda dola 808, kwa hiyo unaweza ukaona soko kubwa tulilonalo kwenye hilo eneo, mimi siongelei uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji ni *investment* ambayo tunaenda kufanya pale ya zaidi ya trilioni 8.7 hiyo tuiache, lakini baada ya hapo Taifa linapata nini baada ya uwekezaji. Tuko na ajira za kutosha tuko na *power* yaku - *supply* kwenye viwanda, tuko na gesi ya ku - *supply* kwenye magari. Kwa sababu dunia inapoenda leo tunaenda kwenye *clean energy*. Unapoongelea *clean energy, LNG* hata kwenye *EACOP* nadhani kwenye mkutano, *LNG* leo wanavyochoma kwenye gari au ukachoma sehemu nyingine ina 40 *percent gas* ya *carbon dioxide* tofauti na *diesel* au tofauti na petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unapoongelea hapo ina *less than* 35 *percent* ya *Sulphur oxide*, zile ni gesi mbaya na ni gesi ambazo zinaua, lakini leo tunapoingia kwenye *project* kubwa kama hii ya Kitaifa. Siyo tu kwamba tunaenda kujulikana duniani lakini tunaenda kutoa kitu cha maana, kitu ambacho kitaitangaza hii nchi kwa miaka na miaka nenda rudi. Nilikuwa naandika hapa na nilikuwa napitia, umeongelea gesi hii *for more than 500 years* wanansema *stock* tuliyonayo au *reserve* ya gesi

tuliyonayo ni *more than 500 years* tunaweza kuitumia hiyo gesi *at current rate*. Kwa hiyo, unaona ni mradi mkubwa ambao unaenda kulipeleka hili Taifa miaka na miaka na miaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza zaidi uamuzi wenu wa kumfanya *TPDC* akawa mbia, maana tumekuwa tunafanya miradi hii unaweza ukaleta Mkandarasi lakini leo chochote kitakachotokea *as long as* mradi huu umeanza *we are the owners,* sisi ni wa wabia tutakaopata faida na zaidi ya kupata faida tutapata kodi kwenye hizi bidhaa. Kwa hiyo, kitu kikubwa ambacho mmekifanya leo kwa ajili ya kulinyanyua Taifa hili *history* ya nchi hii itawakumbuka lakini zaidi uwekezaji mkubwa ambao anaufanya Mheshimiwa Rais kuzunguka huku na huku na hatimae maongezi haya akawa ameyakamlisha ni lazima tumpe sifa na ni lazima tumpongeze kwa juhudi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama hili jambo limeenda muda mrefu halikufanyika ni kwamba kuna imani ambayo watu wameijenga mpaka wakaamua kuja hapa. Unapoongelea kampuni kubwa kama *Shell* leo unaingia nao mkataba wa ku - *run LNG project* siyo kampuni ndogo. Ina visima 12 vya gesi duniani ambavyo inachimba leo, ina visima vingine vitatu ambavyo inajenga kwenye nchi mbalimbali, ina maana na Tanzania tunaingia kwenye ramani ya kufanya kazi na kampuni kubwa kama *Shell.* Kwa hiyo, kitendo cha kuingia kwenye ramani hii haitatutangaza tu kwenye upande wa gesi, inaenda kututangaza pia kwa *investors* wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa unatafuta watu wa kuwekeza lazima kuna watu wengine wataanza kujiuliza Tanzania kuna nini? Kwa hiyo, kama wanajiuliza Tanzania kuna nini maana yake miradi na uwekezaji mkubwa utakuja hapa. Kwa hiyo hilo jambo nilitaka niligusie. Niwapongeze sana kwa bidii kubwa naamini Mungu atatutangulia sawa na hiyo mikataba ambayo mmesema imeandaliwa ya *Inter Governmental* vilevile mkataba wa *operation* iende ikafanikiwe salama kwa maslahi ya Taifa hili, lakini kikubwa katika kupitia nimeona hata gawio kwamba tutakuwa tunagawana 50 *per cent* ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli leo mtu ana - *invest* katika kiwango kikubwa kama hicho, mnaenda kugawana faida kubwa kiasi hicho, jamani tunataka nini zaidi ya kumshukuru Mungu aliyetupa hili Taifa. Kwa sababu unavyoongelea gesi leo ya *LNG,* upande huu wa ukanda huu wetu wote huu, soko kubwa ni China, soko kubwa ni India. Maana yake meli zitakuwa zinakuja hapa zinabeba gesi zinapeleka kule. Hii siyo gesi ya mabomba labda tuelezee kwa sababu huenda mtu mwingine anaweza akaanza kuwaza kwamba utalaza *pipe* hapa mpaka India, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi hii inakuwa *compressed*. Ni gesi inachimbwa inakandamizwa kwa moja ya mia sita, yaani tumezoea moja ya mbili, moja ya tatu lakini unaongelea kwamba *volume* inayochimbwa inakandamizwa kwa moja ya mia sita ya *original volume*. Kwa hiyo, baadae ikitiwa kwenye meli zile zinazoondoka itaenda kuuzwa kule, kwa hiyo itauzwa sehemu yoyote ile duniani. Siyo gesi ya kutumia mabomba kwa sababu *LPG* ndiyo wanapampu kwenye bomba lakini hii itaenda *direct* kuuzwa kwenye maeneo hayo ya nchi hizo ambapo itauingizia faida lakini zaidi ya kutuingizia faida inatuletea pia kutangaza pia hili Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomalizia nikiondokana na gesi. Tulihudhuria utiaji wa saini za mikataba ile ya kuimarisha gridi ya Taifa au gridi imara Ikulu pale. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri zaidi ninampongeza Mheshimiwa Rais, ambaye amekubali kuwekeza zaidi ya trilioni 4.42 kwa ajili ya kuimarisha gridi yetu ya Taifa. Kwa nini nasema hayo, Ndugu zangu umeme una-*stage* ya kuuzalisha, Wahandisi wanaelewa. Unakuwa na sehemu ya *production* lazima uanze kuzalisha umeme kabla ya kufanyia *transmission,* sasa wote ni mashahidi hata *engine* ya gari ukichukua gari lililotengenezwa mwaka 2023, ukachukua gari *the same type* na *same engine* iliyotengenezwa mwaka 2010 au labda 1995 ulaji wake wa mafuta unakuwa tofauti, *efficiency* inapungua kadri linavyoendelea kubaki. Kwa hiyo, *investment* mnayoifanya leo ukiunganisha na mradi wa Mwalimu Nyerere maana yake mnatuweka kwenye sehemu nzuri hata wawekezaji mnaowaleta hapa wataweza kuja na watakubali kuja kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni aibu unaona mtu anataka aje awekeze kwa matrilioni ya shilingi, halafu mtu huyohuyo anatakiwa aje na pesa ya kununua *generator megawatt* moja, *megawatt* mbili, *megawatt* tatu, lakini yote haya tunavyofanya *stabilization* ya gridi ya Taifa maana yake hali ya kukatikakatika kwa umeme haitakuwepo. Kwa hiyo, *investor* anachokuja anakiwaza ni kuja kufanya biashara, kuzalisha na kupata faida na hatimae aweze kuajiri Watanzania walio wengi. Siyo aanze kuwaza ku-*run generator* kwa sababu, *generator* la *megawatt* moja unaweza ukajua linakula mafuta kiasi gani, kwa hiyo, walio wengi *at the end of the day* anakuwa amewekeza, lakini hawezi kuzalisha kwa sababu, aki-*invest* kwenye mafuta hataweza kuuza akashindana na watu wengine wanaozalisha kwenye soko katika umeme ule wa maji au umeme wa gesi ambao tunautumia leo kwa asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ninakushukuru kwa mara nyingine, lakini niwapongeze Mheshimiwa Byabato, Mheshimiwa Makamba, kwa kazi kubwa mnayoifanya. Mungu awatangulie, haya tunayoshauri Wabunge leo myachukue, hasa kwenye upande wa *REA* mkatusaidie wananchi wapate umeme, hapo ndiyo tutakapokuja hapa tukaanza kuimba wimbo mmoja na wimbo wa parapanda tutauimba kipindi tunaelekea huko mbele. Asanteni sana nawashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mhandisi Ezra.

Mheshimiwa Cecil David Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninashukuru sana pia kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Niungane na wenzangu wote ambao kwa namna ya pekee kabisa wamempongeza Mheshimiwa Waziri, wamewapongeza Wasaidizi wake wote akiwemo Naibu Waziri, *REA* na mimi niwapongeze kwa namna ya pekee na niwataarifu kwamba, ule mradi wetu wa kuweka taa kwenye Jimbo la Ndanda wenye thamani ya shilingi milioni 400 tunategemea kuusaini hivi karibuni

na Mheshimiwa Waziri umenisaidia sana kwenye hili, sasa Ndanda kwenye Kata zote za eneo la barabara kuu inayoelekea Masasi linakwenda kuwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kazi zako nzuri ndizo zinazotufanya leo tusimame na kukupongeza kwa sababu, kwa namna ya pekee kabisa umetugusa kwenye maeneo yetu. Tulipoanza mijadala ya masuala ya *REA*, mimi binafsi nilikuja ofisini kwako tukiwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Mtwara na nikakuambia pamoja na *scope* kubwa iliyopo kwenye Jimbo la Ndanda ninaomba *concentration* tupeleke kwenye maeneo mawili. Ulinikubalia na nimshukuru sana pia, Mkurugenzi wa *REA* na yeye alinielewa ombi langu na kazi sasa ya kuweka umeme kwenye vijiji vyote vya Kata ya Mpanyani na vijiji vyote vya Kata ya Msikisi inaendelea. Nafikiri kufikia mwezi Julai kwa sababu kuna baadhi ya maeneo wameshaanza kuwasha na mimi nitakwenda kushiriki zoezi hili la uwashaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiyasema haya siyo maana yake kwamba, kazi imekamilika kwa asilimia 100, bado mahitaji ni makubwa ya masuala ya umeme kwenye Jimbo la Ndanda ukiangalia vijiji vya Mbemba, Mbaju na vijiji vingine vingi vinavyozunguka Jimbo la Ndanda tuna mahitaji ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naweza nikakuambia Mheshimiwa Rais ameamua ugomvi. Wewe mwenyewe unakumbuka juzi tulipokuja ofisini kwako mimi pamoja na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Mtwara tulikuja kweli tuna kilio kwako kwamba Mtwara tuna tatizo kubwa, umeme umekuwa unakatika kila mara maeneo yote ya Mkoa wa Mtwara, hasa kwenye Wilaya ya Masasi, Wilaya ya Newala, Mtwara Mjini na Wilaya zingine zote, lakini umetuhakikishia ndani ya miezi mitatu ijayo unapeleka *turbine* yenye uwezo wa kufua umeme megawati 20 ambayo itakuwa kama ni suluhisho la awali la kuhakikisha Mkoa wa Mtwara unapata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ndiyo maana nasema Mama ametuamulia ugomvi. Wewe mwenyewe umetuelekeza na umetuambia kwamba, pamoja na mradi huu wa *REA*

unaotokea Songea wa Gridi ya Taifa kuleta umeme Masasi umepata pesa nyingine ambayo itatoa sasa umeme Masasi kupeleka Mahumbika. Kwa hiyo, maeneo yote ya Ndanda, Chikukwe, Chigugu na vijiji vyote vya katikati hapa vitakuwa vinapata umeme wa uhakika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na hayo mazuri ambayo wewe unakusudia kwenda kuyafanya nizidi kukupongeza. tumeshuhudia hapa suala la mradi wa *LNG* na faida zake sisi kama Watanzania wote tunazifahamu. Bado narudia kauli yangu ile ile ya mwazo kwamba, mama ametuamulia ugomvi, Wabunge wa Mkoa wa Mtwara tulikuwa hatueleweki kwa wananchi wote wa Mkoa wa Mtwara kwa sababu, Mkoa wetu miaka kumi iliyopita ulikuwa juu kimaendeleo kwa sababu ya miradi mbalimbali ya gesi. Walikuwa na hamu kubwa ya kusubiri ili waweze kuona sasa utekelezaji wa miradi hii utafanyika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndoto kubwa tuliyoisubiri kwa muda mrefu na mimi niwatangazie Wabunge wenzangu, niwatangazie wananchi wa Mtwara na Lindi, sasa inakwenda kutimia, inakwenda kuwa kitu halisi. Kwa namna ya pekee kabisa pia, nimpongeze na Mheshimiwa Hamida kuhakikisha amepambana na wewe Mheshimiwa Waziri kupata pesa za fidia kwa ajili ya wananchi wa eneo la Kikwetu na lile eneo lote ambalo ni kama *5.5 billion* wanafidiwa. Hii tafsiri yake ni kwamba, mradi sasa unakwenda kutekelezwa. Haya ni mambo mazuri Mheshimiwa Waziri ambayo tulikuwa tunayasubiri kwa muda mrefu, lakini tunakushauri sasa hakikisha shughuli zinazofuata kutokea sasa za kutiliana saini tuseme, utekelezaji wa miradi, maandalizi yanafanyika kwenye maeneo ya Lindi na Mtwara ili kuweza kusisimua uchumi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, shughuli zitakazofanyika kwenye maeneo haya, badala ya kutumia Uwanja wa Ndege wa Dar-es-Salaam, badala ya kutumia Bandari ya Dar-es-Salaam, hakikisha unawasisitiza hao wawekezaji, ikiwezekana tena kwa mikataba maalum kwamba, mizigo yao, shehena zao zishukie Bandari ya Mtwara, zishukie Bandari ya Lindi kama wataboresha, pamoja na kuondoa mizigo, lakini pamoja na Uwanja wa Ndege

wa Lindi ili tuweze kunufaika zaidi. Hayo tu ni baadhi ya mambo ambayo tutakuwa tunayapata pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nikusisitize, tumesikia kuhusu miradi mikubwa sana ya kimkakati, ndio maana hawa ndugu zetu wa Ludewa wanalia mpaka leo kuhusiana na suala la Liganga na Mchuchuma. Bado mradi huu umekuwa unatajwa lakini hautekelezwi. Tuiombe Serikali sasa kwa sababu, wawekezaji wameshapatikana jambo hili lifanyike kwa haraka ili sisi tuweze kuanza kuona manufaa haya ikiwezekana kabla hata mwaka huu wa fedha kuisha kazi hizo zianze kufanyika, eneo lile la Lindi lichangamke, maeneo ya Mtwara yote yachamke na wananchi waone kwamba,Serikali yao sikivu inawasaidia kuhakikisha haya yanafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo Mheshimiwa Waziri, nikukumbushe jambo moja, Mheshimiwa Kingu hapa asubuhi aliongea vizuri sana suala la *SONGAS*. Kwa sasa hivi mahitaji ya umeme ni makubwa, hatujakamilisha bado mradi wa *LNG* Lindi, ule mradi wa Mtwara wa *megawatt* 300 haujakamilika na mradi wetu wa Bwawa la Nyerere haujakamilika. Kwa hiyo, ona namna ya kukaa na watu wa *SONGAS,* boresheni hii mikataba inayotumiwa sasa hivi ili wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala jingine limeongelewa hapa na ukienda kwenye ukurasa wa 36 wa taarifa ya Kamati wanasema kwamba, jukumu la vinasaba ambalo lilikuwa *EWURA* mwanzoni lilipelekwa *TBS,* kimsingi inachosema Kamati ni kwamba *TBS* wameshindwa kufanya hii kazi, kutokuweza kufanya hii kazi maana yake ni kwamba, gharama za mafuta zinaongezeka kwa sababu, sasa hivi wanasema *TBS* iwezeshwe ili iweze kutengeneza vinasaba, wanataka waanze kutengeneza vinasaba sasa hivi wakati bei ya mafuta inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* iongezewe watumishi, urasimu wa kupata watumishi unaufahamu na kuna taratibu zake za kupata, tuachane na hawa *TBS* kwenye hili jambo tuwape watu ambao wana uwezo wa kulifanyia kazi ili twendenao sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema pale toka mwanzo kwamba, kutokana na umahiri wako kwenye kazi zako, maeneo yetu sisi yanatofautiana. Kuna maeneo ambako kuna tatizo kweli la umeme, lakini nadhani una nia njema ya kwenda kutekeleza hilo, lakini kuna maeneo ambapo kuna afadhali, sasa tukamilishe haya maeneo yote mawili yaweze kufanana. Mkoa wa Mtwara una vijiji zaidi ya 780 vijiji 800, lakini katika vijiji hivi karibia vijiji 300 havina umeme. Kwa mikakati ambayo umetueleza sisi juzi na ndio maana nakwambia hapa tena kwamba, Mheshimiwa Rais ameamua ugomvi kati yetu sisi Wabunge wa Mkoa wa Mtwara na wewe, lakini kati ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Lindi pamoja na Serikali yao sikivu ya Chama cha Mapinduzi. Tatizo kubwa ambalo lilikuwepo la umeme kwenye Mikoa ya Mtwara na Lindi sasa linakwenda kuisha kwa hatua ulizotueleza za muda mfupi, muda wa kati pamoja na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasisitiza tu kwamba, hawa watu wanaokuja kuwekeza kwenye masuala ya gesi ninaamini ofisi zao ziko Dar-es-Salaam, ofisi zingine uliniambia wakati ule ziko Arusha na ulisema kwamba, mko kwenye *a cell,* kwenye *contained room* ili muweze kufanya majadiliano kwa karibu zaidi. Nikuombe sasa Mheshimiwa Waziri tayari tumeshafikia hatua nzuri na tunakwenda kwenye *implementation.* Ninaamini na wewe unatamani kufika Lindi kila mara ukaone namna tunavyoishi watu wa Lindi, tunavyoishi watu wa Mtwara, kuwarudisha watu hawa nyumbani tafsiri yake tunakwenda tena kusisimua uchumi wa maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu tumekuwa tunategemea korosho tu, lakini sasa tunakwenda kutegemea mazao ya gesi, ikiwa ni pamoja na masuala ya mbolea, lakini pamoja na usafirishaji. Bandari yetu ya Mtwara Serikali imeweka pesa nyingi sana kuhakikisha inatumika. Sasa tunapata bahati nyingine mradi wa Gesi unakwenda kutekelezwa kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana, ninaamini una timu sikivu na jana nilipata taarifa pia, timu yako watu wengine tayari wameshashuka chini kwenda kufanyia kazi haya malalamiko ambayo tulikuletea ofisini kwako. Mheshimiwa Waziri,

mimi niungane na wote waliokupongeza, sasa tunataka tuyaone yale uliyotuambia juzi yanakwenda kutekelezwa. Tatizo la kukatikakatika kwa umeme Masasi, Ndanda na maeneo mengine yote ya Mtwara pamoja na Wilaya za Lindi yawe yamekwisha kwenye kipindi tulichokubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku 90 siyo nyingi, tutarudi tena hapa, tutakuja kuulizana kwamba, Mheshimiwa Waziri ulituahidi kwamba, ndani ya siku 90 matatizo haya ya umeme yatakuwa yamekwisha, kwa hiyo tunataka tuone haya mambo unakwenda kuya-*implement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze tena sana Mheshimiwa Rais na nitumie ileile kauli yangu ya mwanzo kwamba, Mheshimiwa Rais ametuamulia ugomvi Wabunge wa Mtwara. Ahsante sana kwa nafasi hii, nikupongeze kwa kazi zako, ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo. Mheshimiwa Jafari Wambura Chege ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara yetu ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutujalia uzima kukutana jioni ya leo, pili, kama ambavyo wamepongeza wengine, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake kuifanya sekta hii sasa angalao tunaona tunaenda, hii inaonesha wazi kwenye miradi mbalimbali ambayo tunaisimamia, ukiwemo mradi mkubwa wa Mwalimu Nyerere ambao utaweza kutotolea megawati 2,115 ambazo zitaweza kusambaza umeme katika nchi nzima. Kwa hiyo, jambo hili ni kubwa, linastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Ndugu yangu Mheshimiwa Januari Makamba pamoja na Naibu wake Ndugu yangu Mheshimiwa Byabato, Katibu Mkuu pamoja na Wakuu wa Taasisi wote walioko kwenye Wizara hii ya

nishati. Wanafanya kazi nzuri, tunaona kazi zao, tuna-*enjoy* kazi zao na kwa hakika wanatupa heshima kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kama ambavyo tumesema tunaona tunaelekea vizuri kwenye miradi ya *REA* - umeme vijijini. Tumeambiwa na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake asilimia karibia 82 sasa tuna-*cover* nchi nzima. Ni jambo zuri tunaona tunabakia kama na asilimia 18. Asilimia 18 inaonekana kuna miradi iko kazini, iko *on progress* kitu ambacho ni kizuri sana. Nataka nishauri tu mfano kwenye Jimbo langu la Singida Mashariki nilikuwa na ugomvi mkubwa na Wizara yako Mheshimiwa Waziri, nilikuwa na tatizo la Tarafa nzima ya Mungaa. Tarafa nzima ya Mungaa ilikuwa haina umeme hata Kijiji kimoja katika vijiji vile 26 leo ninavyoongea vijiji vyote vimewekewa nguzo na asilimia 40 viemshawashwa umeme. Maana yake ni kwamba, tunaona dalili njema na sisi ya kuonja keki ya Taifa kwenye upande wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikuhakikishie kwamba, tutakapofika mpaka Disemba kama Wakandarsi wataenda hivi, tunaamini tutamaliza vijiji vyote vilivyobaki. Hilo nalisema kwa sababu, kuna Tarafa ya Ikungi ambayo ilianza kupata umeme ilikuwa ina tatizo la baadhi ya vijiji kama Ng'ongosoro, Matongo, pamoja na pale Mwanjiki, hivi ninavyoongea saa hizi hatuna ugomvi na wewe umeme unaenda kuwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni ambayo tunaisema wote hapa, tunaenda kumaliza vijiji Mheshimiwa Waziri, tuna tatizo la vitongoji. Nikuombe sana vitongojini ndiko waliko wananchi. Nikuombe sana huo mpango ambao umesema angalao vitongoji 15, Mheshimiwa Waziri havitoshi, tutakuwa na kelele kubwa sana. Nikuombe sana kama utaweza unapokuja ku-*wind up* hapo kesho utueleze namna ambavyo utakuwa na mipango ya muda mfupi ya kuongeza angalao ili tuweze kuvifikia vitongoji vingi kwani vitongoji hivyo ndiko waliko watu, ndiko ziliko kaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilometa mbili ambazo tulikuwa tunapata hazitoshi kwenda popote, ninaamini zinagusa maeneo machache sana. Kwa hiyo, kwa sababu umeme kila mmoja

anapouona anatamani na kwake upatikane. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, ninajua wewe ni msikivu, ni kijana mwenye nguvu, Mheshimiwa Rais amekuamini, hebu simamia hii sekta. Wananchi wa kule kijijini nao waweze kupata umeme kama ambavyo wengine wanapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza eneo hili nihamie kwenye eneo la mambo kama matatu ambayo ni mahsusi nataka niyaeleze. Mheshimiwa Waziri kwenye eneo hili la umeme wa maji tumekuwa tukisema tunaongeza uwezo, lakini tumeona umesaini mkataba juzi wa umeme wa jua pale Kishapu ni jambo zuri sana, lakini tumekuwa na kilio cha muda mrefu cha umeme wa upepo. Umeme wa upepo tumezungumzia Makambako, tumezungumzia Singida, hivi ninavyoongea kuna watu wameonesha nia ya kuweza kuwekeza, lakini mpaka sasa bado hatujaona dalili yoyote ya kuanza kwa umeme huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wenye uhakika ambao hautakuwa unaangalia tabianchi, ninaamini kabisa tukiongeza kwenye gridi ya Taifa umeme wa upepo naamini kabisa uta-*cover* nchi yetu vizuri. Nikuombe sana unapokuja utuambie mipango mahsusi ya Wizara yako na wewe tunakuamini unaweza kuongeza hili jambo na kuongeza *speed* pale tulipokwama. Kumekuwa na siasa nyingi, naomba hizo siasa tuziondoe, tuhakikishe kama mradi ule wa Singida uanze mapema ili tuweze kuingiza kwenye Gridi ya Taifa wakati tunasubiri vyanzo vingine. Ninaamini hili utalifanya na litatuongezea uwezo mkubwa wa kusambaza umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili kwenye eneo la kiwanda. Kiwanda ili kiweze kufanya kazi, kwa maana naongelea Shirika la *TANESCO,* lazima uwe na vitu kama mitambo na mashine na *technology,* jambo la pili lazima uwe na fedha za kuwekeza ambazo tunazitafuta wote, tatu ni rasilimali watu. Ukishakuwa na rasilimali watu yenye furaha, yenye motisha, yenye kupewa *support* muda wote, utafanya kiwanda kifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimemsikia Mheshimiwa Mkundi amesema asubuhi, kumekuwa na manung'uniko kidogo, kwa upande wa wafanyakazi wa *TANESCO,* kumekuwa na dalili ya kwamba, mnaweza mkapunguza wafanyakazi. Leo hii Shirika unao wateja milioni nne nchi nzima katika nchi yetu, lakini unao wafanyakazi 9,900 tu wastani wa mfanyakazi mmoja anahudumia wateja 424. Maana yake ni kwamba, kuna mfanyakazi mmoja anahudumia wateja wengi sana, maana yake huwezi kutegemea tija pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo unapotaka kwenda kupunguza wafanyakazi maana yake unaenda kupunguza uwezo wa kuwahudumia wateja ambao leo tunasema tuende vijijini tukaongeze idadi ya wateja wetu. Usitegemee kupata ufanisi kama hili jambo lipo kweli na tumeendelea kupata taarifa kwamba mnaendelea kupita kwenye Mikoa kuwaambia kuna mpango wa kupunguza, mfano kama Mkoa wa Ilala wa ki-*TANESCO,* kuna wafanyakazi 288 unasema utabakiza wafanyakazi 86, unategemea uta-*cover* vipi huduma pale katika Mkoa wa Ilala? Mkoa wa Dodoma kadhalika una wafanyakazi 162, unategemea wabaki 86, watahudumiaje wateja wa Mkoa huu? Maana yake ni kwamba, unaenda kuanguka, unaenda kufeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Waziri najua hili huna taarifa, kumekuwa na fukuto ndani kwa ndani linaendelea kwenye Menejimenti, lifanyie kazi, waite kama Vyama vya Wafanyakazi mzungumze ili muwafanye wafanyakazi hawa waendelee kufanya kazi ambayo tunaitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana niongelee jambo moja la mwisho ambalo ni kuhusiana na wenzetu hawa ambao wanafanya vinasaba, ambao ni *TBS*. Mheshimiwa Waziri umesikiliza Wabunge wengi wanaongea, kumekuwa na kampuni ya *SISPA* ilifanya kazi hiyo ya kuweka vinasaba na ilikuwa ina uwezo mkubwa lakini cha kushangaza tulivyowapa *TBS* wanatoka hawana uwezo wa kutengeneza vinasaba wanaenda tena kwa *SISPA* kuchukua tena vinasaba wanavileta huku. Mheshimiwa Waziri wakati tunaamua maamuzi mengine tuwe tunafikiria kwa

kina, tunaweza kuwa tunataka Serikali ifanye, lakini mwisho wa siku uwezo tunao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kujikuta wenyewe, kama hivi mmeambiwa Mheshimiwa Mwambe anakwambia tunaongeza gharama ya mafuta, tunamtesa nani, tunamtesa mlaji ambaye ni mwananchi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri eneo hili ukalifanyie kazi, ninaamini kabisa tunayo nia njema wote kama Taifa, kuna baadhi ya mambo kama tumefeli tuangalie nyuma tulikotoka turekebishe ili nchi yetu iweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, niendelee tena kurudia kuomba sana kwenye kuhakikisha kwamba, umeme unakuwa wa uhakika. Mnajua mna miradi ya gridi imara, mnafanya kazi vizuri, niombe sana tuangalie maeneo yote. Tunayo maeneo ambayo umeme unakatika mara kwa mara, mfano leo Wilaya ya Manyoni na Ikungi umeme unakatika bila utaratibu, kumekuwa na malalamiko mengi sana. Ninaamini kabisa tuki-*stabilize* umeme tutafanya uchumi uende mbele na tutafanya watu wafanye kazi zao vizuri kwa uhakika na waendelee ku-*enjoy* kazi nzuri inayofanywa na Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya Mheshimiwa Waziri ninaomba sana suala la vitongoji tutazame tuweze kumalizia vitongoji vilivyobaki ili tuende pamoja kama Taifa. Mungu akubariki sana na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote tumpitishie ndugu yangu aweze kupita aende kufanya kazi zake vizuri. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege. Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani ya hotuba ya Wizara ya Nishati. Kwanza nianze kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa hakika tumekuwa tukisema kwamba, hakuna kilichosimama na hilo limedhihirika kwa mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambao sasa umefikia asilimia 86.89 na kwa kweli tunaimani kubwa kwamba, ule muda uliowekwa wa kukamilika Juni 2024 tunakwenda kuingia kwenye historia nyingine katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendela kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, wananchi wa Mkoa wa Mtwara habari ya mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia tulishasahau na tukajikatia tamaa, kwa sababu kwenye bajeti ya mwaka jana ni kama hatukuiona hivi, lakini kwenye kitabu cha bajeti ya mwaka huu kwa maneno yaliyoandikwa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Mtwara kwa sababu shughuli ya gesi asilia ilikuwa imelala kwa miaka hii yote, tunaendelea kuwa na matumaini makubwa sana na Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika wananchi wa Mtwara na Watanzania wengine wote kule Mtwara mlitukimbilia sana, watu walijenga hoteli, walifungua shughuli mbalimbali za kibiashara lakini baada ya kuona huu mradi kama umekwama waliondoka, kwa hotuba ya leo tunaamini Watanzania watarudi Mtwara kwa sababu nimeuona mradi upo kwenye kitabu na nitakuja kusema mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kwa nia njema. Lakini kipekee nimpongeze kwa usikivu, unyenyekevu na kuchukua hatua. Kwa nini, nitasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze katika Mkoa wa Mtwara ninapoitumikia nafasi yangu ya uwakilishi. Tunazo changamoto mbili kubwa, ya kwanza ni upatikanaji wa umeme, kwetu sisi imekuwa ni changamoto kubwa sana. Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Mbunge aliyekaa sasa hivi anasema kwao kunakatika katika umeme, lakini nitamkaribisha aje Mtwara, alikuja kwenye shughuli moja ya kikazi, Mtwara ndiko mahali ambako umeme kwa siku unaweza kukatika mara 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua nguvu ya umeme na kwa kukatika huko hakuna shughuli za kiuchumi ambazo zinaendelea vizuri, wajasiriamali wadogo wamekuwa wakilalamika, wanaotunza samaki kwenye friji, wanaofanya shughuli za uchomeleaji, yaani wajasiriamali wote ambao wanatumia umeme wamekuwa wakitoa kilio kikubwa sana. Matokeo yake inasimamisha mtiririko ule wa shughuli za kiuchumi kwa sababu mambo yanasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitangulia kusema hapa, Mheshimiwa Waziri ametuambia, na kwenye kitabu chake cha hotuba mimi nampongeza kwa sababu ameweka hoja mahsusi kwa Mkoa wa Mtwara, ametujibu kwamba tutasubiria kwa miezi mitatu (siku 90) lakini kwa hatua za awali tumeona na tumemsoma. Ninaamini pia tutaanza kuona hayo matokeo ya kukatika katika kwa umeme mwishoni mwa mwezi Juni, tuna matumaini, tunamwomba Mwenyezi Mungu atuweke mpaka Desemba ili tuone na tuthibitishe kwa vitendo hayo ambayo ameyasema kwenye hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ukiacha changamoto nyingine, lakini kwetu sisi nishati ya umeme ni changamoto. Tunaamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu na kwa kuwa imedhamiria kutuondolea hii changamoto hata yale madai niliyokuwa nayo ya wananchi ya kuunguziwa friji, *TV* na vitu vingine, ninayaweka nyuma nisubiri suluhisho ambalo limetolewa na Mheshimiwa Waziri na kwamba ninaamini tutakwenda kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ni upatikanaji wa umeme vijijini katika Mikoa ambayo vijiji vyake bado havijafikiwa kwa asilimia 50 kwa Mradi wa *REA* unaoendelea sasa ni Mkoa wa Mtwara. Tunao Wakandarasi wawili *NAMES* pamoja na *Central,* mmoja anaendelea vizuri lakini huyu mwingine anasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka kuwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi itafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Nishati zikiwemo pia na changamoto ambazo tunakumbana nazo za Mkandarasi wa Mtwara, hili ninaamini kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri unalichukua na umelipa

kipaumbele na ndiyo maana umeweka mkakati wa muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusiendelee kusubiri vile vijiji 200, 300 ambavyo pengine Mkandarasi anasema anavifanyia kazi tukasubiri mpaka Desemba; tunaamini *deadline* ni Desemba lakini basi tuanze kuona hayo matokeo, ikishindikana hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria, yaani suluhisho litakuwepo tu. Waitwe watu wengine waje kufanya kazi ambayo mkandarasi ameshindwa ili na sisi kwenye hivi vijiji, mnajua Mtwara tuna ardhi kubwa, tuna msitu mnene, tupate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kule kwetu, hasa maeneo ya Newala, ukiona mahali kunawaka taa wanasema kwa Ali Ma-solar, yaani ni kwamba tumezoea kwenda dukani kununua ile *panel* ndogo na kuweka kwa sababu umeme bado haujafika vijijini. Hizo ndizo changamoto kubwa ambazo tukitatuliwa na Serikali kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ametuahidi, tutakwenda kupona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshukuru sana, kwa mara ya kwanza najaribu namna ya kurudisha sauti yangu, ninaishukuru Serikali na ndiyo maana nilimpongeza Mheshimiwa Waziri, nimeona maeneo kadhaa ambayo Mkoa wa Mtwara umetajwa. Kwanza ni huu mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa megawati 300 kutoka Mtwara, na wote tunajua. Ndiyo maana Mtwara kwa maana ya gesi ya Madimba iko kwenye chanzo kimoja wapo cha umeme katika nchi hii. Sasa lililonipa faraja ni kwamba Serikali itaanza kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la ujenzi wa kituo na mipaka ya Mkuza kuanzia Mtwara kwenda Somanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba muanze sasa, ukimaliza bajeti hamia kule Mzee, ukaanze kuwaambia wananchi wa Mkoa wa Mtwara namna ambavyo huo utaratibu mzima wa kulipa fidia na kwenye maeneo yote ambayo tunaweza tukanufaika ili kuepusha ile migogoro wanasiasa tutakaporudi kule tuambiwe mbona hakuna kitu. Kwa hiyo, ukitangulia utakuwa umeturahisisishia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia *(LNG)*. Hapa niseme kwa dhati ya moyo wangu kwamba, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amerejesha matumaini ya Wanamtwara kwa asilimia 100. Hii gesi ambayo huko nyuma ilituletea vilio na kutupatia misiba, lakini sasa Mama tunasema ahsante kwa sababu tunajua kurejeshwa kwa huu mradi kwetu utakuwa ni furaha na matumaini ya pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tunajua sasa hata zile Wizara nyingine ile Miji ya *satellite* ambayo tulikuwa tunaiona itakwenda kutekelezwa, Mheshimiwa Waziri wale watu wa Madimba na maeneo yanayotoka kule nendeni mkaone namna ambavyo mtawatia moyo hata kabla hamjafika hatua ya mbali kwa kuboresha shughuli zao za kijamii, shule, vituo vya afya, zahanati na nyumba zao pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo nilipata nafasi ya kwenda kwenye nchi ambayo inazalisha gesi wanaiita Trinidad *and* Tobago tuliona. Tunatamani kuona manufaa kama ya nchi hizo ambazo wamekuwa wakizalisha gesi kwenye maeneo yao, mabadiliko yale ya haraka ya kimaendeleo tunayapata na kule kwetu Mtwara kwenye maeneo ambayo gesi inatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuna eneo la kwenda kuwaelimisha wananchi na hapa tumeambiwa jitihada mahsusi itawekwa katika Mkoa wa Mtwara. Mheshimiwa Waziri mimi naona kama utakuwa unachelewa, kwamba tusubiri mpaka Julai 01, lakini naomba wakati unapokwenda kufanya hili litakuwa kwetu la heshima sana kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Mtwara sasa wataelimishwa namna ambavyo wao watashiriki na kunufaika na huu mradi ili sasa tusiwe wasikilizaji na ndugu watazamaji. Tunataka sisi tushiriki kikamilifu ili tuweze kwenda pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la mradi ambalo kwenye kitabu cha hotuba nimeona linalotupa faraja ni usambazaji wa gesi asilia ambao unatekelezwa na *TPDC* ambao sasa umefika asilimia 60 na utakamilika Juni, 2023. Hapa tumeambiwa kwa kuanzia Mkoa wa Mtwara ndiyo umeanza na

nyumba 209 zitakuwa zimefikiwa. Tunakusihi sasa ukiweka tu kwenye nyumba hizi 209 lakini tunajua Mtwara ina Wilaya zake Tano za Serikali na za Kichama Sita na huko hatujawahi kuwa na viwanda hata vidogo kwa kutokuwa na umeme wa uhakika, tusipopata hii miradi ya gesi kwenye taasisi za umma kama vile shule, hospitali, vituo vya afya na kwingine kote kunakohitaji, bado kwetu manufaa tutachelewa sana kuyafikia, ninakusihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliosoma zamani kama jirani yangu hapa, kwenye shule zao za sekondari walikuwa wanapika kwa gesi. Hivyo, kwa nini sasa hivi wananchi wakakate marundo ya kuni kule. JKT, Shule za Sekondari, Shule za Msingi, Vituo vya Afya, Magereza na maeneo mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Agnes.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutoa fedha nyingi kuiwezesha Wizara hii lakini pia kuhakikisha angalau miradi mingi ya kimkakati na miradi ambayo kimsingi ndiyo msingi wa uchumi na uzalishaji wa umeme inakwenda kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili nami naungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa dhati kabisa kwa namna ambavyo anaendelea kuwashika mkono na kuhakikisha angalau Wizara hii inaweza kutimiza yale ambayo ni malengo halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo kwanza ulivyo mbunifu, ulivyo mpole, namna ambavyo unasikiliza hoja za Wabunge, pia naamini kabisa namna ambavyo umeamua kutengeneza mfumo upya na kuliunda Shirika *(TANESCO)* kwa maslahi mapana ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kukuomba sana kama kijana mwenzetu uendelee kuwa hivyo, ninaamini kabisa kwamba ukiendelea kuwa hivyo basi utatufikisha mbali sana kwenye hili ambalo ni kusudio letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kwanza pia kukushukuru sana, pamoja na kwamba mwanzoni tulianza kusuasua katika utekelelezaji wa umeme wa *REA* kwenye Wilaya yangu na Mkandarasi anayeitwa *GIZA Cable,* nitumie nafasi hii kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ulivyoingilia. Leo mimi nazungumza, katika vijiji 13 vilivyokuwa vimesalia kwa ajili ya kupeleka umeme wa *REA,* vijiji vyote sasa ninavyozungumza tayari umeme umefika na amebakiza vijiji viwili tu kuweza kuwasha umeme huo. Kwa hiyo, ni jambo la heri na mimi niendelee kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza na wewe Vijiji vya Nyihara, Kenyamsama, Borere, Wamaya, Urio, Tabati, Nyamusi, Nyahera pamoja na Masike, tayari umeme umeshafika, vimebaki vijiji viwili tu kwa ajili ya kuwasha. Nitumie nafasi hii kuwashukuru sana watendaji wa *TANESCO* kwa kusimamia hili na kuhakikisha angalau linatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya ambayo tunakupongeza na kukushukuru, nadhani leo tukushauri, ninatamani nikushauri maeneo mawili ili angalau uendelee kufanya mazuri zaidi kwa maslahi mapana ya Taifa. Kwanza, nimesikiliza hotuba yako na nikiangalia kwenye aya ya 22 ya hotuba yako ambapo ulikuwa unazungumzia hali ya uzalishaji wa nishati umeme na mahitaji halisi ya wananchi juu ya uzalishaji kutumia nishati ya umeme, mwenyewe kabisa kwenye hotuba yako kwenye aya ya 22 umekiri hadharani kwamba haiendani na

kasi na namna ambavyo wananchi wanahitaji umeme na uzalishaji wenyewe ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukienda kwenye vipaumbele vyako kwenye hiki kitabu ulichotupatia, kipaumbele cha kwanza kabisa umezungumzia hilohilo, kwamba ni kuhakikisha angalau vile vitongoji vyote vilivyosalia, vitongoji 36,101 vinapata umeme safi na salama. Pia ukienda kwenye aya ya 113, mpango maalum wa kuhakikisha kwamba angalau umeme wa *REA* unafika kwenye maeneo ya vitongoji vyote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza haya yote maana yake kuna jambo ambalo nadhani unakusudia kulifanya lakini kwenye hotuba yako humu ndani labda hujaliweka sawa. Ninatamani sana utakapopata nafasi ya kufanya majumuisho kesho utuambie mpango mkakati uliojipanga kuhakikisha angalau vitongoji vyote 36,101 vinafikiwa na umeme nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka na utakubaliana na mimi kwamba kila wakati ukisimama ndani ya Bunge unaona Wabunge namna wanavyohoji umeme ndani ya vitongoji. Nami mwenyewe ndani ya Jimbo langu nina vitongoji 507, lakini vitongoji ambavyo vina umeme havizidi 200. Kwa hiyo, maana yake zaidi ya asilimia 60 ya vitongoji vilivyosalia havina nguzo wala miundombinu yoyote ya umeme, na ndivyo ilivyo katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu dhamira yako umeionesha kwenye hotuba yako, ningetamani mwishoni Mheshimiwa Waziri utuambie, na usiogope, kama kuna namna nyingine bora ya kupata fedha, tuambie Bunge hili lijue, kama kuna namna ya ku-*impose* hata *rate* kidogo kwenye gharama za mafuta kwa maana ya shilingi 50 mpaka shilingi 100 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba umeme unapata fedha nyingi, zaidi ya shilingi trilioni 6.7, kwenda kutatua vitongoji vyote nchi hii, wewe tuende huko useme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Rais amekuwa akilizungumza hili, kwamba ndani ya miaka mitano matarajio yetu ni kwamba vitongoji vyote 36,000 vinakwenda

kupata umeme. Sasa Mheshimiwa Waziri ukiliacha hili likawa fumbo na kuendelea kututesa maana yake inawezekana ndani ya miaka mitano usilifikie. Nenda fanya kazi, fanya utafiti, kaa na Wizara ya Fedha, hata ikibidi kama unaweza kuweka shilingi 50 mpaka shilingi 100 kwenye nishati ya mafuta ili angalau iweze kuzunguka nchi nzima ili vitongoji vyote viweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ambacho ninatamani nikushauri pia ni namna ya utekelezaji wa umeme kwenye maeneo ya Miji ambayo inakua. Mimi nina Mji pale unakua unaitwa Shirati, tumekuwa tukiuita Mamlaka ya Mji Mdogo lakini ni mamlaka ambayo haina *GN,* haipo kisheria, hata uki-*google* hapo Mamlaka ya Mji Mdogo Shirati hautaiona, lakini *rates* wanazochajiwa wale wananchi, wanalipa zaidi ya shilingi 321,000 kwa nguzo moja wakiambiwa kwamba ile ni Mamlaka ya Mji Mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hawajapata usajili hakuna *GN*, hakuna mratibu na wala haijiendeshi iko chini ya Halmashauri, ninaomba sana Mamlaka ya Mji Mdogo, kwa maana ya Shirati, Kata za Mkoma na Raranya, tuendelee kuwaungia umeme kwa bei ileile ya zamani, shilingi 27,000, badala ya kuwaongezea bei. Kwa sababu tunawaongezea bei kwa sababu ile ni Mamlaka ya Mji Mdogo lakini mamlaka haipo, kwa hiyo inatengeneza taharuku na sababu ambazo hazipo. Ningetamani sana kesho wakati wa majumuisho utamke tu kwamba wananchi wa maeneo haya, hizi Kata mbili, kwa sababu bado mamlaka haijaanza kufanya kazi, haipo na haijasajiliwa, basi waendelee kuunganishiwa umeme kwa bei ileile wenzao wa vijiji vingine wanayounganishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika hilo ni fidia ya wahanga wangu ambao walikubali toka 2011. Nilikwambia hili kwamba waliridhia kwa hiari yao kupisha umeme mkubwa uwe maeneo mengi, vijiji vingi tu. Zaidi ya wananchi 200 toka mwaka 2011 hawajalipwa fidia. Ninaomba pia kesho ukipata nafasi utamke juu ya hawa wananchi. Kwa nini toka 2021 Mkoa mzima wa Mara vijiji vyote vimelipwa kasoro Wilaya yangu ya Rorya. Wilaya zote zimelipwa kwa ajili ya kupisha umeme ule kasoro Wilaya yangu ya Rorya. Hawa wananchi wamekuwa wakifuatilia

kwa muda mrefu, kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu nilikuambia mwaka jana ninaamini kesho ukipata ridhaa ya ku-*conclude* utatoa tamko juu ya adha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu katika hilo ni hawa watu wa *ETDCO* hii kampuni tanzu ambao wanafanya kazi. Yawezekana ikawa inafanya kazi vizuri sana, nimeona humu wanazungumza wanapata faida mpaka bilioni mbili na pointi kwa mwaka, lakini kwangu nadhani kuna sehemu hawajafanya vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, toka mwaka 2021 leo ni 2023, wamepewa miradi mitano, hawajawahi kufika hata mradi mmoja. Sasa haya ndiyo yanaleta manung'uniko mengi, wakati mwingine Mheshimiwa Waziri unaweza ukavishwa mzigo ambao siyo wa kwako. Kama *ETDCo* hawana uwezo bado wa kufikisha umeme maeneo haya, apewe Mkandarasi mwingine ili apeleke vitongoji hivi vyote alivyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ana miradi maeneo matano, na nitakutajia, anayo Kasino, Kongo, Isegere, Buturi, Kyamwama na Nyamunga. Maeneo haya toka 2021, leo tunazungumza 2023/2024 hakuna Mkandarasi *site* wala chochote kinachoendelea. Kwa hiyo, unaweza ukaona wananchi wana haki ya kulalamika lakini kuna mtu mwingine tu ambaye amepewa mradi inawezekana anashindwa kutimiza. Niombe na lenyewe hili utakapopata nafasi kesho uweze kulisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kukatikakatika kwa umeme. Mimi Wilayani kwangu, kama nilivyokuwambia sehemu kubwa ya uzalishaji inategemea umeme. Kwa sababu umesema kwamba sasa hivi unaweka fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu, niombe sana Wilaya ya Rorya uingalie, kwa sababu mpaka sasa ninapozungumza na wewe haiwezi kupita wiki, siku tatu umeme haujakatika, unakatika kwa sababu ya miundombinu inawezekana ikawa imechoka sana. Kwa hiyo, nikuombe kwenye hili nalo uone namna unavyoweza kunisaidia kwenye upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, unafanya kazi vizuri sana, maeneo haya yote unayofanya kazi unafanya kazi kwa ushirikiano na Wabunge, kwa sababu bado ni mtu ambaye unasikiliza maoni na ushauri wa Wabunge, niendelee kukuomba endelea hivyohivyo kwa sababu msingi na dhaminra yako ni njema huko mbele utakapokwenda. Kwa hiyo, ninaomba haya niliyoyasema kwa nia njema kabisa kwa maslahi ya watu wangu wa Rorya ili uweze kuwakumbuka, ninatamani sana kesho, kama nilivyosema utoe angalau majibu kwa sababu haya yamekuwa yakilalamikiwa miaka nenda rudi. Suala la Shirati, kama nilivyosema, walipe 27,000 kama wanavyolipa maeneo mengine, kwa sababu bado hakuna mamlaka, hii ndiyo imekwamisha sasa shughuli za kiuchumi na kuvuta umeme pale limekuwa dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuungana na Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza Wizara kwa uwasilishaji wa taarifa yao ya bajeti ambayo imepunguza maswali mengi ya Waheshimiwa Wabunge na imetupa matumaini makubwa kwamba bajeti hii sasa inakwenda kutekeleza miradi mingi katika nchi yetu na kuendelea kuleta mapinduzi makubwa ya nishati katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, January Makamba, kwa kuweka Wiki ya Nishati. Imetusaidia sana kwa sababu tumepata elimu tosha na imeweza kutupunguzia maswali mengi ambayo tungeweza kuyauliza ama kuchangia hoja katika Bunge letu hili. Kwa hiyo, nikupongeze lakini

niendelee kukutakia heri katika mipango mizuri ya utekelezaji ambayo tunategemea 2023/2024 tunakwenda sasa kuleta mapinduzi ya ukweli katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kuendeleza Gridi ya Taifa. Mkoa wa Lindi kwa maana ya Lindi tunategemea sana umeme kutoka Somanga, umeme kutoka Mtwara, pia Mtwara panapotokea changamoto ya mashine zao kufeli, maana yake Lindi tunapata umeme wa mgao kwa hiyo inakua ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafarijika kuona kwamba mradi wa Gridi ya Taifa unaotoka Makambako – Songea – Masasi – Maumbika kwenye *power extension,* maana yake tutakuwa sasa na umeme wa uhakika na sasa tutakaribisha uwekezaji katika Mkoa wetu wa Lindi kama ambavyo tumejipanga kuhakikisha kwamba fursa za uwekezaji Lindi ziko nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu wa Gridi ya Taifa ambao tunautegemea kutoka Makambako pia utakwenda kutoka Masasi kuelekea Nachingwea – Liwale, lakini kutoka Nachingwea kuelekea Ruangwa. Kwa hiyo, tunausubiri kwa hamu sana. Lakini tunaona kwamba mradi huu umechukua muda mrefu, ni mpango wa zaidi ya miaka mitatu, nikuombe kuhakikisha kwamba mradi huu unakwenda kwa haraka na sisi Wanalindi na Mtwara tuendelee kufaidika na Gridi ya Taifa ili uwekezaji wetu uweze kuwa rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na niwapongeze, Waheshimiwa Wabunge leo waliochangia mradi wa *LNG* maana kila mmoja amehamasika kuchangia mradi huo wa *LNG* nakuona sasa tunakwenda ukingoni katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *LNG* ulianza karibia miaka saba iliyopita lakini tunashukuru kwamba Serikali yetu imekuwa Sikivu, imepitia hatua mbalimbali na hatimaye wananchi wetu wameweza kulipwa fidia katika eneo la mradi na hatua mbalimbali shirika la *TPDC* wameweza kuchukua. Katika eneo

wameanzisha barabara za ndani kwa ndani tunashukuru vijana wa Lindi wameweza kupata ajira, lakini tulichokuwa tunategemea sasa katika eneo lile *TPDC* waje kufanya usafi wa mazingira pale kuhakikisha kwamba eneo linakuwa safi. Walianza kwa hatua nzuri lakini ghafla wakasimama hatuelewi sababu ya kusimama kwao ni nini lakini tunategemea kwamba eneo lile liwe safi kwa ajili ya maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu wa *LNG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi huu tumeendelea kupata fursa mbalimbali, tumewapokea *EPZA* wamekuja Lindi na tumewaonesha maeneo mbalimbali ya uwekezaji, kwa hiyo tunategemea sasa fursa nyingi kuja Lindi kuongeza mzunguko na uchumi mkubwa lakini kuongeza ajira katika Mikoa yetu ya Lindi na Mtwara na hatimae nchi nzima ya Tanzania. Kwa hiyo, sisi kwetu ni maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaipongeza Wizara ya Nishati kwa kusimamia uwekezaji wa ujenzi wa chuo cha masuala ya umeme pale Lindi katika eneo la Kata ya Mbanja, Kata ambayo unakwenda kutekelezwa mradi wa *LNG* na Mtaa wa Makasialeo ndipo ambapo Chuo hiki kitajengwa na hatua mbalimbali wameanza kutekeleza katika ujenzi wa chuo hiki. Sisi kwetu ni mapinduzi makubwa na ni faraja kubwa kwa sababu watakao faidika wa kwanza na mradi huu wa *LNG* ni sisi wana Lindi. Tunashukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba inakwenda mbio katika kuhakikisha mradi huu unakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *REA*. Tunashukuru mradi wa *REA* umetekelezwa kwa kiwango kikubwa na sasa hivi tunaona kwamba vijiji vingi vinapata umeme, vijiji vilivyobakia ni hatua ndogo na Mungu akijalia mpaka 2024 itakuwa vijiji hivi vimeweza kukamilika na wananchi watanzania tutakuwa tumepata umeme kila kona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana nilikuletea kilio kutoka Lindi Manispaa, ipo mitaa ambayio ilikuwa haijapata umeme. Tunajua kwamba mradi wa *Peri-urban* ilibidi utufikie pale Lindi Manispaa lakini kutokana na changamoto mbalimbali maana yake mradi ule umechelewa na wala

hatutegemei kuja Lindi kutekeleza mradi wa *Peri-urban*. Ninakushukuru sana umekuwa msikivu, tulipoleta maombi yetu ya mitaa kadhaa itekelezwe mradi huu wa *REA* ulitukubalia. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametutengea fedha bilioni tano katika kutekeleza mradi huu wa *REA* katika eneo la Lindi Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utatekeleza kilomita 26.4 njia kubwa lakini njia ndogo ni kilomita 13.7, kwa hiyo ninategemea kwamba baada ya bajetii kukamilika Mkandarasi ataanza kazi kwa sababu mkandarasi tayari ameshakuja kuripoti na maeneo tayari yameshafanyiwa kazi, tunasubiri tu fedha itoke ili Mkandarasi aingie kazini aweze kutekeleza mradi huu wa *REA*. Watakao nufaika na mradi huu ni ndugu zetu wa Mtaa wa Jangwani, Nyange, Chikonjwi, Ruaha Mnazi Mmoja pamoja na maeneo mengine. Mheshimiwa Waziri kwa hiyo nakushukuru sana Mungu akubariki na tuendelee kukuombea ili Watanzania tuweze kupata huduma kutoka Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mradi wa matumizi ya gesi majumbani. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Nishati kwa kampeni hii mahsusi ya kumtua mama kuni kichwani, kwa kweli tunaiunga mkono Waheshimiwa Wabunge maana yake sasa tunakwenda kwenye kampeni maalum ya kuhakikisha kwamba wananchi wanaondokana na matumizi ya kuni na mkaa lakini wanakwenda kutumia nishati iliyo safi. Hili ni jambo jema kwetu kwa sababu matumizi ya kuni na mkaa yana athiri afya ya mwanadamu na tunajua ya kwamba matumizi ya gesi yanarahisha katika matumizi ya kupika pamoja na mambo mengine badala ya kutumia muda mrefu unatumia muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Lindi Manispaa Mnazi Mmoja tuna *power extension* ya matumizi ya gesi majumbani, Serikali ilituahidi nyumba mia mbili mtatufungia lakini mpaka leo hatujaona utekelezaji wa nyumba mia mbili kufungiwa matumizi ya gesi majumbani. Mheshimiwa Waziri kwa hiyo ningeomba utakapokuja ku-*wind up* utuambie ni lini utakuja kutekeleza na kukamlisha mradi huu wa nyumba mia mbili kuweza kufungiwa

gesi majumbani ili wananchi waendelee kutumia kadri wanavyoweza kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya gesi ni muhimu sana kwetu na mimi niendelee kuiomba Serikali kwa sababu wananchi wanapenda kutumia gesi, wanapenda kutumia umeme lakini vifaa vya matumizi hayo kwa mfano majiko ya umeme, majiko ya gesi yamekuwa ya gharama kubwa. Wananchi wetu hawawezi kumudu kununua majiko ya gesi na majiko ya umeme. Niombe sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha katika bajeti hii inayokuja kuona namna gani wanapunguza kodi ili Watanzania walio wengi waweze kumudu kununua majiko ya gesi ili tuendeleze kampeni hii ya kumtua mama kuni kichwani tuone tumefikia kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni jambo jema litatuletea tija na Watanzania wengi wataondokana na matumizi ya kuni na mkaa majumbani kwa sababu tunaona uharibifu wa mazingira unaendelea kukua kwa kasi kubwa sana na tunaona hali ya mabadiliko ya tabianchi, joto limekuwa kali mvua hazipatikani kadri tunavyotumaini. Kwa hiyo, tuone namna bora ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanaondokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono kwa asilimia mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka atafuatiwa na Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Engineer Mwanaisha Ng'anzi Ulenge ajiandae.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara hii muhimu, Wizara ya Nishati ambayo kwetu na wananchi wetu ni huduma muhimu lakini ni siasa kubwa katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Wizara pamoja na watumishi wote na Mashirika yanayohusiana na Wizara hii, kwani wamekuwa wakiendelea kufanya kazi nzuri ya kutoa huduma hii kwa

wananchi wetu. Katika Jimbo letu la Kibaha Mjini au Mji wa Kibaha ni Mji unaokua kwa haraka, lakini ni Mji ambao pembezoni mwa Mji huu kuna maeneo mengi ambayo bado yako katika mfumo ule wa *REA* na hakikia wananchi wake wengi hawawezi ku-*afford* kufungiwa umeme kwa ile gharama ambayo siku zote wanachaji ile ya Mjini ya kati ya shilingi laki tatu na ishirini mpaka laki tatu na Hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Wizara kwa sababu siku za karibuni Waheshimiwa Wabunge tuliombwa tuainishe yale maeneo ambayo hakika hawawezi kufikia gharama hizo ili waingizwe katika utaratibu wa *REA* wa kulipa shilingi 27,000 na kuweza kufungiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wangu wa Kibaha, maeneo hayo ni pamoja na Mbwawa, Hekani, Kichangani, Kidugalo, Miomboni, Ghaza, Jerusalemu, Mtaa wa Vitendo, Zogoale, Saenii, Yonuga, Simbani, Sagale, Muheza, Mbwate, Bungo, Kokotimiza, Pumba, Galagaza, Rulanzi, Mwanaugali na Mwale vilevile Mkombozi na Lumumba. Maeneo haya tulikwisha yawasilisha *REA* na tayari tulikwisha ahidiwa kwamba utaratibu unafanyika ili na wenyewe waunganishwe katika ule utaratibu wa *REA* waweze kufungiwa umeme kwa hii gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Wizara au kwa Serikali, sasa utaratibu ufanyike wa haraka kupitia bajeti hii ili wale wananchi wanaosubiri kupata huduma hii waweze kufungiwa umeme huu na wenyewe waweze kunufaika na kufurahia matunda ya kazi kubwa yanayofanywa na Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara hii kwenda kuwapelekea wananchi umeme wa bei nafuu, kwa maana mbali na kazi za kiuchumi, mbali na kwamba umeme ni biashara lakini kimsingi kwa wananchi hawa ni huduma kubwa kwao ambayo inakwenda kuwakomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi wa kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi hadi Arusha ule wa Msongo wa *KV 400*. Nafahamu Serikali ilikwishafanya jitihada ikawalipa wale wananchi ambao maeneo yao yalichukuliwa kupisha mradi huu, lakini bado kuna wananchi ambao hawajalipwa na wananchi hawa hawajalipwa kwa sababu maeneo yao yalihesabiwa chini

ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha sasa malipo yalipofanyika taasisi za Serikali ziliwekwa pembeni au zilisemekana kwamba zitachelewa kulipwa wananchi walipwe kwanza, lakini kimsingi kwa maana ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha kuna wananchi wengi ambao maeneo yao bado yalikuwa chini ya Halmashauri kwa sababu ya kiumilikaji na hadi leo bado hawajaweza kupata fidia, kwa hiyo wamekuwa wakinung'unika wakati wenzao tayari walikwisha pata fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Wizara kwa Mheshimiwa Waziri kabla hatuja-*wind up* kesho, basi ningeomba Wizara itoe tamko ni namna gani hawa na wenyewe wanakwenda kupatiwa fidia ili sasa na wenyewe waweze kuwa sawa na wale wengine ambao tayari walikwishapata fidia kwa kupisha mradi huu wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba Shirika letu la *TANESCO* ni kubwa na linahitaji ufanisi mkubwa, tunafahamu utawala una mikakati ya kufanya *transformation* kubwa au mabadiliko makubwa ya kimuundo lakini kiutawala na kiutendaji. Mimi naunga mkono jambo hili kwa sababu ndiyo njia pekee ya kuendesha shirika hili kisasa, tunafahamu wazi katika kwenda kulitekeleza hili zitatokea fursa nyingi kwenda katika sekta binafsi na ndiyo mtindo wa kisasa wa kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi mahali popote Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu kwa shirika hili au kwa Wizara, tunaomba sana wakati wanaenda kufanya mabadiliko haya kipaumbele cha kwanza au watu wa kwanza kufikiriwa ziwe ni kampuni za nyumbani kwa maana zisimamie ipasavyo *local content* ili makampuni ya ndani ya nchi ya wazawa waweze kupata nafasi ya kushiriki katika kazi hii au shughuli hizi kubwa zitakazotokana na mabadiliko ya kiutendaji na kiutawala ambayo yatakwenda kufanywa na shirika hili la *TANESCO,* ili tija ile isiishie tu kuliboresha Shirika lakini tija ile vilevile iweze kwenda kwa makampuni yetu, wananchi na hatimae kupeleka uchumi kwa wananchi wengi kama wanavyosema wenzetu waingereza kwamba tuwe na ile *economical multiply effect* kwenda chini kwa Watanzania wengi ambao

watashirikishwa katika utaratibu huu wa kwenda kufanya *transformation* katika shirika letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuipongeza Wizara hakika tulisharudi nyuma sana kwa kuacha kuchukua nafasi ya awali kwenda kujenga ile *LNG plant* kule Lindi. Tulianza vizuri na watu walichangamka kweli kweli, Mtwara ilichangamka, Lindi ilichangamka na hata wawekezaji wa ndani na nje walifanya kazi kubwa ya kuanza kuwekeza katika maeneo haya, lakini baadae kwa bahati mbaya tukasuasua wenzetu wa Msumbiji wakaenda mbele, lakini nina imani kwa mkakati tulionao sasa siku si nyingi mradi huu mkubwa kupita miradi mingi ambayo imekwishafanyika hapa nchini unakwenda kutimizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kwamba kwa kuwa tumekwishaamua tusirudi nyuma kwa maana nishati hii tayari inakwenda kuwa muhimu sana katika matumizi mbalimbali Mjini, lakini inakwenda kutuondolea adha kubwa ya kutumia nishati ambayo inatuathiri kimazingira na hususan ukataji wa miti pamoja na matumizi ya kuni na mkaa ambayo inakwenda kutuathiri katika ustawi na upatikanji wa mvua na hatimae kufanya nchi yetu ipatwe na janga la kiangazi. Kwa hiyo, ombi langu na ushauri wangu ni kwamba kwa kuwa tayari kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumekwisha fikia mahali pazuri basi niombe Serikali na yenyewe iendelee kuweka nguvu ili mradi huu uweze kufanyika na uweze kukamilika ili matunda yake tuweze kuyaona ndani ya nchi na hata kwenda chini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa ni huo na niunge mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Koka, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Engineer Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika sekta hii ya nishati, kipekee nikupongeze Waziri wa Nishati, Kaka yangu Mheshimiwa Makamba hongera sana kwa kweli unachapa kazi. Ninakupongeza Wakili Msomi Naibu Waziri, ni msikivu, unafikika na unapokea simu muda wote, niwapongeze Watendaji nikianza na Mtendaji Mkuu *Engineer* Mramba ambaye ni Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu Ndugu yangu Athumani Mbuttuka kwa kweli mnachapa kazi na kazi inaonekana katika Wizara hii, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina changamoto kubwa sana lakini jana Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema maneno ya faraja wakati anakagua ile wiki ya nishati pale kwenye mabanda. Amesema acha wao waseme Wizara chapeni kazi. Mheshimiwa Makamba chapa kazi. Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kulikuwa na maneno mengi sana, lakini umesema kwenye mawasilisho yako hapa tumefikia asilimia 87 sasa hivi, bado kumi na tatu tu hongera sana. Tunao mradi wa *REA,* mradi mkubwa na Afrika kwa sasa hivi tunaongoza *coverage* ni vijiji asilimia 82, tumebakiwa na asilimia 18 hongereni sana, chapeni kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nijielekeze kwenye mradi wa *LNG*. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kama wenzangu walivyosema mradi huu ulienda kwa kasi sana huko nyuma, baadae miaka saba mradi huu ulisinzia lakini kwa upendo wake Dkt. Samia Suluhu Hassan akaagiza majadiliano yaanze tena kwa kasi. Ninakupongeza Mheshimiwa Waziri Makamba kwa kusimamia hayo majadiliano na ku-*fast track* majadiliano na tuliona ulitualika Wabunge wa Mtwara na Lindi pale Ikulu wakati kuna *signing ceremony* ya makubaliano ya awali, lakini kwenye taarifa yako umesema makubaliano, majadiliano mmeshahitimisha mna-*draft* mkataba, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wachangiaji waliopita wenzetu wa Jimbo la Cabo Delgado Msumbiji wakati tunasinzia na mazungumzo wao walianza kwa kasi mwaka 2019, hivi karibuni nafikiri watakamilisha, lakini kwa jitihada zako nafikiri kutangulia siyo kufika ili mradi sisi tumetoka nyuma lakini kwa kasi kubwa tutafanikiwa, kwa hiyo endelea hapo na tunakuombea

kila la kheri hatua iliyobaki ikamilike ili wananchi wa Mtwara na Lindi kama walivyosema wenzangu na Watanzania kwa ujumla wanufaike na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina ushauri kuhusu mradi wa *LNG*. Wakati mradi huu ulipoanza Serikali na wale wawekezaji waliunda Kamati mbili kubwa. Kamati ya kwanza ilikuwa kwa ajili ya upatikanaji wa ardhi *(Land acquisition)* na Kamati ya pili ilikuwa ni kuihusisha jamii kwenye mradi *(community engagement)* na Kamati hizi zilifanya kazi zake kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo husika ya mradi kule Likong'o – Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi limekwishakamilika kama ulivyosema nikupongeze Mheshimiwa Hamida kwa kufuatilia na sasa wananchi wake wengi wamepata fidia. Suala la kuishirikisha jamii naomba Waziri Kamati hii iendelee, kuna mambo mengi ya kufanya kwenye jamii. Vijana, wanawake, wazee na makundi ya kijamii ni lazima yajulishwe hatua zinazoendelea katika mradi huu, waelezwe fursa zilizopo, waeleze jinsi watakavyonufaika na mradi huu na mipango ya Serikali kuwa – *engage* wao katika mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri umesema vizuri kwamba unajenga chuo kikubwa pale Lindi lakini huko nyuma tulikuwa tunawapeleka vijana wapate elimu ya kati katika Chuo cha *VETA* Mtwara na *VETA* Lindi ili wapate ujuzi na maarifa ambayo mradi ukianza wataweza kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu Kamati hii ina kazi ya kuwaelimisha jamii jinsi ya kuishi na mradi. Miradi hii Kwa wenzetu ambao wametangulia kuna changamoto nyingi, wanaweza kuja watu wakaichonganisha jamii na Serikali yao, tujifunze yaliyotokea Nigeria kuhusu Boko haramu, lakini Jimbo la Cabo Delgado Msumbiji kuna maharamia ambao wanahujumu mradi, wamekwenda kule wakashawishi vijana kwamba Serikali inafanya mradi huu lakini ninyi hamtanufaika wakaanza kufanya zile vurugu. Kwa hiyo, sisi tuwatayarishe vijana wetu, wananchi wetu kuishi na mradi kama sehemu ya jamii ili yale yanayotokea kule Cabo Delgado Msumbiji na Boko Haram kule Nigeria yasitokee nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya kusaini makubaliano ya awali pale Ikulu, Mheshimiwa Rais alitoa maagizo makubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri alisema "wananchi wa maeneo husika ya mradi wasiishi kama walivyo sasa hivi" tunatarajia kwamba mradi ukianza Lindi haitakuwa kama ilivyo leo tunatarajia sasa Uwanja wa Ndege wa Lindi sasa ujengwe ili wawekezaji watumie uwanja ule wa Lindi. Tunatarajia sasa barabara za Lindi na Mtwara zitaimarishwa kwa sababu tuna kundi la watu zaidi ya 10,000 kwa ajili ya ajira rasmi na zisizo rasmi, watu hao ni wengi lazima tupanue huduma za afya huduma za elimu na huduma za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuntarajia sasa hivi kwamba hata upatikanaji wa maji, wananchi wa Lindi wasitegemee mradi wa Ng'apa tu, tuwe na miradi mingine ili kuhakikisha wageni watakapokuja kusiwe na changamoto ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili utahusu changamoto za umeme Mkoani Mtwara kama walivyosema wenzangu. Mheshimiwa Waziri ninakupongeza kwa usikivu wako tulifanya kikao juzi na sina haja ya kurudia mambo tuliyokubaliana, ninakuomba sasa kayatekeleze yale, nikupongeze kwa sababu nimepata taarifa timu yako sasa iko Mtwara, kwa hiyo, yale tuliyokubaliana kwanza yale ya muda mfupi kwambab utapeleka sasa *turbine* kutoka Dar es salaam ili iende Mtwara ikazalishe *megawatt* 20 basi kazi hiyo ifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, furaha kwetu wana Mtwara umesema kwenye hotuba yako kwamba ule mradi mkubwa wa *megawatt* 300 wa eneo la Naumbu pale Mtwara utaanza kutekelezwa tunakushukuru sana. Tunaomba mazungumzo na Serikali ya Japan yaendelezwe kama ulivyosema kwamba wameahidi kutoa fedha yaharakishwe, fedha zipatikane mradi ujengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule umesema utajenga *line* ya kilometa 208 kutoka pale Mtwara hadi Somanga Fungu hapo unatudhihirishia kwamba sasa umeme wa uhakika kwa Mikoa yetu ya Mtwara na Lindi utakuwa unapatikana. Si hivyo tu,

umetuthibitishia sasa kwamba ile kazi ambayo inafanywa kutoka Songea hadi Tunduru – Masasi kuiunganisha Mtwara kwenye gridi ya Taifa, basi fedha zimepatikana ili kazi iendelee kutoka Masasi hadi Mahumbika - Lindi. Ukifikisha gridi ya Taifa pale Mahumbika tuna uhakika sasa Lindi na Mtwara tutakuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wa *TANESCO* nawaombeni sasa yale ambayo tumekubaliana basi mtembee katika matamshi yenu na sisi tuna imani na ninyi na tutaendelea kuwapa *support* na pale tutakapohitaji kuwakumbusha tutawakumbusheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishoni usambazaji wa….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikota, muda wako umeisha malizia sekunde thelathini.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la langu la tatu ni usambazaji wa gesi asilia majumbani. Tumeona hapo taarifa ambayo imeandikwa kwamba Mtwara hadi sasa kuna nyumba 420 tu, Lindi kuna nyumba 209, naomba fedha zitengwe kasi iongezwe ili wananchi wa Mtwara na Lindi wanaufaike na gesi asilia pia tupunguze matumizi ya kuni majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ngenda, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajindae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye enzi na utukufu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa muda na wakati kama huu. Nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa

anayoifanya ya kuboresha hali ya maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika kazi kubwa amefanya katika Wizara mbalimbali, katika Wizara hii ya leo mahsusi kabisa hakika Mama amefanya mengi ambayo tunapaswa kuyasemea vizuri bila woga kabisa. Mama amefanya ubunifu katika suala zima la kumalizia mradi mkubwa huu wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pia ameongeza ubunifu mkubwa katika usambazaji, usafirishaji wa umeme nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika nimeisikiliza vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hotuba hii imesheheni mikakati mizuri na mikubwa ambayo Serikali wameipanga kuhakikisha kwamba tunakwenda kupata umeme wa uhakika. Niwaombe ndugu zangu Wabunge mapungufu madogo madogo yaliyokuwepo kwa mikakati hii iliyotajwa leo, ninahakika inakwenda kuisha kabla ya kufika 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu gani? Sasa hivi shirika la umeme nchini linauwezo wa kufua *megawatt* 1822 mpaka kufikia Mei, 2023 mahitaji halisi ni 1431. Maana yake *TANESCO* kwa uboreshaji wa mitambo iliyokuwa chakavu sasa inakwenda kuzidi kiwango kinachotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nimepita kwenye banda pale nimeona kwenye *real time display* majira ya saa nane mchana, umeme ulikuwa unazalishwa *megawatt* 1,426 na vituo vyote kuanzia Mtera, Pangani, Kihansi, Hale mitambo yote ilikuwa *on time* inafanya kazi zake sawa sawa. Vilevile, hata mashine sita za Songas zote zinafanya kazi vizuri sasa hivi. Ni mashine moja tu pale Songas ndiyo inafanyiwa matengenezo na pale kwetu Hale mashine moja tu ndiyo ambayo ilikuwa haifanyi kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali ifanye hima na kumalizia matengenezo katika kituo cha Hale, vilevile na ile mashine moja ya pale Songas iweze kuzalisha umeme ipasavyo. Naiona dhamira kubwa na njema ya Serikali yetu kuhakikisha tunapata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee kidogo mradi unaoendelea wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Hakika juzi nimepita kwenye *Boots* zile za nishati na nimeweza kushuhudia mradi ule kupitia *Visual video* ya mradi ule mzima. Hakika binfasi nime–*fall in love with that project.* Hakika natamani nipate kama siku tatu au nne niende nikatembelee mradi ule. Ni mradi mtamu sana kwa mafundisho makubwa ya Taifa letu na ni mradi wa kihistoria kabisa. Ninaiomba sana Serikali na hii naamini ni shemu ya *contract administration,* tuhakikishe kwamba *material* yote yaliyotumika katika mradi ule yanahifadhiwa mahali maalum, iwe kama ni *museum* ya mradi ule kwa ajili ya vizazi vijavyo kuendelea kujifunza kwenye bwawa lile, nina hakika hata kwa ajili ya *future maintenance program, material* zile zilizotumika sasa zikihifadhiwa vizuri itajulikana kwa urahisi zaidi kwa ajili ya matengenezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona wenzetu wa *hitches on bridge* wameweza kufanya *museum* ambayo kila anayekwenda anaona *material* yote ya mradi ule ulivyotengenezwa lakini kama ninyi ambavyo mmeonesha ubunifu wa *cameras* zile ambazo tumefanya *visual observation* ya mradi ule vilevile, na wao wameweka darubini ambayo mtu anaweza akaingiza hela pale na akawa anaona *hitches on bridge* jinsi ambavyo ina-*operate*. Kwa hiyo, kwa namna hiyo tunaweza tukapata hela ndogo ndogo kwa ajili ya kufanya utalii wa ndani kupitia mradi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeona Aswan *Dam* ya Egypty, tumeona Akasombo *Dam* ya Ghana, wenzetu wanatumia *Dam* zile kiutalii pia. Niombe sana Kaka yangu naamini ubunifu wako, umeonesha makubwa ndani ya kipindi chako na hili mkashirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii tuweze kupata utalii wa ndani kwa maana ya kupata *boat* tuweze ku–*sell around the dam* na tuweze ku–*enjoy* neema kubwa ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendeza zaidi kwa sababu tayari kuna mbuga ya Mwalimu Nyerere katika eneo lile, ni nafasi nzuri kabisa ya kutengeneza *kind of resorts* ndani ya maeneo yale ili kuweza kuvutia zaidi watalii na liingizwe bwawa lile katika utalii

wa Afrika. Kwa sababu ni bwawa ambalo naamini kwa ukubwa litakuwa ndilo la pili ukitoa la Ethiopia. Wenzetu wa Egypt ambao wanatujengea nao tumekwishawapiga chini, wapo na 2110 sisi tuna 2115. Kwa hiyo, ni mradi wa heshima ni mradi wa kihistoria kwa Taifa leu. Ninawapongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa mnazozifanya kuhakikisha mradi huu unakamilika vizuri na hakuna longo longo pigeni kazi, msiogope maneno ya wanaosema, kazi yenu inaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kaka yangu January nikutie nguvu na nikutie moyo kwamba katika Quran sura ya 41 katika ayatul hashir inasema hivi "*Tahsabuhum Jami'an wa qulubuhum Syattaa*" utawaona watu wameunganisha nguvu kama vile ni wamoja lakini nyoyo zao zina uadui. Wanaunganisha tu nguvu ili wa *defeat the strong, you know you can't strengthen the weak by weakening the strong.* Kwa hiyo, Kaka yangu nikwambie piga kazi, kazi yako ni kubwa na mimi nimeielewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuipongeza Serikali kwa kutuletea *transformer* ya *megawatt* 55 pale katika kituo cha Majani mapana. Kazi hii tunaishukuru sana Serikali kwa sababu wale wawekezaji na wenye viwanda waliokuwa wakilalamika kwa sababu ya *low voltage* tatizo hilo Tanga linakwenda kuisha kabisa. Naomba kutumia fursa hii kuwambia wawekezaji popote walipo karibuni Tanga, tuna uwezo mkubwa wa umeme wa kuhudumia viwanda vyote vya Tanga vilivyopo sasa hivi na hata viwanda vingine vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa *transformer* ile ambayo sasa hivi imekwishafika *site* na inafungwa bado tu *Commissioning.* Tunashukuru sana Serikali, Watendaji wa *TANESCO,* Ndugu yangu Maharage kazi yako ni njema, mmejipanga vizuri na sisi tunaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika nakumbuka kuunganishiwa umeme ilikuwa inachukua mpaka miezi mitatu, chini ya uongozi wa Maharage sasa hivi baada ya kulipia umeme unakufikia nyumbani ndani ya siku nne. Ni mapinduzi makubwa ambayo Watanzania tunapaswa kuwapa nguvu na moyo ndugu zetu hawa ambao wana nia njema ya kuliendeleza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze Serikali nimeona mmetenga fedha kwa ajili ya gridi imara, ni jambo kubwa ambalo litaimarisha umeme wa maeneo yetu. Kule Simiyu, Ruvuma, Kilindi kote tunakwenda kunufaika na mradi huu wa gridi imara. Hakika ninayaona mapinduzi makubwa katika sekta hii ya nishati kwa uboreshaji huu wa gridi imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 130 kutoka Vyuo Vikuu vya Jijini Dodoma wanaounda taasisi isiyo ya Kiserikali ya kizazi cha Kimataifa *(Mutual Generation International),* karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuendelea kufanya kazi ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niendelee kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Wapo watu wachache sana ambao Rais anaposifiwa huko nje wanaumia kweli kweli, ninachotaka kusema tunaosimama hapa na kumsifia Mheshimiwa Rais ndiyo tunaoijua kazi ambayo Serikali inafanya. Kwa mfano, leo ninaposimama hapa kumsifia Rais, ninamsifia kwa kuutoa mradi wa Mwalimu Nyerere kutoka asilimia 37 alizozikuta hadi asilimia 87 leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapomsifia Rais wetu tunamsifia mradi mkubwa wa kusambaza gesi asili katika nchi yetu unapokwenda kupata mwanga chini ya Waziri wake January Yusuf Makamba ndiyo maana tunamsifia Rais. Kwa hiyo, wale

wachache wanaoona tunamsifia Rais wanaumia, mimi nashauri tu tunapoanza kuzungumza kama hivi wawe na glasi ya maji wanakunywa huwa inasaidia sana kupooza chuki na hasira. Mtu mwenye chuki, hasira, wivu ukinywa maji inapungua lakini Mama Samia anastahili sifa hizi na tutaendelea kuzitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni miongoni mwa Wabunge wanaohudumu katika Kamati inayosimamia Wizara hii, Kamati ya Nishati na Madini. Kwanza kabisa ningependa niipongeze kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wao wote kwenye taasisi zote hizi Sita zinazosimamiwa ambazo ni *TANESCO, TPDC, EWURA, REA, PBPA Na PURA)* ambapo taasisi hizi zote ziko chini ya Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili kwamba, katika mjadala tulikuwa tunatazama na kuishauri Serikali hata taasisi mbili ambazo zinajihusisha na shughuli za nishati na haziko chini ya Wizara ni vizuri sasa Serikali ifikirie kuzichukua taasisi hizo ziwe chini ya Wizara. Taasisi kama vile *TIPER* na *PUMA energy* ambazo ziko chini ya Msajili wa Hazina lakini zinafanya kazi za nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano leo hii *TIPER* ingekuwa inasimamiwa na Wizara ya Nishati moja kwa moja inawezekana kabisa kufanya kazi kubwa na nzuri zaidi kuliko saa hivi imebaki kama kazi yake ni ku - *store* mafuta tu yanayowekwa katika matenki ya *TIPER*. Kwa hiyo, naishauri Serikali hizi taasisi mbili zisimamiwe na Wizara ili Wizara ambayo inasimamia shughuli za maendelo ya nishati izipangie kazi zaidi na kuleta tija zaidi kuliko kusimamiwa na Msajili wa Hazina ambae kazi yake ni kuangalia hisa zetu na faida ambazo zinazozalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nirudie pongezi zangu kwa Serikali, kwa kazi kubwa iliyofanywa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, hii inakwenda kutusaidia kufanya mambo makubwa katika Taifa letu. Kigoma tumejiandaa kuipokea neema hii, maana tunakwenda kuunganishwa na umeme wa *kilovolt 400* kutoka Nyakanazi kuja Kidahwe na Mkoa wetu mzima utaunganishwa na Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi hii unayoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais, endelea kuchapa kazi na sisi tunakuunga mkono. Kupitia nafasi hii nikuombe Mheshimiwa Waziri katika Jimbo langu la kigoma Mjini, eneo la Kagera na Businde, Kata ya Kagera na Businde pamoja na kwamba ziko katika Manispaa ya Kigoma Ujiji lakini haya ni maeneo ya *peri urban,* mradi wa *REA* uendelee kuwapa huduma wananchi katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo nataka nizungumze ni suala la bei ya mafuta, nimewahi kulizungumza hapa nalirudia tena. Nalirudia tena nakujua Mheshimiwa January Makamba ulivyo mtu msikivu, mchapakazi mwadilifu na mzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mafuta inatofautiana kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine katika nchi yetu lakini bei ya umeme ni moja nchi nzima, uwe ni umeme wa mafuta, uwe ni umeme wa gesi, uwe ni umeme wa maji waliounganishwa kwenye *grid* ya Taifa wanaotumia umeme wa majenereta wote umeweka *unit* ni bei moja. Kwa nini mafuta ya nishati yasiwe bei moja nchi nzima? Jambo hili naomba ulifanyie kazi linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza Kigoma lita moja ya mafuta ya *diesel* na *petrol* ni shilingi 3,034 lakini Dar es Salaam ni shilingi 2871, ukinunua lita 1,000 tu tofauti yake ni karibu shilingi 180,000 kutoka Dar es Salaam kuja Kigoma, na huku ambako bei inakuwa kubwa ndiko ambako watu wana maisha magumu, ndiko ambako kila kitu ni bei kubwa, hebu kaa na wataalamu wako, unao watu wazuri mtazame jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni lile ambalo limeelezwa na wenzangu kuhusu mafuta, suala la vinasaba. Tulikaa hapa Bungeni tukaishauri Serikali baada ya kuona kwamba kuna baadhi ya mambo hayaendi vizuri katika suala zima la vinasaba kwenye mafuta, suala hili likahamishwa kutoka kusimamiwa na *EWURA* likapelekwa *TBS.* Huko sasa ndiyo mambo yanaonekana magumu zaidi. Ndugu zangu tunataka tufahamu kitu kimoja, kujikosoa na kukosoana ni silaha ya mapinduzi. Sisi

tunaweza tukajikosoa katika mambo ambayo tunaona tumeamua lakini tumekwenda kwenye utekelezaji hayaendi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo yanajitokeza sasa hivi, baadhi ya Vinasaba vinawekwa lakini *EWURA* wanapokwenda kukagua wanakuta hakuna vinasaba ni kwamba lipo tatizo. Pia chini ya *EWURA* kabla haijaenda *TBS* hizi kampuni za *SICPA* na *GFT* zilikuwa zinafanya vizuri, hawa *SICPA* wameendelea kufanya kazi hapa nchini kwa uaminifu na sasa hivi wanafanya kazi na *TRA*, kwa nini jambo hili tusilirudishe tena *EWURA* wakalitazama na wakafika mahala wakalifanya vizuri zaidi, *TBS* wana mlolongo wa vitu vingi sana wanavyoviangalia katika ubora, lakini *EWURA* ni maji na mafuta peke yake. Kwa hiyo, bado tunaishauri Serikali kurudi nyuma kujitazama si jambo baya katika kujiimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tumepiga hatua kubwa sana chini ya Waziri January Makamba, tunaona mwanga wa kwenda Kumtua Mama Kuni Kichwani, kupata nishati safi. Nilikueleza hata tukiwa kwenye semina, umeme ukiwa na shilingi 1,000 unanunua umeme wa 1000 unawasha taa, ukiwa na shilingi 2000, ukiwa na 3000 lakini gesi kuna mtungi wa chini unaanza sijui shilingi 23,000 unakwenda 50,000, kwa wananchi wa kwetu huko vijijini wanapata shida. Kwa hiyo fikiria kuwa na gesi inaanzia shilingi 1000 mtu anakwenda anajaza gesi yake ya 1000 anatumia. Siku akipata 3000 anajaza 3000 anatumia. Kukusanya shilingi 22,000 kwa baadhi ya familia ni suala la kikao cha familia nzima watu wakae kujadili kupata shilingi 23,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja nawatia moyo sana, endeleeni kuchapa kazi kwenye Wizara hii mnakwenda vizuri sana. Ahsanteni.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupeleka fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo iliyopo katika sekta hii ya nishati ambayo kwa sasa inakwenda kwa *speed* kubwa lakini inatekelezwa kwa ufanisi mkubwa sana, nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo kwa kushirikiana na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, pamoja na Viongozi wa Taasisi mbalimbali zilizo chini yake wanavyoisimamia vizuri miradi hii, kwa kweli miradi inakwenda vizuri nawapongeza sana, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mradi *LNG* umeanza kutekelezwa, unapozungumzia Mradi wa *LNG* kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ni mradi ambao ni *very sensitive* kwa kweli, pale katikati ulipokuwa umekwama kwa miaka saba watu wengi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara walisononeka sana. Pia, napongeza namna ambavyo Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere unavyotekelezwa, nimefarijika sana kusikia kwamba pale Mkoani Lindi kunaenda kujengwa Chuo cha Masuala ya Umeme, Masuala ya Mafuta pamoja na Gesi tena chuo chenyewe ni chuo chenye hadhi ya Kimataifa hongera sana Mheshimiwa Waziri na timu yako kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maeneo kadhaa ya kushauri, katika Mkoa wetu wa Lindi tuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa umeme, umeme umekuwa ukikatikakatika mara kwa mara inafika wakati, kwa mfano kama katika Wilaya yangu ya Kilwa ndani ya massa 24 umeme unaweza ukakatika hata masaa nane, mara nane kwa hiyo hii ni changamoto kubwa lakini hata taarifa nilizonazo kule kwa Mheshimiwa Kuchauka - Liwale, kule kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu - Ruangwa, Nachingwea na hata Manispaa ya Lindi kwa kweli kadhia hii imekuwa kubwa sana, ninamuomba Mheshimiwa Waziri ule mwarobaini anaopeleka Mkoani Mtwara basi pia aweze kuuleta katika Mkoa wetu wa Lindi ili wananchi wetu wapate umeme wa uhakika.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo ningependa kuizungumza ambayo niliizungumza pia mwaka jana na Wabunge wengi walichangia mwaka jana, kumekuwa katika maeneo fulani ya vijiji watu wetu wananchi wetu wamekuwa wakitozwa gharama ya shilingi 320,000 kwa ajili ya kuunganishiwa umeme, hiyo kadhia bado ipo inaendelea, ningeomba wizara ichukue hatua katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa vijijini wanaendelea kulipa kiasi cha shilingi 27,000 badala ya 320,000 kuna vijiji vya Somanga Kaskazini, Somanga Kusini, Masoko, Kivinje, Nangurukuru wanatozwa 320,000 kuunganishiwa umeme, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri tusaidie katika hili jambo ili wananchi wetu waweze kuunganishiwa umeme kwa ile ada ambayo wanatakiwa kutozwa katika *level* ya vijiji.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yetu ya Kilwa ilikuwa ikipata *CSR* kubwa tu inayozidi bilioni moja kwa mwaka kutoka taasisi ambayo inachakata gesi pale Wilayani Kilwa katika eneo letu la Somanga, Taasisi inaitwa Pan African lakini kadri miaka inavyoendelea mbele kile kiasi ambacho tulikuwa tunapatewa kama *CSR* kimekuwa kikipungua sana, sasa hivi tunapata chini ya nusu ya kiwango ambacho tulikuwa tunapata mwaka 2005 wakati mradi huo ulipoanza kutekelezwa. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri tunajua pale Kilwa tumepata miradi mingi tu tumetekelezewa kupitia hiyo *CSR,* kwa mfano pale Somanga Kituo cha Afya kimejengwa, Chumo Kituo cha Afya kimejengwa, Songosongo hivi sasa Kituo cha Afya kinajengwa, zile fedha zinatusaidia sana, kwa hiyo niombe lile fungu lile la *CSR* lirudi kama lilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ulipaji wa fidia katika Kitongoji cha Cheketu, Kijiji cha Somanga Kusini. Tangu mwaka 2017 ilifanyika tathmini ili lile eneo ijengwe miundombinu ya umeme ya *TANESCO,* lakini mpaka leo zaidi ya milioni 300 wale wananchi wanadai hazijaweza kulipwa, mwaka jana tuliahidiwa mwaka huu wa fedha zile fedha zingelipwa, ninaomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili na wale wananchi walipwe haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la umeme wa *REA*. Katika

Wilaya yangu ya Kilwa utekelezaji wa umeme wa *REA* unakwenda vizuri katika vile vijiji vilivyolengwa. Tunayo shida tu kidogo katika visiwa vilivyopo kwenye Bahari ya Hindi. Kilwa Kisiwani, Songomnara, havijaainishwa katika utekelezaji wa umeme wa *REA* katika kipindi hiki, kwa hiyo ningeomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna maeneo ambayo ni umbali mrefu sana kutoka Kijiji kimoja kwenda kingine wakati kuna vijiji vya Mkoa wa Pwani kule kwa mpwa wangu Mheshimiwa Mchengerwa vyenyewe vinakaribiana na tayari vilishaletewa huduma ya umeme. Kwa mfano kuna Kijiji cha Ngalambilienga, chenyewe ni kilomita saba unakwenda kwenye Kijiji cha Wilaya ya Rufiji, kile Kijiji cha Wilaya ya Rufiji tayari kilishafikishiwa umeme katika zile awamu za awali za utekelezaji wa umeme wa *REA*, ningeomba badala ya kwenda kuchukua umeme Makao Makuu ya Kata ya Kandawale ambako ni kilomita 38, tutengeneze utaratibu wa kuvuta huu umeme kilomita hizi saba toka Mkoa wa Pwani ili tuweze kufanya *serving* ya zile kilomita 31 ambazo ningependekeza zipelekwa sasa maeneo mengine kwa mfano, kuna kitongoji ambacho kinakua kwa kasi sana katika Kijiji cha Zinga Kibaoni kilomita 22, ningependa ile ziada ya kilomita 31 ipelekwe kule ili wananchi wa kule nao waweze kupata matumaini kwani tayari walishakuwa wamekata tamaa. Kwa hiyo ningeomba hilo lifanyike lakini zile kilomita zitakazobaki basi zinaweza zikapelekwa katika Makao Makuu ya Tarafa za Kipatimu, Njinjo pamoja na Miteja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo sina la ziada, zaidi ya kuendelea kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri wanayofanya, naomba nihitimishe kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kwa dhati kabisa kuunga mkono bajeti hii kwa mipango mizuri ambayo Mheshimiwa Waziri amekuja kutuonesha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono nizungumzie utekelezaji wa mradi wa *REA* katika Jimbo la Mbinga Vijijini. Ninaipongeza Serikali kwa nia ya dhati kabisa kwamba ina lengo la kutekeleza mradi huu ifikapo mwaka wa fedha ujao, kwamba ifikapo mwaka wa fedha ujao basi vijiji vyote vitakuwa na vimefikiwa na umeme kupitia mradi huu wa *REA*. Ninaipongeza sana Serikali na kwa kweli imeonesha dhati hiyo kwa sababu vijiji vingi katika Majimbo mengi asilimia ya utekelezaji ni kubwa sana, lakini napata shida kubwa sana mradi huu namna unavyotekelezwa katika Jimbo la Mbinga Vijijini, na napata hofu kubwa kama lengo hili la Serikali litafikiwa kwa namna Mheshimiwa Waziri alivyolisema hapa wakati anatuhutubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbinga Vijijini lina vijiji 117, vijiji 44 tu mpaka leo ndivyo vilivyofikiwa na umeme wa *REA,* vijiji zaidi ya 70, mahala pengine ni Majimbo mawili haya, hawajafikiwa na umeme huu. Vijiji 30 hata nguzo hazijafika, kilichofanyika katika vijiji hivyo ni *survey* tu. Naomba nikusomee hapa Mheshimiwa Waziri usifikirie natamka tu, vijiji 30 havijafanyiwa kazi kilichofanyika ni *survey* tu, hamna nguzo hamna mashimo, hamna chochote, vijiji hivyo ni Kijiji cha Mkalite, Kijiji cha Mkoa wa Asili, Kijiji cha Langiro, Kijiji cha Makonga, Kijiji cha Ndanga, Liyombo, Ukombozi, Kizota, Kitumbi, Muhilo, Matuta, Lingomba, Mkoha, Langilo Mkaoni, Mkuka, Kihongo, Kitesa, Ugano, Tunolo, Njombe, Ndembo, Ulorela, Silo, siyo wewe Mwenyekiti, hiki ni Kijiji chetu kule. Kijiji cha Mpawa, Sara, Kihumboburu, Mapipili, Liwii na Kiangimauka. Vijiji hivi hata nguzo hazijafika huko sasa napata shida sana ikiwa lengo hili linaweza kufikiwa kama alivyotamka Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, Mheshimiwa Waziri mimi nakuamini sana wewe namuamini pia Naibu Waziri, pia na wataalam wa mradi huu *REA* nawaamini wako vizuri, uzuri nimefika kwako ulinikutanisha na hao wataalamu tukapanga mkakati mzuri wa namna ya utekelezaji wa huu mradi, lakini

nikuambie Mheshimiwa Waziri tangu tulivyokutana naye mwaka jana mwezi wa nane amewasha vijiji viwili tu, pamoja na mpango mzuri aliousema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tuliongea na Mheshimiwa Waziri na hivyo vijiji vimewashwa baada ya mimi kuja kwako, vijiji viwili tu vya Charukalasi na Kijiji cha Lihale. Vijiji hivyo vingine vyote havijawashwa, sasa huu toka mwaka jana mpaka mwaka huu na anasubiri pengine bajeti inakuja ndiyo wanafanya fanya hizi kazi ikiisha hii bajeti kimya. Ombi langu la kwanza, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, hebu njoo Jimbo la Mbinga Vijijini, najua kufika kwako wanasema mgeni aje mwenyeji apone, inawezekana kabisa ukifanya ziara katika Jimbo hili mabadiliko yanaweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niombe Mtendaji wa *REA* amenihakikishia, hapa naipongeza Serikali kwa sababu fedha zipo shida siyo fedha, kama shida ni huyu Mkandarasi basi ifanyike namna kuliko tunakaa maeneo mengine miradi inaenda mpaka hii kilomita mbili hizi watu wametekeleza sisi kule kilomita mbili hatujaanza, hatujui tutaanza lini bado tunahangaika na ile kilomita moja hivi vijiji 70 vyote havina kitu. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri na niko chini ya miguu yako nyumba yangu inaungua moto kule njoo uizime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine niombe Wilaya ya Mbinga kunakatika sana umeme na hapa yamezungumzwa sana. Nilisema mwaka jana lakini niliuliza swali hapa, Serikali iliahidi itafanya utekelezaji bajeti inayokuja ya 2024/2025, sasa kwa sababu mipango yetu ni mizuri na inaenda vizuri, mimi niombe ule mpango muurudishe uanzie mwaka huu kwa sababu hali inavyokatika umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ni kwamba ile *lane* ni ndefu sana ukianzia Songea, ije Mbinga mpaka *Nyasa lane* ni moja. Kwa hiyo, ninaomba sana ile mipango ya ujenzi wa *substation* basi na sisi awamu hii mtufikirie tuwe na *substation* pale, kwa sababu ukuaji wa Mbinga ni mkubwa sana, sasa hivi tuna Uchimbaji wa makaa ya mawe watu wameongezeka sana na tuna viwanda vingi sana viko pale vya kahawa na viwanda

vingine vya maji, kwa hiyo wanahitaji umeme kwa ajili ya uzalishaji. Nikuombe Mheshimiwa waziri utufikirie tupe *substation* ili na sisi tusahau shida hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa nchi hii, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kufanikisha mazungumzo haya ya *LNG,* kwa sababu mazungumzo haya kwa kweli yalikwama muda mrefu sasa yanaonesha njia kabisa kwamba tunaenda kupata mradi huu mkubwa wa kuingizia pato kubwa nchi yetu. Hongereni sana, hongereni sana hongereni sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee lile suala la hofu ya mradi ule wa *Songas,* mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri wakati tunaenda na miradi hii mikubwa hata ile miradi midogo midogo ambayo ilikuwa inatusaidia wakati tuna *crisis* ya umeme tusiisahau, tusiiache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukumbu zangu kama niko sawa sawa mradi huu ni wa *PPP* na unaunda na wabia wa nchi tatu, Tanzania ikiwemo Norway na Uingereza. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri, ule mkwamo uliopo wa hofu iliyopo katika kampuni hii, kwamba mkataba inawezekana Serikali haina haja ya kuendelea na mkataba, kwamba *TANESCO* ndio inaweza kuendesha huu mradi. Aah! mimi nikuombe Waziri fanya mambo, kama kuna vipengele katika ule mkataba havifai na mimi najua wewe uko makini pengine linaloonesha hapa kukwamakwama kidogo ni vipengele vya mikataba wa ule mkataba, ikiwemo Naibu Waziri ni Mwanasheria mzuri sana lakini najua una wanasheria wazuri sasa hivi katika Wizara yako, kaeni chini mjadili, wekeni vipengele kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua huu mradi umetusaidia sana, sasa hivi pale Lindi pamechangamka sana, sasa huu mradi ukiwa unaondoka kwa kweli tutaparudisha nyuma na mimi niko eneo hilo la Mikoa ya Kusini ya Ruvuma, Lindi na Mtwara ni Mikoa inayoingiliana, kuchangamka kwa Lindi, kuchangamka kwa Mtwara ndiko kuchangamka kwa Ruvuma. Tukuombe sana Mheshimiwa Waziri endeleza mazungumzo hayo, kwamua huu

mradi uendelee kuwepo, wananchi waendelee kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho nizungumzie suala la mradi huu mkubwa wa Bwawa la Nyerere. Hatua iliyofikiwa na maneno aliyotuambia hapa Mheshimiwa Waziri yamenitia faraja kubwa sana na wananchi wangu Mheshimiwa Waziri wamenipigia simu kwamba walikuwa wanasikia hadithi. Sasa maneno uliyoyasema hapa wamefarijika sana, wanakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, pia wanampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu hakurudi nyuma alikwenda mbele kutoa fedha na sasa tunaambiwa baada ya wiki moja bwawa lile lina uwezo wa kuzalisha umeme, lina uwezo wa kuanza kuzalisha umeme. Hongera sana Mheshimiwa Waziri lakini hongera sana kwa Awamu ya Sita kwa kutenda kazi hii njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu anayefuata nadhani ni wa mwisho Mheshimiwa Selemani Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii muhimu sana ya bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi ambazo anaendelea kutuletea Majimboni mwetu, kutatua kero za wananchi ikiweko suala zima la usambazaji wa nishati muhimu ya umeme, pia nipongeze sana Wizara ya Nishati chini ya Mheshimiwa Waziri Makamba na Naibu Waziri Byabato kwa kazi kubwa ambayo wanafanya ambayo inaonekana kwa wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na suala la umeme vijijini. Usambazaji wa umeme vijijini kwenye Jimbo langu unakwenda vizuri, nichuke nafasi hii kumpongeza Mkandarasi *SILO Power* ambaye anafanya kazi vizuri. Katika Jimbo langu lenye vijiji 81, vijiji

vyote shughuli ya usambazaji wa umeme inafanyika isipokuwa kijiji kimoja tu cha Ikindwa na ambacho leo nilipokuwa kwenye banda la maonyesho pale, nilikutana na Mratibu wa *REA* na Mkandarasi *SILO Power* na wamenihakikishia kwamba wiki ijayo, kijiji cha Ikindwa kazi kwa sababu *survey* walishafanya, kazi ya kuchimba mashimo na kusima nguzo itaanza ili kukamilisha vijiji vyote 81 vya Jimbo la Bukene. Kwa hiyo kazi kubwa inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningependa kushauri ni kwamba haraka iwezekanavyo Wizara iende sasa kwenye mpango wake wa kuhakikisha sasa tunasambaza umeme kwenye ngazi ya vitongoji. Hesabu ya vijiji inaweza ikaku – *mislead*, kwa mfano mimi Jimbo langu lina vijiji 81 na *almost* vyote tayari umeme umefika lakini umeme umefika kwenye makao makuu ya kijiji. Mimi nina vijiji vingine ambavyo nitatoa mfano, Kijiji cha kakongwa, Kijiji cha Kagongwa kina vitongoji saba, lakini ni kitongoji kimoja tu kati ya saba ndicho kimepata umeme, vitongoji sita vyote havijapata lakini ukihesabu kijiji na Kagongwa unaihesabu kwamba imepata umeme lakini kumbe ni kitongoji kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina Kijiji cha Kayombo, Kijiji cha Kayombo kina vitongoji 11, katika vitongoji 11 ni kitongoji kimoja tu ndiyo kina umeme, makao makuu ya kijiji lakini ukihesabu kijiji unasema Kayombo imepata umeme ambayo Kayombo ina vitongoji 11 lakini ndani ya vitongoji 11 ni kimoja tu ndiyo kina umeme. Kwa hiyo, tuende sasa kwenye hatua ya vitongoji ili tuhakikishe sasa wananchi wetu wengi wanapata umeme lakini tuendane na malengo ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 2030 ambako lengo Namba Saba linasema ifikapo mwaka 2030 tuhakikishe wananchi wetu wanapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni usawa katika gharama za kuunganisha umeme maeneo ya vijijini. Mheshimiwa Ndulane amezungumza, ninafahamu mantiki ya kuwa na utofauti kati ya maeneo ya vijijini kuunganishiwa umeme kwa 27,000 na maeneo ya mijini kwa 320,000, lakini sasa kilichotokea ambayo sijui kwa sababu zipi,

unakuta maeneo hayo hayo ya vijijini, kwa mfano Jimbo langu la Bukene lote ni vijiji lakini humo ndani ya vijiji kuna Kijiji cha Itobo na Kijiji cha Bukene eti vimewekwa kwenye *group* la Miji kwa hiyo kuunganisha umeme wateja wanatozwa shilingi 320,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Bukene na Itobo ni vijiji tu vina wenyeviti wa vijiji, vina Serikali ya vijiji, vinaendeshwa na kama vijiji tu. Kwa hiyo, kuvi - *group* kwenye *group* la Miji na kuwatoza 320,000 badala ya 27,000 hatuwatendei haki. Kijiji cha Itobo na kijiji jirani cha Lakui au Chamwabo vyote ni vijiji vinafanana, wote wanategemea kilimo, maisha yanafanana, lakini wananchi wa Itobo kwa sababu ni ka-*center* tu kidogo anatozwa 320,000 tofauti na mwananchi wa Lakui au Chamwabo ambao wanatozwa 27,000. Kwa hiyo, hii mimi naona siyo haki na ninashauri kwa kuwa eneo, kwa mfano Jimbo la Bukene lote ni vijijini kwa hiyo tusibague tena kwamba kijiji hiki kiwe mji, kijiji hiki siyo mji vyote ni vijiji vina wenyeviti wa vijiji vina Serikali ya vijiji, kwa hiyo kuwabagua kwamba wengine walipe 320,000, wengine 27,000 hatutendei haki baadhi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilipenda kuzungumza ni kuhusu mradi mkubwa wa bomba la mafuta. Nimeshazungumza pale kwenye Jimbo langu kuna *coating yard,* karakana kubwa ya kuyapaka *special* rangi maalum haya mabomba. Sasa juzi kwenye semia ya *EACOP* tuliambiwa kwamba mzigo wa kwanza wa mabomba unaingia Desemba mwaka huu na baada ya hapo utaanza kusafirishwa kutoka Bandarini Dar es Salaam kwenda Sojo Jimboni kwangu kwenye kituo cha kuyapaka rangi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kilipo pale ni *rough road* ukifika Nzega unaingia *rough road* kama kilometa 65, hata ukizungukia kule kwa Mheshimiwa Kishimba ukifika Kagongwa ni *rough road* tena mpaka kufika pale Sojo. Sasa siku zote nimekuwa nasema kwamba hiki kipande cha kilometa 65 kutokea Nzega kupita Itobo - Mwamala mpaka Sojo ni barabara nyembamba, madaraja membamba ni *rough road,* huo mzigo mkubwa wa mabomba hautaweza kupita. Juzi kwenye semina ya *EACOP* wale *EACOP* wenyewe walisema wako tayari na wameanza mazungumzo na Serikali ili kuchangia gharama ya kuimarisha

kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami kutoka Nzega Mjini – Itobo – Mwamala mpaka kufika pale Sojo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Wizara ya Nishati kwamba pengine Wizara ya Ujenzi wao umuhimu wa hiyo *coating yard* hawauoni lakini pale ni uwekezaji wa bilioni 600 na mabomba yote yatakayolazwa kilometa 1,440 lazima yafikishwe pale kwanza, yapakwe *special* rangi hiyo ili yaweze ku – *maintain temperature* ili mafuta yasigande yaweze kutiririka. Sasa hayo mabomba yanafika *port* ya Dar es Salaam Desemba yataanza kusafirishwa, yatafikaje pale *coating yard* kama kipande cha barabara cha kilometa 65 hakitamudu kuyabeba hayo mabomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo mabomba ni mazito sana karibu tani 240,000 mabomba saba tu yanajaza lori moja. Kwa hiyo kale kabarabara kaliko pale, hivi sasa hayataweza kupita, nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa sababu wewe uzito na umuhimu wa ile *coating yard* unaufahamu ni vizuri ukakaa na Wizara ya Ujenzi kwa sababu wao pengine umuhimu wa *coating yard* hawauoni ndio maana *priority* ya kutengeneza ile barabara inakua haipo *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika bajeti nimepata fedha kidogo tu kama kilometa chache tu za hiyo barabara, sasa mabomba hayatafika pale kama hicho nilichoshauri hakitafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa kifupi kwamba pamoja na kwamba bado tuna mahitaji makubwa sana ya umeme na nishati nyingine lakini niseme kazi kubwa sana imefanyika katika Wizara hii ya Nishati ikilinganishwa na hali ilivyokuwa hapo nyuma. Katika Bunge la 2010, Mheshimiwa Waziri Makamba tulikuwa naye Kamati moja ya Nishati na Madini alikuwa Mwenyekiti wangu, hali ilivyokuwa wakati huo, hali ya nishati ilivyokuwa wakati huo na sasa ni vitu viwili tofauti kubwa. Kuna kazi kubwa sana imefanyika. Uthubutu wa kupeleka umeme vijijini, ndani ya Tanzania tunaweza tukaona ni jambo dogo la kawaida lakini ni jambo kubwa sana, miongoni mwa nchi za *SADC*, nchi ambayo inafanya kazi kubwa sana kwenye *Village*

*Electrification* Tanzania inaongoza na iko mbali mno, iko mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukajiona hatujafanya jambo kubwa lakini wenzetu wa nje wanavyoona namna ya uthubutu na uwekezaji mkubwa wa kupeleka umeme vijijini, wanashangaa na wanaona ni jambo kubwa sana. Kwa hiyo, baada ya maneno hayo, ninaunga mkono hoja na niwapongeze sana Mheshimiwa Makamba na Naibu Waziri pigeni kazi, kazi yenu inaonekana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati ya Ndugu yangu Mheshimiwa January Makamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye mchango wangu naomba nichukue fursa hii kwanza kabisa, kwa kipekee kabisa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama yetu, Mama wa Watanzania, Mama mpenda maendeleo, Mama la Mama, Mama mwenye mvuto kati ya Marais wanawake Duniani, kwa kazi kubwa sana ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan anaifanya kuhakikisha kwamba Taifa letu linaendelea na linakuwa la mfano Barani Afrika na Duniani kwa ujumla.

Mheshmiwa Mwenyekiti, mama yetu anaupiga mwingi, Mama yetu anaonesha mapenzi na mahaba makubwa kwa Watanzania, Watanzania fuatilieni mambo anayoyafanya *Doctor* Samia Suluhu Hassan, muone upendo anaounyesha kwetu na sisi Watanzania kazi yetu iwe ni kumuombea *inshallah* na kumuhakikishia kumuombea ili Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya aweze kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nipende kumshukuru na kumpongeza January Makamba, yule Mtoto wa Yusuf Makamba

Waziri wa Nishati na Kaka yangu Byabato - Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mkurugenzi wa *REA* na Wakurugenzi wote wanaoendesha taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati, hawa watu wanafanya kazi kama nyuki. Kama ni mpira uwanjani wanapeana pasi, wanapiga magoli tu na ndio maana tunaona hii Wizara ya Nishati ndugu Watanzania, tunaona Wizara ya Nishati hii kuna ubunifu mwingi sana ni kwa sababu kuna *master minder* January Makamba ambaye ameonyesha ubunifu mkubwa katika kuendesha Wizara ya Nishati hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania ni mashuhuda, Watanzania wanafahamu kwamba mwaka 2010 lilitokea jambo kubwa kwenye historia ya nchi yetu. Wataalam wetu wa *TPDC* wakishirikiana na jopo la watalaam lililotoka nje ya nchi, walifanya utafiti na kugundua uwepo wa gesi asilia kubwa sana kwenye bahari iliyopo ndani ya Taifa letu. Ugunduzi huu umeiweka Tanzania kwenye sura ya dunia na kutufanya sasa Tanzania tutambulike kama Taifa ambalo lina gesi asilia safi duniani ukilinganisha na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru *Doctor* Samia Suluhu Hassan ambaye baada ya kimya kirefu cha muda wa miaka saba Rais wetu ameona sasa ni muda muafaka tuweze kuendeleza rasilimali yetu hii ambayo Mwenyezi Mungu ameweza kutupatia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Watanzania wote tuweze kuelewa dhamira nzuri ya Rais wetu nasi Wabunge na Wananchi wa Jimbo la Ngara tunawaunga mkono, tunamuunga mkono Rais, tuna muunga mkono Waziri na timu yote ya Wizara ya Nishati na madini, nendeni mkawekeze kwenye eneo hili la gesi asilia. Wekeni fedha za kutosha ili Watanzania tuondokane na adha mbalimbali ambayo tumeipata kutokana na kutumia nishati chafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamkini tokea asubuhi wazungumzaji wameelezea nishati chafu, watu wanafikia hawajaelewa vizuri, naomba sasa mimi niwaambie Watanzania, tunaposema nishati chafu, tunazungumzia matumizi ya kuni, mkaa na matumizi ya mafuta ya taa kwenye kupikia. Kuna mahali katika nchi hii kuna

wanaume walikua hawatoi mahari maana wanafahamu kwamba mabinti wazuri wanakwenda kutafuta kuni mbali. Anachokifanya yeye anajipanga binti ameenda kutafuta kuni mbali, jioni anambemba mgongoni ameshaoa na mahari hatoi. Sasa, hii kazi nzuri inayofanywa na January Makamba ya kutuleta nishati safi inaenda kuwafanya kina mama sasa wasiende kutafuta kuni mbali na wale waliozoea kubeba, sasa inakwenda kuwa mwisho. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ukombozi mkubwa sana kwa wakinamama wa Tanzania waliokuwa wanapata adha kwenda huko porini kutafuta kuni, sasa hawatofanya hivyo, watapata nishati safi na wataweza kuitumia. Kuna Watanzania kutokana na macho yao yanaathiriwa na moshi, maeneo kama ya Kanda ya Ziwa baadhi ya wazee vikongwe waliuliwa wakitwa ni wachawi kwa sababu wanapikia kuni na matokeo ya zile kuni ni ule moshi wenye *carbon* na kemikali nyingi zinaua macho yao yanakuwa mekundu. Watu walipigwa panga kwa sababu ya nishati chafu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunamuona Rais yuko mbele, leo hii tunamuona Waziri yuko mbele, wanakwenda kuwaokoa Watanzania kutoka kwenye hiyo adha ambayo tulikuwa tukiipata. Naomba Watanzania waelewe tunaposema nishati safi ni kuondokana na hii adha ya kutumia nishati chafu ambayo imegharimu maisha mengi ya Watanzania. Achana na hilo, muda tu kina mama waliokuwa wanaupoteza kwenda kutafuta kuni ulikuwa ni muda ambayo kwa sasa badala ya kwenda kutafuta kuni ulikuwa ni muda ambao kwa sasa badala ya kwenda kutafuta kuni sasa watautumia kwenye uzalishaji mali na wataweza kuongeza tija katika uwekezaji na kazi wanazozifanya kwenye familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, achilia mbali macho mekundu, achilia mbali kupoteza muda, achilia mbali watu kutumia fursa hiyo kubeba mke hata bila kutoa mahari, njoo kwenye suala la uharibifu wa mazingira. Miti imekatwa kweli kweli, watu wanafanya nishati chafu kama chanzo cha biashara. Kuna mtu yeye kazi yeye yake tokea awe mtu mzima miaka 18, yeye ni kukata miti na kuchoma mikaa na kuuza mikaa, ameharibu

vyanzo vya maji, wameharibu misitu, matokeo yake Dar es Salaam sasa hivi kuna kipindi tunaingia kwenye *crisis* ya ukosefu wa maji kwa sababu miti mingi imekatwa kwenye Mto Ruvu ambapo maji ndiko yanapozalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na huu mradi wa *LNG* unakwenda kuokoa Watanzania. Ninawaomba Wizara ya Nishati, endeleeni mbele, wekeni hela ya kutosha katika hilo eneo, Wabunge tunawaunga mkono kwa sababu tunafahamu jambo zuri mnalolifanya kwa ajili ya Watanzania. Tunakuomba Mheshimiwa Makamba usirudi nyuma kwa watu wanaopiga vijembe huko vijiweni ambao hawaelewi, mimi hapa ni Mwakilishi wa wananchi, nimesimama kuelezea faida kubwa za Mradi huu wa *LNG* kwa Taifa. Ninaomba Watanzania waweze kutuelewa, dhamira nzuri uliyonayo Mheshimiwa Waziri sisi tunakuunga mkono, endelea moja kwa moja, usirudi nyuma, weka fedha za kutosha, wote tutapitisha miradi hii iende ikatekelezwe iweze kutusaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *REA* tunakushukuru Mheshimiwa Waziri umefanya kazi kubwa sana. Tunafahamu Tanzania ina vijiji zaidi ya 10,800. Kati ya vijiji 10,800; vijiji zaidi ya 10,000 vimeweza kuwashwa umeme vimebaki vijiji vichache nchi nzima. Hii kazi ambayo umeshaifanya Mheshimiwa Waziri ni kubwa na ni nzuri na inatambulika kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Kagera Mkandarasi anaendlea vizuri. Amepeleka nguzo maeneo yote ambayo yanahitaji umeme. Hata kule kwangu Ngara Mheshimiwa Waziri tumejipanga kuanza kuwasha umeme kijiji kimoja baada ya kingine mara tu baada ya Bunge hili kuisha. Nichukue fursa hii Mheshimiwa Waziri nikukaribishe uungane nami twende tukawashe umeme Murusagamba. Murusagamba tokea Mwenyezi Mungu awaumbe hawajawahi kuona umeme. Ni sasa hivi wewe Mheshimiwa January Makamba umetuletea mkandarasi, mkandarasi amepeleka umeme kwenye taasisi na hivi tunavyozungumza tunashirikiana kufunga umeme kwenye vijiji. Tuende tukawawashie umeme Murusagamba na maeneo mengine ambayo wanahitaji huduma ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mradi wa *densification* Mheshimiwa Waziri. Kwa unyenyekevu mkubwa nikuombe kule Ngara nisaidie angalau niongezee vitongoji hata 10 kwa neno lako tu Mheshimiwa Waziri unaweza ukanipa vitongoji hata 10 Mheshimiwa Waziri. Kule kwangu Mheshimiwa Waziri sijui ilikuwaje sijui ni *typing error* badala ya kuniandikia vitongoji 50, waliniandikia vitongoji vitano. Sasa nikajiuliza ndugu yangu sasa huyu January Makamba nini tena hii? Nikasema sasa Mheshimiwa Waziri leo nikuombe kwa unyenyekevu mkubwa niongezee kidogo pale nipe hata 20 viongezwe kwenye vile vilivyopo ili Mheshimiwa Waziri vile vitongoji ambavyo vinahitaji huduma ya umeme na vyenyewe tuweze kuvipelekea umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri utakumbuka ulipokuja Ngara kutembelea mradi wetu wa Rusumo nilikuomba unisaidie kwenye mitaa 17 ya Rulenge ambayo haina huduma ya umeme kabisa, ile ni mamlaka ya mji lakini ile mitaa yake yote ni vijiji. Mheshimiwa Waziri nilikuelezea kuhusu hili, ninakushukuru ulituma Wataalam wakaja wakakagua pale wakakuta kweli vile ni vijiji vinatakiwa kuhudumiwa. Kwa unyenyekevu mkubwa naomba unisaidie tena vitongoji vyangu hivi 17 vya Mamlaka ya Mji Rulenge viweze kupata huduma ya umeme angalau mimi niogelee inapofikia 2025 Mheshimiwa Waziri nafikiri unajua nachokimaanisha ni nini. Nikipita pale iwe ni shangwe na vigelegele wala hakuna maswali mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri endeleeni kuchapa kazi. Watanzania wanaona kazi nzuri mnazozifanya, sisi ni mashuhuda wa mambo makubwa mnayoyafanya, tunawaunga mkono wewe na timu yako yote, Mwenyezi Mungu awabariki awape afya njema muendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, muda ukiruhusu Mheshimiwa Deo Sanga atamalizia.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ambayo ni mwanga wa nchi na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu, maneno hayatoshi jinsi gani ya kumpongeza Rais kwa jinsi ambavyo ameamua kweli kututumikia Watanzania na kututoa hapa tulipo kutufikisha kwenye nchi ambayo ni ya asali na maziwa, kikubwa cha kumuombea ni uzima na afya njema ili malengo yake haya yatimie ya kuifanya nchi hii kuwa nchi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze Waziri na Naibu wake, vijana hawa wanamtendea Mama haki kwa sababu wanafanya kazi ile ambayo Mama anaitaka kwa weledi na kwa upendo na kwa uhakika mkubwa, ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, kichwa chako kimetulia mimi nakufahamu vizuri ni kichwa ambacho kinaweza kufanya mambo makubwa katika nchi hii. Nikutie moyo fanya kazi, sisi tuko nyuma yako tunakuamini na tutaendelea kukupa ushirikiano wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda leo mchango wangu ujikite sana *TANESCO* na *TANESCO* nataka niende kwenye suala la bei za umeme. *TANESCO* inafanya biashara ya umeme kwenye *tariff* lakini pia sehemu ndogo mimi ninaiita ndogo kwenye kuunganisha umeme. Kuunganisha umeme kwa shilingi 320,000 ni sehemu ambayo *TANESCO* inategemea iingize mapato, lakini watu wanaoweka umeme kwa shilingi 320,000 ambao ni watu wa mijini, *rate* yao ya kuweka umeme ni ndogo sana, kwa sababu ya gharama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi ambacho ilitangazwa kwamba umeme uwekwe kwa shilingi 27,000 nchi nzima maombi ya kuweka umeme yalijaa *TANESCO* mpaka wakashindwa kufanya kazi lakini watu hawa ambao walipeleka maombi mengi ni watu wa mjini ambao wana matumizi makubwa ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hii ni fursa ambayo tumeiacha, ni bora tungetumia gharama ya kuhakikisha tunaweka umeme kwa shilingi 27,000 lakini baada ya muda mfupi watu hawa wote wanatumia umeme na *TANESCO* wataingiza umeme kwa *tariff* kwa sababu watu wa mjini wana matumizi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaweza kupeleka umeme zaidi ya kilometa 200 kutoka kijiji kimoja kwenda kijiji kingine na tunafika kwenye kijiji kile kaya zitakazoweka umeme ni kaya labda 10,15 mpaka 20, kama Serikali hii inakubali hiyo gharama ya kupeleka huduma hiyo kwa wananchi tunaachaje kumuwekea mwananchi wa mjini umeme kwa shilingi 27,000 ambaye nguzo moja, kuna maeneo ambayo nguzo moja ya umeme inaweza kubeba mpaka mita 10,15 nguzo moja. Sasa hiyo nguzo moja kwa shilingi 27,000 ikabeba nyumba 15 maana yake watu hao wa mjini ndiyo wenye friji, ndiyo wenye nini matumizi ni makubwa na *TANESCO* itaingiza fedha nyingi sana kupitia *tariff* za hawa watu kuliko kuwawekea shilingi 320,000 halafu hawavuti umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunakusanya *property tax* kubwa sana nchi hii kupitia mita za umeme. Leo hata mtu aliyeko kijijini mwenye nyumba ya tembe akivuta tu umeme atalipa shilingi 12,000 kwa mwaka ya *property tax* kwa sababu atalipa shilingi elfu moja moja kwenye mita kila mwezi. Kwa nini tusitumie hii fursa ya kukusanya *property tax* kubwa kwa kuhakikisha watu wengi wanavuta umeme na ili watu wengi wavute umeme maana yake tukifanya shilingi 27,000 watu wote watavuta umeme. *TANESCO* watafanya kazi masaa 24 ili kuweza kuweka haya maombi yaweze kutimia kwa sababu watu wote wa mijini wataweka umeme na matokeo yake ni kwamba *property tax* itakuwa kubwa kwa sababu watu wote hawa watakuwa wanatozwa shilingi 12,000 kwenye mita zao kwa mwaka kwa hiyo mapato ya Serikali yataongezeka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena katika hili ina maana hata tunaweza tukaweka asilimia kidogo ya hii *property tax* ikaenda *REA* kwa sababu *REA* wanaongeza watu wa kutumia umeme matokeo yake wanaongeza *property tax* kuwa kubwa, maana

yake kama tukichukua hata *percent* tatu tu kwenye ile *property tax* ikaenda *REA* maana yake tayari tutakuwa tumeipa *REA* uwezo mkubwa zaidi wa kuongeza watumiaji wa umeme kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hii inayoenda kwenye vitongoji maana yake vitongoji vitakwenda vingi kwa wakati mmoja kama *REA* ina pesa na kadri wanavyoingia maana yake *property tax* inaongezeka, mapato ya Serikali yanaongezeka. Hii ni *win win situation* ambayo ningeomba hii *property tax* angalau ipelekwe asilimia chache ziende *REA* ili mita nyingi ziongezwe kwa shilingi 27,000. Nyumba ni nyingi mjini tuko wengi milioni 61 na nyumba ni nyingi hii ni fursa ya kukusanya mapato ambayo tunaiacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri na *TANESCO* mkae muangalie hili suala la shilingi 27,000 liende nchi nzima ili watu waweke umeme wa kutosha tutapata mapato ya kutosha kwa *TANESCO* na tutapata mapato ya kutosha kwenye Serikali kupitia *property tax. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye shilingi 27,000 kwa mfano mimi katika Jimbo langu, Iguguno ni kijiji, Nduguti ni kijiji, Makao Makuu ya Wilaya waliangalia *geographical position* hawajaangalia kwamba uchumi au wakaangalia kwamba sijui wana nyumba nyingi Hapana! Walichoangalia ni kwamba Nduguti ni katikati ya Wilaya ya Mkalama, hapa ndiyo patakuwa makao makuu lakini ni kijiji. Iguguno ni kijiji maisha ya wananchi ni ya kawaida ya kijijini. Sasa unapomwambia alipe shilingi 320,000 kuweka umeme ni kama ni kumnyima umeme tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wakati unalifikiria hili la kuweka nchi nzima shilingi 27,000 basi haya kwenye maeneo yetu ya vijijini kama Iguguno na Nduguti ianze mara moja shilingi 27,000 kwa sababu ni wanakijiji kama walivyo wanakijiji wengine ili kuweza kuvuta umeme katika maeneo haya. Kwa kuwaambia watu wa Nduguti, watu wa Iguguno wavute umeme kwa shilingi 320,000 ni kuwaambia wasitumie umeme jambo ambalo kwa kweli sidhani kama ni jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine hapo hapo kwenye hizi mita, *TRA* wanatumia kukusanya *property tax* kwa mita lakini sasa uzembe wao pia wanataka kukuponza Mheshimiwa Waziri. Wamekadiria vibaya nyumba zao. Kuna nyumba zinatakiwa zilipe zaidi ya shilingi 12,000 kwa mwaka. Matokeo yake hawakuwaambia mwanzoni wakakata shilingi elfu moja moja yakajilimbikiza madeni, leo wanashtuka wanakwenda kujaza kwenye mita madeni ya mwaka mzima, lawama zinakuja kwako Waziri, lawama zinaenda *TANESCO* kwa uzembe wa *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushtuka kwa nini wasingeingiza hata kidogo kidogo kwa sababu wao wenyewe walikadiria hawakuingiza kwenye mita madeni yanavyotakiwa. Leo hii kuna watu wanakuja kukosa kununua umeme kwa sababu amewekewa deni la mwaka mzima ambalo siyo makosa yake ni uzembe wa *TRA* kwenye kuingiza. Leo inaingizwa kwenye mita wewe Mheshimiwa Waziri unaonekana wewe kwenye mita zako ndiyo kuna tatizo. Kaa nao *TRA* uzembe wao wasikuponze wewe kijana tunakujua ni kijana mwema, mchapakazi, uzembe wa *TRA* usiingizwe kwako Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tena hapo hapo, *TANESCO* wamekuja sasa wanakusanya madeni yao ya nyuma mengine ya miaka 20 iliyopita. Waliokuwa wanadaiwa wameshakufa wengine, hawa-*exist.* Leo hii wameshtuka sijui wapi linakusanywa deni mtu unashangaa kwenye mita unaambiwa unadaiwa shilingi 2,000,000, 1,500,000 mwananchi wa kawaida deni hujui lilikotoka. Nyumba zingine mtu alishafariki nyumba wanaishi wapangaji wengine hata hawajui kilichotoka unaambiwa mnatakiwa mlipe deni. Naomba Mheshimiwa Waziri hili jambo *TANESCO* mkae chini muangalie upya namna ya kukusanya madeni, kuna madeni mengine yanatakiwa yafe tu. Mtu miaka 20 mlikuwa wapi siku zote?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Isack.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba nimalizie kwa kusema kwamba *TANESCO* hili jambo waliangalie vinginevyo itabidi watu wengine wako

tayari kushtaki, wanaenda *EWURA* kushtaki kwa jambo ambalo linaweza kukaa chini na kuzungumzika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niungane na Wabunge wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa rehema zake, baraka zake lakini kama Taifa kwa jinsi anavyotulinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais kuna mambo mengi tunampongeza kwa ajili ya Serikali kutekeleza mambo mengi, ukiacha Wizara moja moja, kwa ujumla katika nchi yetu twendeni kila Mbunge kwenye Majimbo yetu tukaeleze yale mafanikio ya Serikali ili agenda hii ya kumpongeza Rais iwe agenda yenye mashiko na inayoonesha taswira nzuri kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza kwa sehemu kidogo Mheshimiwa Waziri lakini pia nimweleze duku duku na maeneo ambayo ninadhani pengine kupitia ujumbe wangu huu yataboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na eneo la Mbulu Mjini, Jimbo la Mbulu Mji ina mitaa 58, Kata sita za mji, vijiji 34 na Kata 10 ziko vijijini. Siyo kama tunavyozungumza Mbulu Mji kama Mji, Mbulu Mji una sura mbili, nianze na sura ya eneo la mji na kwa sababu hali hii ipo katika maeneo mengine hata kwa Majimbo yetu kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Mbulu Mji wale wa pale katikati utakuta yuko ndani ya kilometa moja kutoka katikati ya mji lakini hajafungiwa umeme lakini amemaliza *wiring* na yuko ndani ya mita 30 ya nguzo. Hapa ushauri wangu ni kwamba niungane na mwenzangu Mheshimiwa Francis Isack

alivyozungumza, twendeni tukafanye tathmini ya maeneo ya miji yetu na hali ya uhitaji wa umeme na wale waliofanya *wiring,* hapa tunatafutiana ajali za kisiasa kwa sababu moja kwa moja wananchi waliofanya *wiring* leo unapowaambia waunganishiwe umeme kwa shilingi 320,000 wakati shilingi 27,000 ingeunganisha wao wana matumizi makubwa lakini pia wako ndani ya mji kwa maana ya ndani ya kilometa moja ama mbili. Hali hii itaifanya matumizi makubwa ya umeme kupatikana lakini na uzalishaji kuja juu na kwa vyovyote wananchi wale watakuwa wamefunga umeme huu katika majumba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuelimishane au tuambizane na tutazame kwa sura tofauti kila Mbunge kwenye eno lake, kwa hali ya uchumi wa wananchi wetu ni mwanancni gani ana uwezo wa kulipa shilingi 320,000 akafanya *wiring* tena kwa shilingi 320,000 na mambo mengine, umeme wenyewe kwenye jengo hilo moja shilingi 700,000? Hii ni hali ambayo kwa vyovyote haiwezekani Mheshimiwa Waziri, utakapokuja pale toa kauli kama Serikali eneo hili la uunganishwaji wa umeme wa awali Serikali ije na njia mbadala ya kuunganisha umeme kwenye makazi ya watu kwa maeneo ya mjini na vijijini kwa sababu eneo hili la mji zamani wakati wanafanya *wiring* wananchi walitegemea sana kwamba eneo hili wanaunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000 wao wanapata gharama ya kufanya *wiring* kwa maana ya kufanya uunganishaji wa waya kwenye majengo yao ili wapate huduma ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la vijijini kwa Mbulu Mji utakuta kijiji cha mwisho kilometa 40, ndani ya kijiji hicho tunapopeleka kilometa mbili, kwenda kwenye vitongoji utakuta kitongoji kutoka katikati ya kijiji ni kilometa 20 ama 15 tena, kwa hiyo, nguzo za kwenda huko ni nyingi. Mimi ushauri wangu kwenye eno hili nilikuwa naangalia tunapoanza kuweka umeme kwenye maeneo ya vijijini tuangalie utaratibu ambao utashika kaya nyingi na nyumba nyingi ili ziingizwe kwenye mfumo huu wa kuunganisha umeme. Eneo hili la vijijini ndiko waliko wananchi wengi, matumizi yao siyo makubwa, wao sana sana watatumia umeme kwa taa, kuchaji simu na huduma zingine ndogo ndogo lakini mambo ya friji na mambo ya mitambo mingine haitakuwepo sana zaidi ya mashine za kusaga na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nafikiri kama inawezekana eneo hili litazamwe na Wizara. Mheshimiwa Waziri timu yako imepita mara nyingi na mara nyingi umetuletea mipango hii ya vipaumbele kwenye vikao vyetu vya bajeti, kwa bahati nzuri baadhi ya maeneo mengi Serikali imejitahidi kuangalia ni namna gani umeme unakwenda. Kwa hiyo Jimbo langu la Mbulu Mji, vijiji vyote umeweka nguzo, vingine vina miezi miwili, vingine miezi mitatu, vingine sita umeme haujawaka. Hali ambayo nguzo zile zinazidi kuoza, mimi nilikuwa nafikiri uwekaji wa nguzo utegemeane na waya na vifaa vingine ambapo ukisimika nguzo hizo, walau umeme unawaka kwenye hicho kijiji ili unahamia kijiji kingine kuleta sura ya matumizi lakini na pia sura ya kutoa huduma kwa wananchi kwa wakati uliosahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeruka maeneo mengi ya taasisi za umma, migodi, pampu za maji, taasisi binafsi na mashirika ya umma, nadhani kuna haja ya kufanya tathmini upya ili hayo maeneo ya taasisi za umma yakiwemo makanisa na taasisi zingine na shule lakini pia na visima na maeneo mengine ya muhimu kama migodi tukaona namna ya uunganishwaji wa umeme. Mimi kule kuna wachimbaji wadogo wako mwaka wa 10 nadhani wanachimba lakini umeme haujafika mpaka leo, wakisubiri umeme waunganishiwe na kule kuna uzalishaji mkubwa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi zingeachwa kwanza ili tuokoe muda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issaay taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

## TAARIFA

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji amesema kwamba kweli kunatakiwa umeme ufikishwe kwenye baadhi ya taasisi, kwa mfano kwenye nguzo na hii minara ya simu, minara ya simu mingi inaendeshwa kwa ma-*generator* kwa hiyo mimi nilifikiri kwamba ingetoka sera

kabisa kwamba, pamoja na kwamba unapozungumzia taasisi tuzungumzie vilevile kwenye minara ya simu kote kufikiwe na umeme.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia taarifa unaipokea.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea ni ufinyu wa muda tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia eneo hili la kukatia kwa umeme na migao ya umeme. Hili ni janga na hii ni ajali ya kisiasa pia. Wabunge Majimboni hatukai, umeme unakatika wananchi wanatulalamikia, umeme unakuwa wa mgao, wananchi wanatulalamikia, tuangalie mgao huu namna ambavyo tutaupunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbulu Mji linaongoza kwa mgao wa umeme na kukatika kwa umeme, nafikiri kama inawezekana sababu zitolewe mapema na wananchi wajiandae kwa sababu umeme ni uchumi, umeme ni huduma, umeme pia unaleta mafanikio kwa wananchi kufanya shughuli zao kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili litazamwe ili ukataji wa umeme na mgao upungue, tumekuwa na matatizo makubwa kwenye eneo hili hasa kwa mwaka huu tulionao pengine ni umeme ulikuwa mdogo kutokana na mabadiliko ya tabianchi lakini pia na hali ya maji kwenye mabwawa, tuangalie pia utaratibu wa kuzalisha umeme kwa njia ya upepo. Eneo hili la Kanda ya Kati tunao uwezo wa kuzalisha umeme wa upepo. Tafiti zilishafanyika, Serikali iangalie utaratibu sasa wa kuzalisha huo umeme ili uweze kunufaisha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuangalie utaratibu huu wa nauli. Mheshimiwa Waziri ruzuku ya Serikali tumeweka kwenye mafuta, Serikali tunaishukuru kwa kuweka ruzuku ya fedha kwenye ununuzi wa mafuta, hali hii haijapunguza mpaka leo. Wakati tunaweka ruzuku lita ya mafuta ilikuwa shilingi 3,350 saa hizi lita ya mafuta ni shilingi 2,930. Kuna tofauti ya karibu shilingi 500 kwa lita

lakini nauli haijapungua. Tutazame eneo hili kama sababu zinatosha za gharama za nauli kubaki pale halafu huku tumeweka ruzuku ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ni eneo ambalo tunapenda kuishauri sana Serikali itoe fedha za Wizara hii kadri ambavyo zimeombwa na Mheshimiwa Waziri na Wizara yake ili walau mgongano huu wa kulia umeme na kuomba umeme mara kwa mara upungue, kwa sababu yale yaliyowekwa kwenye vipaumbele hivi na Mheshimiwa Waziri viweze kutekelezwa na ili vitekelezwe ni fedha tulizoomba Serikali ijitahidi namna ya kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ingawa siyo kwa umuhimu, ninaomba basi hali hii ya baadhi ya maeneo kwenye mji, Mheshimiwa Waziri tuma timu, fanya ziara mahususi na wewe kwenye maeneo ya Miji kama Mbulu na vijiji vyake. Ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri tuliyowaambia Mbulu Mji una maeneo mawili na maeneo hayo mawili kwa ujumla yameweza kutembelewa na kila Wizara iliona jitihada zake na kuongeza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii ni Mheshimiwa Deo Sanga. *(Makofi)*

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niungane na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wakati Waziri anawasilisha bajeti hapa nimeisikiliza kwa makini, wakati anawasilisha sikuona kuna mahala ametaja ma-‘bi’, bajeti hii imetajwa ni ma-‘ti’ na ma -‘ti’. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mama Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha nyingi za miradi katika Wizara hii ya Nishati ya ma -‘ti’ na ma -‘ti’. Tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunampongeza Waziri January Makamba pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu pamoja na *DG* wa *REA* pamoja na Msaidizi wake na wote wanaotusaidia kazi katika Wizara hii January umeitendea haki Wizara hii unafanya kazi nzuri. Leo Wabunge wenzangu hapa wakati wanachangia wamesema hapa ilikuwa ipitishwe lakini Mheshimiwa Spika akasema kwa utaratibu ni lazima tuseme, tuchangie nakupongeza tena naungana na wenzangu kwa kazi nzuri chapa kazi. Wako watu ambao huwa najiuliza wanapokusoma namna fulani au mnamabifu huko mitaani? Hayo mabifu wayapeleke huko shughuli za Wizara umeiweza kweli kweli chapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri nije kwenye maombi sasa kwa Jimbo la Makambako, nina maombi machache sana, kwenye Jimbo la Makambako nina maombi mawili, matatu. Ombi la kwanza kuna wale wawekezaji waliokuwa wanakuja kuwekeza umeme wa upepo, jambo hilo limechukua miaka zaidi ya kumi na nane, ishirini. Wananchi wale hawawezi kufanya jambo lolote na kufanya shughuli za maendeleo yeyote yale, nikushukuru walikuja walionana na Wizara yako na watalam wako walikaa, ulimwagiza Naibu Waziri alikutana nao, walizungumza lakini mpaka sasa hatujui kinachoendelea. Nikuombe wananchi wa Makambako Viongozi wanakuja hapa kesho, kesho kutwa watakuwa Bungeni hapa ukutane nao ili uweze kuwapa majibu lakini utakapokuwa unahitimisha kesho pia ni vizuri ukasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuna Kata ya Mlowa, Makambako pale ni Halmashauri ya Mji, Kata hii kimsingi ni vijiji lakini kwa sababu ni Halmashauri ya Mji hawa wanahesabika wanalipa gharama wananchi wa Mlowa kama mjini gharama za laki tatu na kitu. Ninakuomba tuma timu yako ya watalaam waungane na wasaidizi wako pale Makambako, wakaone hivi ni vijiji *typical* kabisa wanatakiwa kulipa gharama wanazostahili kulipa wanakijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu katika hilo kuna Kata ya Mahongole, kijiji cha Mpanga, tangu nguzo zimewekwa *transformer* sasa ni zaidi ya miezi saba haijawahi kuwekwa,

ninakuomba wawekewe *transformer* watu hawa ili waweze kuungana na wenzao kupata umeme. Kwa hiyo, *transformer* haipo Mtanga, *transformer* haipo kijiji cha Mahongole, vijiji viwili havina *transformer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wamezungumza Wabunge wenzangu hapa juu ya gharama hizi za umeme. Mimi nilikuwa nashauri kama mwananchi huyu kulipa gharama ile hawezi, kwanini wasikopesheke wawe wanalipa kidogo kidogo, badala mtu kulipa zile laki tatu kwa wakati mmoja? kwa sababu anahitaji kupata nishati awekewe zile gharama ambazo zinatakiwa kulipwa kila mwezi awe analipa kidogo kidogo mpaka tutapomaliza tutapata wateja wengi kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine Meneja wangu wa Mkoa wa Njombe wa *TANESCO* anafanya kazi nzuri sana pamoja na Wasaidizi wake ndani ya Wilaya, Meneja huyu hajathibitishwa na Makambako pale ni *TANESCO* Kiwilaya lakini anafanya kazi hajathibitishwa kama Meneja wa Wilaya. Kwa hiyo, nikuombe ili wafanye najua hata baadhi ya maeneo inawezekana hicho kitu cha namna hiyo, ninakuomba kama anazo sifa mimi nina imani anasifa, wathibitishwe ili waweze kufanya kazi kwa uhakika za kujituma kwa sababu ni watu ambao tumewaamini na ninyi mmewaamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine wananchi wa Njombe ambayo sasa umetuwasilishia bajeti hapa, kulikuwa na mradi ule unaitwa Ruhuji wa Njombe, ndugu zangu wa Njombe Serikali ya Mama Samia ikiongozwa chini ya Rais wetu na wasaidizi wake kijana mchapakazi January Makamba na timu yake zimetengwa shilingi huko ndiyo kwenye ma- 'B' sasa, zimetengwa shilingi bilioni tano na milioni mia mbili, Tunakushukuru sana mradi huu utawasaidia Watanzania, utasaidia Wananjombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Njombe kuna Mradi Rumakali uko katika Mkoa wa Njombe Wilaya ya Ludewa huko nako zimetengwa shilingi Bbilionisita na milioni mia mbili na sabini, hiki kitu siyo kidogo! Ndiyo maana tunaposema Mama anaupiga

mwingi anastahili sifani kwa sababu ya Ma- B na Ma- B yanayokwenda maendeleo katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa Mheshimiwa January wamesema wenzangu hapa mradi wa *LNG* ambao ulikwama kwa miaka saba leo Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan amekukabidhi kazi hiyo. Sasa mradi huu unakwenda kuanza, tunampongeza Mama, tunakupongeza January. Kwamba Watanzania sasa mradi huu ambao ulikwama walikuwa hawana imani sasa tayari wanakwenda, mradi huu unakwenda kuanza na kuwasaidia Watanzania. January Makamba chapa kazi, Mzee Makamba angekuwepo ningesema Mzee Makamba nikupe na zawadi kwa kumzaa kijana huyu, ana maono mazuri huo ndiyo ukweli, penye ukweli lazima tuseme ukweli. Ndiyo maana tunasema Mama amedhamiria Watanzania kuhakikisha anawapa maendeleo katika nchi nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye maji mambo ni Ma- B, ukienda kwenye barabara mambo ni ma-‘bi’, ukienda kwenye elimu mambo ni ma-‘bi’. Leo Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo Kamati hii, Kamati ya Bunge ya Nishati ilikwenda kule Bwawa la Mwalimu Nyerere, leo Wabunge Bwawa la Mwalimu Nyerere tumeliona hapa hapa Dodoma tumeliona Mheshimiwa Makamba tunakutakia kila la kheri na timu yako na Katibu Mkuu wako na Katibu Mkuu yuko imara, huo ndiyo ukweli na *DG* wa *REA* na timu yake tunawatakia kila la kheri Mungu ambariki Mama, tuendelee kumuombea achape kazi kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana lakini vilevile na wewe Spika umeliweza kusimamia Bunge tunakupongeza na wewe kwa kazi nzuri unayofanya. Mwenyekiti na timu yako tunawashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia mbili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga. Waheshimiwa Wabunge, orodha ya jioni hii imekamilika kwa hiyo tumefikia mwisho wa shughuli za Bunge kwa jioni hii ya leo,

tunawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia naamini upande wa Serikali pia umesikia mapendekezo yenu, hoja, pamoja na ushauri kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.50 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis, Tarehe 1 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*